**28 APRILI, 2025**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 28 Aprili, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**SPIKA:** Ahsante sana, Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, Waheshimiwa Wabunge tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, sasa aulize swali lake.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaomba swali langu lipate majibu kwa niaba ya watumishi wote.

**SPIKA:** Swali namba ngapi?

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, swali Namba 152.

Na. 152

### Malalamiko ya Watumishi dhidi ya Kikokotoo

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza: -

Je, lini Serikali itasikiliza malalamiko ya watumishi dhidi ya Kikokotoo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwa sikivu muda wote kunapojitokeza hoja zinazohusu kikokotoo cha mafao kwa wastaafu. Katika kuonesha usikivu wake, kuanzia Julai, 2024 Serikali imeongeza malipo ya mkupuo kutoka 33% hadi 40% kwa

wastaafu na kuanzia mwezi Januari, 2025 Serikali imefanya mabadiliko katika malipo ya pensheni kwa wastaafu kwa kupandisha kiwango cha chini cha pensheni kutoka shilingi 100,000 hadi 150,000 kwa Mifuko yote miwili, *PSSSF* na *NSSF*.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuonesha usikivu huo, Serikali imepandisha kiwango cha malipo ya pensheni kwa mwezi kwa wastani wa asilimia mbili kwa mwaka na kuwa Mifuko imeanza kulipa ongezeko hilo tangu mwezi Januari, 2025.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaishukuru Serikali kwa kuwa sikivu kupandisha hizi asilimia za malipo ya mkupuo kutoka 33% hadi kufika 40%. Swali la kwanza; kwa nini sasa, Serikali isikubali kurudi kwenye kiwango au gawio la zamani kutoka hizi 40% kwenda 50% ambapo kwa hali hii wafanyakazi wakistaafu wanaweza kupata mafao bora?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa kiwango cha sasa ni 40%. Je, huoni sasa ni wakati mzuri wa kuwapandishia hawa watumishi wanaostaafu kwenda 50% ya kiwango cha zamani, maana zamani walikuwa wanagawanya ile 500 kwa 80 kuliko ilivyo sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Flatei, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza, tunazidi kukubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge na ikumbukwe vizuri katika Bunge lako hili Tukufu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kulikuwa na hoja za Waheshimiwa Wabunge zilizoomba kufanya mabadiliko katika viwango vya pensheni. Kwa usikivu wa

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alimwelekeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu alituelekeza namna ya kuweza kufanyia kazi jambo hilo. Tulifanya marekebisho hayo kutoka kwa wale waliyokuwa wanalipwa 50% ya mkupuo kwa kipindi kile, kutoka 30% kwenda 40% lakini kwa wale waliokuwa wakilipwa 33% wamepandishiwa mpaka kufikia 35% kwa wale waliyokuwa wanalipwa 25% kabla ya mabadiliko ya Mfuko.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mabadiliko ya pensheni ni endelevu na tunazingatia sana kufanya tafiti, lakini pia kufanya *actuarial evaluation* ambazo zinaendelea na kwa mujibu wa sheria kila baada ya miaka mitatu tunafanya *actuarial evaluation* na kuangalia hali ya uchumi na ustahimilivu wa Mifuko na tunafanya mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba zingatio hilo limeendelea kuwepo na ndiyo maana hata mwaka huu mwezi Januari tumeongeza kiwango cha pensheni kutoka ile iliyokuwa inalipwa shilingi laki moja kama kiwango cha pensheni kwenda shilingi laki moja na nusu. Kwa hiyo, hayo ni mazingatio ambayo tumeendelea kuboresha na Mifuko yetu kwa kweli imeboreka na sasa changamoto za masuala ya pensheni ni chache sana na ni kwa *specific cases*. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Latifa Khamis Juakali, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake, kwa niaba yake Mheshimiwa Ally Mohamed.

Na. 153

**Elimu kwa Vijana Juu ya Mikopo ya Asilimia 10**

**MHE. ALLY M. KASSINGE K.n.y. MHE. LATIFA KHAMIS JUAKALI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia vijana elimu kuhusu mikopo ya asilimia 10?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekuwa zikitoa mikopo kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu inayotokana na 10% ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kuzingatia Kifungu cha 37A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 na Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za mwaka, 2024.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 38 ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za mwaka 2024, Mamlaka ya Serikali ya Mitaa zinapaswa kutoa mafunzo kwa vikundi vinavyoomba na kupata mkopo ikiwemo masuala ya uwekaji wa akiba, uundaji wa vikundi vyenye tija, uongozi, usimamizi wa fedha, uendeshaji wa miradi na utoaji wa taarifa na usimamizi wa marejesho ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni hiyo katika mwaka wa fedha 2024/2025, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetoa mafunzo kwa vikundi 2,827 vya vijana ambavyo vilipewa mikopo ya 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mohamed, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninatoa ushauri kwa Serikali kuwa licha ya kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya kuweza kuwawezesha vijana wetu, lakini bado inaonekana kuna hatua ambazo siyo nzuri sana ya utoaji wa elimu kwa sababu wanapata mikopo, lakini baadaye wanashindwa kuifanyia kazi vizuri. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali iendelee kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa vijana wetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, pokea ushauri huo. Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu Mbunge wa Singida Mashariki, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Martha Gwau.

Na. 154

**Ujenzi wa Vituo vya Afya – Singida Mashariki**

**MHE. MARTHA N. GWAU K.n.y. MHE. MIRAJI J. MTATURU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Afya vya kimkakati kwenye Kata za Isuna, Mang'onyi na Siuyu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mpango wa ujenzi wa vituo vya afya katika Kata za kimkakati kwa awamu. Katika mwaka 2024/2025, Serikali imetenga shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya kwenye Kata ya Misughaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali kupitia fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Singida imetenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Isuna. Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo vya afya katika Kata za Kimkakati zikiwemo Kata za Mang'onyi na Siuyu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Gwau, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri, nina swali moja la nyongeza. Je, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya cha mkakati cha Misughaa ambacho Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo Miraji Mtaturu alishakiombea fedha? Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE.ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika mwaka huu wa fedha 2024/2025 shilingi milioni 250 zitatolewa kwa

ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha afya cha kimkakati kwenye Kata ya Misughaa.

Mheshimiwa Mbunge Mtaturu amekuwa akipaza sauti yake kuiomba Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iweze kuleta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki cha afya cha mkakati na Serikali sikivu, imemsikia na italeta fedha hizi kwa ajili ya kujenga kituo hiki cha afya ili kiweze kuwanufaisha watu wa Singida Mashariki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Livingstone Lusinde, swali la nyongeza.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali itatukumbuka Kituo cha Afya Kata ya Mvumi *Mission* kama ambavyo tumekuwa tukiomba siku zote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE.ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifanya ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha kwamba Kituo cha Afya cha kimkakati kinajengwa katika Kata aliyoitaja. Ninaomba nimtupe taarifa njema Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Awamu ya Sita italeta shilingi milioni 250 katika mwaka huu wa fedha, kwa ajili ya kuanza kujenga Kituo cha Afya cha kimkakati hicho ulichokitaja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, Kata za Jangalo, Lahoda na Mpendo ni Kata za mpakani na ziko mbali sana na huduma za afya. Ni upi mkakati wa Serikali wa kutoa fedha ili tuweze kujenga vituo vya afya kwenye Kata hizo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inatambua umuhimu mkubwa sana wa kuimarisha huduma za afya ya msingi na ndiyo maana katika kipindi cha miaka nine cha utawala na uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, jumla ya shilingi trilioni 1.29 zimewekezwa katika kuimarisha Sekta ya Afya Msingi. Katika kipindi hicho cha miaka minne vituo vya afya 367 vimejengwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Monni kwamba Serikali kwa kutambua umuhimu wa vituo vya afya alivyovitaja katika Jimbo lako kwa awamu itaendelea kuleta fedha kwa ajili ya kuvijenga vituo hivyo vya afya ili viweze kuwanufaisha wananchi wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Ngongowele ni cha mwaka wa fedha 2021/2022, lakini kilipata shilingi milioni 250 tu mpaka leo kituo kile hakijapata pesa zingine na Kituo cha afya cha Mpengele hakina jengo la *OPD*.

**SPIKA:** Mheshimiwa, sasa hapo swali au unachangia, swali lako ni la nyongeza? Kituo kimoja cha afya unataka mchango, hebu uliza swali lako la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza ni kwamba, ni lini Kituo cha Afya cha Mpengele na Ngongowele vitapatiwa fedha ili viweze kukamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta na kutoa fedha kwa ajili ya kuendelea kuimarisha huduma za afya msingi na imekuwa ikifanya hivyo kwa kuimarisha miundombinu katika sekta hii muhimu kabisa katika hospitali vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali italeta fedha katika vituo vya afya alivyovitaja kwa ajili ya kuvikamilisha ili viweze kutoa huduma za afya msingi nzuri kwa wananchi wake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Itigi Jimbo ninaloliwakilisha, tuliahidiwa na Serikali kwamba tutaletewa pesa kwa ajili ya kujengewa kituo cha afya cha mkakati. Je, nasi tutapata katika awamu hii? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE.ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Massare amekuwa akifanya ufuatiliaji wa karibu kabisa ili kuhakikisha kwamba kituo cha afya cha kimkakati kinajengwa katika Jimbo lake. Ninaomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka huu wa fedha 2024/2025 kabla haujaisha, Serikali italeta shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya ambacho amekuwa akikipazia sauti.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha afya katika Kata ya Uyui ambayo iko kijijini katika Manispaa ya Tabora Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa njema Mheshimiwa Mwakasaka kwamba katika Mwaka huu wa Fedha 2024/2025 kabla haujaisha, Serikali italeta shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuanza kujenga kituo cha afya cha kimkakati katika Jimbo lako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 155

**Hatua kwa Waliohusika na Udanganyifu kwenye Mikopo ya Asilimia 10 ya Halmashauri**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Je, Serikali imechukua hatua gani kwa Vikundi hewa na udanganyifu kwenye mikopo ya asilimia 10 kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mara inapobaini uwepo wa vitendo vya udanganyifu na uwepo wa vikundi hewa wakati wa utoaji wa mikopo ya 10% kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutoa elimu kwa wanufaika zipo hatua mbalimbali zinazochukuliwa kutokana na udanganyifu ikiwa ni pamoja na kusitisha mikopo kwa vikundi vinavyohusika, kuanzisha uchunguzi, pamoja na kuwachukulia hatua watumishi wa umma walioshiriki au kushindwa kutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria, kanuni, na taratibu za utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha utaratibu wa utoaji wa mikopo ya 10% unakuwa bora, Serikali imeanzisha mfumo wa kidigitali unaojulikana kama "*Wezesha Portal*" ambao unahakikisha vikundi vyote vinathibitishwa kwa njia ya kielektroniki kabla ya kupewa mkopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, mikopo ya 10% ya wanawake inavyotolewa katika Halmashauri haina uwiano sawa, kwa sababu kuna Halmashauri zingine zina mapato madogo sana, kwa mfano chini ya shilingi bilioni tano lakini zingine zina mapato ya zaidi ya shilingi bilioni sitini kuendelea. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya kutoa mikopo hii kwa msawazisho ili zile Halmashauri ambazo hazina mapato makubwa na zina uhitaji mkubwa wa mikopo hii waweze kuziongezea fedha?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kumekuwepo na malalamiko sana kutoka kwenye kundi la wazee kwamba na wenyewe hawajafikiriwa kwenye mikopo hii, tunajua kwamba mikopo hii ni kwa ajili ya makundi maalum, sasa hivi inatolewa kwa vijana wanawake na watu wenye ulemavu. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuweza kuongeza kundi la wazee kwenye hii mikopo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kutokana na sera ya ugatuzi wa madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa, kuna *component* muhimu sana ya *D-by-D* ambayo inaitwa ugatuzi wa fedha, *fiscal decentralisation* ambayo inataka Serikali zetu za Mitaa ziweze kukusanya mapato na kupanga matumizi.

Mheshimiwa Spika, ninaelewa hoja ya Mheshimiwa Mbunge, lakini kwa sababu, kila halmashauri inajitegemea kukusanya mapato kwa kalenda yake yenyewe na kuweza kupanga matumizi, kwa ajili ya watu wake. Basi hatuwezi, kama Serikali, kukusanya yale mapato na kuanza kuyagawa sawa kwenye halmashauri zote japokuwa inaweza ikaonekana kwamba, kuna baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zina mapato makubwa, lakini pia, tuzingatie maeneo hayo, nitatoa mfano.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, yenyewe jumla ya 10% ya Watanzania wote inatoka Jiji la Dar es

Salaam. Kwa hiyo, unaweza ukaona pia, uhitaji unakuwa ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano, mwaka jana kulikuwa na mapato ya ndani yametengwa, kwa ajili ya kutoa hii mikopo ya 10%, shilingi bilioni 13, lakini maombi yaliyojitokeza ni shilingi bilioni 19. Kwa hiyo, utaona kwamba, kuna uhitaji mkubwa pia, katika haya maeneo ambayo tunaona yana mapato makubwa. Kwa hiyo, Serikali inaelewa hoja yako na tutaendelea kuziwezesha Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa ili ziweze kujitengenezea mapato, kujitegemea na kupanga matumizi kusaidia haya makundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na swali lako la pili, kuwajumuisha wazee katika hii 10% ya mapato ya ndani kwenye hii mikopo. Serikali ina vyanzo vingi vya kuwawezesha wananchi wake. Sasa 10% ya mapato ya ndani, hii mikopo inatoka mahususi, kwa ajili ya kundi la vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Bado kuna Mifuko na fursa nyingine ambazo zinawezesha makundi mengine, ikiwemo wazee. Mfano, kwenye Sheria yetu ya Manunuzi *(PPRA)* inataka kila Taasisi ya Serikali itenge 30% ya manunuzi yake, kwa ajili ya makundi maalum likiwemo kundi la wazee. Kwa nini?

Mheshimiwa Spika, sasa wazee wanaweza wakaunda kikundi, wakaajiri vijana, wakapata kazi. Wakaingia kwenye mfumo wa manunuzi, ule wa *NeST,* wakaomba kazi, wakapata na ikawa ni sehemu ya wao kuwa wamejipatia mtaji na fursa, kwa ajili ya kufanya shughuli za uzalishaji. Huku kwenye Mfuko huu wa 10% ya mapato ya ndani ya halmashauri tunataka tuwaone wahusika wao wenyewe na tunawakagua kwa shughuli zao wanazozifanya kwenye vikundi, tofauti na huu utaratibu mwingine ambao wazee wanaweza wakaajiri vijana wakawafanyia kazi, wakapata zabuni kupitia Mfumo wa *NeST* na wenyewe wakaweza kuwa wanajipatia kipato. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Ninapenda kuuliza swali hili kwamba, kuna vikundi vingine ambavyo havirejeshi kabisa hizo fedha. Hizo fedha zipo katika mzunguko, ina maana zinapotemwa katika mzunguko vikundi vingine tena vinachukua. Je, Serikali inachukua hatua gani kwa watu wasiorejesha fedha hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, lengo la kuanzisha mfuko huu ambao unatokana na fedha za 10% za mapato ya ndani ya halmashauri ni kutengeneza mitaji, kwa ajili ya kuwezesha haya makundi. Mfuko huu ni mfuko ambao tunataka tuendelee kukopesha vikundi vingi zaidi (Mfuko wa Mzunguko). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba, Mfuko huu unaendelea kudumu na kunufaisha makundi mengine mengi, basi tunachukua hatua mbalimbali ikiwemo hatua za kisheria. Tunafanya ufuatiliaji, kufuatilia wahusika wale ambao hawarudishi mikopo hii. Wale ambao wanajihusisha na udanganyifu tunawachukulia hatua za kisheria kwa kuazisha mashauri kupitia Mahakama. Watumishi wa umma ambao wanashiriki katika udanganyifu huo au wanakwepa kutimiza wajibu wao na kusababisha hasara hiyo ya upotevu wa fedha kupitia hizi zinazokopeshwa, basi na wenyewe taratibu za utumishi wa umma zinachukuliwa taratibu za kinidhamu kwa mujibu wa sheria na kanuni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 156

**Kuzifanya Shule Chache za Kata Kuwa za Bweni**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutenga Shule chache za Kata kuwa za bweni kwa kuwa, matokeo ya wanafunzi si mazuri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa shule kuwa na mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia, ikiwemo uwepo wa mabweni. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024 – 2024/2025, Serikali imetumia shilingi bilioni 70.33 kujenga mabweni 537 katika shule za kata 270, ili zipandishwe hadhi kuwa kidato cha tano na sita. Kipaumbele cha Serikali kwa sasa ni ujenzi wa shule mpya za kutwa ili kupunguza msongamano wa wanafunzi na watoto kutembea mwendo mrefu na kuongeza nafasi katika shule za kidato cha tano na sita.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze Serikali kwa kupeleka fedha za ujenzi wa mabweni ya kuongeza shule za kata kuwa kidato cha tano na cha sita. Swali langu la kwanza; kutokana na ufaulu ambao kwa kweli, siyo mzuri kwa kidato cha nne na hii inatokana na jiografia za kata, shule hizo kuwa mbali na maeneo ambayo watoto wanatoka. Je, Serikali haioni ni muda sahihi sasa kutoa ruhusa kwa wadau mbalimbali kujenga angalau *hostel* kwenye maeneo ya shule, ili watoto wa kidato cha kwanza mpaka cha nne waweze kukaa jirani?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa, lengo mama la ujenzi wa shule hizi ni kuongeza pia, idadi ya watoto wengi watakaofika elimu ya sekondari, lakini kutokana na matokeo ya kidato cha nne kutokuwa mazuri sana. Je, Serikali imeshafanya tafiti au haioni haja ya kufanya tafiti kubaini tatizo la watoto wa kidato cha nne kutokuwa na ufaulu mzuri, ili tuweze kuondoa tatizo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la ujenzi wa *hostel* kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi wanaosoma katika shule zetu za sekondari waweze kuwa karibu zaidi na shule na iweze kuwasaidia katika kupata utulivu wa masomo yao; ninaomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge, huo ndio utaratibu. Serikali tunatoa nafasi na tunashirikiana na wadau mbalimbali, ikiwemo wazazi pia, kujenga *hostel* katika shule kuanzia kidato cha kwanza na cha nne, kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi waweze kupata sehemu ambayo wataweza kufanya masomo yao kwa utulivu.

Mheshimiwa Spika, ili kutatua changamoto ya umbali kwa wanafunzi wetu kufika shule; ndiyo maana kuna mradi mahususi kabisa wa kuendelea kuongeza miundombinu ya shule zetu hizi, Mradi unaofahamika kama *SEQUIP,* ambao unaboresha miundombinu ya shule zetu kwenye upande wa elimu ya sekondari. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kujenga Shule hizi za Kata ambazo ni za kutwa katika maeneo yenye uhitaji mkubwa ili kupunguza msongamano na kupunguza wanafunzi wetu kutembea umbali mrefu kufika katika shule ili waweze kupata utulivu na muda mzuri wa kuweza kujisomea masomo yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ufaulu; vilevile, Serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti kabisa za kuendelea kuimarisha utoaji wa elimu nchini. Ndiyo maana utaona katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, uwekezaji zaidi ya shilingi trilioni 5.1 umefanyika katika Sekta ya Elimu. Yote hiyo, kwanza ni kuendelea kuboresha miundombinu ya shule pia, kuendelea kuajiri na kuwawezesha kimafunzo walimu wetu.

Mheshimiwa Spika, pia, kuboresha namna gani ya kutoa elimu, kwa maana ya kuongeza vifaa na vitendea kazi, kwa ajili ya walimu wetu, matumizi ya teknolojia za TEHAMA, kujenga maabara, ili kuendelea kuboresha elimu inayotolewa. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali

ya Dkt. Samia Suluhu Hassan itaendela kufanya uwekezaji huo mkubwa ili kuendelea kuimarisha elimu inayotolewa kwa vijana wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, Shule ya Kata ya Mikumbi iliyopo Jimbo la Newala Vijijini tumeanzisha ujenzi wa bweni la wasichana ili kuwakinga na madhara kwa sababu, wanatoka maeneo ya mbali sana na shule ilipo. Je, ni lini Serikali itaunga mkono juhudi za wananchi wa Jimbo la Newala Vijijini kuipatia fedha, ili bweni lile liweze kukamilika? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha miundombinu katika Sekta ya Elimu na hasa Elimu Msingi. Ninaomba nitumie nafasi hii kumtaarifu Mheshimiwa Maimuna Mtanda kwamba, Serikali itaunga mkono jitihada hizo za wananchi ambao wameanza kujenga miundombinu hiyo muhimu kabisa katika Sekta ya Elimu, ili iweze kukamilika na iweze kuwasaidia wananchi wetu, kwa maana ya watoto wao, kupata sehemu nzuri ya kupatia ellimu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi ya kuuliza swali. Shule nyingi za vijijini zipo mbali sana na wananchi walipo, kwa maana ya wanafunzi wanakopatikana. Kwa nini Serikali isiamue kwamba, shule za kata zote za vijijini zijenge mabweni, kwa ajili ya shule hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa sasa shule zetu zinazotoa elimu ya kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne ni shule za kutwa. Serikali kwa wakati huu inaweka

kipaumbele zaidi katika kuhakikisha inajenga hizi shule za kata nyingi zaidi katika maeneo yenye uhitaji, ili kupunguza umbali wa wanafunzi kutembea kufika kwenye shule, pia, kupunguza msongamano na kuwapatia fursa vijana wetu kupata elimu.

Mheshimiwa Spika, shule ambazo zinajengewa mabweni ni shule za kidato cha tano na sita, ambazo ni shule za kitaifa, kwa maana zinachukua wanafunzi kutoka maeneo yote ya Tanzania. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuna njia nyingine ambazo zinatumika, kwa mfano Serikali inashirikiana na wadau mbalimbali, kwa ajili ya ujenzi wa *hostel* kwa kushirikiana na wazazi ili wanafunzi waweze kupata sehemu ya kuendelea kupata utulivu wanapokuwa wanapata masomo yao. Kipaumbele cha Serikali kwa wakati huu ni kujenga shule za kata maeneo ambayo bado yana uhitaji na hizi shule za kata ni shule za kutwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe, sasa aulize swali lake.

Na. 157

**Usambazaji wa Umeme wa *REA* Vitongoji vya Mbogwe**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha usambazaji wa umeme wa *REA* kwa vitongoji ambavyo bado havijapatiwa umeme wa *REA* Mbogwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbogwe lina jumla ya vitongoji 335 ambapo kati ya hivyo, vitongoji 140 vimepatiwa umeme, vitongoji 82 Wakandarasi wanaendelea na utekelezaji wa miradi na vitongoji 63 zabuni imetangazwa ili kupata Wakandarasi wa kutekeleza kupitia Mradi wa Kupeleka Umeme Vitongojini Awamu ya Pili *B.* Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini itaendelea kutenga fedha ili kugharamia utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme katika vitongoji 50 vilivyosalia. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; ninafahamu mpango wa Serikali ni kutuwekea *Substation* Mbogwe ili kuondoa hali ya kukatika umeme kwenye wilaya hiyo. Je, lini sasa itaanza kujengwa hiyo *substation*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Kata ya Nanda, Masumbwe, Nyakafuru na Lugunga *transformer* zilishazidiwa na haya maeneo yana viwanda vya mchele. Kila wakati mashine zinapowashwa umeme unakosa nguvu. Lini sasa katika maeneo haya Serikali itatubadilishia *transformer* ili wananchi wa maeneo yale waweze kufanya shughuli zao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge. La kwanza, kuhusiana na *substation* (kituo cha kupoza umeme) ya Mbogwe; Serikali inao mkakati wa kujenga kituo cha kupoza umeme pale Bukombe, kwa ajili ya majimbo mawili, Bukombe na Mbogwe na vilevile, kujenga *line* ya msongo wa kilovoti 220 kutoka Bulyanhulu mpaka Bukombe.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tupo katika awamu ya kwanza ya kutekeleza mradi wa gridi imara ambao umeshafikia 42% na tukimaliza tutakuja kwenye awamu ya pili, ambapo na Mbogwe pia, watapata kunufaika na kituo cha kupooza umeme kupitia kile ambacho kitajengwa Bukombe.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la maeneo ambayo ameyataja ya Nanda, Lulembela, Lugunga pamoja na Masumbwe; ninafahamu Mheshimiwa Mbunge alishaniambia, kulikuwa na maeneo 13 na tayari maeneo saba tumeshayafanyia kazi kwa kuyawekea *transformer* ambazo zinafanana na mahitaji ya maeneo husika. Nimhakikishie Mbunge na kata hizi ambazo zimebakia na zenyewe tutazifanyia kazi. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, maswali mafupi na moja kwa moja kwenye swali, shukrani nimeshazipokea.

Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Je, ni lini Serikali itaenda kutoa fedha, kwa ajili ya kumalizia vijiji na vitongoji 188 katika Wilaya ya Nyang'hwale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, tunayo miradi ambayo inaendelea, ukiwemo Mradi wa Vitongoji 15 kwenye kila Jimbo, ambapo pia na Nyang'hwale inanufaika. Katika mradi huu ambao unatarajiwa kuanza hivi karibuni Nyang'hwale pia, itaendelea kunufaika kwa vitongoji katika jimbo hilo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mkakati wa Serikali upo na tayari unafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ipo, ikiwemo huu mradi ambao upo sasa hivi unakaribia kuanza. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali mna mpango gani au mkakati gani wa kumaliza kutoa nguzo za miti na kuweka za zege ndani ya Jimbo la Temeke ili umeme usikatikekatike tena?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali upo na unaendelea. Kwa kila mwaka wa fedha tunatenga fedha, kwa ajili ya kufanya miradi hiyo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Temeke tunafanya hivyo, kwa ajili ya ukarabati kuhakikisha tunaendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme. Tunaendelea kufanya hivyo, ili wananchi wa Temeke waendelee kupata umeme wa uhakika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, swali la nyongeza.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Spika, ni lini sasa mkandarasi wa kupeleka umeme kwenye Vitongoji vya Wilaya ya Mbarali ataripoti? Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ipo mikoa mitatu ambayo tulikuwa hatujapata wakandarasi, ikiwemo Mbeya, Singida na Tanga, lakini tulishapata wakandarasi na wiki hii wataenda kutambulishwa kwa Wakuu wa Mikoa na kukabidhiwa *site,* ikiwemo Mbeya na hususan kwenye Jimbo la Mbarali la Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Sasa hapo, mbona Mbeya Mjini hujaitaja?

Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 158

**Kupeleka Umeme Vitongoji vya Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Je, lini Vitongoji vya Hendelo, Ngaloi na Muheza, Lushoto, vitapata umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kitongoji cha Muheza kilichopo Kijiji cha Rwandai, Kata ya Rwandai, kitapatiwa umeme kupitia Mradi wa Kupeleka Umeme Vitongojini, Awamu ya Pili *B*, ambao zabuni ya kuwapata Wakandarasi imetangazwa na inatarajiwa kufunguliwa hivi karibuni. Vitongoji vingine vilivyosalia, ikiwemo Hendelo na Ngaloi vitaendelea kupelekewa umeme kupitia miradi ijayo kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, Vitongoji vilivyopimwa toka mwaka juzi, ambavyo ni Vitongoji vya Kwemishai, Kwemkashi, Kwebarabara, Magunga, Zeta, Kiuzai, Ula, Mpalai pamoja na Mzizima, ukizingatia vitongoji hivi vina Taasisi za Dini na Shule za Msingi. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake hiyo ya kuweka umeme katika vitongoji hivyo nilivyovitaja kwa kuwa, vina sifa zote za kupata umeme?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kila Mbunge aliahidiwa vitongoji 15; hivyo vitongoji 15 tulishawahamasisha wananchi na tukawaambia wanapata umeme. Je, ni lini utekelezaji wake utaanza? Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nijibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika vitongoji ambavyo amevitaja, hivyo vyote vimewekwa katika mradi wa kupeleka umeme kwa vile vitongoji 15 vya kila Mbunge. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo tumeahidi, basi ndio hivyohivyo vitongoji vitapatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mkandarasi, nilitaja hapo awali, ipo mikoa mitatu ambayo wakandarasi walikuwa

hawajapatikana. Mbeya, Singida pamoja na Tanga, Lushoto, kwa Mheshimiwa Mbunge, Mkandarasi ameshapatikana ataenda kutambulishwa wiki hii na atakabidhiwa *site*. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 159

**Ukarabati wa Mahakama za Mwanzo Arumeru Mashariki**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ukarabati wa Mahakama za Mwanzo *West Meru* na Nkoaranga, ambazo zimeachwa na kubakia magofu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania imeendelea kutekeleza mpango wake wa ujenzi na ukarabati wa Majengo ya Mahakama wa mwaka wa fedha 2021/2022 – 2025/2026 kwa kuimarisha majengo katika ngazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujenga majengo mapya na kukarabati yaliyopo. Majengo haya yanajengwa na kukarabatiwa kwa awamu kwa kuzingatia Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama na kadri ya fedha zinavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa Mahakama ya Mwanzo Nkoaranga na Mahakama ya Mwanzo West Meru utafanyika kwa bajeti ya 2025/2026. Aidha, kutokana na mahitaji makubwa katika jimbo la Arumeru, mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imejenga

jengo la kisasa la Mahakama ya Mwanzo Maji ya Chai, na lipo katika hatua za mwisho kukamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina swali moja la nyongeza. Kata za Ngalinanyuki, Uwiro, na Ngabobo ziko nyuma ya mlima Meru Kaskazini ambako ni mbali sana na mahakama ya mwanzo ya maji ya chai. Je, Serikali ina tamko gani kuhusu ukarabati wa Mahakama ya Mwanzo iliyoko Ngarenanyuki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, oh! Samahani; Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumefanya katika Mahakama ya Maji ya Chai pamoja na Oldonyosambu, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda kuhakikisha kwamba tunafanya ukarabati katika Mahakama hii ya Ngarenayuki kwa fedha ambayo tutapitisha kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha 2025/2026.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, Kata ya kikunde na Kata ya Pabi halikadhalika na Kata ya Tuhuli zina umbali takribani kilomita 80 kutoka Makao Makuu ya Wilaya ambapo kuna Mahakama ya Mwanzo. Je, kuna mpango mkakati gani wa kuhakikisha kwamba kata hizi zinakuwa na Mahakama za Mwanzo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimesema, Agosti 2022 Mahakama ilizindua mpango wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama. Mpango huo haujaacha kata yoyote, tarafa yoyote wilaya yoyote na mkoa wowote. Kata ya Kinguli na kata zingine kwa Mheshimiwa Omari nao umezingatiwa katika mpango na tutafanya ukarabati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninataka kufahamu, je, wamefikia hatua ipi katika ujenzi wa Mahakama katika Wilaya ya Ileje?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mahakama katika Wilaya ya Ileje unaendelea na tunategemea kwamba utakamilika mwaka ujao wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Fedha Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 160

**Hitaji la Kituo cha Forodha Mukikoro – Ngara**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuanza ujenzi wa Kituo cha Forodha Kijiji Mukikoro Kata ya Mugoma – Ngara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha ujao wa 2025/2026, Serikali ina mpango wa kujenga jumla ya vituo sita vya forodha mipakani na imekwishakutenga jumla ya shilingi bilioni 1.1. Kati ya vituo hivyo Kituo cha Forodha Mugoma - Ngara kitajengwa maeneo ya Mugoma, katika Wilaya ya Ngara, mpakani mwa Tanzania na nchi ya Burundi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninalo swali moja la nyongeza. Mchakato wa ujenzi wa kituo hiki cha forodha katika Kijiji cha Mkikomero Kata ya Mugoma, Wilaya ya Ngara ulianza una miaka zaidi ya miwili sasa tangu uanze. Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa kituo hicho ili kuweka hata makontena tusiendelee kupoteza mapato katika Serikali yetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Oliver kwa kazi kubwa sana na juhudi anayofanya katika ufuatiliaji wa ujenzi wa kituo hicho. Ninaomba nimhakikishie kwamba juhudi yake imezaa matunda mazuri na hivi karibuni kwa sababu fedha imekwishatengwa kituo hicho kitaanza kujengwa mara tu baada ya mwaka wa fedha unaokuja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 161

**Tatizo la Maji Wilaya za Mkoa wa Kigoma**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza tatizo la upungufu wa Maji katika Wilaya za Mkoa wa Kigoma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa Mkoa wa Kigoma ni wastani wa 72.8% vijijini na 79.8% mijini. Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 imekamilisha utekelezaji wa miradi 17 katika Wilaya za Buhigwe, Kigoma, Kibondo, Kasulu, Kakonko pamoja na Uvinza mkoani Kigoma. Aidha, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi 47 ya usambazaji maji pamoja na uchimbaji wa visima 30 katika wilaya hizo ambapo ujenzi wa miundombinu rahisi ya kutolea huduma *(point source)* 13 umekamilika na zinatoa huduma wakati 14 zinaendelea na ujenzi kwa kila jimbo kupitia Programu Maalum ya Uchimbaji wa Visima 900.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali itatoa kipaumbele cha kukamilisha miradi inayoendelea sambamba na kufanya upembuzi yakinifu wa kutoa maji Ziwa Tanganyika kwa lengo la kunufaisha Mikoa ya Kigoma, Rukwa na Katavi. Lengo ni kuhakikisha kwamba wananchi wa Wilaya zote za Mkoa wa Kigoma wanapata huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la maji Mkoani Kigoma kwa kutumia chanzo cha Mto Malagalasi?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; katika Halmashauri ya Kibondo, Kata ya Mabamba, Shule ya Sekondari Kumgogo maji hutoka mara moja moja na hivyo wanafunzi wanapata shida ya maji. Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la maji katika shule hiyo ya Sekondari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya kwa Mkoa wa Kigoma kwa kuhakikisha kwamba anawapigania akinamama wa Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan inatambua kwamba zao la maji na ndiyo suluhisho la kudumu kwa maji kutoka mara moja moja. Kama ambavyo amesema katika ile shule inayopatikana Kibondo ni kwamba Serikali imeendelea kuongeza *program* nyingi. *Program* ya kwanza ni ya visima 900 lakini *program* ya pili ni mradi wa miji 28 ambapo unagharimu bilioni 35 ambao uko katika 45% ya utekelezaji ambao tunatumia Mto Ruchugi lakini vile vile tuna mradi ambao RUWASA wanaendelea nao, ambao miradi takribani miradi 37 yenye gharama ya bilioni 13.5

Mheshimiwa Spika, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, Mradi wa Maji Mto Malagarasi awali tulifanya usanifu ili uweze kuhudumia maeneo ya Kaliua pamoja na Urambo lakini baadaye Ziwa Victoria likaleta kwa sababu ndicho chanzo cha uhakika.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu tunakwenda kutumia mradi wa Ziwa Tanganyika kama ambavyo nimejibu katika jibu la msingi tayari Serikali imeanza kutafuta mtaalam mshauri ili afanye upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa kina ili aweze sasa kuona namna gani tutatumia maji ya Ziwa Tanganyika kwa Mikoa ya Kigoma, Rukwa pamoja na Katavi. Kwa hiyo tunaamini kwamba maji hayo yataweza kuwa suluhisho la kudumu kwa wananchi wa Mikoa ya Kigoma Rukwa pamoja na Katavi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ninataka kujua mkakati wa Serikali wa kumaliza tatizo la maji katika Kijiji cha Unyali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na pia nimshukuru Mheshimiwa Gerete kwa swali lake. Mradi huo wenye gharama ya milioni 830 tayari mwezi Februari Mheshimiwa Waziri wa Maji alielekeza milioni 141 ifike pale kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mkandarasi anaendelea na utekelezaji wa mradi huo. Hivyo mradi huo unaendelea kutekelezwa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kutosha ili kumalizia Mradi wa Maji wa Munyo katika Jimbo la Ikungi Magharibi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba inatekeleza miradi yake yote nchini kulingana na upatikanaji wa fedha. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kwa upande wa Singida tuna miradi mingi inaendelea. Mradi huu ni kipaumbele kwetu na fedha tayari tumeshawasilisha hati za madai Wizara ya Fedha kwa ajili ya mkandarasi kulipwa ili mkandarasi aweze kukimbiza kazi na ikamilike kwa wakati. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Chagula, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la maji katika Wilaya ya Chato?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya maji katika Wilaya ya Chato Mkoani Geita, lakini vilevile Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan amewekeza fedha nyingi katika utekelezaji wa Mradi wa Miji 28 katika Mji wa Chato. Huu

mradi utakapokamilika Wanachato watakuwa wameondokana kabisa na tatizo la maji. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Uchukuzi Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo.

Na. 162

**TPA Kuendeleza Bandari ya Kyamkwikwi – Muleba**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO K.n.y. MHE. CHARLES J. MWIJAGE** aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali kuendeleza Bandari ya Kyamkwikwi na kujenga barabara ya kuunganisha Bandari na Barabara Kuu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TPA* imekamilisha kazi ya kuhuisha Mpango Kabambe wa Mwaka 2021 - 2045 wa Uendelezaji wa Miundombinu ya Bandari Nchini.

Mheshimiwa Spika, Mpango huo umeainisha mahitaji ya uendelezaji wa Bandari nchini ikiwa ni pamoja na Bandari ya Kyamkwikwi katika Ziwa Victoria. Mpango Kabambe huo unatekelezwa kupitia Mpango Mkakati wa miaka mitano mitano ambapo kwa sasa *TPA* imeanza na ujenzi wa Gati la kuhudumia shehena na abiria katika maeneo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Muleba ina visiwa vingi na tumekuwa tukitegemea Meli ya *Clarious* kutoa huduma ambayo si salama kwa kipindi hiki. Swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani wa kutupatia vyombo salama na imara kwa ajili ya kuhudumia watu wetu wa Muleba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Wilaya ya Muleba mwaka juzi alitoa maelekezo *TPA* kujenga bandari ndogo ya Katembe Magarini. Je, lini *TPA* ina mpango wa kutekeleza hilo agizo? Ninashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Kikoyo pamoja na Mheshimiwa Mwijage kwa sababu wamekuwa ni Waheshimiwa wanaofuatilia kwa ukaribu sana maboresho makubwa sana ya kibandari katika ziwa letu, Ziwa Victoria ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Kikoyo kwamba Serikali imefanya mambo mengi katika Ziwa Victoria ili kuimarisha usalama na kuhakikisha kwamba usafiri unaokuwepo unakuwa ni wa uhakika. Kwa awali ninapenda kumhakikishia na kumweleza kwamba tayari Serikali imefanya maboresho ya kujenga bandari tatu ikiwemo Bandari ya *North* Mwanza, Bandari ya Kemondo na Bandari ya Bukoba. Bandari ya Kemondo imekamilika North Mwanza pamoja na Bukoba zinaendelea. Hiyo ni hatua ya kwanza ya kuhakikisha kwamba usafiri kwenye ziwa hilo unakuwa ni wa uhakika na wenye usalama.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali imechukua jukumu kubwa ya kujenga vituo mbalimbali vya uokoaji katika Ziwa Victoria. Vingine vimejengwa Sengerema, vingine Victoria pale, kwa maana ya Mwanza na Geita na maeneo mengine. Aidha, tayari Serikali imetenga fedha za kutosha na tupo kwenye hatua za mwisho wa

kujenga meli kubwa MV Mwanza Hapa Kazi Tu ambayo tunategemea itakamilika siyo muda mrefu kuanzia sasa. Itakapokamilika hiyo itakuwa imaimarisha usafiri wa uhakika kati ya Mwanza, Bukoba kwa maana ya Mkoa wa Kagera, pamoja na maeneo kama *Port Belly* na maeneo mengine ambayo yanazunguka kwenye ziwa hilo.

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye hoja yake ya visiwa vile vya kawaida alivyovisema ikiwa ni pamoja na vilivyopo katika eneo la Muleba, tayari Serikali inatambua umuhimu wa meli hiyo kuwepo, ambayo ni ya Serengeti. Tumekwishaanza utaratibu wa kuainisha mahitaji, kwa sababu meli hii ilisimama 2019 lengo letu tutazame mahitaji ni kiasi gani tuikarabati na ianze kufanya kazi ambayo itakwenda kwenye visiwa vidogovidogo ikiwa ni pamoja na ambavyo Mheshimiwa Kikoyo amevisema.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo tayari meli ya mizigo ya *ML* Wimbi ambayo ambayo yeye anaifahamu ambayo inabeba mizigo midogomidogo, ikiwemo bidhaa za dukani pamoja na dagaa na vitu vingine vingine iko mwishoni ikikamilika itakwenda pia kwenye eneo hilo la Muleba kwa ajili ya kuhakikisha tunawasaidia wananchi wetu hao.

Mheshimiwa Spika,  swali lake la pili amezungumzia kuhusu agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu. Wizara yetu inatekeleza maelekezo ya viongozi wakuu wote kwa msisitizo na uzito unaostahili, ikiwa ni pamoja na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, na kwa kuanzia tayari tumeshaanza mchakato kwa ajili ya kuhakikisha tunatazama namna ya kuweka kwenye bajeti ijayo. Hata hivyo ikumbukwe kwamba nchi hii ina bandari 693, uwezo wa Serikali kuanza kuzijenga zote kwa wakati mmoja hauwezekani. Tunaanza kidogo na tumeshaanza kurasimisha mpaka mwaka 2021 tulikuwa tumerasimisha bandari 80 na Mheshimiwa Dkt. Samia suluhu Hassan amekwenda kwa kasi kubwa zaidi zimeongezeka zaidi ya bandari 50. Hivyo

nimuombe awe na subira tutajitahidi hatua kwa hatua na kwake tutamfikia tena. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako. Ah! Kuna Mbunge; Mheshimiwa Felix Kavejuru, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, lini ujenzi wa Bandari ya nchi Kavu ya Gungu Mjini Kigoma utaanza kwa sababu Serikali imekuwa ikiahidi kwa muda mrefu sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, samahani nilikuwa sijasikia bandari gani?

**SPIKA:** Bandari kavu.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, bandari ya nchi kavu Gungu Mjini Kigoma.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, Serikali kwa Kigoma inafanya mpango wa kujenga bandari kavu iliyopo Kigoma mjini ili kuunganisha kati ya nchi yetu na nchi jirani. Hii aliyoitaja ninaomba nichukue na tuanze kulifanyia kazi kulingana na mahitaji sambamba na uwepo wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kavejuru hiyo uliyoitaja iko jimbo gani?

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, iko Jimbo la Kigoma Mjini na tayari Serikali ilikwishaweka fensi kwa muda mrefu na ilipa fidia wananchi waliokuwa wanaishi pale wakaondoka kabisa kwa muda mrefu, zaidi ya miaka 10 sasa; na pana fensi. Sasa kwa muda mrefu wananchi wa Kigoma wamekuwa wakisubiri ujenzi wa bandari hiyo ya nchi kavu mpaka sasa hivi hakuna kitu kinachoendelea.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Sasa umepata ufafanuzi Mheshimiwa Naibu Waziri ni hiyohiyo ya mjini uliyoijibia, ndiyo hiyohiyo na yeye anayoiulizia ahsante sana.

Haya, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Rose Vicent Busiga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 163

**Mafao ya Mashujaa wa Vita vya Kagera na Uganda**

**MHE. ROSE V. BUSIGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa mafao yao mashujaa wa Vita vya Kagera na Uganda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mashujaa wote waliopigana vita vya Kagera na waliostahili malipo ya viinua Mgongo na Pensheni walikwishalipwa na wengine wanaendelea kulipwa kwa mujibu wa Sheria ya Pensheni na Viinua Mgongo ya Mwaka 1966; ikiwemo pia malipo ya ulemavu na ustaafu.

Mheshimiwa Spika, kundi ambalo lilishiriki vita na halikuwa limeajiriwa na vyombo vya ulinzi na usalama, baada ya vita lilipewa nafasi ya kujiunga katika vyombo vya ulinzi na usalama kwa kufuata taratibu. Kwa wale walioamua kutojiunga na wale waliokosa sifa katika kundi hilo walilipwa kifuta jasho, Ahsante Nyerere kiasi cha Shilingi 5,000 ambayo kwa wakati huo ilikuwa pesa ya kutosha na kurejeshwa makwao.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa ikikabiliana na changamoto mbalimbali kuhusiana na maveterani wa Vita ya Kagera. Miongoni mwa changamoto hizo ni madai ya

mavetenari wote kuingizwa katika daftari la Pensheni licha ya kuwa baadhi yao hawakidhi vigezo kwa mujibu wa Sheria, madai kuwa pensheni ni ndogo na maombi ya kupewa Bima ya Afya.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imeandaa mapendekezo ya maboresho ya Sheria ya Pensheni na Viinua Mgongo ya mwaka 1966 na kuiwasilisha Serikalini, yakijumuisha maveterani waliopigana Vita vya Kagera. Aidha, Wizara imewasilisha Serikalini mapendekezo ya kuona uwezekano wa kuwaingiza maveterani waliopigana Vita vya Kagera kwenye utaratibu wa bima ya afya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Busiga, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ni lini maboresho ya Sheria ya Pensheni na Kiinua Mgongo ya Mwaka 1966 yataletwa Bungeni?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa mashujaa hawa wengi wao wana hali ngumu ya kimaisha, ni lini Serikali itaweza kuwapa msaada wa dharura ili waweze kusaidika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kuwapigania ma-*veteran* hawa. Swali hili limeulizwa Wabunge wengi sana, mara kadhaa hapa Bungeni na nimekuwa nikilitolea majibu baada ya kuona kwamba majibu haya hayawaridhishi Wabunge. Kama Wizara tulifanya tathmini ya kina ili kuweza kujua tatizo ni nini. Kwa hiyo, tumekwishafanya tathmini ya kina kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, swali lake mahususi kwamba ni lini tutaleta marekebisho ya sheria, utaratibu uliopo ni kwamba mafao na stahiki za wanajeshi zinaongezwa na *National Defense*

*Act Cap. 192* ya Mwaka 2002 na Kanuni zake ambazo ni *Defense Service Pension and Gratuity Regulations* na hizi huwa zinakwenda kwenye halmashauri ya majeshi. Baada ya hapo inapelekwa kwa Amiri Jeshi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hatuleti hapa Bungeni, lakini tumekwishakamilisha taratibu zote. Halmashauri hiyo ya majeshi imeshakaa; nami ndiyo Mwenyekiti. Tumeshapitisha na tumeshawasilisha kunakotakiwa. Kwa hiyo, mara baada ya hapo basi tutaleta mrejesho tumefikia hatua gani.

Mheshimiwa Spika, ni suala ambalo tumetoa kipaumbele sana kwa sababu mara nyingi nimeulizwa swali hili na sisi tukaona kwamba tulifanyie kazi. Ninapenda sana kumshukuru Waziri wa Fedha kwa kutoa ushirikiano mkubwa sana ambao umetuwezesha kukamilisha uchambuzi na mapendekezo tuliyokuja nayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa dharura; mpango wa dharura ndiyo huu tunaokwenda nao, lakini pale ambapo wapiganaji hawa (Ma-*veteran)* wanakuwa na shida mahususi za kidharura huwa hatuwaachi, tunawasaidia kadiri inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENEYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, baadhi ya hawa ma-*veteran* (mashujaa wetu wa Vita ya Kagera) malalamiko yao siyo mafao basi shukrani. Wao wanasema baada ya vita Mwalimu Nyerere alitamka ahsante. Sasa wanachouliza, je, ahsante pekee inatosha? Wanaiomba Serikali iwakumbuke.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, majibu yake ya msingi umeyasikia? Walipewa neno ahsante na shilingi elfu tano kwa wakati huo. *(Kicheko)*

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ni sahihi kabisa lakini kumbuka hawa wazee bado wapo wanaishi…

**SPIKA:** Sasa majibu, Mheshimiwa Waziri ameshatoa. Wanaoishi wanaendelea kuhudumiwa kwa kadri Serikali ilivyojipanga, yaani ninataka uulize swali lako kwa sababu ni la nyongeza, uliza swali maalum la nyongeza kwenye majibu haya aliyotoa Mheshimiwa Waziri.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kuwatambua hawa wazee na kujua hasa shida zao au malalamiko yao ni yapi na kuyafanyia kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, tunawatambua na changamoto zao tumeshazifanyia tathmini na ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimesema kwamba changamoto tulizoziainisha ambazo zimekuwa zikijitokeza mara kwa mara ni kutaka kuingizwa kwenye Mfuko wa Pensheni kwa wale ambao hawakustahili.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya pili ni matibabu na mapendekezo ndiyo tumekuja nayo waweze kupewa bima ya afya, lakini na hata wale ambao hawakustahili kupewa pensheni kwa hilo unalolisema kwa kutambua mchango wao tuone tunaweza kuwaingiza kwa namna gani. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Changamoto ya Vita ya Kagera bado inaonekana kwenye maeneo hayo mpaka leo. Utaona umaskini mkubwa katika maeneo ya Kyaka na bado wanaendelea kusingizia kwamba ni changamoto ya vita.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Serikali isione umuhimu wa kupeleka miradi, kama miradi ya ujenzi wa majengo au nyumba ambazo wanaweza kuwakopesha wale waliopigana vita na wazee wakawa wanalipa taratibu taratibu ili kuweza kuboresha maisha yao tofauti na ilivyo leo wanavyoendelea kulalamika?

**SPIKA:** Baadhi ya haya maswali jamani mpaka Spika anapata wakati mgumu kuikabidhi Serikali ijibu. Sasa hawa wanatafuta pensheni, wataweza kulipa huo mkopo Mheshimiwa Anatropia? *(Kicheko)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, wanadai pensheni kwa sababu ya ugumu wa maisha. Ninatamani siku moja utembelee yale maeneo ambayo bado yako duni vilevile.

**SPIKA:** Swali langu hujalielewa. Ninasema hivi, umesema wajenge maghorofa wawakopeshe. Watalipaje wakati umeshasema ni masikini?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, wakishawapatia hayo majengo hata hizo pensheni pengine watakuwa wanawakata taratibu ku-*compensate* wakipata maeneo yenye hadhi ya kuishi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri pokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge. Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mwantumu Zodo.

Na. 164

**Changamoto ya Mawasiliano Kata ya Kipugila – Rufiji**

**MHE. MWANTUMU M. ZODO K.n.y. MHE. HAWA M. CHAKOMA** aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali juu ya changamoto ya mawasiliano ya simu katika Kata ya Kipugila Rufiji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Kipugila, inapata huduma ya mawasiliano kupitia minara iliyojengwa katika Vijiji vya Kipo kwa mnara wa *Halotel* na Kipugila mnara wa *TTCL.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameuliza swali kuhusu jitihada za Serikali katika kutatua changamoto ya mawasiliano katika kata hii, inaashiria kuwa bado kuna changamoto. Wizara kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* itafanya tathmini kwenye kata hii ili kubaini mahitaji halisi ya mawasiliano na endapo ikibainika kuwepo kwa tatizo la mawasiliano katika kata husika, itaingizwa katika zabuni ya miradi itakayotekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Kipugila ambayo Mheshimiwa Hawa ameuliza swali kuna mnara mmoja wa *halotel,* lakini bado kuna mawasiliano ya kusuasua. Swali la kwanza; je, ni lini sasa Serikali itajenga minara mingine kama mnara wa *Halotel, Voda* na *Mixx By Yas* ili kuhakikisha wananchi hao wanapata mawasiliano ya uhakika?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; katika maeneo ya Jimbo la Tanga Mjini, yaani maeneo ya Mwang'ombe na Kange palepale mjini pia bado kuna mawasiliano ya kusuasua na minara ipo. Je, ni nini changamoto hasa katika maeneo hayo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, katika eneo hili la Kipugila kuna mnara wa *Halotel* lakini mawasiliano hayajakaa vizuri. Ninaomba tu nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba kama mnara upo

basi kwa niaba ya Waziri nitoe maagizo kwa watoa huduma wa Halotel kuhakikisha wanakwenda kuboresha kwa ku-*upgrade* mnara huu, kuhakikisha teknolojia zote zinaweza kuwekwa. Kama *2G* ndiyo inayofanya kazi basi *3G* na *4G* pia wakazi-*upgrade*.

Mheshimiwa Spika, kwa watoa huduma wengine nje ya *Halotel (Voda, Yas* na *TTCL)* nao kuweza kupatikana kama namna alivyowataja. Basi kuna matumizi ya pamoja ya miundombinu ili kuokoa muda, wanaweza kuwasiliana na watu wa *Halotel* wakatumia mnara huu kwa pamoja kama *co-location*. Pia, wanaweza wakafanya *roaming* ili wananchi waweze kupata huduma ya haraka na yenye uhakika.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusiana na Tanga pale Maweni, maeneo haya yana mawasiliano ya shida. Niweze tu kumwomba Mheshimiwa Zodo, tuwasiliane tupate *location* sahihi kabisa za hili eneo ili tuweze kuwaagiza wataalam wetu waweze kufuatilia kwa nini eneo lile lina minara, lakini bado hakuna mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, sasa wakati mwingine huenda kwa sababu kuna *blockage* tu kama maghorofa marefu ama miti ama ni jiografia (miinuko na mabonde), lakini kama hivi vyote havipo basi tukiipata *location* hizi *coordinates* zitatusaidia kuona tatizo ni nini ili tuje tutatue. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali kwa kifupi.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa minara ya mawasiliano ya simu ya *TTCL* katika Vijiji vya Marendego, Makolo na Kandawale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fransis Ndulane, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, minara hii ya *TTCL* katika vijiji hivi ulivyovitaja Mheshimiwa Mbunge nitavisimamia kwa kuhakikisha wataalam wanakwenda kuona hawa wakandarasi wanajenga huu mnara ndani ya wakati wa mkataba. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza. Katika Jimbo la Moshi Vijijini Kata ya Okaoni, Uru Shimbwe, *Old* Moshi Mashariki na kwingine kuna shida kubwa ya mawasiliano. Ni lini Serikali itapeleka minara ili wananchi hawa waweze kufaidika na mawasiliano? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Felista Njau, dhamira ya Serikali kote alikokutaja ni kuhakikisha vijiji, vitongoji na maeneo yote yanapata mawasiliano ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, hivyo, tunaendelea na ujenzi wa minara mbalimbali, kama unavyofahamu minara ya 758 utekelezaji unaendelea na tunatarajia Mei kukamilika na tuna minara 632 na bado tuna *batch* nyingine za minara mbalimbali ya *TTCL* tutakuja kuyafikia maeneo yote haya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Lukumbule katika Kijiji cha Kazamoyo na Imani kilichopo mpakani mwa Mto Ruvuma kina tabu sana ya mtandao. Ni lini Serikali itajenga mtandao katika maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mpakate, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo yote ya mpakani tunaendelea kuyafanyia kazi na nimeshafanya ziara baadhi ya mipaka ili kuhakikisha maeneo yote ya mipakani sasa kupitia changamoto tunazokutana nazo katika ziara yanaweza kufanyiwa kazi. Hivyo, nimtoe hofu hata hii kata aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa tuwasiliane kwa karibu ili niweze kufuatilia kwa ukaribu na kuhakikisha mawasiliano yanaweza kufikishwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Monduli ina changamoto kubwa ya mawasiliano hususan kwenye Kata za Engaruka, Selela na Esilalei. Je, ni upi mkakati wa Serikali sasa kutatua changamoto hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zaytun Swai, Mbunge wa Viti Maalum, kwamba maeneo ya Monduli kuna maeneo kwenye hii kata aliyoitaja mawasiliano hayaridhishi, ninaomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira. Sisi kama Serikali tutaendelea kuhakikisha tunayafikia maeneo yote haya na kata hii aliyoitaja nitakufikia hapo ili tuweze kuwasiliana kwa karibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, kwenye Kata za Kilema, Marangu Magharibi na Mwika Kaskazini kule Vunjo kuna shida sana ya mawasiliano na mawasiliano yaliyopo ni hafifu yanaingiliwa sana mawasiliano ya nchi jirani. Je, ni lini mtagawa hiyo minara 638 kwa awamu ya pili ili tuweze kupewa minara ya kutosha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, maeneo haya yote aliyoyataja yapo katika mikakati ya Serikali. Kadri tunavyopata fedha nimhakikishie tutayafikia na kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya ndani ya nchi na si minara ya nchi jirani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Zahor Mohammed.

Na. 165

**Kauli ya Serikali Juu ya Wanawake Wanaotupa Watoto**

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI K.n.y. MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali juu ya Wanawake wanaotupa watoto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inakemea na kulaani kitendo cha baadhi ya wanawake kutupa watoto kwa lengo la kukwepa jukumu lao la msingi la kusimamia malezi, makuzi na maendeleo

ya awali ya mtoto. Hivyo, ninapenda jamii itambue kuwa Serikali itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya wanawake watakaokutwa na hatia ya kutenda kosa hilo na kuadhibiwa kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto, Sura ya 13, Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 pamoja na sheria nyingine za nchi zilizotungwa kwa suala hilo.

Mheshimiwa Spika, ninawasihi wanawake na jamii kwa ujumla kuacha tabia ya kutupa watoto. Aidha, endapo itatokea kuna mtu ameshindwa kutekeleza jukumu la malezi ya mtoto basi atoe taarifa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hususani Ofisi za Ustawi wa Jamii ambapo watawajibika kuweka mpango wa huduma mbadala kwa mtoto husika sawa na matakwa ya kifungu Na. 94(5) cha Sheria ya Mtoto Sura ya 13. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zahor Mohammed, swali la nyongeza.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Serikali. Swali la kwanza; je, ina takwimu halisi ya mambo haya, kwa sababu inaonekana yamekuwa yakiongezeka kila siku?

Mheshimiwa Spika swali la pili; kwa sababu ya nyongeza hiyo ambayo kila siku imekuwa ikipigiwa kelele, Serikali haioni sasa ipo haja ya kuboiresha sheria hii ili ziwe kali zaidi? Ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeleta mafanikio makubwa kupitia mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika hatua ambazo zimechukuliwa. Kuna madawati 1,103 lakini kuna Mahakama 131 za Watoto ambazo zimefunguliwa na kumeanzishwa vituo 3,963 vya kulelea Watoto; pia, tuna vituo vya kulelea watoto mchana 2,649. Serikali

itaendelea kuhakikisha kwamba tunawatunza watoto, kuwalea na kuwapa stahiki zao zote jinsi zinavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, Serikali inaendelea kuchukua sheria kali; sheria ambazo nimezieleza katika jibu langu la msingi; Sheria ya Mtoto, Sura Namba 13, ni adhabu kali ya faini isiyozidi shilingi milioni tano. Pia, kuna kifungo cha miezi sita na mengineyo ambayo jinsi matokeo ya udhalilishaji yanavyotokea basi adhabu hizo zinaweza zikatolewa kwa pamoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Wanawake hawa wanaowatupa watoto hawawatupi kwa sababu wanapenda. Kunakuwa kuna visababishi vingi vinavyosababisha wafikie hatua hiyo. Kwanza, kuanzia utungwaji wa mimba...

**SPIKA:** Mheshimiwa Paresso, uliza swali.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, sijui ninaulizaje. Je, Serikali haifikirii kwamba iko haja ya kuanzisha vituo vya utoaji wa nasaha kwa wanawake hawa kuliko tu kutumia sheria?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina madawati 420 katika vituo vya polisi na katika jamii zetu nchini. Tunawaomba wananchi wanapofikwa na tatizo hilo basi moja kwa moja waende katika ofisi ya ustawi wa jamii wamwone afisa ustawi ili kumwelekeza na kumpa taratibu zote za malezi na makuzi kwa ajili ya Watoto.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inawapenda sana na inawajali watoto na ndiyo maana

ameweka vitu vingi kwa ajili ya watoto ili waendelee hadi wanapofika umri wa miaka 18 kuweza kujitegeme. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 166

**Kupima Ardhi ya Vijiji vyote Tanzania Bara**

**MHE. FATMA HASSAN TOUFIQ** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha upimaji wa ardhi unafanyika katika Vijiji vyote Tanzania Bara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika ardhi za vijiji, jumla ya vijiji 10,987 kati ya vijiji 12,333 vilivyosajiliwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI vimepimwa mipaka yake. Vijiji vilivyoandaliwa Mipango ya matumizi bora ya ardhi ni 4,346 sawa na 35.24% ya vijiji 12,333. Uandaaji wa mipango hiyo umewezesha kutambua vipande vya ardhi 259,080 na kutolewa hatimiliki za kimila.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutenga fedha kupitia bajeti ya Serikali ambapo kila mwaka Serikali hutenga fedha kwa ajili ya kazi hiyo. Ni matarajio ya Serikali kukamilisha zoezi hili kutegemea upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili. Swali la kwanza; nini kauli ya Serikali kwa vijiji vilivyosajiliwa, lakini bado kuna migogoro ya mipaka?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali ina mkakati gani wa kuharakisha mipango ya matumizi bora ya ardhi ili walau ifikie 60%? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum na nitayajibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, anataka kujua kauli ya Serikali kwa vijiji vilivyosajiliwa, lakini bado kuna migogoro ya ardhi. Kimsingi tumeendelea na juhudi mbalimbali za kutatua migogoro ya ardhi hapa nchini, juhudi ambazo kimsingi ninadhani Waheshimiwa Wabunge wanakiri kwamba sasa tunakwenda kwa mwendo ambao ni mzuri zaidi. Kauli ya Serikali ni kuendelea kutatua migogoro hii ambayo kimsingi wakati mwingine haianzishwi na ile mipaka ila ni utashi tu wa kibinadamu ambao wananchi wanaweza wakawa wametofautiana katika uelewa wao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili; mkakati wa Serikali katika kupandisha viwango vya kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi kutoka hiyo 35% angalau ifike 60%. Kwa kweli tunaishukuru sana Serikali ya Mama Samia na hapa ninapoongea hivi karibuni tumepewa karibu shilingi bilioni tano ziko kazini, vijana wako kazini wanaendelea kupitia vijiji mbalimbali kuviwekea mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yetu kwamba, upatikanaji wa fedha kadri utakavyowezeshwa na Serikali, Wizara itaendelea kuweka mipango mizuri ya matumizi katika maeneo ya vijiji vyetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na Serikali kuweza kutoa majibu kwenu. Nitaleta matangazo yaliyoko hapa mbele kwanza tutaanza na wageni.

Tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika:-

Wapo wageni 24 wa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko ambaye ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati; hawa ni Viongozi Wakuu, Watendaji na Maafisa kutoka Wizara hiyo. *(Makofi)*

Wapo Mhandisi Felchesmi Jossen Mramba ambaye ni Katibu Mkuu; Dkt. James Mataragio, Naibu Katibu Mkuu Petroli na Gesi; Dkt. Khatib Kazungu, Naibu Katibu Mkuu Umeme na Nishati Jadidifu; Mhandisi Innocent Luoga, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu; Ndugu Goodluck Shirima, Kamishna wa Petroli na Gesi; na Dkt. Rhimo Nyansaho, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)*. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Balozi Ombeni Sefue, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC);* Mheshimiwa Balozi Meja Jenerali Mstaafu Jacob Kingu, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini; Ndugu Victoria Elangwa, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA);* Ndugu Halfani Halfani, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli *(PURA);* na Dkt. Lutengano Mwakahesya, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Uagizaji wa Pamoja wa Petroli. *(Makofi)*

Tunao pia Profesa Shubi Kaijage, Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya kuendeleza Joto Ardhi Tanzania; Mhandisi Abubakari Issa, Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme; Ndugu Jema Msuya, Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Nguzo za Zege Tanzania; na Mhandisi David Ngula, Mwenyekiti wa Bodi ya

Baraza la Ushauri la Watumia Huduma za Nishati na Maji chini ya Udhibiti *(EWURA)*. *(Makofi)*

Wapo Ndugu George Nchwali, Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Mafuta Tanzania *(TANOIL);* Ndugu Julius Mkoji, Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Gesi Tanzania *(GASCO*); na Mhandisi Ngosi Mwihava ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)*. *(Makofi)*

Tunaye Dkt. James Andilile, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za… *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hata sijamaliza kusoma, haya ahsante. *(Makofi/Vigelegele)*

Haya ahsanteni sana. Sasa nilikuwa sijamaliza kusoma bado. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa sijamaliza kusoma. Huyu ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)*. *(Makofi)*

Wapo pia Ndugu Musa Makame, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC);* Mhandisi Hassan Said, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini *(REA);* Mhandisi Charles Sangweni, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli *(PURA);* Ndugu Erasto Simon, Mtendaji Mkuu Wakala wa Uagizaji wa Pamoja wa Petroli; Ndugu Renata Ndege, Kaimu Mkurugenzi Mkuu Shirika la Umeme *(TANESCO);* Mhandisi Mathew Mwangomba, Meneja Mkuu Kampuni ya Kuendeleza Joto Ardhi Tanzania; na Ndugu Sadock Mugendi, Meneja Mkuu Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme. *(Makofi)*

Wengine ni Mhandisi Yusuph Kitivo, Meneja Mkuu Kampuni ya Nguzo za Zege Tanzania; Mhandisi Baltazar Mrosso, Meneja Mkuu Kampuni ya Gesi Tanzania; Ndugu James Sanawa, Meneja Mkuu Kampuni ya Mafuta Tanzania; Ndugu Stella Lupimo, Katibu

Mtendaji Baraza la Ushauri la Watumia Huduma za Nishati na Maji chini ya Udhibiti wa *EWURA CCC;* na Ndugu Michael Lushinge, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, Mkoa wa Mwanza. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wawili wa Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI na hawa ni Ndugu Shamsa Salum ambaye ni mama yake mdogo na Meja Nabeel Khatib ambaye mtoto wake. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Halima James Mdee ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam, Wakili Edson Kilatu na Ndugu Peter Magwi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi ambaye ni Ndugu Delphine Kaiza, Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi Mahesabu wa Ofisi ya Mashtaka Taifa kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 13 wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Lubala Mabula ambao ni wafanyakazi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Tauhida Gallos Nyimbo ambao ni wasafirishaji watalii kutoka Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ambao ni ndugu zake wakiongozwa na mama yake mdogo kutoka Bunda mkoani Mara. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Rose Vicent Busiga ambaye ni Ndugu Kennedy John, mwanafunzi kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo:-

Tunao viongozi 80 wa Serikali ya Wanafunzi kutoka Taasisi ya Uhasibu Tanzania *(TIA)* Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 114 na walimu saba kutoka Shule ya Msingi Petro Marcelino kutoka Kihonda Morogoro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Walimu 27 kutoka Wilaya ya Chamwino Mkoani Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na tangazo hilo la wageni kuna tangazo hapa ambalo linatoka kwa Mheshimiwa Cosato David Chumi ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pia ni Kapteni wa *Bunge Football Club* anatutangazia kwamba; kulikuwa na mechi ya kirafiki kati ya *Bunge FC* na *Kunduchi Veterans*, Bunge ilishinda kwa mabao mawili na kunduchi walipata goli moja. Kwa hiyo, wafungaji wa magoli walikuwa ni Mheshimiwa Festo Sanga Mbunge wa Makete na Ndugu Shadrack ambaye ni Mtumishi wa Bunge. Mechi ilichezwa Jumamosi, tunawapongeza sana ndugu zetu wa *Bunge Football Club. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii pia kuwapongeza *Simba Sport Club* kwa kufikia hatua ya fainali na tunawatakia kila la heri, sasa warejeshe kombe hapa nyumbani; tunawatakia kila la heri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaendelea na ratiba yetu. Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko ambaye ndiye mwenye hoja, Waziri wa Nishati pia Naibu Waziri Mkuu aje awasilishe hoja ya Wizara yake. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti mwaka wa fedha2024/2025 kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Nishati na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuendelea kuwajalia afya njema Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Viongozi wengine na hivyo kutuwezesha kuendelea kuwatumikia Watanzania. Kipekee nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunijalia afya na kuniwezesha kusimama leo mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, 27 Novemba, 2024 Taifa letu lilimpoteza Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika na Mbunge wa Jimbo la Kigamboni. Aidha, tarehe 13 Aprili, 2025, Taifa lilimpoteza aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* Mhandisi Boniface Gissima Nyamo-Hanga. Kwa masikitiko makubwa ninaungana na Wabunge wenzangu kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, familia za marehemu, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na viongozi hawa. Sisi tuliwapenda, lakini Mungu aliwapenda zaidi. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi kwa kufanikisha Mkutano Mkuu Maalum wa CCM

uliofanyika Jijini Dodoma tarehe 18 na 19 Januari, 2025. Katika Mkutano huo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipitishwa kwa kishindo na Wajumbe na kuwa mgombea wa nafasi ya Urais kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Mheshimiwa Hussein Ali Mwinyi kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi katika uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ninampongeza Komredi Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuteuliwa na kuthibitishwa na Wajumbe kuwa Mgombea mwenza wa nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninampongeza Mheshimiwa Stephen Masato Wasira kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie pia fursa hii kumshukuru vilevile Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo na miongozo wanayonipatia katika kutekeleza majukumu yangu ikiwa ni pamoja na usimamizi wa Sekta ya Nishati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu samahani. Waheshimiwa Wabunge wale ambao wana mijadala ya lazima kabisa milango iko mingi sana ya kutokea huku pembeni. Tunahitaji utulivu wakati tukisikiliza Hotuba ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nikiri kuwa maelekezo na miongozo ya Viongozi wetu Wakuu hawa ni chachu na msingi wa mafanikio ya utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza

Bunge letu Tukufu kwa weledi na umahiri mkubwa. Ni wazi kuwa, chini ya uongozi wenu, Bunge letu limeendelea kuwa mahiri zaidi katika kuisimamia na kuishauri Serikali kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali ili kuboresha maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee ninampongeza Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, pamoja na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa ushauri na maoni yao na kuendelea kuisimamia vyema Sekta ya Nishati kwa manufaa ya uchumi wa nchi yetu na uendelevu wa watu wetu. Ninapenda kuahidi kuwa Wizara ya Nishati itaendelea kuzingatia ushauri wa Kamati wakati wa utekelezaji wa majukumu yake katika mwaka unaokuja 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwapongeza Mawaziri wote walioaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kusimamia Wizara mbalimbali na ninawashukuru kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Naibu Waziri wa Nishati kwa uchapakazi wake mahiri usio na kifani na ushirikiano mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, ninamshukuru Mhandisi Felchesmi Mramba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati kwa utendaji wake mahiri katika kutekeleza majukumu ya kila siku ya Wizara. Vilevile, nimshukuru sana Dkt. James Peter Mataragio, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya petroli pamoja na Dkt. Khatibu Malimi Kazungu, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya umeme na nishati jadidifu kwa utumishi wao makini katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu hii ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana pia Wakuu wa Vitengo, Idara, Taasisi, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi zote za

Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati na Watumishi wote wa Wizara kwa ujumla kwa ushirikiano na juhudi zao za kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda nitumie fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Bukombe kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo ya Jimbo letu. Kutokana na majukumu mengi niliyonayo ya kuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kuna wakati wananikosa jimboni, lakini kwa wema na upendo wao wanaendelea kunivumilia na kunipa ushirikiano mkubwa wakati wote. Ninaomba niwaahidi kuwa nitaendelea kuwa mtumishi wao mwaminifu na anayejituma katika kutekeleza majukumu yote jimboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee, ninaomba nimshukuru sana mke wangu mpenzi Benadetha Clement Mathayo kwa maombi na upendo wake wa dhati kwangu pamoja na watoto wetu. Amekuwa mvumilivu katika kipindi chote ninapokuwa ninatekeleza majukumu yangu ya Ubunge, pamoja na majukumu mengine niliyonayo, yeye amebeba jukumu la kuendelea kuisimamia familia yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatambua umuhimu wa vyombo vya habari katika kuhabarisha na kuelimisha umma wa Watanzania kuhusu maendeleo ya Sekta ya Nishati. Ninaomba nivishukuru sana na kuvipongeza sana vyombo vyote vya habari nchini, vikiwemo redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa Wizara ya Nishati na waliotupa kwa mwaka unaomalizika wa 2024/2025. Ni matumaini yangu kuwa, ushirikiano huu utazidi kuimarika katika mwaka 2025/2026 kwa manufaa ya Taifa letu na wananchi wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya hotuba ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha

taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika mwaka wa fedha 2024/2025 uliongozwa na vipaumbele mbalimbali vilivyowekwa, ikiwa ni pamoja na kuendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji, usafirishaji, usambazaji wa umeme, kupeleka nishati vijijini, kutekeleza miradi ya kielelezo na mikakati ya mafuta na gesi asilia ikiwemo mradi wa kuchakata ya kusindika gesi asilia kuwa kimiminika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi pia wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima - Uganda hadi Tanga – Tanzania, na kutekeleza shughuli za utafiti na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati vya Songo Songo Magharibi, Mnazi *Bay* Kaskazini, Eyasi – Wembere pamoja na kusambaza gesi asilia viwandani, katika taasisi na majumbani na kuimarisha matumizi ya *CNG* katika magari.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vingine vilivyowekwa katika mwaka 2024/2025 ni kuendelea na kuimarisha upatikanaji na matumizi ya nishati safi ya kupikia *(clean cooking energy)* nchini, kuhakikisha nchi inakuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta na petroli na ufanisi katika kushughulikia upatikanaji wa bidhaa hizo. Kuendelea kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa Taasisi/ Mashirika yaliyo chini ya Wizara ambayo ni *TANESCO*, *TPDC, EWURA, PURA, REA, PBPA*. Pamoja na kampuni tanzu ili yaimarishe tija, ufanisi, uwajibikaji na ubora katika uendeshaji na utoaji wa huduma kwa wananchi na kuendelea kuimarisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia pamoja na rasilimali watu ya Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, sehemu (b) ya hotuba yangu ukurasa wa saba hadi wa 124 inaeleza kwa kina kuhusu hatua iliyofikia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara mwaka wa fedha 2024/2025. Mafanikio yaliyopatikana katika maeneo ya uzalishaji, usafirishaji, usambazaji wa umeme, upelekaji wa umeme wa vijijini kuwezesha wananchi kutumia nishati safi ya kupikia pamoja na shughuli za

utafutaji, uendelezaji na usambazaji wa matumizi ya mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Nishati iliidhinishiwa na kutumia jumla ya shilingi trilioni moja, bilioni mia nane themanini na tatu, milioni mia saba hamsini na tisa, mia nne hamsini na tano elfu. Ambapo shilingi trilioni moja, bilioni mia saba tisini na nne, milioni mia nne sitini na sita, mia nane thelathini na mbili elfu ambazo ni sawa na 95.3% ya bajeti yote ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Shilingi bilioni themanini na nne, milioni mia nane tisini na mbili, mia sita ishirini na tatu elfu ni sawa na asilimia 4.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, hadi mwisho wa mwezi Machi, 2025. Wizara ilipokea jumla ya shilingi trilioni moja na milioni mia tatu na mbili, mia sita ishirini na nne elfu na sitini na tisa ambapo shilingi bilioni kumi na nane, milioni mia mbili kumi na nne, mia nne sabini na tatu elfu, mia moja na tisini ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni mia tisa themanini na mbili na milioni themanini na saba, mia saba na hamsini elfu, mia nane na sabini na tisa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nieleze kidogo kwenye sekta ndogo ya umeme na nishati jadidifu. Kutokana na jitihada zilizotekelezwa na Serikali katika kuimarisha uzalishaji wa umeme nchini kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali, nchi yetu imeendelea kushuhudia ongezeko kubwa la uzalishaji wa umeme. Ninaomba kutumia fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika kipindi cha mwaka mmoja, uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa gridi ya Taifa umeongezeka na kufikia *MW* 4,031.71 Aprili 2025, sawa na ongezeko la 86.6% ikilinganishwa na Megawati 2,138 zilizokuwepo Machi, 2024.

Aidha, kutokana na Serikali ya Awamu ya Sita kuendelea kuweka kipaumbele na msukumo madhubuti katika kuhakikisha Tanzania inakuwa na umeme wa kutosha na uhakika, kumekuwepo vilevile na ongezeko la uzalishaji wa umeme katika mfumo wa Gridi ya Taifa. Mwaka 2020/2021 uwezo wa mitambo

ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa ulikuwa MW 1,601.84, kwa sasa uwezo wa mitambo uliopo umefika MW 4,031.71, sawa na ongezeko la 151.7% kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 2. katika hotuba yangu ukurasa wa 13.

Mheshimiwa Spika, kufikia mwezi Aprili, 2025, mitambo ya kuzalisha umeme ambayo haijaungwa katika Gridi ya Taifa ina jumla ya MW 328.17 ambayo inajumuisha mitambo inayomilikiwa na *TANESCO* yenye uwezo wa kuzalisha MW 20.19 na MW 307.98 inayozalishwa katika kampuni binafsi kwa ajili ya matumizi ya kampuni hizo na inayoonekana katika Kiambatisho Na.2. kwenye Hotuba yangu ukurasa wa 182.

Mheshimiwa Spika, ni vema kutambua pia kuwa kutokana na jitihada hizi, nchi yetu imeweza kwa sasa kuondokana na mgao wa umeme uliokuwa ni changamoto kubwa kwa kipindi cha miaka mingi na kuwa na ziada ya umeme kwa ajili ya kuwahudumia Watanzania. Aidha, kupatikana kwa umeme wa uhakika kumewezesha kupunguza gharama za uzalishaji na kufanya biashara nchini ziweze kuwa rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuzimwa kwa mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta ya uendeshaji wake ambao ulikuwa ni gharama kubwa na kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika vijijini na uendeshaji wa treni ya kisasa ya *SGR* katika Mikoa ambayo ilikuwa haijaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa. Aidha, upatikanaji wa umeme huu umekuwa uhakika, umechangia kukua kwa Pato la Taifa na kukabiliana na mfumuko wa bei kutokana na athari chanya za upatikanaji wa umeme huo katika shughuli za kiuchumi na upatikanaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hilo limetokana na kukamilika kwa miradi mbalimbali ya kuzalisha umeme katika kipindi husika, hususan mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Julius Nyerere ambao hadi mwezi Aprili, 2025 mitambo yote tisa imekamilika. Aidha, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kukarabati mitambo mbalimbali ya kuzalisha umeme ambayo imechangia pia kuimarisha uzalishaji wa umeme na upatikanaji wake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na jitihada kubwa za makusudi zinazotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita, hususan kukuza uchumi wa nchi kunakoambatana na mahitaji ya umeme, kuimarika kwa huduma za kijamii unaohitaji uendeshaji wa umeme, kukua kwa sekta ya usafirishaji hasa uwepo wa treni ya *SGR,* ongezeko la matumizi ya nishati safi ya kupikia; na kuimarika kwa uunganishaji wa umeme vijijini kumekuwepo na ongezeko kubwa la mahitaji ya umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya umeme nchini katika Gridi ya Taifa yameongezeka hadi kufikia MW 1,921.44 zilizofikiwa tarehe 9 Aprili, 2025 Saa Tatu Usiku ikilinganishwa na MW 1,590.10 zilizofikiwa tarehe 26 Machi, 2024, saa tatu usiku hili ni ongezeko sawa na 20.84%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana katika uzalishaji wa umeme ni pamoja na Ujenzi wa Mitambo ya Kuzalisha Umeme wa Kinyerezi *Extension* wa MW 185 ambao umefikia 98.4% ambapo mitambo yote minne kwa sasa inafua umeme wa kiasi cha MW 40 kila mmoja, hivyo kuwezesha kiasi cha umeme *MW* 160 kuingizwa kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Kutumia Maji wa Rusumo wa MW 80 unaotekelezwa kwa ushirikiano wa nchi tatu Tanzania, Burundi na Rwanda kwa mgawanyo wa sawa wa umeme umekamilika na hivyo kuiwezesha Tanzania kupata jumla ya MW 26.67 za umeme. Kukamilika kwa mradi huu kumeboresha upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na kuunganishwa kwa gridi yetu ya Tanzania na nchi jirani za Burundi na Rwanda hivyo kutoa fursa ya kuziuzia nchi hizo umeme endapo watahitaji.

Mheshimiwa Spika, Tatu, Utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Jua Mkoani Shinyanga wa MW 150 inayohusisha uzalishaji wa MW 50 umefikia 51%. Aidha, mkataba wa ufadhili kati ya Serikali ya Tanzania na Shirika la Maendeleo la Ufaransa *(AFD)* kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya pili ya MW 100 ulisainiwa tarehe 6 Desemba, 2024 na unatarajia

kuanza utekelezaji wake Julai, 2025 baada ya kukamilika kwa taratibu za zabuni ya kumpata mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea vilevile kutekeleza miradi mingine ya kuzalisha umeme ikiwa ni pamoja na Malagarasi MW 49.5, Ruhudji MW 358, Rumakali MW 228, Kakono MW 87.8 ambapo utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali. Aidha, miradi ya kuzalisha umeme wa kutumia joto ardhi ikiwa ni pamoja na Mradi wa Ngozi wa MW 70, Kiejo – Mbaka MW 60, Natron MW 60 iliendelea kutekelezwa lengo ni kuhakikishia nchi yetu inakuwa na vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nieleze kidogo kuhusu usafirishaji na usambazaji wa umeme. Kuzalisha umeme ni jambo moja lakini ili umeme huo uweze kufikia walaji na kutumika hauna budi kusafirishwa na kusambaza, Serikali imeendelea na upanuzi wa miundombinu wa kusafirisha umeme, ambayo imefikia jumla ya urefu wa kilometa 8,140 ikiwa ni ongezeko la asilimia tano ikilinganishwa na kilometa 7,745 ya mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, miundombinu ya usambazaji umeme imeongezeka kutoka kilometa 176,750.9 mwezi Aprili, 2024 hadi kufika kilometa 200,266.25 mwezi Aprili, 2025 sawa na ongezeko la 13.3%.

Mheshimiwa Spika, hatua hiyo iliyofikiwa katika miradi mbalimbali ya kusafirisha umeme ni pamoja na:-

(i) Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 160 kutoka Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Julius Nyerere hadi Chalinze Mkoani Pwani umekamilika kwa 99.8% na ujenzi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Chalinze umekamilika kwa 97.6%. Aidha, kwa sasa mradi huu upo katika hatua za uangalizi na miundombinu hiyo inaendelea kutumika kuingiza umeme unaozalishwa katika Bwawa la Julius Nyerere kwenye Gridi ya Taifa.

(ii) Mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 wenye urefu wa kilomita 414 kutoka Singida

hadi Namanga kupitia Babati na Arusha umekamilika na hivyo kutuwezesha kuunganisha Gridi ya Tanzania na Kenya na hivyo kutufanya tuwe na nafasi nzuri ya kufanya biashara na nchi jirani. Kukamilika kwa mradi huu una manufaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwezesha kufanyika kwa biashara ya umeme baina ya nchi ya Tanzania na nchi za Afrika Mashariki kupitia *East African Power Pool (EAPP)*.

(iii) Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya – Tunduma, mradi unaoitwa *TAZA* umefika 38% na unatarajia kukamilika itakapofika Mei, 2026. Kukamilika kwa mradi huu kutaimarisha upatikanaji wa umeme katika mikoa ya nyanda za juu kusini pamoja na kuunganisha Gridi ya Taifa na nchi za kusini mwa Afrika na hivyo kuwezesha kufanyika kwa biashara baina ya nchi yetu na nchi za ukanda huo chini ya mpango *Southern African Power Pool (SAPP)*.

(iv) Kukamilika kwa ujenzi wa njia kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma ambao umefanikisha kuunganisha Mkoa wa Kigoma katika Gridi ya Taifa na kuwezesha kuzimwa kwa mitambo ya umeme wa mafuta. Aidha, *TANESCO* itaokoa kiasi cha shilingi bilioni 58.4 zilizokuwa zinatumika kwa mwaka kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya *diesel* kwa ajili Mkoa husika.

(v) Kukamilisha kwa ujenzi wa kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 115 kutoka Tabora – Urambo na kuwezesha kuimarisha upatikanaji wa umeme katika Wilaya ya Urambo. Aidha, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 383 kutoka Tabora hadi Katavi kupitia Sikonge – Ipole – Inyonga umefikia 96%, unatarajia kukamilika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mingine ya kusafirisha na kusambaza umeme kama ilivyoelezwa kwa kina kwenye hotuba yangu ukurasa wa 26 hadi 40 ikiwa ni pamoja na mradi wa kuimarisha gridi ya Taifa na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa Msongo wa kilovoti 220 kutoka Benaco hadi Kyaka. Aidha, kutokana na jitihada hizo za kusafirisha na kusambaza umeme zilizotekelezwa na Serikali wateja waliounganishwa na umeme nchini wameongezeka pia kutoka milioni mbili laki saba sitini na sita mia saba na arobaini na tano mwaka 2021 hadi kufika milioni tano laki nne na arobaini tisa mia mbili na sabini na nane mwezi Aprili, 2025 hili ni ongezeko la 97%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa nishati vijijini; Mwaka wa Fedha. 2024/2025, Serikali iliendelea kutekeleza azma yake ya kuhakikisha kuwa huduma ya umeme inafika vijijini kote Tanzania Bara. Napenda kutumia fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imeweza kuvifikia vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara kupitia miradi mbalimbali ya umeme iliyotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)*. Aidha, kupitia utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini jumla ya taasisi na maeneo ya huduma 66,140 yameunganishwa na umeme kutoka taasisi kumi na tano elfu, mia mbili mwaka 2020. Hili ni sawa na ongezeko la 315%.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukamilisha kwa kazi ya uunganishaji umeme vijijini, Serikali imeendelea kupeleka umeme kwenye vitongoji, ambapo jumla ya vitongoji 33,657 kati ya vitongoji 64,359 vya Tanzania Bara sawa na 52% tayari vimeunganiswa na umeme. Aidha mengine ya nishati vijijini yaliyotekelezwa ni pamoja na miradi ya ujazilizi, mradi wa kusambaza umeme katika vijiji miji, mradi wa kupeleka umeme kwenye maeneo ya migodi midogo, viwanda vidogo na maeneo ya kilimo na miradi ya kupeleka umeme katika minara ya mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Spika, aidha, ili kuboresha upatikanaji wa huduma ya nishati ya mafuta vijijini. Serikali iliendelea kutekeleza mradi wa kuwezesha ujenzi wa vituo vidogo vidogo vya kusambaza bidhaa za petrol vijijini, ambapo kiwango cha juu cha

mkopo kinachoweza kutolewa kwa kila mwendelezaji ni milioni mia moja thelathini na mbili na laki sita, ambacho kinatakiwa kurejeshwa ndani ya miaka saba kwa riba ya asilimia tano.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka Serikali iliandaa na kushiriki Mkutano Mkuu wa Nchi za Afrika wa Nishati *(African Heads of States Energy Summit*) uliofanyika tarehe 27-28 Januari, 2025 Jijini Dar es Salaam. Pamoja na mambo mengine kupitia mkutano huo Mpango wa Kitaifa wa Nishati Tanzania *(*Tanzania *National Energy Compacts)* ulizinduliwa ambapo unaendelea kuongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme nchini hadi kufikia 100% itakapofika mwaka 2030, kutoka kiwango cha sasa cha 78.4%.

Mheshimiwa Spika, kuongeza kasi ya kuunganisha umeme nchini hadi kufika 75%. Katika kipindi hicho kutoka 46% za sasa. Kuongeza kiwango cha matumizi ya nishati safi ya kupikia kutoka asilimia 6.9 ya mwaka 2021 hadi kufika 75% itakapofika mwaka 2030, kuongeza mchango wa sekta binafsi katika sekta ya nishati kwa kiasi cha dola za kimarekani bilioni 4.5 sawa na taribani trilioni 11.7 ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huo wa Wakuu wa Nchi walisaini azimio la utekelezaji wa mpango huo *(The Dar es Salaam Declaration by the African Heads of States Energy Summit*). Ikiwa ni makubaliano ya pamoja ya wakuu hao ya kuunganisha nguvu za jitihada za pamoja za kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha zitakazoweza kusaidia huduma ya umeme wa uhakika kwenye Bara la Afrika, uendelevu wa gharama nafuu kwa watu milioni 300 katika Bara la Afrika itakapofika mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kupitia Bunge lako Tukufu, kumpongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwa Mwenyeji wa Mkutano wa Nishati Afrika *(Mission 300*) kwa Mwaka 2025. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na taasisi zilizo chini yake inakamilisha uandaaji wa Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Mpango kazi huo wa Taifa ambao utekelezaji wake utaanza Mwaka wa Fedha 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nieleze kidogo kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia. Serikali chini ya uratibu wa Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka 2024 – 2034 uliozinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 8 Mei, 2024. Lengo la mkakati huo ni kuhakikisha kuwa 80% ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Mheshimiwa Spika, manufaa ya utekelezaji wa mkakati huu ni pamoja na kuwaepusha Watanzania ama wananchi na athari za kiafya zitokanazo na matumizi ya nishati zisizokuwa safi za kupikia na kukabiliana na uharibufu wa mazingira unaotokana na matumizi ya nishati zisizokuwa safi za kupikia.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau inaendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa nishati safi ya kupikia pamoja na kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya nishati ya kupikia katika taasisi za umma na binafsi zinazohudumia zaidi ya watu 100 kwa siku, ikiwemo Jeshi la Magereza, Jeshi la Kujenga Taifa na Shule za Sekondari. Aidha, zoezi la kusambaza mitungi 452,445 ya gesi ya kupikia *LPG* kwa bei ya punguzo la hadi hadi asilimia 50 linaendelea. Kupitia programu hii jumla ya mitungi 154,224 imesambazwa hadi kufika Aprili, 2025.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa ili kuimarisha matumizi Nishati Safi ya kupikia nchini ni kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa kusambaza majiko banifu 200,000 yaliyotengenezwa kwa teknolojia yenye ubunifu na kupunguza matumizi ya kuni na mkaa, hivyo kuwezesha kupunguza uharibifu wa mazingira katika maeneo ya vijijini. Hadi Aprili 2025, Wakala wa Nishati Vijijni *(REA)* imeshapata kampuni sita za kusambaza majiko banifu 192,038 katika maeneo ya vijijini na vijiji - miji kwenye Mikoa 23 kwa bei ya ruzuku ya hadi 75%. Aidha, *REA* katika hatua za mwisho za kuwapata watoa huduma watakaosambaza majiko hayo katika Mikoa miwili iliyobaki ya Njombe na Katavi inaendelea.

Mheshimiwa Spika, nieleze kidogo sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia. Mwaka 2024/2025 Serikali kupitia Wizara ya Nishati iliendelea kusimamia na kuendeleza sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia katika maeneo ya utafutaji, uendelezaji, uzalishaji, uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa bidhaa za mafuta na gesi kwa lengo la kuhakikisha kuwa mchango wa sekta hii kwenye pato la Taifa unaendelea kuimarika, ambapo utekeleza ulikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Shughuli za utafutaji na uendelezaji wa mafuta ya gesi asilia ziliendelea katika vitalu vya Mnazi *Bay* Kaskazini, Eyasi – Wembere, Songo Songo Magharibi, Vitalu Na. 4/1B na 4/1C, Mnazi *Bay* na Ruvuma katika eneo la Ntorya kama ilivyofafanuliwa katika hotuba yangu ukurasa wa 70-75 kuhusu kazi zilizotekelezwa.

(ii) Majadiliano baina ya Serikali na wawekezaji kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Kuchakata Gesi Asilia ya *LNG* yaliendelea kwa kuzingatia maoni yaliyotolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wadau wengine katika mitakaba ya awali, ambapo kwa sasa yapo katika hatua za mwisho.

(iii) Mradi wa Bomba la kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania *(East African Crude Oil Pipeline* (*EACOP))* uliendelea kutekelezwa, ambapo umefikia 55%. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilisha na kuanza kazi za karakana za kuweka mfumo wa joto kwenye mabomba kwa kuwasili nchini kwa mabomba yenye uwezo wa kujenga kilometa 900, kuweka mfumo wa kuhifadhi joto katika ma888888bomba yenye urefu wa kilometa 443.7, kupelekwa kwenye maeneo ya mradi mabomba yenye mfumo wa kuhifadhi joto yenye uwezo wa kujenga kilomita 364.3, kuendelea kwa ujenzi wa matanki manne katika Eneo la Chongoleani, ambao umefikia 74.2% na ujenzi wa *jet* ya kupakia mafuta ambao umefika 69.1%.

(iv) Serikali kwa kishirikiana na sekta binafsi iliendelea kuchukua hatua za kuimarisha upatikanaji wa gesi asilia, *CNG,* nchini kwa matumizi ya vyombo vya moto. Aidha, ujenzi wa Kituo

Mama cha *CNG (CNG Mother Station)* katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam umekamilika. Kukamilika kwa vituo vidogo vya *CNG (CNG Receiving and Storage Station)* vimejengwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Kiwanda cha Dawa cha Kairuki kilichopo Eneo la Viwanda vya Zegereni, Kibaha Pwani, uliendelea. Vilevile, usanifu wa kina wa kihandisi, kwa ajili ya kuunganisha gesi asilia katika migahawa 12 katika eneo la Mlimani *City* pamoja na maabara na migahawa mitatu katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam *(DUCE)* umekamilika.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2025, jumla ya vituo tisa vya *CNG* vimekamilika na vinatoa huduma ikilinganishwa na vituo viwili huko tulipotoka na mwelekeo wa Serikali ni kuwa na angalau vituo 20 ifikapo Juni, 2026. Aidha, Serikali imeendelea kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika utoaji wa huduma ya *CNG,* ambapo kampuni 69 zimekwisharuhusiwa kufanya biashara ya *CNG* hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TPDC* vilevile imeendelea na utaratibu wa kununua vituo sita vya *CNG* vinavohamishika *(Mobile CNG Filing Stations)* ambapo, vituo vitatu vitakuwa katika Jiji la Dar es Salaam, kimoja Morogoro na viwili vitakuwa Dodoma. Hatua hii itaimarisha upatikanaji wa *CNG,* kwa ajili ya vyombo vya moto nchini na kuchochea matumizi ya nishati hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuimarika kwa matumizi ya *CNG* nchini katika vyombo vya moto, hususan magari na bajaji, umekuwa na manufaa makubwa ikiwemo kuwapatia wananchi unafuu wa gharama za uendeshaji wa vyombo hivyo pamoja na kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni katika uagizaji wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, miradi mbalimbali ya ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha gesi asilia iliendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na usambazaji wa gesi asilia katika Mikoa ya Dar es Salam, Pwani, Lindi na Mtwara. Ujenzi wa bomba la gesi asilia kuanzia Kinyerezi Dar es Salaam hadi Chalinze, Pwani, Mradi wa Bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Tanzania hadi Uganda na Mradi wa kusafirisha gesi asilia kutoka Dar es Salaam hadi Mombasa Kenya.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Nishati iliratibu vilevile na kushiriki katika Kongamano la 11 la Petroli la Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2025 lililofanyika tarehe 5–7 Machi, 2025. Kongamano hilo lilihudhuriwa na washiriki zaidi ya 1,000 kutoka nchi mbalimbali duniani, ambapo nchi yetu iliweza kutangaza fursa ya uwekezaji katika mnyororo wa thamani ya mafuta na gesi asilia ikiwemo *CNG* na kutangaza nia ya Serikali ya kunadi vitalu 26 vya kutafuta mafuta na gesi asilia kupitia duru ya tano.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja *(Bulk Procurement System)* unaendelea kutumika katika uagizaji wa bidhaa ya mafuta ya petroli nchini na hivyo kuwezesha nchi yetu kuendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta. Aidha, taarifa za kina za mwenendo wa bei za mafuta na petroli katika Soko la Dunia na la Ndani kama inavyoonekana katika ukurasa wa 101 na 104 wa hotuba yangu zimefafanuliwa vizuri. Mwenendo wa uagizaji wa mafuta na upatikanaji wa bidhaa hizo ni kama inavyoonekana katika ukurasa wa 107 hadi 109 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa udhibiti wa Sekta ya Nishati kupitia *PURA* na *EWURA*. Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli *(PURA)* pamoja na Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)* iliendelea kutekeleza kazi mbalimbali za usimamizi na udhibiti wa Sekta ya Nishati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja; Serikali kupitia *PURA* iliendelea na maandalizi ya duru ya tano ya kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia, ambapo maandalizi ya nyaraka zinazotumika katika kunadi vitalu ikiwemo mikataba ya kifani ya ugawaji wa mapato *(PSA 2025)* yaliendelea. Aidha, *PURA* ilikamilisha uwekaji wa mikataba katika vitalu 26 vilivyopendekezwa kuingia kwenye mnada na kuandaa vifurushi vya dhati *(data package)* na taarifa za kitaalam kwa vitalu hivyo umekamilika na nyaraka za zabuni zitakazotumika wakati wa kunadi vitalu husika.

Mheshimiwa Spika, mbili; *PURA* iliendelea kudhibiti shughuli mbalimbali za Mkondo wa Juu wa Petroli ikiwa ni pamoja na kusimamia shughuli za uzalishaji wa gesi asilia kwa vitalu vya Songosongo na Mnazi *Bay* na kukamilika kwa maandalizi na rasimu ya uwajibikaji wa kampuni kwa jamii katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia ambayo ipo katika hatua za mwisho za uidhinishwaji. Kanuni hizo pamoja na mambo mengine zitawezesha utekelezaji wa *CSR* wenye tija katika maeneo ya Mkondo wa Juu wa Petroli Nchini.

Mheshimiwa Spika, tatu; *EWURA* iliendelea kusimamia shughuli za udhibiti wa mkondo wa juu kati na chini wa gesi asilia ambapo ulitoa vibali 10 vya ujenzi wa Vituo vya *CNG* katika Mkoa wa Dar es Salaam, Pwani na Morogoro. Kutoa leseni tano za uendeshaji wa Vituo vya *CNG*; vibali nane kwa jili ya ujenzi wa mabomba ya kupeleka gesi asilia kwenye Vituo vya *CNG* na vibali sita vya ujenzi wa mabomba ya kupeleka gesi asilia kwenye viwanda, taasisi, migahawa ya chakula na majumbani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko la ujenzi wa Vituo vya *CNG* na unafuu wa gharama unaopatikana wa matumizi ya *CNG* kama nishati mbadala ya mafuta katika vyombo vya moto na mwamko mkubwa wa wananchi wa kutumia nishati hiyo, nitumie fursa hii kutoa wito kwa baadhi ya taasisi zinazohusika katika mnyororo wa matumizi ya *CNG*, ikiwemo Bodi ya Usajili wa Wakandarasi *(CRB)*, Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)*, Baraza la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* na *EWURA*, kuhakikisha pia, wanasimamia ipasavyo majukumu hayo katika suala zima la matumizi ya *CNG* nchini, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa wamiliki wa karakana zinazohusika na ubadilishaji wa mifumo ya magari, ili kutumia *CNG* kwa kusimamia kwa karibu wakaguzi na ufungaji wa Mifumo ya *CNG* kwenye magari. Kuhakikisha utoaji wa vyeti vya tathmini ya athari ya mazingira kwa wawekezaji kwenye vituo vya *CNG* na kuhakikisha karakana zote na wakaguzi wote wa Mfumo wanawasilisha, kwa mujibu wa sheria, taarifa za vyombo vya moto vilivyobadili mfumo wa taarifa zao kwa matumizi hayo.

Mheshimiwa Spika, *EWURA* pia, ilitoa leseni 580 za biashara ya mafuta, vibali 215 vya ujenzi wa miundombinu ya mafuta na

kusimamia ubora wa bidhaa za mafuta ambapo jumla ya sampuli 334 kutoka vituo vya mafuta na maghala zilipimwa na ubora wa sampuli 321 sawa na 96.1% zilikidhi viwango stahiki vya ubora. Vilevile, *EWURA* ilikagua ubora wa miundombinu 569 ya mafuta, ambapo miundombinu 551 sawa na 76.2% ilikidhi vigezo vya ubora ikiwemo vigezo vya masuala ya afya ya usalama na mazingira. Pia, mamlaka hiyo ilifanya marekebisho ya Kanuni nne ili kuimarisha shughuli za udhibiti na kuboresha utoaji wa huduma pamoja na kutoa leseni 1,378 kwa mafundi umeme, lengo ikiwa ni kuwezesha upatikanaji wa mafundi umeme wenye ujuzi wa uwekaji mfumo bora na salama wa umeme kwa wananchi hususan maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Nishati kama ilivyofafanuliwa kwa kina katika Sehemu B(ii)13 ya hotuba yangu, Ukurasa wa 117 hadi 124, ni vyema pia, kutambua kuwa, miradi ya utafutaji, uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme na gesi asilia inahitaji uwekezaji mkubwa na muda mrefu. Hivyo, pamoja na juhudi kubwa za kutenga rasilimali fedha zinazoendelea kutekelezwa na Serikali, kwa ajili ya uendelezaji wa Sekta ya Nishati, Serikali pia, itaendelea kuhamasisha, kuvutia na kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo ikiwemo sekta binafsi, ili kufanikisha upatikanaji wa rasilimali fedha zinazochangia katika uendelezaji wa sekta hii kwa kuzingatia mchango wake kwa ukuaji wa uchumi na utoaji wa huduma na ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa, ninaomba nieleze kidogo juu ya Mpango wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Baada ya kutoa Taarifa za Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Mwaka 2024/2025, sasa ninapenda kuwasilisha mpango wa bajeti wa mwaka 2025/ 2026 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2025/2026 Wizara iliendelea kuimarisha uzalishaji, usafirishaji, usambazaji wa umeme ikiwa ni pamoja na kufikisha Gridi ya Taifa katika Mikoa iliyosalia ya Rukwa, Kagera, Lindi na Mtwara. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Nishati wa mwaka 2025 - 2030 *(National Energy Compact 2025/2030)* kuhusu upatikanaji wa

uunganishaji wa umeme wa wananchi. Kuongezeka kwa mchango wa nishati jadidifu katika uzalishaji wa umeme na ushiriki wa sekta binafsi katika Sekta ya Nishati.  Vilevile, Wizara itaendelea kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu unapewa kipambele katika mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ya kipaumbele katika mwaka wa fedha 2025/2026 ni kuendelea kusambaza nishati ya umeme katika vitongoji, maeneo ya migodi, kilimo, viwanda na pampu pamoja na vituo vya afya, ili kuwezesha shughuli za uzalishaji na utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Kuhamasisha uwekezaji ama uwezeshaji Watanzania kutumia nishati safi ya kupikia, ili utekelezaji wa Mkakati wa Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia 2024 - 2035 pamoja na Mpango wa Nishati wa mwaka 2025 - 2030.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia itaendelea kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa za mafuta vijijini kupitia ujenzi wa vituo vya mafuta katika maeneo hayo pamoja na kutekeleza shughuli za utafutaji, uendelezaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia ili kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati ya mafuta na gesi asilia, ikiwemo *Mnazi Bay* Kazkazini, Eyasi – Wembere na Mradi wa Kuchakata Gesi Asilia kuwa kimiminika na Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Ohima Uganda hadi Tanga. Miradi hii yote itaendelea kusimamiwa.

Mheshimiwa Spika, jitihada zitaelekezwa pia, katika kusimamia na kuhakikisha kuwa, nchi yetu inakuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa ya mafuta ya petroli pamoja na uimarishaji wa matumizi ya gesi asilia, *CNG,* katika vyombo vya moto. Vilevile, Wizara itaendelea kutekeleza shughuli za udhibiti na kuimarisha ushiriki wa wazawa katika Sekta ya Nishati pamoja na kuimarisha nguvukazi ya kuwezesha upatikanaji wa vitendeakazi, ili kuimarisha tija na ufanisi wa utendaji kazi. Pia, Wizara itaendelea kuimarisha utendaji kazi wa taasisi na mashirika yaliyo chini ya Wizara *(TANESCO, REA, TPDC, PPPA, EWURA* na *PURA)* pamoja na kampuni tanzu, ili yaweze kuimarika zaidi katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi pamoja na tija na ufanisi katika utendaji.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na mambo mengine umezingatia Ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi, kwa ajili ya Uchaguzi wa Mwaka 2020, Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026, Maagizo na Maelekezo ya Viongozi mbalimbali wa Kitaifa kuhusu Sekta ya Nishati, Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Kamati nyingine za Bunge yaliyotolewa kwa nyakati tofauti tofauti, Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na mpango wa utekelezaji wake na Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia. Mpango Mkakati wa Wizara ya Nishati 2021/2022 – 2025/2026 na Mpango Mahususi wa Taifa wa Nishati wa mwaka 2025 – 2030 na Miongozo Mingine iliyozingatiwa, Sera, Mikakati, Programu mbalimbali za Kisekta na Kitaifa pamoja na Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa *(SDGs)* ya Mwaka 2030 kuhusu masuala ya nishati.

Mheshimiwa Spika, Sehemu *C* ya hotuba yangu, Ukurasa wa 125 hadi 175 unatoa ufafanuzi wa maelezo ya kina kuhusu mikakati ya programu na miradi itakayotekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Kwa kifupi Wizara itatekeleza yafuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sekta Ndogo ya Nishati ya Umeme; Uzalishaji; Serikali itaendelea kutekeleza kwa nguvu uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali ili kuhakikisha kuwa, nchi yetu inaendelea kuwa na umeme wa kutosha na ziada kwa kutumia na kuuzwa nje ya nchi na kulipatia Taifa Fedha za Kigeni.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi ya kuratibu na kuzalisha umeme kwa kutumia maji. Mradi wa Julius Nyerere kuhakikisha kuwa, kunakuwepo na utunzaji wa vyanzo vya maji katika Bonde la Rufiji, ili uwezeshaji wa upatikanaji endelevu wa maji, kwa ajili ya mradi huo, uendeshaji wa ufanisi wa mitambo, kukamilika kwa ujenzi wa ghala la kuhifadhia vifaa katika Kituo cha Kupoza Umeme cha Chalinze na malipo ya *retention* kwa Wakandarasi na Washauri Elekezi wa Mradi wa Julius Nyerere, pamoja na njia ya kusafirisha umeme ya Julius Nyerere, *Hydropower Project* na Kituo cha Kupoza Umeme cha Chalinze.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya kuzalisha umeme itakayotekelezwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni pamoja na Mradi wa Malagarasi wa Megawati 49.5, Mradi wa Kakono Megawati 87.8, Ruhudji Megawati 358, Rumakali Megawati 222 na mradi wa kuzalisha umeme wa jua wa Shinyanga, Kishapu, Megawati 150. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafirishaji na usambazaji wa umeme. Katika kuhakikisha kuwa, umeme wa uhakika unapatikana katika maeneo yote nchini Serikali itaendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya kusafirisha nishati ya umeme kwa kutekeleza miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 104 kutoka Chalinze hadi Dodoma, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Chalinze – Kinyerezi – Mkuranga, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Rufiji – Mkuranga na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Dar es Salaam – Tanga – Arusha. Miradi mingine inayotekelezwa ni ujenzi wa njia ya kusafirisha msongo wa kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya – Tunduma *(TAZA),* Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 400 kutoka Nyakanazi – Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia, itaendelea na utekelezaji wa Mradi wa kuimarisha Gridi ya Taifa pamoja na kuendelea kufanya matengezezo ya kinga katika vituo vya kuzalisha umeme, miundombinu ya kusafirisha na usambazaji wa umeme pamoja na vituo vya kupoza umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu nishati vijijini. Serikali kupitia *REA* itaendelea na programu ya miradi ya nishati vijijini kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kijamii katika maeneo hayo. Programu na miradi itakayotekelezwa ni pamoja na Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji, Mradi wa Ujazilizi Awamu ya Pili (B), Mradi wa Ufungaji wa Mifumo ya Umeme wa Jua katia maeneo ya visiwa yaliyo mbali na Gridi ya Taifa pamoja na kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kwa kushirikiana na wadau kwenye sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwenye Sekta Ndogo ya Gesi, Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026 itaendelea kuchukua hatua za kuendeleza na kusimamia sekta ndogo ya mafuta na gesi kwa lengo la kuhakikisha kuwa, mchango wa sekta hiyo katika pato la Taifa unaendelea kuimarika. Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia katika Vitalu vya *Mnazi Bay* – Kaskazini, Eyasi – Wembere, Songosongo – Magharibi, Ruvuma Eneo la Ntorya na Kitalu cha Lindi huko Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea pia na utekelezaji wa Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa kimiminika (*Liquefy Natural Gas (LNG)),* Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania na ujenzi wa Vituo vya *CNG,* miradi ya usambazaji wa gesi asilia katika mikoa mbalimbali nchini pamoja na nchi jirani. Pia, Serikali itaendelea kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa ya mafuta ya petroli pamoja na kutekeleza masuala ya kiudhibiti katika sekta ya nishati, ili kuimarisha tija na ufanisi pamoja na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Nishati itaendelea kushirikiana na washirika mbalimbali wa maendeleo, Jumuiya za Kikanda, nchi wahisani na wadau wengine katika kutekeleza miradi. Kwa niaba ya Serikali ninapenda kuwashukuru sana washirika wa maendeleo na jumuiya ya nchi wahisani ambao wameendelea kushiriki katika kufanikishaji wa majukumu ya Wizara na sekta ya nishati kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutambua mchango wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AFDB),* Benki ya Dunia, *Arab Bank for Economic Development in Africa (BADEA), Economic Development Cooperation Fund, Geothermal Risk Mitigation Facility,* pamoja na Taasisi na Mashirika ya *JICA* kutoka Japan na Ujerumani *AFDB.* Shirika la Fedha Duniani, Sida, *NORAD,* Umoja wa Ulaya, Shirika la Mitaji ya Maendeleo la Umoja wa Mataifa, Shirika la Maendeleo ya Mataifa *(UNDP),* Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda *(UNIDO),* Shirika la Maendeleo la Canada *(CIDA), Saudi Fund for Development (SFD), OPEC Fund*

*for International Development,* Abu – Dhabi *Fund for Development* na wadau wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie pia nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa Serikali za Afrika Kusini, Algeria, Angola, Burundi, Canada, China, Ethiopia, Falme za Kiarabu, Japan, India, Indonesia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Korea Kusini, Malawi, Misri, Morocco, Msumbiji, Namibia, Norway, Oman, Rwanda, Saudi Arabia, Sweden, Ufaransa, Uganda, Ujerumani, Urusi, Zambia na nchi nyingine kwa kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kuendeleza Sekta ya Nishati. Aidha, ninazishukuru sana Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC),* Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* na Umoja wa Afrika *(AU,)* kwa ushirikiano katika masuala ya kikanda yanayohusiana na Nishati.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya nishati katika uchumi wa nchi na mchango mkubwa wa sekta katika maendeleo ya sekta nyingine mijini na vijijini; mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati, programu na miradi inayolenga kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na nishati ya uhakika, nafuu na endelevu. Aidha, mwelekeo wa Serikali ni kuhakikisha kuwa, shughuli za mafuta na gesi asilia zinashamiri na kuwa na mchango wake kwenye pato la Taifa na zinaendelea kuimarika. Katika kufikia azma hiyo, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuhakikisha kuwa, uendelezaji wa sekta hii muhimu na pia, kufuatiliaji kwa karibu utekelezaji wa programu za miradi vinapewa kipaumbele kwenye huu mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Spika, sasa, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha jumla ya shilingi 2,246,745,445,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, shilingi 2,167,513,219,000 sawa na 95.7% ya bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,466,020,274,000 ni fedha za ndani na shilingi 701,492,945,000 ni fedha za nje. Aidha, shilingi 79,232,226,000 sawa na asilimia 3.5 ni kwa ajili ya matumizi ya

kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 69,932,306,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* na shilingi bilioni 9,299,920,000 ni kwa ajili ya mishahara kwa ajili ya watumishi wa Wizara na taasisi pamoja na *PURA*.

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, ninaomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako, Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kunisikiliza kwa muda wote huu. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara kwa anuani ya *www.nishati.go.tz*. Vilevile, hotuba hii na vielelezo mbalimbali vimeambatishwa kwa ajili ya ufafanuzi wa masuala muhimu yanayohusiana na sekta ya nishati. *(Makofi)*

**HOTUBA YA NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA DKT. DOTO MASHAKA BITEKO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2025/26 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2024/25 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa Mwaka 2025/26.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuendelea kuwajalia afya njema Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wengine na hivyo kutuwezesha kuendelea kuwatumikia Watanzania. Kipekee nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunijalia afya na uzima na kuniwezesha kusimama leo mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2025/26.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 27 Novemba, 2024 Taifa letu lilimpoteza Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile (Mb.), aliyekuwa Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika na Mbunge wa Jimbo la Kigamboni. Aidha, tarehe 13 Aprili, 2025 Taifa lilimpoteza aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mha. Boniface Gissima Nyamo-Hanga. Kwa masikitiko makubwa naungana na Wabunge wenzangu kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, familia za marehemu, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na viongozi hawa. Sisi tuliwapenda, lakini Mwenyezi Mungu aliwapenda zaidi. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

**4.** ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Novemba, 2024 Watanzania wenzetu walipatwa na majanga baada ya jengo la ghorofa kuporomoka, Kariakoo Jijini Dar es Salaam. Tukio hilo lilisababisha athari mbalimbali ikiwemo vifo, uharibifu wa mali na miundombinu. Nami naungana na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wote kwa ujumla, kutoa pole kwa Watanzania wenzetu walioondokewa na ndugu, jamaa na marafiki pamoja na waliopoteza mali zao kufuatia kutokea kwa tukio hilo.

**5.** ***Mheshimiwa Spika***, kipekee napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kufanikisha Mkutano Mkuu Maalumu wa CCM uliofanyika Jijini Dodoma tarehe 18 na 19 Januari, 2025. Katika Mkutano huo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipitishwa kwa kishindo na Wajumbe kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Aidha, nampongeza Komredi Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa na kuthibitishwa na Wajumbe kuwa mgombea mwenza wa nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa

Stephen Masato Wasira kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo na miongozo wanayonipatia katika kutekeleza majukumu yangu ikiwemo usimamizi wa Sekta ya Nishati. Nikiri kuwa maelekezo na miongozo ya Viongozi wetu Wakuu hawa ni chachu na msingi wa mafanikio ya utekelezaji wa majukumu yangu.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi na umahiri mkubwa. Ni wazi kuwa, chini ya uongozi wenu Bunge letu limeendelea kuwa mahiri zaidi katika kuisimamia na kuishauri Serikali kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali ili kuboresha maisha ya Watanzania.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nampongeza Mhe. Dkt. David Mathayo David (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Kilumbe Shaban Ng'enda (Mb.), Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa ushauri na maoni yao katika kuendeleza na kusimamia Sekta ya Nishati kwa manufaa ya kiuchumi na kijamii kwa Taifa letu na watu wake. Napenda kuahidi kuwa Wizara ya Nishati itaendelea kuzingitia ushauri wa Kamati wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Nishati kwa Mwaka 2025/26.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwapongeza Mawaziri wote walioaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kusimamia Wizara mbalimbali na ninawashukuru kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Namshukuru pia Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga (Mb.), Naibu Waziri wa Nishati kwa uchapakazi wake mahiri usio na kifani

na ushirikiano mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, namshukuru Mha. Felchesmi Jossen Mramba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati kwa utendaji wake mahiri katika kutekeleza majukumu ya kila siku ya Wizara. Vilevile, nawashukuru Dkt. James Peter Mataragio, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya petroli na Dkt. Khatibu Malimi Kazungu, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya umeme na nishati jadidifu kwa utumishi wao makini katika kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya Wizara.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** nawashukuru pia Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara kwa ujumla kwa ushirikiano na juhudi zao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Bukombe kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo ya Jimbo. Kutokana na majukumu ya kitaifa ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kuna wakati wananikosa jimboni, lakini kwa wema na upendo wao wanaendelea kunivumilia na kunipa ushirikiano mkubwa. Nawaahidi kuendelea kuwa mtumishi wao mwaminifu na anayejituma katika kutekeleza shughuli za maendeleo jimboni. Kipekee, namshukuru mke wangu mpendwa Benadetha Clement Mathayo kwa maombi na upendo wake wa dhati kwangu na watoto wetu. Amekuwa mvumilivu katika kipindi chote ninapokuwa natekeleza majukumu yangu ya Ubunge, Uwaziri na Unaibu Waziri Mkuu na kukubali kubeba na kutekeleza baadhi ya majukumu ya kifamilia.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** natambua umuhimu wa vyombo vya habari katika kuhabarisha na kuelimisha umma wa Watanzania kuhusu maendeleo ya Sekta ya Nishati. Napenda kuvishukuru na kuvipongeza vyombo hivyo vikiwemo redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2024/25. Ni matumaini yangu kuwa, ushirikiano huu utazidi kuimarika katika Mwaka 2025/26 kwa manufaa ya Taifa letu na Wananchi wake kwa ujumla.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya Hotuba ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2024/25 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2025/26.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2024/25, pamoja na Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2025/26.

## B. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2024/25

**15.** ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika Mwaka 2024/25 uliongozwa na vipaumbele mbalimbali vilivyowekwa, ikiwa ni pamoja na kuendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme; kupeleka nishati vijijini; kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati ya mafuta na gesi asilia ikiwa ni pamoja na mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (*Liquefied Natural Gas – LNG*) na ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania (*East African Crude Oil Pipeline - EACOP*) na kutekeleza shughuli za utafiti na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati vya Songo Songo Magharibi, Mnazi Bay Kaskazini, Eyasi – Wembere na 4/1B & 4/1C; pamoja na kusambaza gesi asilia viwandani, katika taasisi na majumbani na kuimarisha matumizi ya CNG katika magari.

**16.** ***Mheshimiwa Spika***, vipaumbele vingine vilivyowekwa katika Mwaka 2024/25 ni kuendelea kuimarisha upatikanaji na matumizi ya nishati safi ya kupikia *(clean cooking energy)* nchini; kuhakikisha nchi inakuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli pamoja na ufanisi katika kushughulikia upatikanaji wa bidhaa hizo; kuendelea kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa Taasisi/ Mashirika yaliyo chini ya Wizara ambayo ni TANESCO, TPDC, EWURA, PURA, REA, PBPA pamoja na kampuni tanzu ili yaimarishe tija, ufanisi, uwajibikaji na ubora katika uendeshaji na utoaji wa huduma kwa wananchi/wateja; na

kuendelea kuimarisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia pamoja na rasilimali watu ya Wizara na Taasisi zake.

**Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha kwa Mwaka 2024/25**

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/25, Wizara ya Nishati iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Nane Themanini na Tatu, Milioni Mia Saba Hamsini na Tisa, Mia Nne Hamsini na Tano Elfu (Shilingi 1,883,759,455,000)** ambapo **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Saba Tisini na Nne, Milioni Mia Nane Sitini na Sita, Mia Nane Thelathini na Mbili Elfu (Shilingi 1,794,866,832,000)** sawa na asilimia 95.3 ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na **Shilingi Bilioni Themanini na Nane, Milioni Mia Nane Tisini na Mbili, Mia Sita Ishirini na Tatu Elfu (Shilingi 88,892,623,000)** sawa na asilimia 4.7 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwishoni mwa mwezi Machi, 2025, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi Trilioni Moja, Milioni Mia Tatu na Mbili, na Mia Sita Ishirini na Nne Elfu, na Sitini na Tisa (Shilingi 1,000,302,624,069)** ambapo **Shilingi Bilioni Kumi na Nane, Milioni Mia Mbili Kumi na Nne, Mia Nane Sabini na Tatu Elfu, Mia Moja Tisini (Shilingi 18,214,873,190)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi Bilioni Mia Tisa Themanini na Mbili, na Milioni Themanini na Saba, Mia Saba Hamsini Elfu na Mia Nane Sabini na Tisa (Shilingi 982,087,750,879)** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo**.**

**B.1 SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU**


**B.1.1 HALI YA UZALISHAJI NA UPATIKANAJI WA UMEME NCHINI**


**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na jitihada zinazotekelezwa na Serikali katika kuimarisha uzalishaji wa umeme nchini kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali, nchi yetu imeendelea kushuhudia ongezeko kubwa la uzalishaji wa umeme. Naomba kutumia fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika kipindi cha mwaka mmoja, uwezo wa mitambo ya kufua umeme

iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa umeongezeka na kufikia **MW 4,031.71** Aprili 2025, sawa na ongezeko la asilimia 86.6 ikilinganishwa na Megawati 2,138 zilizokuwepo mwezi Machi, 2024. Aidha, katika kiasi hicho, **MW 2,716.27** (asilimia 67.4) ni umeme unaotokana na maji; **MW 1,198.82** (asilimia 29.7) gesi asilia; **MW 101.12** (asilimia 2.5) mafuta; **MW 5** (asilimia 0.1) jua; na **MW 10.5** (asilimia 0.3) tungamotaka. ***Kielelezo Na. 1*** kinaonesha uwezo wa kila chanzo cha kuzalisha umeme uliounganishwa katika Gridi ya Taifa.

**20.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na Serikali ya Awamu ya Sita kuendelea kuweka kipaumbele na msukumo madhubuti katika kuhakikisha Tanzania inakuwa na umeme wa kutosha na uhakika, nchi yetu imeshuhudia ongezeko kubwa la uzalishaji wa umeme katika mfumo wa Gridi ya Taifa tangu Mwaka 2020/21. Wakati mwaka 2020/21 uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa ulikuwa **MW 1,601.84**, kwa sasa mitambo hiyo ina uwezo wa kufua **MW 4,031.71,** sawa na ongezeko la asilimia 151.7 kama inavyoonekana katika ***Kielelezo Na. 2***.

**21.** ***Mheshimiwa Spika***, ni vyema kutambua kuwa kutokana na jitihada hizi, nchi yetu imeweza sasa kuondokana na mgao wa umeme ambao ulikuwa changamoto kubwa katika kipindi cha miaka mingi na kuwa na ziada ya umeme. Aidha, kupatikana kwa umeme wa uhakika kumewezesha kupunguza gharama za uzalishaji na ufanyaji biashara nchini; kuzimwa kwa mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta ambayo uendeshaji wake ni wa gharama kubwa; na kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika vijijini, katika uendeshaji wa treni ya kisasa ya SGR na katika mikoa ambayo ilikuwa haijaungwa katika Gridi ya Taifa. Aidha, upatikanaji huu wa umeme wa uhakika umechangia kukua kwa Pato la Taifa na kukabiliana na mfumuko wa bei kutokana na athari chanya za upatikanaji wa umeme huo katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na upatikanaji wa huduma.








Chanzo: **TANESCO**

***Kielelezo Na. 2*: Uwezo wa Mitambo ya Kufua Umeme Iliyounganishwa katika Mfumo wa Gridi ya Taifa, 2020/21 – Aprili, 2025**

| **Mwaka** | **2020/21** | **2021/22** | **2022/23** | **2023/24** | **Aprili, 2025** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Uwezo wa Mitambo (MW)** | 1,601.84 | 1,777.05 | 1,889.84 | 3,091.71 | 4,031.71 |

Uwezo wa Mitambo ya Kufua Umeme




*Chanzo:* ***TANESCO***

**22.** ***Mheshimiwa Spika***, ongezeko hili limetokana na kukamilika kwa miradi mbalimbali ya kuzalisha umeme katika kipindi husika, hususan Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Julius Nyerere ambapo hadi mwezi Aprili, 2025 mitambo yote tisa (9) imekamilika. Aidha, kwa sasa mitambo huingizwa kwenye Gridi ya Taifa kutokana na mahitaji ya umeme yaliyopo na kulingana na uwezo wa miundombinu ya usafirishaji. Serikali pia imeendelea kuchukua hatua za kukarabati mitambo mbalimbali ya kuzalisha umeme ambayo imechangia katika kuimarisha uzalishaji wa umeme nchini. ***Kiambatisho Na. 1*** kinaonesha uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika Gridi ya Taifa hadi mwezi Aprili, 2025.

**23.** ***Mheshimiwa Spika***, kufikia mwezi Aprili, 2025, mitambo ya kuzalisha umeme ambayo haijaungwa katika Gridi ya Taifa ina uwezo wa jumla ya **MW 328.17** ambayo inajumuisha mitambo inayomilikiwa na TANESCO yenye uwezo wa kuzalisha **MW 20.19** na **MW 307.98** zinazalishwa na kampuni binafsi kwa ajili ya matumizi ya kampuni hizo kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Na. 2***.

**24.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TANESCO inanunua umeme wa jumla ya **MW 52** kutoka nje ya nchi ikilinganishwa na **MW 32** ilizokuwa ikinunua Mwaka 2023/24. Kati ya kiasi hicho kinachonunuliwa **MW 36** zinanunuliwa kutoka nchini Uganda kwa ajili ya Mkoa wa Kagera na **MW 16** kutoka nchini Zambia kwa ajili ya Mkoa wa Rukwa. Mahitaji ya mikoa hii yameongezeka, ambapo mahitaji ya Mkoa wa Kagera yameongezeka kutoka **MW 21** hadi **MW 36** katika kipindi cha mwaka mmoja kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya umeme kupitia kiwanda cha sukari cha Kagera, hususan katika shughuli za umwagiliaji wa mashamba ya miwa na kuongezeka kwa wateja wapya 19,116. Aidha, mahitaji ya umeme katika Mkoa wa Rukwa yameongezeka kutoka **MW 10** hadi **MW 16** katika kipindi cha mwaka mmoja kutokana pamoja na mambo mengine, kuongezeka kwa wateja kupitia kuungwa kwa jumla ya vijiji vipya 138 na vitongoji vipya 76.

**25.** ***Mheshimiwa Spika***, mahitaji ya juu ya umeme katika Gridi ya Taifa nchini yameendelea kuongezeka na kufikia **MW 1,921.44** zilizofikiwa tarehe 09 Aprili, 2025 saa 3:00 usiku ikilinganishwa na **MW 1,590.10** zilizofikiwa tarehe 26 Machi, 2024 saa 3:00 usiku sawa na ongezeko la asilimia 20.84. ***Kielelezo Na. 2*** ni mwenendo wa mahitaji ya juu ya umeme katika Mwaka 2023/24 na 2024/25. Aidha, ***Kielelezo Na. 3*** kinaonesha mwenendo wa mahitaji ya juu ya umeme nchini kuanzia mwaka 2020 hadi Aprili 2025.

**26.** ***Mheshimiwa Spika***, ongezeko la mahitaji ya umeme nchini la **MW 740.91** kutoka **MW 1,180.53** za mwaka 2020 hadi **MW 1,921.44** zilizofikiwa tarehe 09 Aprili, 2025 linatokana na jitihada kubwa na za makusudi zinazotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita, hususan kukuza uchumi wa nchi yetu kunakoambatana na mahitaji ya umeme; kuimarisha huduma za kijamii ambazo uendeshaji wake unahitaji umeme; kukua kwa sekta za viwanda na usafirishaji (treni ya SGR); ongezeko la matumizi ya nishati safi ya kupikia; na kuimarika kwa uunganishaji wa umeme kwa wananchi mijini na vijijini.

***Kielelezo Na. 2*: Mwenendo wa Mahitaji ya Juu ya Umeme (MW) Nchini kwa Mwaka 2023/24 na 2024/25**


| 2023/24 | 2024/25 | Tofauti |
|---|---|---|
| 1,466.10 | 1,683.57 | **217.47** |
| 1,482.80 | 1,670.57 | **187.77** |
| 1,413.50 | 1,728.24 | **314.74** |
| 1,399.90 | 1,792.53 | **392.63** |
| 1,389.5 | 1,888.72 | **499.22** |
| 1,339.70 | 1,823.52 | **483.82** |
| 1,434.40 | 1,888.72 | **396.49** |
| 1,510.30 | 1,908.15 | **397.85** |
| 1,590.10 | 1,898.00 | **307.00** |
| 1,590.12 | 1,921.44 | **331.31** |
| 1,461.64 | 1,817.12 | **355.393** |

*Chanzo:* ***TANESCO***

***Kielelezo Na. 3:*** **Mwenendo wa Mahitaji ya Juu ya Umeme Nchini kwa Mwaka 2020 - Aprili, 2025**

| **Mwaka** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **Aprili 2025** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mahitaji ya Juu ya Umeme (MW)** | 1,180.53 | 1,307.36 | 1,354.61 | 1,482.80 | 1,888.72 | 1,921.44 |

**Mahitaji ya juu ya Umeme**




*Chanzo:* ***TANESCO***

**B.1.2 HALI YA USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI WA UMEME**

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na upanuzi wa miundombinu ya kusafirisha umeme ambayo imefikia jumla ya urefu wa kilomita 8,140 ikiwa ni ongezeko la asilimia 5 ikilinganishwa na kilomita 7,745 za Mwaka 2023/24. Ongezeko hilo limetokana na kukamilika kwa mradi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kidahwe mkoani Kigoma na mradi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Urambo.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** miundombinu ya usambazaji umeme imeongezeka kutoka kilomita 176,750.9 mwezi Aprili 2024 hadi kilomita 200,266.25 mwezi Aprili 2025 sawa na ongezeko la asilimia

13.3 ambapo kilomita 80,057.27 ni za msongo wa kati wa kilovoti 11 na 33 na kilomita 120,208.98 ni za msongo mdogo wa kilovoti 0.4. ***Kielelezo Na. 4*** ni mwenendo wa ukuaji wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme.

***Kielelezo Na. 4:*** **Mwenendo wa Ukuaji wa Njia za Kusafirisha na Kusambaza Umeme Mwaka 2021 - Aprili, 2025 (Kilomita)**

| **Msongo** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Njia za Usafirishaji** | | | | | | |
| 400kV | 671 | 414 | | 160 | 280 | 1,525 |
| 220kV | 3,348 | | 333 | 415 | | 4,096 |
| 132kV | 1,825 | | | | 115 | 1,940 |
| 66kV | 580 | | | | | 580 |
| **Jumla** | **6,424** | **414** | **333** | **575** | **395** | **8,141** |
| **Njia za Usambazaji** | | | | | | |
| 33kV | 47,487.88 | 4,763.61 | 4,233.34 | 7,330.87 | 3,426.03 | 67,241.73 |
| 11kV | 11,492.11 | 92.29 | 636.45 | 409.7 | 184.99 | 12,815.54 |
| 0.4kV | 88,570.24 | 7,403.30 | 5,046.39 | 10,351.55 | 8,837.50 | 120,208.98 |
| **JUMLA** | **147,550.23** | **12,259.20** | **9,916.18** | **18,092.12** | **12,448.52** | **200,266.25** |

Chanzo***: TANESCO***

### B.1.3 HUDUMA KWA WATEJA

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANESCO imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha utoaji wa huduma kwa wateja ikiwa ni pamoja na:

(i) Kusimamia mfumo wa huduma ya Nikonekt ambao umewezesha kuunganisha wateja 590,200 kwa kipindi cha Aprili 2024 hadi Aprili 2025;

(ii) Kuanzishwa kwa namba maalumu ya huduma kwa wateja bila malipo ya 180 (*Toll Free*) inayotumika nchi nzima. Huduma hii inawawezesha wateja kupiga simu bila malipo na kupata utatuzi wa changamoto na taarifa mbalimbali za huduma ya umeme kwa wakati;

(iii) Kuanzishwa kwa mfumo wa utoaji taarifa kwa wateja kwa njia ya *WhatsApp* yaani Jisoti ambao umesaidia kuboresha ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wateja na

utatuzi wa changamoto mbalimbali za upatikanaji wa umeme; na

(iv) Kuimarisha utoaji wa huduma kupitia makundi sogozi ya *WhatsApp* yaliyopo nchi nzima na matumizi ya mitandao ya kijamii ambayo yanawarahisishia wateja kupata huduma za TANESCO.

**B.1.4 MIRADI YA KUZALISHA UMEME**

**a) Miradi Iliyopo katika Hatua za Utekelezaji**

**(i) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP – MW 2,115)**

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi huu ulioanza mwezi Juni 2019 umefikia asilimia 99.93 mwezi Aprili 2025, ambapo mitambo yote tisa (9) ya kuzalisha umeme imekamilika. Aidha, mitambo hiyo huingizwa kwenye Gridi ya Taifa kutokana na mahitaji ya umeme yaliyopo na kulingana na uwezo wa miundombinu ya usafirishaji. Kazi zilizokamilika ni ujenzi wa bwawa kuu (*main dam*), njia za kupitisha maji (*tunnels*), kituo cha kuongeza nguvu ya umeme (*switch yard*), nyumba za makazi na ofisi, pamoja na njia ya kusafirisha umeme kutoka kituo cha kufua umeme (*power house*) hadi kituo cha kupokelea umeme. Aidha, kazi ambazo zipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji ni ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme (*power house*) na ujenzi wa barabara za kudumu ndani ya eneo la mradi na matuta madogo *(saddle dams)*.

**(ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension– MW 185**

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwezi Aprili 2025, Serikali imekamilisha ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme ya Kinyerezi I Extension **MW 185** kwa asilimia 98.4 ambapo mitambo yote minne (4) kwa sasa inafua umeme wa kiasi cha **MW 40** kila mmoja, hivyo kiasi cha umeme wa **MW 160** kinaingizwa kwenye Gridi ya Taifa. Mradi huu pia unahusisha uimarishaji wa njia ya

kusafirisha umeme kutoka Kinyerezi kwenda Mbagala kupitia Gongolamboto na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Kinyerezi, Gongolamboto na Mbagala. Kwa ujumla utekelezaji wa kazi hizo umefikia asilimia 70 ambapo transfoma nne (4) za vituo vyote (Kinyerezi – 2, Gongolamboto - 1 na Mbagala – 1) zimeshafungwa katika vituo husika. Kazi nyingine zinazoendelea ni kuimarisha njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 3.5 kutoka Kinyerezi hadi Gongolamboto kwa kujenga nguzo 16 na kuweka nyaya mpya za umeme. Kukamilika kwa mradi huo kutaimarisha huduma ya upatikanaji wa umeme wa uhakika katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

**(iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rusumo – MW 80**

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi huu wa kuzalisha umeme wa **MW 80** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera kwa ushirikiano wa nchi tatu (3) za Tanzania, Burundi na Rwanda kwa mgawanyo sawa wa umeme umekamilika, na hivyo kuiwezesha Tanzania kupata jumla ya **MW 26.67** za umeme. Kukamilika kwa mradi huu kumeboresha upatikanaji wa umeme katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na kuunganishwa kwa Gridi ya Taifa ya Tanzania na Gridi za nchi za Burundi na Rwanda na hivyo kutoa fursa ya kuziuzia umeme nchi hizo endapo zitakuwa na mahitaji.

**(iv) Ukarabati wa Mitambo katika Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Hale**

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kukarabati miundombinu ya kuzalisha umeme katika Kituo cha Hale chenye uwezo wa kuzalisha **MW 21** ili kiweze kuzalisha umeme kwa uwezo wake wa juu badala ya **MW 10.5** zinazozalishwa sasa. Kufikia Aprili, 2025, utekelezaji umefikia asilimia 74 ambapo uchimbaji wa handaki na ujenzi wa barabara mpya yenye urefu wa kilometa 1.3 umekamilika kwa asilimia 100. Kwa upande wa kituo cha kupoza umeme, kazi zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa misingi ya transfoma, ujenzi wa ukuta wa kuzuia moto pamoja na ujenzi wa jengo la *switch gear*. Aidha, kazi zinazoendelea kwa

upande wa *power house* ni uondoaji wa mitambo ya zamani pamoja na lifti ya kuingilia kwenye jengo la mitambo.

**(v) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Malagarasi – MW 49.5**

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 49.5** kwa kutumia maji ya Mto Malagarasi ambao hadi Aprili, 2025 umefikia asilimia 5.2. Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 54 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe mkoani Kigoma ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 92.5. Aidha, usambazaji wa umeme katika vijiji saba (7) vinavyopitiwa na mradi huu ambavyo ni Igamba, Mazungwe, Kazuramimba, Mwamila, Kalenge, Mlela na Kidahwe umefikia asilimia 15.2. Mradi unatarajiwa kukamilika Oktoba, 2027.

**(vi) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Jua Mkoani Shinyanga – MW 150**

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia jua katika eneo la Kishapu mkoani Shinyanga wenye uwezo wa kuzalisha **MW 150**. Utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Mradi huu inayohusisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 50** umefikia asilimia 51. Aidha, mkataba wa ufadhili kati ya Serikali ya Tanzania na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya pili ya **MW 100** ulisainiwa tarehe 6 Desemba, 2024 na unatarajiwa kuanza utekelezaji mwezi Julai 2025 baada ya kukamilika kwa taratibu za zabuni ya kumpata mkandarasi.

**b) Miradi ya Uzalishaji wa Umeme Iliyopo katika Hatua za Utayarishaji**

**(i) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Ruhudji – MW 358**

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliendelea na maandalizi ya ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 358** kwa kutumia maji ya

Mto Ruhudji mkoani Njombe na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 170 kutoka Ruhudji hadi kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Kisada mkoani Iringa. Serikali inakamilisha uidhinishaji wa majedwali ya uthamini kwa ajili ya kuanza malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha mradi huu.

**(ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rumakali – MW 222**

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 222** kwa kutumia maji ya Mto Rumakali, wilayani Makete katika Mkoa wa Njombe pamoja na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 64.5 kutoka kwenye mitambo hadi kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Iganjo mkoani Mbeya. Kwa sasa Serikali inakamilisha uidhinishaji wa majedwali ya uthamini kwa ajili ya kuanza malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha mradi.

**(iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kakono – MW 87.8**

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kuongeza uwezo wa uzalishaji wa umeme katika Gridi ya Taifa na upatikanaji wa umeme wa uhakika katika mikoa ya Kanda ya Ziwa. Mradi utahusisha ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme wa **MW 87.8** kwa kutumia maji ya Mto Kagera na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 38 kutoka Kakono hadi Kyaka. Kufikia Aprili 2025, Serikali imesaini mikataba na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) kwa ajili ya ufadhili wa mradi huo. Aidha, Serikali kupitia TANESCO imesaini Mkataba na Mshauri Mwelekezi wa mradi.

**(iv) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia Mtwara- MW 300**

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wa Mtwara utakaokuwa na uwezo wa kuzalisha **MW 300**. Aidha, Serikali imeanza kulipa fidia kwa wananchi waliopisha mradi ambapo hadi Aprili 2025, Shilingi milioni 500 zimelipwa kwa wananchi wa vijiji vya Kisiwa na Namgogoli katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara.

**B.1.5 MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUSAMBAZA UMEME**

**a) Miradi ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme Iliyopo katika Hatua za Utekelezaji**

**(i) Mradi wa Kusafirisha Umeme kutoka JNHPP hadi Chalinze – Kilovoti 400 na Kituo cha Kupoza Umeme, Chalinze**

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 160 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Julius Nyerere hadi Chalinze mkoani Pwani umekamilika kwa asilimia 99.8 na ujenzi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Chalinze umekamilika kwa asilimia 97.6. Aidha, kwa sasa mradi huu upo katika hatua za uangalizi na miundombinu hiyo inaendelea kutumika kuingiza umeme unaozalishwa JNHPP kwenye Gridi ya Taifa.

**(ii) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga**

**41.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imekamilisha ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 414 kutoka Singida hadi Namanga kupitia Babati na Arusha na hivyo kuwezesha kuunganishwa kwa Gridi za Taifa za Tanzania na Kenya. Kukamilika kwa mradi huu kuna manufaa mbalimbali kwa nchi yetu, ikiwa ni pamoja na kuwezesha kufanyika kwa biashara ya umeme baina ya Tanzania na nchi za Afrika Mashariki kupitia *East African Power Pool (EAPP)*.

**(iii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma (TAZA)**

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Iringa kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga yenye urefu wa kilomita 620 pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Kisada (Iringa), Iganjo (Mbeya), Tunduma na Sumbawanga. Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 38 na unatarajiwa kukamilika Mei, 2026. Kukamilika kwa mradi huu kutaimarisha upatikanaji wa umeme katika mikoa ya nyanda za Juu Kusini pamoja na kuunganisha Gridi ya Taifa na Gridi za nchi za Kusini mwa Afrika na hivyo kuwezesha kufanyika kwa biashara ya umeme baina ya nchi hizo kupitia *Southern African Power Pool (SAPP)*.

**(iv) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma**

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 280 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma. Kufuatia kukamilika kwa njia hiyo, Serikali ilichukua hatua ya kujenga kituo cha dharura cha kupoza umeme cha Kidahwe ambacho kiliwezesha Mkoa wa Kigoma kuunganishwa katika Gridi ya Taifa kwa msongo wa kilovoti 220. Aidha, mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 400 wa Nyakanazi - Kigoma unahusisha pia ujenzi wa kituo cha kudumu cha kupoza umeme cha Kidahwe mkoani Kigoma ambao kufikia mwezi Aprili 2025, utekelezaji wake umefikia asilimia 10.4. Vilevile, usambazaji wa umeme katika vijiji 18 vilivyopo katika eneo la mradi umefikia asilimia 73.

**(v) Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (*National Grid Stabilization Projects)* – Gridi Imara**

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** lengo la mradi huu ni kuimarisha miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme pamoja na vituo vya kupoza umeme katika mikoa mbalimbali, ikiwemo

ufungaji wa mitambo na vifaa vya kisasa, ubadilishaji wa nguzo za miti kwa kusimika nguzo za zege, ufungaji wa nyaya zenye uwezo wa kusafirisha umeme mkubwa pamoja na transfoma. Utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 42 ambapo miradi sita (6) kati ya 27 imekamilika kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Na. 3.***

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizokamilika kupitia mradi huu ni pamoja na kuunganisha Mkoa wa Kigoma katika Gridi ya Taifa kupitia kituo cha Nyakanazi kwa kukamilisha mradi wa kusambaza umeme kutoka Nyakanazi kwenda Wilaya ya Kakonko na kuunganisha Wilaya za Ngara na Biharamulo za Mkoa wa Kagera katika Gridi ya Taifa kupitia kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi. Aidha, miradi mingine iliyokamilika ni pamoja na uboreshaji wa upatikanaji wa umeme katika maeneo ya Kurasini - Dar es Salaam kwa kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 132 kutoka Ilala hadi Kurasini; kuboresha upatikanaji wa umeme katika miji ya Songwe Mkwajuni na Mbangala mkoani Songwe kwa kukamilisha ufungaji wa transfoma katika miji hiyo na kuweka nyaya zenye uwezo mkubwa kwenye njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 kutoka Ubungo kupitia Chalinze hadi Hale.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeendelea na taratibu za utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi wa Gridi Imara ambapo kupitia TANESCO, imekamilisha Upembuzi Yakinifu kwa miradi saba (7) na kuendelea na maandalizi ya Upembuzi Yakinifu kwa miradi nane (8) kama ilivyoainishwa katika ***Kiambatisho Na. 4.*** Kukamilika kwa miradi ya Gridi Imara kutaimarisha upatikanaji wa umeme katika maeneo mbalimbali nchini na hivyo kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii.

### (vi) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 132 Kutoka Tabora hadi Katavi kupitia Sikonge

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 383 kutoka Tabora hadi Katavi kupitia Sikonge, Ipole na Inyonga ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 96. Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha kuunganishwa kwa Mkoa wa Katavi

katika Gridi ya Taifa na kuboresha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika mkoa huo.

**(vii) Mradi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Gridi ya Taifa *TANESCO Transmission Grid Rehabilitation and Upgrading - TTGRUP)***

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kuimarisha Gridi ya Taifa kwa kukarabati na kuboresha vituo nane (8) vya kupoza umeme, kurefusha Mkongo wa Mawasiliano (*Optic Fiber*) na kuboresha miundombinu ya mawasiliano kwa kuondoa *earth wire* na kuweka *optical ground wire* pamoja na kuimarisha mfumo wa uendeshaji na udhibiti wa Gridi ya Taifa. Mradi huu unagharamiwa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kufikia Aprili 2025, uboreshaji wa miundombinu ya mawasiliano umekamilika kwa asilimia 100 na uboreshaji wa mfumo wa udhibiti wa Gridi ya Taifa umefikia asilimia 70.

**(vii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Benaco hadi Kyaka**

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 kutoka Benaco hadi Kyaka yenye urefu wa kilomita 166.2 itakayounganisha Mkoa wa Kagera katika Gridi ya Taifa. Serikali kupitia TANESCO imekamilisha uthamini wa mali za wananchi wanaopisha mradi na kazi zinazoendelea ni pamoja na kuendelea na taratibu za malipo ya fidia na kumpata Mkandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

**(viii) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Mwanza hadi Isaka kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (*SGR Lot V*)**

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 230 kutoka Mwanza hadi Isaka kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya SGR. Serikali kupitia TANESCO inaendelea na taratibu za

malipo ya fidia kwa wananchi wanaoipisha mradi na kazi ya usanifu wa mradi inaendelea.

**(ix) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze - Kinyerezi - Mkuranga (*NEG Phase 1*)**

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 400 kutoka Chalinze hadi Mkuranga kupitia Kinyerezi yenye urefu wa kilomita 135 na vituo vya kupoza umeme vya Chalinze, Kinyerezi na Mkuranga. Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Morogoro. Hadi Aprili 2025, Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya awali ya utekelezaji wa mradi ikiwemo usafishaji wa eneo, uchunguzi wa udongo na ununuzi wa vifaa.

**(x) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Dodoma (*NEG Phase 2*)**

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Chalinze hadi Dodoma yenye urefu wa kilomita 345 na upanuzi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Dodoma. Mradi huu utawezesha kusafirisha umeme unaotoka JNHPP kupitia Chalinze kwenda Dodoma na kusambazwa katika mikoa mbalimbali nchini (*power evacuation*). Serikali imekamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha mradi ambapo kwa sasa Mkandarasi anaendelea na usanifu wa mradi, uchunguzi wa udongo pamoja na kuanza taratibu za awali za ununuzi wa vifaa vya ujenzi.

**(xi) Mradi wa Kuboresha Utendaji Kazi wa TANESCO *(Corporate Management System – CMS)***

**53.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unalenga kuboresha hali ya utendaji kazi wa TANESCO kwa kuweka mifumo inayowezesha kuongeza tija na ufanisi. Kufikia Aprili 2025, utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 89. Kazi zilizokamilika ni pamoja na kutoa mafunzo kwa watumiaji wa mfumo na ufungaji wa vifaa vya

miundombinu katika vituo vya taarifa *(Primary Data Center – NIDC* na *Secondary Data Center – eGA)*.

**(xii) Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Ibadakuli, Shinyanga**

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa kituo kipya chenye uwezo wa kilovoti 400/220/33 na kusimika transfoma kubwa mbili zenye ukubwa wa MVA 315 kila moja katika eneo la Ibadakuli mkoani Shinyanga ili kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na maeneo jirani kwa lengo la kuchochea shughuli za kiuchumi, hususan uchimbaji wa madini, usafirishaji kwa kutumia treni ya SGR na mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka nchini Uganda hadi Tanga (EACOP). Hadi Aprili, 2025 ujenzi wa mradi umefikia asilimia 21.8. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa misingi kwa ajili ya kusimika mitambo.

**b) Miradi ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme Iliyopo Katika Hatua ya Utayarishaji**

**(i) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Segera na Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Segera – Tanga**

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Chalinze – Segera – Same – Arusha; msongo wa kilovoti 220 Segera – Tanga; na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Segera, Tanga na Same. Hadi Aprili, 2025, Serikali imekamilisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA), Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Mradi. Vilevile, Serikali inaendelea na juhudi za utafutaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

**(ii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Segera- Same- Arusha (*Lemugur*)**

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Segera hadi

Arusha kupitia Same, kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Same na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Segera na Lemugur. Kufikia mwezi Aprili 2025, kazi zilizokamilika ni Upembuzi Yakinifu, Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) pamoja na usanifu wa mradi. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

**(iii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Makutopora hadi Tabora kwa ajili Uendeshaji wa Treni ya Umeme (*SGR Lot 3*)**

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 320 kutoka Makutupora hadi Tabora kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme unaendelea. Hadi Aprili 2025, kazi zilizokamilika ni pamoja na Upembuzi Yakinifu wa mradi na kuweka mipaka ya mkuza wa njia ya kusafirisha umeme. Taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi zinatarajiwa kukamilika Juni 2025.

**(iv) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Tabora hadi Isaka kwa ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (*SGR Lot 4*)**

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANESCO inaendelea na utelekezaji wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 130 kutoka Tabora hadi Isaka kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme. Kufikia Aprili 2025, kazi zilizokamilika ni utafiti wa awali na kazi zinazoendelea ni pamoja na Upembuzi Yakinifu na tathmini ya malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi huo.

**(v) Ujenzi wa Njia za Kusafirisha Umeme *(Submarine Cables)* kutoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar na Mafia**

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme Zanzibar, Serikali kupitia TANESCO inaendelea na utekelezaji wa miradi ya njia za kusafirisha umeme za msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 49.95 kutoka Ununio – Dar es Salaam kwenda Unguja na msongo wa kilovoti 132 yenye urefu

wa kilomita 87 kutoka Tanga kwenda Pemba kupitia chini ya Bahari *(submarine cables)*. Aidha, mradi huu unahusisha pia ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 109.2 kutoka Mkuranga hadi Mafia. Hadi kufikia Aprili 2025, kazi zilizokamilika ni pamoja na Upembuzi Yakinifu, usanifu wa awali na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kuwapata Wakandarasi wa ujenzi.

**(vi) Mradi wa Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Tanzania hadi Uganda (Ibadakuli - Masaka)**

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 617 kutoka Ibadakuli – Nyakanazi – Kyaka hadi Masaka, Uganda pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kyaka utawezesha kuunganisha Gridi ya Tanzania na Uganda. Kufikia Aprili 2025, Upembuzi Yakinifu na Tathmini ya Athari kwa Mazingira pamoja na tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi zimekamilika. Taratibu za upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa mradi zinaendelea.

**(vii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 Kutoka Chalinze – Bagamoyo**

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 kutoka Chalinze - Bagamoyo yenye urefu wa kilomita 90 pamoja na ujenzi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Bagamoyo. Kwa sasa Serikali inaendelea na taratibu za upatikanaji wa fedha za kutekeleza mradi huu.

**(viii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Sumbawanga hadi Kigoma Kupitia Mpanda na Kituo cha Kupoza Umeme Mpanda**

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka Sumbawanga hadi Kigoma kupitia Mpanda yenye urefu wa kilomita 480 utaimarisha upatikanaji wa umeme katika mikoa ya Tabora, Katavi na Kigoma. Benki ya

Maendeleo Afrika (AfDB) na Benki ya Exim ya Korea zimeonesha nia ya kugharamia mradi huu. Kwa sasa taratibu za ununuzi wa Mkandarasi wa kutekeleza mradi zinaendelea.

**c) Utekelezaji wa Miradi Mingine na Matengenezo ya Mitambo**

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme nchini, Serikali kupitia TANESCO imeendelea kufanya ukaguzi wa hali ya mitambo ya kufua umeme na kufanya matengenezo na maboresho ya miundombinu ya umeme. Vituo 12 vya uzalishaji umeme vilifanyiwa matengenezo makubwa na madogo na vituo 17 vya kupoza umeme vilifanyiwa maboresho kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Na. 5A*** na ***5B.*** Aidha, kazi ya kuimarisha miundombinu ya usafirishaji umeme iliendelea kwa kufanya ukaguzi wa kina ili kubaini maeneo yenye changamoto na kuyafanyia ukarabati. Ukarabati uliofanyika ulihusisha ubadilishaji wa nyaya chakavu zenye urefu wa kilomita 186.2, vikombe vilivyopasuka katika njia 11 za misongo mbalimbali, vyuma vilivyoibiwa, kuondoa nguzo za miti 1,810 na kuweka nguzo za zege pamoja na ukarabati wa sehemu zilizoathiriwa na mmomonyoko wa udongo na kusafisha mikuza ya njia za kusafirisha umeme. ***Kiambatisho Na. 5C*** kinaonesha maboresho ya njia za kusafirisha umeme.

**64.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TANESCO inatekeleza mradi wa kuboresha na kuongeza uwezo wa mitambo ya kuongoza/ kuendesha Gridi ya umeme (*SCADA-EMS*) ambapo kufikia Aprili 2025 umefikia asilimia 53 na unatarajiwa kukamilika Julai 2025. Mradi huu, una lengo la kuongeza ufanisi wa uendeshaji wa gridi kupitia teknolojia ya kidijitali.

**B.1.6 USHIRIKI WA TANZANIA KATIKA BIASHARA YA UMEME KUPITIA *EASTERN AFRICAN* POWER POOL (EAPP) NA SOUTHERN AFRICA POWER POOL (SAPP)**

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya za Kikanda za Kuuziana Umeme za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika *(Eastern African Power Pool - EAPP* na *Southern Africa*

*Power Pool - SAPP)*. Jumuiya hizo zinatoa fursa kwa nchi wanachama kutumia kwa ufanisi vyanzo vya kuzalisha umeme walivyonavyo na kuuza umeme huo kwa nchi wanachama wenye uhitaji kwa manufaa ya nchi zote. Aidha, uwepo wa Jumuiya hizo ni kichocheo muhimu kwa nchi kushirikiana katika ujenzi wa miundombinu wezeshi inayounganisha nchi na nchi (*power interconnector*) ili kuwezesha kuwa na mizania ya pamoja itakayowezesha biashara ya umeme kufanyika katika Jumuiya hizo.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa Tanzania inashiriki ipasavyo katika biashara ya umeme kupitia EAPP na SAPP, Serikali kupitia TANESCO imekamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 414 kutoka Singida kupitia Arusha hadi Namanga ambayo imeiwezesha nchi kuungwa na EAPP kupitia Kenya. Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 620 (TAZA) itakayowezesha Gridi ya Taifa kuungwa na SAPP na hivyo kuiwezesha Tanzania kuuziana umeme na nchi za Kusini mwa Afrika kupitia Zambia.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa sasa vyanzo vikuu vya kuzalisha umeme nchini vipo katika mikoa ya Pwani na Kusini Mashariki mwa Tanzania (Dar es Salaam, Pwani na Morogoro). Kutokana na umbali na kutokuwa na vyanzo vya uhakika vya kuzalisha umeme katika maeneo mengine ya nchi yaliyobaki ikiwemo Mikoa ya Kanda ya Kaskazini na maeneo mengine ya nchi, usafirishaji wa umeme kwenda katika mikoa hiyo umekuwa ukipelekea changamoto ya ubora wa umeme kwa nyakati tofauti katika maeneo hayo. Aidha, ikiwa ni hatua ya kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inakamilisha taratibu za ununuzi wa kiasi cha **MW 100** za umeme kutoka nchini Ethiopia kupitia Kenya ili kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme katika maeneo husika. Vilevile, kiasi hicho cha umeme utakaonunuliwa kutoka nchini Ethiopia kitahesabiwa kuanzia katika eneo la Namanga lililopo mpakani mwa Tanzania na Kenya ambapo ndipo mita ya mauziano ya umeme huo imefungwa. Eneo hilo la Namanga lipo karibu na mikoa ya Kanda ya Kaskazini na hivyo kusaidia

uimarishaji wa ubora wa upatikanaji wa umeme katika mikoa husika.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** manufaa mengine ya hatua hiyo ni pamoja na kuongeza usalama wa mfumo wa Gridi ya Taifa na uwezo wa kurejesha Gridi kwa haraka iwapo litatokea tatizo la kuzimika kwa Gridi na kusaidia kupunguza msongamano wa kusafirisha umeme ikizingatiwa kuwa baadhi ya njia za kusafirisha umeme zimeelemewa na kushindwa kupitisha umeme wa kutosha. Aidha, hatua hii itakuwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mahsusi wa Tanzania wa Nishati (*National Energy Compact for Tanzania*) ulioridhiwa na Marais wa Afrika katika Mkutano wa Nishati wa Afrika *(Mission 300)* ambapo moja ya nguzo zake ni kuunganisha gridi za umeme za Afrika ili kuwezesha ushirikiano katika kubadilishana umeme.

### B.1.7 UTENDAJI WA KAMPUNI TANZU ZA TANESCO

#### a) Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji Umeme (ETDCO)

**69.** ***Mheshimiwa Spika***, ETDCO inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi wa njia za kusafirisha umeme. Hadi Aprili, 2025, Kampuni hiyo imekamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 115 kutoka Tabora hadi Urambo; miradi ya usambazaji umeme wa msongo wa kilovoti 33 na 11 katika mikoa ya Katavi, Mtwara, Morogoro na Arusha pamoja na mradi wa kuboresha njia za usambazaji umeme katika Kisiwa cha Songo Songo. Aidha, ETDCO inaendelea kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 383, ambapo kipande cha kutoka Tabora hadi Ipole chenye urefu wa kilomita 110 kimekamilika kwa asilimia 100 na Ipole hadi Inyonga chenye urefu wa kilomita 125 ujenzi umefikia asilimia 98 na Mkandarasi anamalizia ukaguzi wa mwisho wa njia hiyo kabla ya umeme kuwashwa. Aidha, kwa kipande cha Inyonga hadi Mpanda chenye urefu wa kilomita 130 ujenzi umekamilika kwa asilimia 95. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 96 na unatarajiwa kukamilika katika mwaka huu wa fedha wa

2024/25. Kukamilika kwa miradi hii kutawezesha kuunganisha Mkoa wa Katavi katika Gridi ya Taifa na kuimarisha upatikanaji wa umeme katika Mkoa wa Tabora. Vilevile, Kampuni hiyo imekamilisha utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme vijijini katika mikoa ya Mbeya, Geita, Katavi na Kigoma na ujenzi wa njia za kusambaza umeme kwenye nyumba 3,000 katika eneo la Msomera wilayani Handeni kwa ajili ya familia zinazohamia kutoka Hifadhi ya Ngorongoro.

### b) Kampuni ya Kuzalisha Nguzo za Zege Tanzania (TCPM)

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANESCO ilitoa mtaji kwa Kampuni Tanzu ya TCPM ili kuwezesha ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha nguzo za zege nchini katika Mkoa wa Tabora. Hadi Aprili, 2025 ujenzi wa kiwanda hicho umefikia asilimia 48. Vilevile, TCPM imeingia ubia wa kujenga viwanda vya kuzalisha nguzo za zege na wawekezaji wazawa 11 katika mikoa ya Arusha (1), Morogoro (1), Dodoma (2), Singida (1), Shinyanga (1), Tanga (2), Lindi (1), Njombe (1) na Kigoma (1) ambavyo vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Kati ya viwanda hivyo, kiwanda cha Arumeru Concrete Works kilichopo mkoani Arusha kimeshaanza uzalishaji na usambazaji wa nguzo na kiwanda cha Mikese Concrete Works cha Mkoani Morogoro kinatarajiwa kuanza uzalishaji mwishoni mwa Mei 2025. Pamoja na manufaa mengine, ujenzi wa viwanda hivyo katika maeneo mbalimbali nchini utasaidia kuongeza ajira na kupunguza gharama za usafirishaji wa nguzo. Aidha, hadi Aprili 2025 TCPM imesambaza jumla ya nguzo 34,181 ambazo zimetumika katika miradi mbalimbali ya usafirishaji na usambazaji umeme nchini ikilinganishwa na nguzo 19,368 mwezi Aprili, 2024 sawa na ongezeko la asilimia 76.

### c) Kampuni ya Uendelezaji wa Rasilimali ya Jotoardhi (TGDC)

**71.** ***Mheshimiwa Spika***, Tanzania ni moja ya nchi chache duniani zilizobarikiwa kuwa na rasilimali ya jotoardhi. Rasilimali hii ikiendelezwa itaimarisha upatikanaji wa umeme endelevu unaotokana na vyanzo mbadala na jadidifu. Serikali kupitia TGDC inaendelea na utekelezaji wa miradi ya jotoardhi ili kuzalisha

umeme kupikitia chanzo hiki. Miradi inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na Ngozi (**MW 70**), Kiejo-Mbaka (**MW 60**) na Natron (**MW 60**). Utekelezaji wa miradi hii upo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:

### (i) Mradi wa Ngozi wa MW 70 mkoani Mbeya

**72. *Mheshimiwa Spika*** mradi huu katika awamu ya kwanza unalenga kuzalisha umeme wa **MW 30** kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 144 sawa na takriban Shilingi bilioni 367.9. Utekelezaji wa mradi umefikia hatua ya tatu ambayo ni uhakiki wa rasilimali ya jotoardhi kwa ajili ya kuzalisha umeme. Hatua hii inatekelezwa kupitia progamu ya uchorongaji wa visima vitatu (3) vya uhakiki vitakavyochorongwa kwa urefu wa mita 1,500 kwa kutumia mtambo wa kuchoronga *(drilling rig)* ulionunuliwa na Serikali. Gharama za utekelezaji wa programu ya uchorongaji ni Dola za Marekani milioni 14.7 sawa na takriban Shilingi bilioni 34.4. Hadi Aprili, 2025, TGDC imetekeleza programu ya uchorongaji kama ifuatavyo:

i. Kukamilisha malipo ya awali kwa Mkandarasi (M/s KenGen) ambapo kwa sasa yupo katika maandalizi ya kuanza programu ya uchorongaji;

ii. Kuanza utaratibu wa ufunguzi wa *Letter of Credit* kwa ajili ya mkandarasi itakayofunguliwa katika Benki Kuu ya Tanzania (BOT);

iii. Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya maji na barabara katika eneo la kuchorongea *(drilling platform)* na kambi kwa ajili ya wafanyakazi katika maeneo ya visima namba NZB 3, NB 5 na NB1*;* na iv. Ununuzi wa vifaa na malighafi *(drilling consumables)* ya kuchorongea visima katika mradi wa jotoardhi wa Ngozi umekamilika kwa asilimia 98. Aidha, ununuzi wa watoa huduma mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza programu ya uchorongaji umekamilika.

**(ii) Miradi ya Kiejo-Mbaka (MW 60) - Mbeya na Natron - Arusha**

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa Kiejo - Mbaka ni mradi mwingine unaotekelezwa na Serikali kupitia TGDC. Mradi huu upo kwenye hatua ya uhakiki wa rasilimali ya jotoardhi itakayotekelezwa kupitia programu ya uchorongaji wa visima vinne (4) vya uhakiki. Mradi ukikamilika utakuwa na uwezo wa kuzalisha hadi **MW 60** za umeme. Kwa kuanzia, mradi unatarajiwa kuzalisha **MW 10** zitakazogharimu Dola za Marekani milioni 75. Hadi Aprili 2025, TGDC imekamilisha kazi zifuatazo:

i. Kulipa ada ya ukodishaji wa ardhi *(land lease payments)* kwa wananchi waliopo katika eneo la mradi; na

ii. Kuendelea na taratibu za ununuzi wa Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kundaa na kusimamia programu ya uchorongaji wa visima vinne (4) vya uhakiki wa rasilimali katika mradi wa Kiejo - Mbaka.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, mradi wa Natron uliopo mkoani Arusha upo katika hatua ya utafiti wa kina wa juu ya ardhi *(detailed surface exploration)*. TGDC katika mwaka 2024/25 imeendelea na taratibu za ununuzi wa Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hii.

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo ilifanikisha kufanyika kwa Kongamano la 10 la Jotoardhi Afrika (*10th African Rift Geothermal Conference – ARGeo-C10*) kuanzia tarehe 21 – 27 Oktoba, 2024, Jijini Dar es Salaam. Kongamano hilo lilifunguliwa rasmi tarehe 23 Oktoba, 2024 na Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na lilihudhuriwa na washiriki zaidi ya 800 kutoka nchi 26 duniani. Kauli mbiu ya Kongamano hilo ilikuwa ni "*Kuharakisha Maendeleo ya Rasilimali za Jotoardhi Barani Afrika, Masoko ya Gesi ya Ukaa na Upunguzaji wa Gesi ya Ukaa*". Aidha, kongamano hilo limetangaza kwa kina fursa zilizopo nchini za uendelezaji wa rasilimali ya jotoardhi na pia lilitoa fursa ya kubadilishana uzoefu na nchi nyingine kuhusu

namna bora ya kukabiliana na changamoto mbalimbali katika uendelezaji wa jotoardhi nchini na Barani Afrika kwa ujumla.

### B.1.8 MIRADI YA NISHATI VIJIJINI

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/25 Serikali iliendelea kutekeleza azma yake ya kuhakikisha kuwa huduma ya umeme inafika katika vijiji vyote Tanzania Bara. Napenda kutumia fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imeweza kuvifikia vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara kupitia miradi mbalimbali ya umeme inayosimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hii ya kufikisha miradi ya umeme katika vijiji vyote Tanzania Bara ina manufaa mbalimbali kwa wananchi wa maeneo hayo, ikiwa ni pamoja na kutoa fursa za ajira kupitia shughuli za uzalishaji mali kama vile kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda vidogo na biashara; kuboresha huduma za jamii ikiwemo afya na elimu pamoja na kuimarisha ulinzi na usalama hususan katika maeneo ya mipakani. Aidha, hatua hiyo imeimarisha huduma za mawasiliano ya simu katika maeneo ya vijijini, huduma za kifedha pamoja na kurahisisha upatikanaji wa habari kwa wananchi kupitia runinga, redio na mitandao ya kijamii, na hivyo kufanya mazingira ya vijijini kuwa ya kuvutia na kupunguza ushawishi kwa wananchi kuhamia mijini.

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kukamilisha kazi ya kuunganisha umeme vijijini, Serikali imeendelea kupeleka umeme kwenye vitongoji na kutekeleza miradi mingine ya kupeleka nishati vijijini kama ifuatavyo:

#### a) Mradi wa Kusambaza Umeme katika Vitongoji – *(Hamlet Electrification Project – HEP IIA)*

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kusambaza umeme katika vitongoji 3,060 vya Majimbo 204 ya Uchaguzi nchini sawa na wastani wa vitongoji 15 kwa kila jimbo ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya usambazaji wa umeme. Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia za umeme wa msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 6,118; ufungaji wa transfoma 3,060 na

kuunganisha wateja wa awali 100,947. Hadi Aprili 2025, kazi zilizofanyika ni pamoja na kuwapata Wakandarasi wa kutekeleza mradi, upimaji wa kina na usanifu wa mradi pamoja na uagizaji wa vifaa. Mradi unatarajiwa kukamilika Septemba 2026.

**b) Mradi wa Kupeleka Umeme kwenye Vitongoji katika Mikoa ya Songwe na Kigoma**

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kupeleka umeme katika vitongoji 667 ambapo vitongoji 360 ni vya Mkoa wa Kigoma na vitongoji 307 ni vya Mkoa wa Songwe. Mradi utahusisha ujenzi wa njia za umeme za msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 726.24; njia za umeme wa msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 1,308; ufungaji wa transfoma 653 na kuunganisha wateja wa awali 28,471. Hadi Aprili, 2025, jumla ya vitongoji 341 kati ya 667 sawa na asilimia 51.12 viliunganishiwa umeme na wateja wa awali 3,178 kati ya 28,471 sawa na asilimia 11.16 wameunganishwa na huduma ya umeme.

**c) Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji Awamu ya Pili B (*Hamlet Eletrification Project – HEP IIB*)**

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa mpango mahsusi wa kuunganisha vitongoji 30,702 ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme kati ya vitongoji 64,359 katika mikoa 25 ya Tanzania Bara. Mradi huu utahusisha uunganishaji wa umeme katika vitongoji 9,009 kupitia ujenzi wa miundombinu ya kilomita 13,180.56 za njia za msongo wa kati, kilomita 14,016.50 za msongo mdogo, ufungaji wa transfoma 9,009 za kVA 100 na 200, na uunganishaji wa wateja wa awali 290,300. Hadi Aprili 2025, kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha uhakiki wa vitongoji ambavyo havijafikiwa na umeme, kufanya usanifu wa kina wa mradi na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kutangaza mradi ili kuwapata wakandarasi. Utekelezaji wa mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mahsusi wa Nishati *(National Energy Compact 2025)* unaolenga kutimiza azma ya kuwafikishia umeme watu milioni 300 katika Bara la Afrika ifikapo mwaka 2030.

**d) Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili B (*Densification IIB*)**

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kupeleka umeme kwenye vitongoji 1,686 katika mikoa tisa (9) ambayo ni Arusha, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Morogoro, Njombe na Songwe. Mradi unahusisha ujenzi wa njia za msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 3,860, ufungaji wa transfoma 1,272 na kuunganisha wateja wa awali 95,334. Kufikia Aprili 2025, jumla ya vitongoji 1,294 kati ya 1,686 sawa na asilimia 77 vimeunganishiwa umeme. Aidha, wateja 24,326 kati ya 95,334 sawa na asilimia 26 wamepatiwa huduma ya umeme.

**e) Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili C *(Densification IIC)***

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi huu unahusisha kuunganisha umeme katika vitongoji 1,906 vya mikoa saba (7) ya Manyara, Iringa, Rukwa, Mtwara, Ruvuma, Simiyu na Mara. Mradi unahusisha ujenzi wa kilomita 5,665 za msongo mdogo, kufunga transfoma 1,915 na kuunganisha wateja wa awali 94,179. Kufikia Aprili 2025, jumla ya vitongoji 300 vimeunganishiwa umeme ambapo kilomita 2,790.87 za msongo mdogo zimejengwa, transfoma 407 zimefungwa na wateja wa awali 2,510 wameunganishiwa huduma ya umeme.

**f) Mradi wa Kusambaza Umeme katika VijijiMiji Awamu ya Tatu (*Peri Urban III*)**

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kusambaza umeme katika vijiji-miji, mitaa, na vitongoji 508 ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme katika maeneo ya pembezoni mwa miji katika mikoa nane (8) ya Geita, Kigoma, Kagera, Mbeya, Mtwara, Singida, Tabora na Tanga. Mradi unahusisha ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 379; ujenzi wa njia za umeme wa msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 753; ufungwaji wa transfoma 314 pamoja na kuunganisha wateja wa awali 16,369. Hadi Aprili 2025, maeneo 479 kati ya 508 sawa na asilimia 94 yamefikiwa na umeme na wateja 14,864 kati ya 16,369 sawa na asilimia 91 wameunganishiwa huduma ya umeme.

### g) Mradi wa Kupeleka Umeme kwenye Maeneo ya Migodi Midogo, Viwanda na Maeneo ya Kilimo

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha kupeleka umeme katika maeneo 605 ya wachimbaji wadogo wa madini, maeneo ya kilimo na viwanda Tanzania Bara kupitia ujenzi wa njia za umeme za msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 1,391.69; ujenzi wa njia za umeme wa msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 999.91; ufungaji wa transfoma 606 pamoja na kuunganisha wateja wa awali 12,904. Kufikia Aprili 2025, jumla ya maeneo 504 kati ya 605 yameunganishiwa umeme sawa na asilimia 83 ambapo kilomita 1,300.69 za msongo wa kati na kilomita 883.55 za msongo mdogo zimejengwa, transfoma 499 zimefungwa na wateja wa awali 5,162 wameunganishiwa umeme.

### h) Mradi wa Kupeleka Umeme katika Minara ya Mawasiliano ya Simu

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni hatua ya kuhakikisha wananchi wa vijijini wanakuwa na uhakika wa upatikanaji wa mawasiliano, Serikali ilibuni mradi kwa ajili ya kupeleka umeme kwenye minara ya mawasiliano ya simu iliyopo katika maeneo ya vijijini na vijiji-miji ambao unalenga kupeleka umeme katika minara 754 ya mawasiliano. Kufikia Aprili 2025, kazi zilizofanyika ni pamoja na kufanya tathmini ya namna ya kufikisha umeme katika minara hiyo. Utekelezaji wa kazi hii unaendelea kwa kushirikiana na TANESCO na Mfuko wa Mawasiliano kwa Umma.

### i) Mradi wa Ufungaji wa Mifumo ya Umeme Jua kwenye Makazi Yaliyopo Visiwani na Mbali na Gridi ya Taifa

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ufungaji wa mifumo ipatayo 7,000 ya kutumia nishati ya umeme jua kwenye makazi yaliyo vijijini ambayo hayajafikiwa na Gridi ya Taifa. Utekelezaji wa mradi huu utanufaisha visiwa 118. Aidha, tarehe 8 Aprili 2025, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini ilisaini mikataba na Wakandarasi sita (6) watakaotekeleza mradi huu.

**j) Mradi *wa* Kusambaza Majiko Banifu kwenye Kaya Zilizopo katika Maeneo ya Vijijini na Vijiji-Miji**

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kusambaza majiko banifu 200,000 yaliyotengenezwa kwa teknolojia yenye ubunifu wa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa na hivyo kuwezesha kupunguza uharibifu wa mazingira katika maeneo ya vijijini na vijiji-miji. Hadi Aprili 2025, REA imeshapata kampuni sita (6) za kusambaza majiko banifu 192,038 katika maeneo ya vijijini na vijiji - miji kwenye mikoa 23 kwa bei ya ruzuku ya hadi asilimia 75. Aidha, REA ipo katika hatua za mwisho za kuwapata watoa huduma watakaosambaza majiko hayo katika mikoa miwili (2) iliyobaki ya Njombe na Katavi.

**k) Mpango wa Utoaji Ruzuku kwa Waendelezaji wa Miradi ya Nishati Jadidifu kwa Kutumia Nguvu ya Maji**

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** mpango huu unalenga kuwawezesha waendelezaji wa miradi ya nishati jadidifu kupitia uchangiaji wa gharama za uendelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko madogo ya maji *(mini hydro)* kwa kutoa ruzuku kwa waendelezaji hao. Mpango huu unahusisha kuwezesha ujenzi wa mitambo ya kufua umeme yenye uwezo usiozidi **MW 10**. Kufikia Aprili 2025, waendelezaji wa miradi hii wameendelea kunufaika kupitia mradi huu ambapo REA imesaini mikataba mitatu (3) na Kampuni za Bwelui Company Ltd (**MW 4.7**) Ileje – Songwe; Ninety Two Ltd (**MW 2**) Ngorongoro – Arusha; na SSI Energy Tanzania Ltd (**MW 10**). Aidha, kampuni hizo zimeanza hatua za awali za utekelezaji wa miradi hiyo.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA iliendelea kutoa motisha kwa waendelezaji wa miradi midogo ya kufua umeme kwa kutumia nguvu ya maji ambapo jumla ya miradi minne (4) ilipata ruzuku hiyo ikijumuisha Ijangala (kW 360) - Makete; Lupali (kW 317) - Ludewa; Lugarawa (MW 1.7) – Njombe; na Kilolo/Maguta (MW 2.4) - Kilolo. Kufikia Aprili 2025, mradi wa Ijangala umekamilika; mradi wa Lupali upo katika hatua ya majaribio; mradi wa Lugarawa umefikia asilimia 96; na mradi wa Kilolo umefikia asilimia 93.

**l) Mradi wa Uwezeshaji Upanuzi wa Miundombinu ya Msongo Mdogo *(Distribution Network)* na Ujenzi wa *"Interconnection Line"* kwa Waendelezaji Wadogo**

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kutoa ruzuku kwa waendelezaji wa miradi ya nishati vijijini ili kuwawezesha kujenga miundombinu ya umeme kutoka kwenye vyanzo vya uzalishaji hadi kwenye miundombinu ya TANESCO kwa ajili ya usambazaji umeme wa uhakika hususan katika maeneo husika. Kufikia Aprili 2025, taratibu za kutangaza mradi zinaendelea ili kuwapata waendelezaji miradi wanaokidhi vigezo vya kupata ruzuku hiyo.

**m) Mradi wa Kuwezesha Waendelezaji Binafsi wa Miradi ya Nishati ya Jua katika Maeneo Yaliyo Mbali na Gridi ya Taifa na Visiwani**

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu kupeleka umeme katika maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa na visiwa vya Tanzania Bara kwa kutumia gridi ndogo zinazozalisha umeme unaotokana na nguvu ya jua kwenye maeneo ya visiwa ambavyo havijafikiwa na Gridi ya Taifa. Kufikia Aprili 2025, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuchambua maombi yaliyowasilishwa; kusaini mikataba miwili (2) ya kupeleka umeme visiwani na kuanza utekelezaji wa miradi katika visiwa hivyo kwa kuunganisha wateja 2,168 kati ya 6,018 sawa na asilimia 36.

**n) Mradi wa Kuwezesha Ujenzi wa Vituo Vidogo vya Kusambaza Bidhaa za Mafuta ya Petroli Vijijini**

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kuimarisha huduma ya upatikanaji wa bidhaa ya mafuta ya petroli kwa wananchi katika maeneo ya vijijini kwa kutoa mikopo kwa waendelezaji wa vituo vya mafuta ili kujenga vituo katika maeneo ya vijijini. Katika mradi huu, maeneo yanayolengwa ni yale yaliyopo umbali usiopungua kilomita 7 kutoka barabara za TANROADS na ambayo hayana kituo kingine cha mafuta. Kiwango cha juu cha mkopo kinachoweza kutolewa kwa kila mwendelezaji ni Shilingi 132,600,000 ambacho kinatakiwa kurejeshwa ndani ya miaka saba (7) kwa riba ya asilimia 5.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2025, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kutangaza awamu ya kwanza ya fursa ya mikopo ya ujenzi na uendeshaji wa vituo vya mafuta vijijini ambapo maandiko 11 kati ya 175 yaliyowasilishwa yalikidhi vigezo. Waombaji ambao hawakukidhi vigezo katika awamu ya kwanza walielimishwa kuhusu maeneo yanayohitaji maboresho katika nyaraka walizowasilisha na kupewa fursa ya kuomba tena katika maombi ya awamu ya pili. Aidha, baada ya maboresho ya mwongozo wa mradi, REA ilitangaza awamu ya pili ya fursa ya mkopo ambapo maombi 21 yalipokelewa na baada ya uchambuzi maombi sita (6) yalikidhi vigezo. Kwa sasa, uhakiki wa nyaraka na maeneo yatakayotumika kutekeleza mradi unaendelea. Vilevile, taratibu za kupata Benki itakayosimamia mikopo hiyo zimekamilika. Serikali inaendelea kutoa wito kwa waombaji waliokosa fursa hii katika awamu ya kwanza na ya pili kuboresha maandiko yao pamoja na waombaji wapya kuwasilisha maombi, kwani dirisha la maombi ya mkopo huu bado liko wazi.

### B.1.9 UTEKELEZAJI WA MIKAKATI NA MIPANGO MBALIMBALI YA UENDELEZAJI WA SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na maandalizi na utekelezaji wa Mipango na Mikakati mbalimbali kwa lengo la kuendeleza Sekta ya Nishati kama ifuatavyo:

#### a) Uhuishaji wa Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme wa Mwaka 2020 (*Power System Master Plan Update 2020)*

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliendelea na zoezi la kuhuisha Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme wa Mwaka 2020 ili kuwa na mpango kabambe wa kuendeleza sekta hiyo kwa miaka 25 ijayo. Maboresho hayo yanalenga kuhuisha Mpango uliopo kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi, viwanda, teknolojia na mahitaji ya kijamii.

**b) Mkakati wa Nishati Jadidifu na Mpango wa Utekelezaji *(National Renewable Energy Strategy and Roadmap)***

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha Mkakati wa Nishati Jadidifu na Mpango wa Utekelezaji ambao unatarajiwa kuzinduliwa kabla ya kukamilika kwa Mwaka 2024/25. Mkakati huo pamoja na mambo mengine unalenga kuimarisha uwezo wa uzalishaji wa nishati jadidifu utakaoliwezesha Taifa kuwa na vyanzo mchanganyiko vya umeme unaoendana na mahitaji ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii, ikiwa ni pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uhamasishaji wa utunzaji wa mazingira.

**c) Mkakati wa Matumizi Bora ya Nishati na Uhuishaji wa Mpango Kazi wa Matumizi Bora ya Nishati *(Energy Efficiency Strategy and Update of the Energy Efficiency Action Plan)***

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** mnamo mwezi Desemba, 2024 lilifanyika Kongamano la Kikanda la Nchi za Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) la Matumizi Bora ya Nishati. Katika Kongamano hilo, Serikali ilizindua Mkakati wa Miaka 10 wa Matumizi Bora ya Nishati (2024 – 2034). Kwa sasa Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mkakati huo katika shughuli mbalimbali zikiwemo usafirishaji kwa kutumia treni ya umeme (SGR), vyombo vya moto vinavyotumia gesi asilia (*Compressed Natural Gas – CNG*) na umeme. Aidha, Mkakati huo unahamasisha matumizi ya majiko ya kupikia yenye ufanisi yanayotumia umeme na gesi. Jitihada hizi zinasaidia kufikia malengo ya matumizi bora ya nishati ikiwemo kutunza mazingira na kuwa na nishati ya uhakika (*energy security*) nchini.

**d) Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kupeleka Nishati Vijijini *(Rural Energy Master Plan-REMP)***

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA imeendelea na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Master Plan-REMP*) ambapo vijiji vyote 12,318 Tanzania Bara vimefikiwa na nishati ya umeme na asilimia 52.3 ya vitongoji vyote

vimeunganishwa na umeme. Aidha, utekelezaji wa Mpango huu utawezesha vitongoji vyote vilivyosalia kuunganishiwa umeme, ujenzi wa vituo vya mafuta maeneo ya vijijini, upatikanaji wa nishati safi ya kupikia pamoja na nishati nyingine katika maeneo hayo.

**e) Ushiriki katika Mkutano wa 29 wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP29)**

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2024 Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliongoza ujumbe wa Tanzania katika Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (*COP29)* uliofanyika tarehe 11 - 22 Novemba, 2024, katika Mji wa Baku nchini Azerbaijan. Katika Mkutano huo pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Makamu wa Rais aliongoza Mkutano wa Kushughulikia Changamoto za Nishati Safi ya Kupikia Barani Afrika (*Addressing Clean Cooking Challenges in Africa: A Call for African Leadership*). Lengo la Mkutano huo lilikuwa kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali fedha na teknolojia ili kuharakisha utekelezaji wa Agenda ya nishati safi ya kupikia Barani Afrika. Vilevile, Serikali ilitumia Mkutano huo kama fursa ya kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali fedha na ushirikiano na taasisi mbalimbali za kimataifa ili kusaidia utekelezaji wa miradi ya nishati safi na rafiki kwa mazingira ikiwemo nishati jadidifu na nishati safi ya kupikia hapa nchini.

**f) Uratibu wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati *(Africa Heads of State Energy Summit)***

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliandaa na kushiriki katika Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika (*African Heads of States Energy Summit*) uliofanyika tarehe 27-28 Januari, 2025 Jijini Dar es Salaam. Mkutano huo uliwakutanisha Wakuu wa Nchi na Serikali za Afrika, Wakuu wa Taasisi za Fedha za Kimataifa pamoja na Wadau wengine wa Maendeleo kwa lengo la kuweka mikakati ya namna bora ya kuwafikishia umeme watu milioni 300 katika Bara la Afrika ifikapo mwaka 2030. Mkutano huo uliwezesha kuzinduliwa kwa Mipango Mahsusi ya Kitaifa ya Nishati (*National*

*Energy Compacts 2025-2030*) ya Mataifa 12 ya Afrika, ikiwemo Tanzania.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango Mahsusi wa Kitaifa wa Nishati wa Tanzania (*National Energy Compact 2025-2030*) uliozinduliwa katika Mkutano huo ulilenga kuongeza upatikanaji wa umeme kutoka asilimia 78.4 ya sasa hadi asilimia 100 ifikapo mwaka 2030; kuongeza uunganishaji wa umeme nchini kutoka asilimia 46 hadi asilimia 75; kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika uzalishaji wa umeme kutoka asilimia 61.8 hadi asilimia 75; kiwango cha matumizi ya nishati safi ya kupikia kutoka asilimia 6.9 ya mwaka 2021 kufikia asilimia 75; na mchango wa sekta binafsi katika Sekta ya Nishati kwa kiasi cha Dola za Marekani bilioni 4.39 sawa na takriban Shilingi trilioni 11.73.

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakuu wa Nchi za Afrika walisaini Azimio la utekelezaji wa Mpango huo (*Dar es Salaam Declaration by the African Heads of States Energy Summit*), ikiwa ni makubaliano ya pamoja ya Wakuu hao ya kuunganisha nguvu na jitihada za pamoja za kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha zitakazowezesha upatikanaji wa huduma ya umeme wa uhakika, endelevu na gharama nafuu kwa watu milioni 300 katika Bara la Afrika ifikapo 2030. Nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu, kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa Mwenyeji wa Mkutano wa Nishati Afrika (*Mission 300*) kwa Mwaka 2025. Aidha, Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na taasisi zilizo chini yake inakamilisha uandaaji wa Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Nishati (*National Energy Compact)* ambao utekelezaji wake utaanza Mwaka 2025/26.

### g) Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia

**104.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali chini ya uratibu wa Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, inaendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 - 2034) uliozinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe

08 Mei 2024. Lengo la Mkakati huo ni kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034. Ili kufikia lengo hilo, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea na utekelezaji wa Mkakati huo kama ifuatavyo:

**(i) Utoaji wa Elimu Kuhusu Umuhimu wa Nishati Safi ya Kupikia**

**105.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuhamasisha wananchi katika maeneo ya mijini na vijijini kutumia nishati safi ya kupikia. Uhamasishaji huo umefanyika kupitia vyombo vya habari ikiwemo redio na televisheni, mitandao ya kijamii, makongamano, maonesho, warsha na mikutano ya hadhara. Aidha, ili kuimarisha utoaji wa elimu kwa wananchi, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inakamilisha uandaaji wa Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano wa Nishati Safi ya Kupikia *(National Clean Cooking Communication Strategy)* ambao unatarajiwa kuzinduliwa mwezi Mei, 2025.

**106.** ***Mheshimiwa Spika***, matumizi ya nishati safi katika kupikia pamoja na mambo mengine, yanajumuisha nishati ya umeme ambapo Serikali kupitia TANESCO imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu faida za kutumia umeme kama nishati ya kupikia. Faida zinazopatikana kutokana na matumizi ya umeme ni pamoja na kupunguza gharama, kuokoa muda, kutunza mazingira na kuepukana na athari za kiafya zinazotokana na matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia. Aidha, Serikali inaendelea kuwezesha upatikanaji wa vifaa vinavyotumia kiasi kidogo cha umeme pamoja na kuandaa viwango vyenye ufanisi wa ubora wa vifaa mbalimbali vinavyotumia umeme kupikia *(Minimum Energy Performance Standards for Cooking Appliances)*.

**(ii) Marekebisho ya Sheria ya Nishati Vijijini ili Kuwezesha Matumizi Endelevu ya Nishati safi ya Kupikia**

**107.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha uwepo wa matumizi endelevu ya nishati safi ya kupikia nchini, Serikali inakusudia kufanya marekebisho ya Sheria ya Nishati Vijijini Na. 8 ya Mwaka

2005 iliyoanzisha Bodi, Wakala na Mfuko wa Nishati Vijijini. Marekebisho hayo yanatokana na hitaji la kuwa na Mfuko Maalum wa Kitaifa kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji na uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi ya kupikia katika maeneo yote ya mijini na vijijini ikiwa ni utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 – 2034). Kwa sasa, Wizara kwa kushirikiana na wadau, inaendelea na taratibu za uandaaji wa nyaraka za Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hiyo katika Baraza la Mawaziri kwa uamuzi.

**(iii) Mpango wa Kuwezesha Taasisi Kutumia Nishati Safi ya Kupikia**

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA imetoa ruzuku ya ujenzi wa miundombinu ya nishati safi ya kupikia katika Taasisi za Umma na binafsi ambazo zinahudumia zaidi ya watu 100 kwa siku, ikiwa ni utekelezaji wa mpango wa uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi ya kupikia katika Taasisi hizo. Kufikia Aprili 2025, Taasisi zilizonufaika na mpango huo ni pamoja na Jeshi la Magereza Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Kupitia mpango huo, kambi za JKT na Magereza zimeanza kutumia nishati safi ya kupikia. Aidha, Shule za Sekondari zipatazo 100 zimeendelea kufungiwa mifumo mbalimbali ya nishati safi ya kupikia na taratibu za kuzifikia shule nyingine nchini zinaendelea. ***Kielelezo Na. 5*** kinaonesha idadi ya mifumo ya nishati safi ya kupikia inayofungwa katika Taasisi za Magereza, Kambi za JKT na Shule za Sekondari.

***Kielelezo Na. 5*: Idadi ya Mifumo ya Nishati Safi ya Kupikia Inayofungwa katika Taasisi za Magereza, Kambi za JKT na Shule za Sekondari**

| Jina la Taasisi | Aina ya Mifumo Inayofungwa | | | |
|---|---|---|---|---|
| | LPG | Bayogesi | Gesi Asilia | Mkaa Mbadala |
| Jeshi la Magereza | 64 | 126 | 1 | 61 |
| Jeshi la Kujenga Taifa | 180 | 9 | - | 60 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (JKT) | | | | |
| Shule za Sekondari | 43 | 9 | - | 53 |
| **Jumla** | **287** | **144** | **1** | **174** |

*Chanzo:* ***REA***

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji ya Maendeleo (UNCDF) kupitia ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU) inaendelea kuwezesha uwekaji wa miundombinu ya nishati safi ya kupikia katika taasisi za elimu zikiwemo shule zinazolisha zaidi ya watu 100 kwa siku. Katika awamu ya kwanza ya programu hii mikoa iliyonufaika ni Mwanza (8), Dodoma (1) na Morogoro (4). Awamu ya pili inayotarajiwa kuanza Mei, 2025 itahusisha shule 58 katika mikoa ya Pwani (15), Dar es Salaam (40) na Mwanza (3).

### (ix) Usambazaji wa Mitungi ya Gesi ya Kupikia (LPG)

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA inaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi katika programu ya usambazaji wa mitungi 452,445 nchini ambapo kila wilaya itapata mitungi 3,255. Kupitia programu hiyo, REA imesaini mikataba na wasambazaji wa mitungi ya LPG ambao ni Kampuni za Oryx, Lake Oil, Manjis pamoja na Taifa Gas ili wananchi waweze kununua mitungi hiyo kwa bei ya punguzo la hadi asilimia 50. Utekelezaji wa programu hiyo unaendelea ambapo kufikia Aprili 2025 jumla ya mitungi 154,224 ilikuwa imesambazwa. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Septemba, 2025.

**111.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo inaendelea kufanya Utafiti Msingi *(Baseline Survey)* ambao pamoja na mambo mengine utatoa picha halisi ya mahitaji ya nishati safi ya kupikia kwa kuzingatia eneo husika. Vilevile, utafiti huo utaainisha mapendekezo kuhusu namna bora ya matumizi endelevu ya nishati safi ya kupikia kwa wananchi hususan katika maeneo ya vijijini. Aidha, Serikali kupitia REA imeendelea kutoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya teknolojia zinazosambazwa hususan katika mitungi ya LPG ili kutatua changamoto zilizopo.

## B.1.10 USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UMEME

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeweka sera, mikakati na taratibu za kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika uzalishaji, usafirishaji na uzambazaji wa umeme nchini. Kwa sasa takriban **MW 338.10** zinazalishwa na wazalishaji binafsi ambapo kati ya hizo, **MW 307.98** zinatumika kwa matumizi binafsi na **MW 30.12** zinanunuliwa na TANESCO na kuingizwa katika Gridi ya Taifa kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Na. 6***. Ushiriki huu wa Sekta Binafsi unachangia kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini. Aidha, wazalishaji wadogo 38 wapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme kwa lengo la kuiuzia TANESCO yenye uwezo wa kuchangia jumla ya **MW 192.93** kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Na. 7***.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA imeendelea kushirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini ikiwemo miradi ya kupeleka umeme katika vitongoji, usambazaji wa nishati safi ya kupikia na uendelezaji wa miradi midogo iliyopo nje ya Gridi ya Taifa. Kuanzia Mwaka 2020/21 hadi Aprili 2025, jumla ya kampuni binafsi 85 zimeshiriki katika utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini ambapo kati ya hizo, kampuni 71 ni za wazawa na kampuni 14 za kigeni. Aidha, sekta binafsi imeshiriki katika kusambaza mitungi ya LPG na majiko banifu katika mikoa mbalimbali nchini. Vilevile, kampuni binafsi tatu (3) ambazo ni Bwelui Company Ltd (**MW 4.7**), Ninety Two Ltd (**MW 2**) na SSI Energy Tanzania Ltd (**MW 10**) zimeingia mikataba na Serikali kupitia REA kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme katika maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa ikiwemo visiwa vya Tanzania Bara.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme imezalisha ajira 31,148. Ajira hizo zilihusisha makundi mbalimbali katika jamii ikiwemo wanawake (4,915), wanaume (26,179) na walemavu (54). Kati ya ajira hizo, miradi ya uzalishaji iliajiri watu 4,018 (wanawake 829, wanaume 3,187 na walemavu 2); usafirishaji iliajiri watu 11,278 (wanawake 2,066, wanaume 9,160 na walemavu 52); na

usambazaji umeme watu 1,104 (wanawake 115 na wanaume 989). Aidha, kati ya ajira zilizopatikana katika miradi ya umeme, ajira 4,307 ni za kudumu na 26,841 ni za muda mfupi.

### B.2 SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

**115.** ***Mheshimiwa Spika*** katika Mwaka 2024/25 Serikali kupitia Wizara ya Nishati, iliendelea kusimamia na kuendeleza Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia katika maeneo ya utafutaji, uendelezaji, uzalishaji, uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa bidhaa za mafuta na gesi, kwa lengo la kuhakikisha mchango wa Sekta hii katika Pato la Taifa unaendelea kuimarika.

### B.2.1: MIRADI YA UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI

#### a) Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini

**116.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi wa utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini unatekelezwa katika kina kifupi cha bahari kilichopo Kusini Mashariki mwa Tanzania. Kufikia Aprili 2025, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuendelea na majadiliano na wawekezaji walioonesha nia ya kuwekeza katika Kitalu hiki ambao ni Kampuni ya Maurel & Prom (M&P) kutoka Ufaransa na First E&P kutoka Nigeria ambao kwa sasa wanafanya tathmini ya kiufundi ya taarifa za utafiti zilizopo kwenye eneo la mradi kabla ya kuanza majadiliano ya kibiashara.

#### b) Kitalu cha Eyasi– Wembere

**117.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unalenga kufanya shughuli za utafutaji wa mafuta katika kitalu cha Eyasi – Wembere kilichopo kwenye Bonde la Ufa la Afrika Mashariki, Kaskazini Mashariki mwa Tanzania. Kufikia Aprili 2025, shughuli zilizotekelezwa katika kitalu hiki ni pamoja na kuendelea na uchukuaji wa taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D zenye urefu wa kilomita 1,100 ambapo kilomita 430 zimekamilika; ulipaji fidia kwa wananchi 544; upimaji wa umri wa miamba; kuendelea na taratibu za kumpata mkandarasi wa kuchakata na kutafsiri taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D *(Infill*

*2D Seismic survey – Phase II)*; na kukamilisha kazi ya kutafsiri taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D zenye urefu wa kilometa 260.

### c) Kitalu cha Songo Songo Magharibi

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika kitalu cha Songo Songo Magharibi, kilichopo mkabala na kitalu kinachozalisha gesi asilia cha Songo Songo. Kufikia Aprili 2025, TPDC imekamilisha maandalizi ya mpango wa uchukuaji wa taarifa za mitetemo za mfumo wa 3D unaojumuisha uchukuaji wa taarifa za kijiolojia, kijiofizikia na kimazingira.

### d) Vitalu Na. 4/1B na 4/1C

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vitalu Na. 4/1B na 4/1C vinapatikana katika kina kirefu cha bahari Kusini mwa Tanzania. Hadi Aprili 2025, Serikali kupitia TPDC imeendelea kutafuta mwekezaji wa kimkakati *(strategic partner)* kwa kuzingatia uwezo wa kiufundi na fedha. Pamoja na mazungumzo ya awali na kampuni za CNOOC kutoka China na kampuni ya Mafuta ya Taifa ya Msumbiji – ENH ambazo zimeonesha nia ya kushirikiana na TPDC ili kuharakisha upatikanaji wa mwekezaji, vitalu hivi vinatarajiwa kunadiwa katika Duru ya Tano ya kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia inayotarajiwa kuzinduliwa mwezi Mei 2025.

### e) Kitalu cha Lindi - Mtwara

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika kitalu cha Lindi - Mtwara ili kuongeza uzalishaji gesi hiyo nchini. Kufikia Aprili 2025, Serikali kupitia TPDC imekamilisha tathmini ya awali na kubaini uwepo wa mashapo ambayo yanahitaji kufanyiwa utafiti zaidi ili kutambua kiasi halisi cha gesi iliyopo. Kwa sasa Serikali inaandaa mpango wa uchukuaji wa taarifa za mitetemo za mfumo wa 3D katika eneo la kilomita za mraba 780 ili kubaini maeneo ya kuchoronga visima vya utafutaji.

### B.2.2: MIRADI YA UZALISHAJI NA UENDELEZAJI WA GESI ASILIA

#### a) Kitalu cha Uzalishaji wa Gesi Asilia cha Mnazi Bay

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kitalu cha Mnazi Bay kilichopo mkoani Mtwara kimeendelea kuzalisha gesi asilia ambapo kufikia Aprili 2025, jumla ya gesi iliyozalishwa katika kitalu hiki ilikuwa futi za ujazo bilioni 25.51 ambao ulizingatia mahitaji katika kipindi husika. Pamoja na uzalishaji huo, shughuli nyingine zilizotekelezwa katika kitalu hiki ni pamoja na ukarabati wa miundombinu ya uzalishaji wa gesi asilia ikiwemo ubadilishaji wa *flowlines* kutoka kisima cha MB-2 hadi MB-3 na kutoka kisima cha MB-4 hadi MB-3; ubadilishaji wa *Christmas Tree* kwa visima vya MB-2, MB-3, MB-4 na MS-1X; uchukuaji wa taarifa za ubora wa kisima (*caliper logging*) kwa visima vya MB-2, MB3 na MS-1X; na kuendelea na maandalizi ya uchorongaji wa visima viwili vya uzalishaji vinavyotarajiwa kuongeza kiasi cha futi za ujazo milioni 50 kwa siku. Uchorongaji wa visima hivyo unatarajiwa kufanyika kuanzia mwezi Septemba, 2025.

#### b) Kitalu cha Uzalishaji wa Gesi Asilia cha Songo Songo

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kitalu cha Songo Songo kilichopo kisiwa cha Songo Songo mkoani Lindi kimeendelea kuzalisha gesi asilia ambapo kufikia Aprili 2025, jumla ya gesi iliyozalishwa katika kitalu hiki ilikuwa futi za ujazo bilioni 21.93 kulingana na mahitaji katika kipindi hicho. Aidha, shughuli nyingine zilizotekelezwa katika kitalu hiki ni pamoja na uchukuaji wa taarifa za uzalishaji *(production logging)* katika visima vya SS3, SS5 na SS10 ili kubaini uwezo wa uzalishaji katika visima hivyo na kuweza kujipanga na hali ya uzalishaji kwa kuzingatia mgandamizo wa gesi kadiri uzalishaji unavyoendelea.

#### c) Kitalu cha Ruvuma (Eneo la Ntorya)

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa uendelezaji wa gesi asilia iliyogunduliwa katika eneo la Ntorya unahusisha uchorongaji na ukarabati wa visima vya uzalishaji pamoja na ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia hadi eneo la Madimba kwa ajili ya

uchakataji. Hadi Aprili 2025, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kutolewa kwa leseni ya uendelezaji wa kitalu; kukamilika kwa ulipaji wa fidia na utwaaji wa ardhi kwa wananchi waliopisha mradi; kukamilika kwa taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa bomba; na kukamilika kwa maandalizi ya uchorongaji wa kisima cha utafiti cha Chikumbi-1. Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza uzalishaji wa gesi asilia kuanzia futi za ujazo milioni 40 hadi 60 kwa siku hadi futi za ujazo milioni 140 kwa siku.

**d) Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia Kuwa Kimiminika (Liquefied Natural Gas – LNG)**

**124.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea na maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa LNG utakaohusisha uchakataji na usindikaji wa gesi asilia iliyogunduliwa katika Vitalu Na. 1, 2 na 4 katika kina kirefu cha bahari. Hadi Aprili 2025, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuendelea na hatua za mwisho za majadiliano na wawekezaji katika vitalu husika. Aidha, Serikali imeendelea kutoa elimu kuhusu manufaa ya mradi kwa makundi mbalimbali ya kijamii pamoja na utekelezaji wa miradi ya uwajibikaji kwa jamii ikiwemo ujenzi wa Shule ya Msingi Likong'o iliyopo Manispaa ya Lindi inayojengwa na TPDC kwa kushirikiana na Kampuni za Shell na Equinor ambayo imefikia asilimia 10 ya ujenzi.

**B.2.3: MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI WA GESI ASILIA**


**a) Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani**

**125.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahusu ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kwa njia ya mabomba pamoja na vituo vya kujazia gesi asilia *(CNG)* kwenye vyombo vya moto. Hadi Aprili 2025, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa Kituo Mama cha CNG (*CNG Mother Station*) katika eneo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na kuendelea kukamilisha vituo vidogo viwili vya CNG *(CNG receiving and storage stations)*

vinavyojengwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na Kiwanda cha Madawa cha Kairuki kilichopo eneo la viwanda Zegereni Kibaha, Pwani. Vilevile, usanifu wa kina wa Kihandisi *(Detailed Engineering Design)* kwa ajili ya kuunganisha gesi asilia katika migahawa 12 katika eneo la Mlimani City pamoja na maabara na migahawa mitatu (3) katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) umekamilika.

**126.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili, 2025 jumla ya vituo 9 vya CNG vimekamilika na vinatoa huduma, ikilinganishwa na vituo viwili (2) Mwaka 2020/21. Mwelekeo wa Serikali ni kuwa na vituo 20 ifikapo Juni, 2026. Aidha, matumizi ya CNG katika vyombo vya moto yameendelea kuongezeka nchini kama inavyoonekana katika ***Kielelezo Na. 6.*** Kuimarika kwa matumizi ya CNG katika vyombo vya moto hususan magari na bajaji kumekuwa na manufaa makubwa, ikiwemo kuwapa wananchi unafuu wa gharama katika uendeshaji wa vyombo hivyo pamoja na kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni katika uagizaji wa mafuta.

***Kielelezo Na. 6:* Mwenendo wa Matumizi ya CNG kwenye Vyombo vya Moto kuanzia Mwaka 2021 hadi 2024**




*Chanzo:* ***EWURA***

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC inaendelea na taratibu za ununuzi wa vituo sita (6) vya CNG vinavyohamishika *(Mobile CNG filling stations)* ambapo vituo vitatu (3) vitakuwa katika Jiji la Dar es Salaam, kimoja (1) Morogoro na viwili (2) Dodoma. Kwa sasa TPDC inakamilisha taratibu za upatikanaji wa maeneo yatakayosimikwa vituo hivyo. Vilevile, Serikali imeendelea kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika shughuli za mafuta na gesi asilia ambapo kampuni 61 zimeruhusiwa kufanya biashara ya CNG nchini. Hatua hii itaongeza upatikanaji wa CNG kwa ajili ya vyombo vya moto katika mikoa mbalimbali nchini.

**b) Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Kujaza Gesi Asilia *(Compressed Natural GasCNG)* katika Bohari za Dar es Salaam na Dodoma**

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) inafanya maandalizi ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa vituo vya CNG katika bohari za Dar es Salaam na Dodoma ambapo GPSA itanunua magari maalumu ya kusafirisha CNG kutoka katika vituo vinavyoshindilia gesi (*mother CNG stations*) ikiwemo kituo kikuu cha TPDC kilichopo katika eneo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kupelekwa kwenye vituo hivyo. GPSA imeshapata idhini ya kufanya biashara ya CNG kutoka TPDC na kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na kutafuta wazabuni na wazalishaji wa vifaa vya utekelezaji wa mradi huo.

**c) Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Lindi na Mtwara**

**129.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kwa njia ya mabomba katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Aidha, mwishoni mwa mwezi Februari 2025, Mkandarasi alianza kazi ya ujenzi wa miundombinu ya kuunganisha kaya 451 katika eneo la Mnazi Mmoja mkoani Lindi ambapo ujenzi umefikia asilimia 42 na utakamilika mwezi Juni, 2025. Kukamilika kwa mradi huu kutachochea kasi ya matumizi ya nishati safi ya kupikia majumbani kupitia gesi asilia.

**d) Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Gesi Asilia kuanzia Kinyerezi - Dar es Salaam hadi Chalinze – Pwani**

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ipo katika maandalizi ya ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Kinyerezi - Dar es Salaam hadi Chalinze - Pwani ambapo kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kufanya mapitio ya tafiti mbalimbali za masoko ili kujenga bomba la gesi asilia la kusambaza nishati hiyo kwa viwanda vilivyopo katika ukanda wa kongani za viwanda maeneo ya Kibaha hadi Chalinze. Kwa sasa Mshauri Mwelekezi anaendelea na kazi ya utambuzi wa mkuza wa kupitisha bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Dar es Salaam hadi Chalinze ambapo baada ya kukamilika kwa kazi hiyo ataendelea na usanifu wa michoro ya kihandisi wa mradi pamoja na kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira, Uchumi na Kijamii.

**e) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia Kutoka Tanzania hadi Uganda**

**131.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahusu ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Tanzania hadi Uganda na kusambaza gesi hiyo katika maeneo yatakayopitiwa na bomba hilo. Kufikia Aprili 2025, Mshauri Mwelekezi wa kufanya kazi ya Upembuzi Yakinifu amepatikana ambapo kwa sasa Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukubaliana na Mshauri Mwelekezi namna bora ya utekelezaji wa kazi hiyo.

**B.2.4: MIRADI YA KUHIFADHI, KUSAFIRISHA NA BIASHARA YA MAFUTA**

**a) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima – Uganda hadi Tanga – Tanzania *(East African Crude* Oil Pipeline – EACOP)**

**132.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Uganda kwa kushirikiana na wawekezaji zimeendelea na utekelezaji wa mradi huu ambapo kufikia Aprili 2025, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuendelea kukamilisha ujenzi wa makambi na vituo vya kuhifadhia mabomba; kukamilika

na kuanza kazi kwa karakana ya kuweka mfumo wa joto kwenye mabomba *(Thermal Insulation System (TIS) Plant);* kuwasili nchini kwa mabomba yenye uwezo wa kujenga kilomita 900; kuwekwa mfumo wa kuhifadhi joto katika mabomba yenye urefu wa kilomita 443.66; kupelekwa kwenye maeneo ya mradi kwa mabomba yenye mfumo wa kuhifadhi joto yenye uwezo wa kujenga kilomita 364.3; kuendelea kwa ujenzi wa matenki manne (4) katika eneo la Chongoleani ambao umefikia asilimia 74.2; na ujenzi wa jeti ya kupakilia mafuta umefikia asilimia 69.1. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia asilimia 55.

**b) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi Kutoka Tanzania Hadi Zambia**

**133.** ***Mheshimiwa spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta safi kutoka Dar es Salaam - Tanzania hadi Ndola – Zambia lenye urefu wa kilomita 1,710. Lengo la mradi ni kukidhi mahitaji ya sasa na baadae ya usafirishaji wa bidhaa za mafuta kwa nchi za Tanzania na Zambia. Bomba hili litakuwa na uwezo wa kusafirisha tani zisizopungua milioni 5 kwa mwaka. Aidha, bomba hilo linatarajiwa kuwa na matoleo matano (5) ambapo matatu (3) yatakuwa upande wa Tanzania (Morogoro, Makambako na Songwe) na mawili (2) upande wa Zambia (Kalonje na Ndola). Hadi Aprili 2025, kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu na Mshauri Mwelekezi kuwasilisha ripoti ya kazi hiyo kwa ajili ya mapitio. Kwa sasa Timu ya Wataalamu inaendelea na mapitio ya ripoti hiyo ili kuweza kushauri namna bora ya utekelezaji wa mradi kwa kuzingatia muda na gharama za mradi huo.

**c) Ushiriki wa TPDC katika Biashara ya Mafuta kupitia Mfumo wa Uagizaji kwa Pamoja *(Bulk Procurement System* - BPS)**

**134.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta nchini, Serikali kupitia TPDC imekuwa ikishiriki katika zabuni za uagizaji wa bidhaa za mafuta kupitia Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (BPS). Aidha, Serikali imeendelea kuijengea uwezo TPDC na hivyo kuweza kushiriki katika zabuni za uletaji wa mafuta nchini kila mwezi. Hadi Aprili 2025, TPDC

imeweza kuingiza nchini tani 308,713 za mafuta ya dizeli zenye thamani ya Shilingi bilioni 591.19.

**d) Mradi wa Uanzishwaji wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta *(Strategic Petroleum Reserve - SPR)***

**135.** ***Mheshimiwa Spika***, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuendelea na uratibu wa uanzishwaji wa hifadhi ya kimkakati ya mafuta (SPR) katika maeneo mbalimbali nchini kwa kuzingatia mahitaji ya nchi na mazingira yaliyopo sasa, pasipo kuongeza gharama za mafuta na kuathiri usalama wa mafuta nchini. Timu ya wataalamu kutoka taasisi mbalimbali za Serikali imekamilisha kazi ya kuandaa andiko la awali kuhusu uanzishwaji wa SPR ambapo hatua inayofuata ni kupata maoni ya wadau mbalimbali kuhusu Andiko hilo.

**e) Ukarabati wa Tenki Namba 8**

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zinazoendelea ni pamoja na kukamilisha tathmini ya athari kwa mazingira na jamii na usanifu wa tenki pamoja na kuanza kazi ya ukarabati wa tenki hilo kwa ajili ya hifadhi ya mafuta. Kufikia Aprili 2025, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kupatikana kwa Mshauri Mwelekezi wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira; kupatikana kwa Mshauri Mwelekezi wa usanifu wa ukarabati wa tenki ambaye amekabidhiwa eneo la mradi na kazi alizotekeleza ni kukusanya taarifa za awali za hali ya tenki ili kushauri namna bora ya kutekeleza mradi.

**f) Ukarabati wa Vituo Vitatu (3) vya Musoma, Tarime (Mara) na Segera (Tanga) pamoja na Kujenga Kituo Kipya Kimoja (1) Makuyuni (Arusha)**

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua za awali za utekelezaji wa mradi huu zimeanza ambapo kwa sasa Mshauri Mwelekezi amewasilisha taarifa za awali (*brief report)* ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA) kwa kituo cha Makuyuni na Ukaguzi wa Mazingira (*Environmental Audit*) kwa vituo vya Segera, Musoma na Tarime. Taarifa hizo zinafanyiwa maboresho kwa kuzingatia maoni na

ushauri uliotolewa na NEMC ili kuwezesha upatikanaji wa vibali vya mazingira kwa ajili ya kuendelea na ukarabati na ujenzi wa vituo hivyo.

### B.2.5: MRADI WA KUJENGA UWEZO WA KUSIMAMIA NA KUENDELEZA RASILIMALI ZA NDANI NA UTAWALA WA RASILIMALI ZA ASILI TANZANIA

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umeendelea kutekelezwa ambapo kufikia Aprili 2025, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuwezesha mapitio ya Mkataba Kifani wa Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (*Model Production Sharing Agreement - MPSA 2013*) utakaotumika katika Duru ya Tano ya kunadi vitalu vilivyo wazi ili kuvutia uwekezaji katika utafutaji wa mafuta na gesi; kuwezesha utafiti na maandalizi ya Mkakati wa Uendelezaji na Uhamasishaji wa Matumizi ya Gesi ya Mitungi (LPG) na Gesi Iliyoshindiliwa (CNG); kuwezesha uanzishaji wa vituo vya kujenga uwezo kwa Wananchi kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC); na kuwajengea uwezo wataalam wa Wizara ya Nishati, PURA, TPDC, EWURA na Watumiaji wa Mfumo wa Uondoshaji Shehena Mipakani.

### B.2.6: UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMPUNI TANZU ZA TPDC (TANOIL na GASCO)

#### (i) TANOIL Investments Limited

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** TPDC kupitia kampuni yake tanzu ya TANOIL Investments Limited inaendelea kushiriki katika biashara ya kununua na kuuza mafuta kwa jumla. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2024 hadi Machi 2025, TANOIL iliagiza na kuuza lita milioni 22.2 za mafuta ya dizeli na lita milioni 2.4 za mafuta ya petroli. Aidha, vituo vya mafuta vya TANOIL vilivyopo Geita na Singida vimeanza uuzaji wa mafuta baada ya kupata wabia wa sekta binafsi wa kuviendesha. Vilevile, TANOIL imeendelea na taratibu za kutafuta Washauri Waelekezi watakaoshauri namna bora ya kuingia kwenye biashara ya LPG na vilainishi vya vyombo vya moto na mitambo. Tathmini ya zabuni za kuwapata Washauri hao inaendelea na imefikia hatua ya wazabuni kuwasilisha *Request for*

*Proposal*. Ushiriki wa TANOIL katika biashara ya LPG pamoja na mambo mengine, utaongeza uhakika wa upatikanaji wa nishati hiyo na kuchochea matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini.

**(ii) Gas Company (GASCO)**

**140. *Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya GASCO imeendelea na uendeshaji na matengenezo ya miundombinu ya gesi asilia nchini ambapo hadi Aprili 2025, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuendelea na uchakataji wa gesi asilia ambapo wastani wa futi za ujazo milioni 88.17 kwa siku zilichakatwa kutoka kitalu cha Mnazi Bay na wastani wa futi za ujazo milioni 21.38 kwa siku zilichakatwa kutoka kitalu cha Songo Songo; na kufanya matengenezo mbalimbali yaliyopangwa na ya dharura ambayo yameongeza ufanisi na kufanya miundombinu yote ya gesi asilia kuwa na utayari (*reliability and availability*) wa asilimia 99.37 wa kufikisha gesi asilia kwa wateja wake. Aidha, katika kipindi husika, GASCO imeendelea kushiriki kwenye zabuni za ujenzi wa miundombinu ya mafuta na gesi asilia na kufanikiwa kushinda zabuni zenye thamani ya Shilingi bilioni 4.85 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kuunganisha gesi asilia katika vituo vitano (5) vya CNG na kuunganisha miundombinu ya gesi asilia katika majiko ya kupikia eneo la biashara la Mlimani City na DUCE mkoani Dar es Salaam.

### B.2.7: URATIBU NA USHIRIKI KATIKA KONGAMANO LA 11 LA PETROLI LA NCHI WANACHAMA WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI LA MWAKA 2025 (EAPCE'25)

**141. Mheshimiwa spika**, mnamo tarehe 5 – 7 Machi, 2025 Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Kongamano la 11 la Petroli la Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki lililoambatana na maonesho ya shughuli za petroli zinazotekelezwa na wadau mbalimbali wa Sekta ya Mafuta na Gesi. Kauli mbiu ya Kongamano hilo ilikuwa *"Kufungua Fursa za Uwekezaji Katika Nishati: Mchango wa Rasilimali za Mafuta Katika Kupata Nishati ya Uhakika kwa Maendeleo Endelevu ya Afrika Mashariki"*. Kongamano hilo lilihudhuriwa na washiriki zaidi ya 1,000 kutoka

nchi mbalimbali duniani ambapo nchi yetu iliweza kutangaza fursa za uwekezaji katika mnyororo wa thamani wa mafuta na gesi asilia ikiwemo CNG na kutangaza nia ya Serikali ya kunadi vitalu 26 vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia kupitia Duru ya Tano (5) inayotarajiwa kufanyika mwezi Mei, 2025.

### B.2.8: USIMAMIZI NA UDHIBITI WA SEKTA YA NISHATI KUPITIA PURA NA EWURA

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) zimeendelea kutekeleza majukumu ya usimamizi na udhibiti wa Sekta ya Nishati kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora zinazotokana na utekelezaji wa majukumu ya Sekta.

### B.2.8.1: UDHIBITI WA SHUGHULI ZA MKONDO WA JUU WA MAFUTA NA GESI ASILIA KUPITIA PURA

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia PURA iliendelea na maandalizi ya Duru ya Tano (5) ya kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia ambapo imekamilisha maandalizi ya nyaraka muhimu zitakazotumika katika kunadi vitalu ikiwemo Mkataba Kifani wa Ugawanaji wa Mapato (MPSA, 2025) ambao upo katika hatua za maamuzi kupitia Baraza la Mawaziri. MPSA hiyo itatumika kama mwongozo wa majadiliano na mkataba kati ya Serikali na wawekezaji watakaopatikana kutokana na mnada wa vitalu utakaofanyika. Aidha, PURA imekamilisha uwekaji wa mipaka katika vitalu 26 vilivyopendekezwa kuingia kwenye mnada (vitalu 23 katika kina kirefu cha Bahari na vitalu vitatu (3) katika Ziwa Tanganyika). Vilevile, Mamlaka hiyo imeandaa vifurushi vya data *(data package)* na taarifa za kitaalamu kwa vitalu hivyo na kukamilisha nyaraka za zabuni zitakazotumika wakati wa kunadi vitalu husika.

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutangaza fursa za uwekezaji kwa lengo la kuvutia wawekezaji katika sekta ya mafuta na gesi asilia nchini kupitia makongamano mbalimbali ya

mafuta na gesi asilia duniani yakiwemo Kongamano na Maonesho ya 11 ya Petroli ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCE'25) lililofanyika Jijini Dar es Salaam; Mkutano wa Nishati Afrika Magharibi (Accra); Wiki ya Nishati Afrika Kusini (Cape Town); Wiki ya Mafuta Afrika Kusini (Cape Town); na Wiki ya Nishati India (New Delhi) ambapo ilitumia makongamano na mikutano hiyo kutangaza vivutio vya uwekezaji katika Sekta ya Nishati nchini ikiwemo mafuta na gesi asilia.

**145. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia PURA, iliendelea na udhibiti wa shughuli mbalimbali za mkondo wa juu wa petroli ikiwa ni pamoja na kusimamia shughuli za uzalishaji wa gesi asilia katika vitalu vya Songo Songo na Mnazi Bay; uchukuaji wa taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D katika eneo la Eyasi-Wembere; uchukuaji wa data (*Production Logging*) kwenye visima vitatu (SS-3, SS-5 na SS-10) katika kitalu cha Songo Songo kwa ajili ya ufuatiliaji wa mwenendo wa uzalishaji katika visima hivyo; na ukarabati wa visima vinne (MB-2, MB-3, MB-4 na MSX-1) katika kitalu cha Mnazi Bay ili kuhakikisha upatikanaji wa gesi asilia nchini. Aidha, PURA imekamilisha maandalizi ya rasimu ya Kanuni za Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi *(The Petroleum (Corporate Social Responsibility) Regulations)* ambayo ipo katika hatua za mwisho za uidhinishwaji. Kanuni hizo pamoja na mambo mengine, zitawezesha utekelezaji wa CSR wenye tija katika maeneo ya mkondo wa juu wa petroli nchini.

**146. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia PURA inaendelea kufanya uhakiki na ukaguzi wa mapato na gharama za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji katika mikataba ya uzalishaji na ugawanaji mapato kati ya Serikali na waendeshaji wa vitalu (*PSA Auditing*) ambapo hadi Aprili 2025, zaidi ya Shilingi bilioni 360 zimeokolewa kwa kurudishwa kwenye mfuko wa kugawana mapato kati ya Serikali na Waendeshaji wa vitalu. Aidha, PURA imetoa idhini kwa kampuni za Maurel & Prom na ARA Petroleum kuendelea na taratibu za ununuzi wa Wakandarasi wa kuchoronga visima ikiwemo MB-5, MS-2 na Kasa katika Kitalu cha Mnazi Bay na Chikumbi-1, uchakataji wa gesi itakayozalishwa,

ukarabati wa kisima cha NT-1 pamoja na majaribio ya kisima cha NT-2 katika eneo la Ntorya.

### B.2.8.2: UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI KUPITIA EWURA

#### a) Usimamizi na Udhibiti wa Shughuli za Mkondo wa Kati na Chini wa Gesi Asilia

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** EWURA iliendelea kusimamia shughuli za udhibiti katika mkondo wa kati na chini wa gesi asilia kwa kufanya kaguzi katika miundombinu ya uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia na vituo vya kujazia gesi hiyo kwenye magari (CNG) katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam. Hadi Aprili 2025, jumla ya kaguzi 24 zilifanyika katika miundombinu ya gesi asilia zikijumuisha kaguzi 15 katika miundombinu ya usambazaji na vituo vya CNG, na kaguzi tisa (9) katika miundombinu ya uchakataji na usafirishaji. Miundombinu iliyokaguliwa ilikidhi viwango vya ubora unaotakiwa.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufikia Aprili 2025, EWURA ilitoa vibali 10 vya ujenzi wa vituo vya CNG katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro kwa Kampuni za PUMA Energy Tanzania Limited kwa ajili ya ujenzi wa kituo kikuu (*Mother Station*) - Tegeta na kituo kidogo (*Daughter Station*) kwenye kiwanda cha Alliance One - Morogoro; Energo Tanzania Limited - Mikocheni, Victoria Service Station Limited - Kipawa, Rafiki CNG Station – Tabata Relini, Tanzania States Natural Gas Holdings Company Limited - Goba, Puma Energy – Mbezi Beach na Puma Energy – Ubungo External, Natenergy – Kigamboni. EWURA pia ilitoa kibali cha ujenzi wa kituo cha kupokelea gesi asilia iliyoshindiliwa (*CNG Receiving Facility*) kwa kiwanda cha Kinglion - Kibaha. Pia, EWURA ilitoa leseni tano (5) za uendeshaji vituo vya CNG kwa kampuni za Tembo Energy - Tabata, TPDC - Mlimani, TAQA Dalbit - Sam Nujoma, Rafiki CNG Station - Tabata na leseni ya usafirishaji wa CNG (*CNG Supply License*) kwa Kampuni ya Tan Health Limited.

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** EWURA ilitoa vibali nane (8) kwa ajili ya ujenzi wa mabomba ya kupeleka gesi asilia kwenye vituo vya CNG. Vibali sita (6) vilitolewa kwa Kampuni ya TPDC kwa ajili ya

kuunganisha gesi asilia katika vituo vya: Puma Energy Tanzania Limited (Mbezi Beach); TPDC (Mlimani); TAQA Dalbit (Ubungo Mawasiliano); Energo Tanzania Limited (Mikocheni); na BQ Contractors (Goba) na vibali viwili (2) vilitolewa kwa Kampuni ya Pan African Energy Tanzania Limited (PAET) kwa ajili ya kuunganisha gesi asilia katika vituo vya: Victoria Service Station Limited (Kipawa); na Rafiki CNG Station (Tabata).

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** EWURA pia ilitoa vibali sita (6) vya ujenzi wa mabomba ya kupeleka gesi asilia kwenye viwanda, taasisi, migahawa ya chakula na majumbani. Kati ya vibali hivyo, kibali kimoja (1) kilitolewa kwa Kampuni ya PAET kwa ajili ya ujenzi wa bomba la kupeleka gesi asilia kwenye kiwanda cha Aluminium Africa (ALAF) Jijini Dar es Salaam na vinne (4) kwa Kampuni ya TPDC kwa ajili ya kuunganisha gesi asilia kwenye nyumba 451 katika maeneo ya Mnazi Mmoja (Lindi), nyumba 529 maeneo ya Mkuranga (Pwani), Mlimani City Mall na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE). Aidha, kibali kingine kilitolewa kwa kampuni ya Rashal Energies kwa ajili ya ujenzi wa bomba la usambazaji gesi asilia kutoka eneo la Kisemvule hadi Mbagala.

**151.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na ongezeko la ujenzi wa vituo vya CNG, unafuu wa gharama unaopatikana katika matumizi ya gesi asilia kama nishati mbadala ya mafuta katika vyombo vya moto na mwamko mkubwa wa wananchi kutumia CNG, idadi ya watumiaji wa gesi hiyo katika vyombo vya moto inatarajiwa kuendelea kuongezeka kwa kasi. Hivyo, ili kuimarisha usalama kwenye vyombo vya moto vinavyotumia CNG, natoa maelekezo yafuatayo:

i. Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB) iimarishe usimamizi wa wamiliki wa karakana zinazohusika na ubadilishaji wa mifumo ya magari ili kutumia CNG kwa kuhakikisha kuwa zinafanyiwa usajili na karakana bubu zifungiwe au wamiliki wajisajili kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo. Aidha, mafundi wa karakana hizo wawe na taaluma husika;

ii. Shirika la Viwango Tanzania (TBS) liwasimamie kwa karibu wakaguzi wa ufungaji wa mfumo wa CNG kwenye magari (*CNG inspectors*) ili kuhakikisha wana weledi wa kutosha na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria pale wanapokiuka masharti ikiwemo kuwaondoa kwenye mfumo wa ukaguzi;

iii. CRB na TBS wahakikishe karakana zote na wakaguzi wa mfumo wa CNG wanawasilisha taarifa za vyombo vya moto walivyovibadili katika Mfumo wa Taifa wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (*National Petroleum and Gas Information System*) kwa mujibu wa sheria;

iv. NEMC iharakishe utoaji wa vyeti vya Athari kwa Mazingira (*EIA certificates*) kwa wawekezaji wa vituo vipya vya CNG ikiwemo kutoa '*EIA variations*' kwa wakati kwa wamiliki wa vituo vya mafuta wanaotaka kuongeza vituo vya CNG kwenye maeneo yao ili kuimarisha upatikanaji wa CNG;

v. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Halmashauri ziharakishe utoaji wa vibali vya matumizi ya ardhi kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya CNG kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo; na


vi. EWURA iendelee kusimamia kwa karibu maendeleo ya CNG nchini na itoe vibali vya ujenzi na leseni kwa haraka kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo.

**b) Usimamizi na Udhibiti wa Shughuli za Bidhaa za Mafuta ya Petroli**

**152. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA imeendelea kusimamia mkondo wa kati na chini wa Sekta Ndogo ya Mafuta ili kuhakikisha upatikanaji wa uhakika, usalama na ubora wa miundombinu na bidhaa za mafuta nchini. Usimamizi huo umefanyika kwa kutoa vibali vya ujenzi wa mindombinu, leseni za biashara pamoja na kufanya kaguzi mbalimbali. Aidha, hadi Machi 2025, EWURA ilitoa leseni 580 za biashara ya mafuta

ambapo kati ya hizo, leseni 204 zilikuwa mpya na 376 zilikuwa zinahuishwa. Mchanganuo wa leseni hizo ni kama inavyoonekana katika ***Kielelezo Na 7***.

***Kielelezo Na. 7:* Leseni za Biashara ya Mafuta Zilizotolewa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025**




*Chanzo:* ***EWURA***

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufikia Aprili 2025, EWURA ilitoa vibali 215 vya ujenzi wa miundombinu ya mafuta ambapo vibali 182 vilitolewa kwa vituo vya mjini na vibali 26 kwa vituo vya vijijini. Aidha, vibali vitano (5) vilitolewa kwa ajili ya miundombinu ya kuhifadhi mafuta kwa watumiaji wakubwa kama vile viwanda na migodi, na vibali viwili (2) kwa ajili ya maghala ya kuhifadhi na kujaza LPG.

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa na EWURA ni kusimamia taratibu za uagizaji na usambazaji wa mafuta nchini; na kusimamia ubora wa bidhaa za mafuta ambapo jumla ya sampuli 334 kutoka katika vituo vya mafuta na maghala zilipimwa ubora na sampuli 321 sawa na asilimia 96.1 zilikidhi viwango stahiki vya ubora. Taratibu za kisheria zilichukuliwa kwa vituo ambavyo

vilibainika kuwa na mafuta yasiyokidhi viwango vya ubora. Aidha, EWURA ilikagua ubora wa miundombinu 569 ya mafuta ambapo miundombinu 451 sawa na asilimia 76.2 ilikidhi viwango vya ubora ikiwemo vigezo vya masuala ya afya, usalama na mazingira.

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA ilifanya maboresho ya Kanuni nne (4) ambazo ni: *The Petroleum (Wholesales Storage Retail and Consumer Installation Operations) (Amendment) Rules, 2025,* ili kurekebisha masharti ya leseni na kuondoa takwa la kuondoa miundombinu ya mafuta baada ya kutotumika kwa miezi mitatu kwa kuwa inaweza kutumika baada ya kipindi hicho; *The Petroleum (Waste Oil Recycling Operations (Amendment) Rules, 2025,* kwa lengo la kuboresha taratibu za maombi na uidhinishwaji wa vibali vya ujenzi wa miundombinu ya kuchakata mafuta machafu; *The Petroleum (Condensate Operations) (Amendment) Rules, 2025,* kwa lengo la kuboresha taratibu za maombi ya leseni na taratibu za maombi na uidhinishwaji wa vibali vya ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi *condensate*; na *The Petroleum (Marine Loading and Offloading Operations) (Amendment) Rules, 2025,* kwa ajili ya kuboresha taratibu za maombi na uidhinishwaji wa vibali vya ujenzi wa miundombinu ya kupakia na kupakua mafuta kutoka kwenye meli na kuongeza muda wa uhai wa hati ya usajili wa kampuni zinazofanya kazi za kupima kiasi cha mafuta kilichopokelewa kwenye maghala.


### c) Utekelezaji wa Programu ya Uwekaji Vinasaba katika Mafuta

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA iliendelea kutekeleza programu ya uwekaji vinasaba katika mafuta ili kudhibiti ubora na kuhakikisha Serikali inapata mapato stahiki ya kodi kwenye mafuta. Kwa sasa, uwekaji wa vinasaba hivyo unafanyika kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Aidha, TBS itaendelea kuboresha utoaji huduma hiyo kwa kujenga vituo vya kupima vinasaba kwa hiari kabla mafuta hayajafika kituoni *(voluntary check points)*. Hadi Machi 2025, TBS ilikuwa imekamilisha ujenzi wa vituo vitatu (3) katika maeneo ya Iringa, Nzega na Korogwe. Aidha, hadi Machi 2025, kiasi cha lita bilioni 1.47 za mafuta ya petroli, lita bilioni 2.05 za mafuta ya dizeli na lita milioni 4.92 za mafuta ya taa ziliwekwa vinasaba. Hii ni sawa na

ongezeko la asilimia 11.7 na asilimia 7.8 kwa mafuta ya petroli na dizeli mtawalia na pungufu ya asilimia 28.7 kwa mafuta ya taa yaliyowekwa vinasaba kwa kipindi kama hicho Mwaka 2023/24.


**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** wastani wa matumizi ya mafuta kwa siku nchini umeendelea kuongezeka na kufikia lita milioni 5.46 kwa petroli na lita milioni 7.58 kwa dizeli ikilinganishwa na lita milioni 4.80 kwa petroli na lita milioni 6.90 kwa dizeli Mwaka 2023/24. Ongezeko hilo linaashiria kuendelea kukua kwa shughuli za kiuchumi na kijamii nchini zikiwemo ujenzi, usafirishaji na maendeleo ya viwanda. Mwenendo wa wastani wa matumizi ya mafuta ya petroli na dizeli kwa siku ni kama inavyoonekana katika ***Kielelezo Na. 8 na Kielelezo Na. 9***.

***Kielelezo Na. 8*:** **Mwenendo wa Wastani wa Matumizi ya Petroli kwa Siku kwa Mwaka 2023/24 na 2024/25**




*Chanzo:* ***EWURA***


***Kielelezo Na. 9*: Mwenendo wa Wastani wa Matumizi ya Dizeli kwa Siku kwa Mwaka 2023/24 na 2024.25**




*Chanzo: **EWURA***

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** matumizi ya mafuta ya taa yameendelea kupungua kutokana na juhudi za Serikali zinazoendelea katika kuunganisha umeme vijijini na kwenye vitongoji pamoja na matumizi ya taa zinazotumia nishati ya jua. Matumizi ya mafuta ya taa yameendelea kupungua kutoka wastani wa lita 25,152 kwa siku Mwaka 2023/24 hadi lita 18,014 kwa siku Mwaka 2024/25. ***Kielelezo Na. 10*** kinaonesha mwenendo wa matumizi ya mafuta ya taa kwa miaka 2023/24 na 2024/25.

***Kielelezo Na. 10:* Mwenendo wa Wastani wa Matumizi ya Mafuta ya Taa kwa Siku kwa Mwaka 2023/24 na 2024/25**




*Chanzo:* ***EWURA***

**B.2.8.2.1: MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA**

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** bei za mafuta katika Soko la Dunia ziliendelea kushuka ambapo kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025 bei ya mafuta ghafi ilishuka kwa asilimia 10.5 na kufika wastani wa Dola za Marekani 76 kwa pipa ikilinganishwa na wastani wa Dola za Marekani 84 kwa pipa kwa kipindi kama hicho Mwaka 2023/24. Kupungua kwa bei za mafuta ghafi katika Soko la Dunia kulichangiwa na ongezeko la uzalishaji wa mafuta ikilinganishwa na mahitaji na kupungua kwa matumizi ya mafuta nchini China kulikosababishwa na ongezeko la matumizi ya magari ya umeme na magari makubwa yanayotumia gesi asilia *(LNG powered trucks)*. ***Kielelezo Na. 11*** kinaonesha mwenendo wa bei za mafuta ghafi katika Soko la Dunia.

***Kielelezo Na. 11*: Mwenendo wa Bei ya Mafuta Ghafi katika Mwaka 2023/24 na 2024/25 (Dola/Pipa)**


| Mwezi | 2023/24 | 2024/25 |
|---|---|---|
| Julai | 80 | 84 |
| Agosti | 85 | 79 |
| Septemba | 92 | 73 |
| Oktoba | 91 | 75 |
| Novemba | 83 | 73 |

| | | |
|---|---|---|
| Desemba | 78 | 73 |
| Januari | 80 | 78 |
| Februari | 83 | 75 |
| Machi | 85 | 71 |
| **Wastani** | **84** | **76** |
| Badiliko | | **-10.5%** |

*Chanzo:* ***EWURA***

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwenendo huo wa bei za mafuta ghafi katika Soko la Dunia ulisababisha kushuka kwa bei za mafuta yaliyosafishwa ambapo bei za mafuta ya petroli, dizeli na taa/ndege zilishuka kwa wastani wa asilimia 12.5, asilimia 16.4 na asilimia 16 mtawalia. Kufikia Machi 2025, bei za mafuta yaliyosafishwa katika Soko la Dunia zilikuwa wastani wa Dola za Marekani 687 kwa tani ya petroli, Dola za Marekani 661 kwa tani ya dizeli na Dola za Marekani 694 kwa tani ya mafuta ya taa/ndege ikilinganishwa na wastani wa Dola za Marekani 785 kwa tani ya mafuta ya petroli, Dola za Marekani 797 kwa tani ya dizeli na Dola za Marekani 832 kwa tani ya mafuta ya taa/ndege katika kipindi kama hicho Mwaka 2023/24. ***Kielelezo Na. 12*** ni wastani wa mwenendo wa bei za mafuta yaliyosafishwa katika Soko la Dunia kwa Mwaka 2023/24 na 2024/25.

***Kielelezo Na. 12:* Mwenendo wa Wastani wa Bei za Mafuta Yaliyosafishwa katika Soko la Dunia kwa Mwaka 2023/24 na 2024/25**





*Chanzo:* ***EWURA***

### B.2.8:2.2 MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA iliendelea kutoa bei kikomo za bidhaa za mafuta kwa kuzingatia Sheria na Kanuni. Aidha, wastani wa bei za mafuta nchini umeendelea kushuka ikilinganishwa na mwaka uliopita. Mathalani kwa Mkoa wa Dar es Salaam bei za mafuta kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 zilishuka kwa wastani wa asilimia 4 kwa mafuta ya petroli, asilimia 7.4 kwa mafuta ya dizeli na asilimia 2.3 kwa mafuta ya taa/ndege, ambapo wastani wa bei ya petroli kwa lita ilikuwa Shilingi 3,005, dizeli Shilingi 2,884 na mafuta ya taa Shilingi 2,975 ikilinganishwa na wastani wa bei za mafuta hayo kwa kipindi hicho Mwaka 2023/24 ambapo zilikuwa petroli Shilingi 3,129, dizeli Shilingi 3,113 na mafuta ya taa Shilingi 3,047 kwa lita. ***Kielelezo Na. 13*** kinaonesha wastani wa mwenendo wa bei za mafuta nchini.

***Kielelezo Na. 13*: Wastani wa Mwenendo wa Bei za Mafuta Nchini**




*Chanzo*: ***EWURA***

### B.2.8:2.3 USIMAMIZI NA UDHIBITI WA SHUGHULI ZA UMEME

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufikia Aprili 2025, Serikali kupitia EWURA imetoa leseni saba (7) kwa kampuni za kuzalisha umeme kiasi cha **MW 58.16** kwa ajili ya matumizi binafsi, leseni tano (5) za muda mfupi kwa kampuni zinazotarajia kuzalisha umeme kiasi cha **MW 21.34** kwa ajili ya kuiuzia TANESCO na kusajili kampuni mbili (2) za

kuzalisha umeme kiasi cha **MW 0.47**. Utekelezaji wa miradi hiyo, utaongeza ajira kwa Watanzania pamoja na uzalishaji umeme nchini. Vilevile, EWURA imeidhinisha mikataba nane (8) ya kuuziana umeme *(Power Purchase Agreements)* kati ya TANESCO na wazalishaji ya jumla ya **MW 61.93** na hivyo kufanya uzalishaji wa umeme kufikia jumla ya **MW 141.90** kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Na. 8A na 8B***.

**163.** ***Mheshimiwa Spika***, leseni 1,378 za mafundi umeme zilitolewa ikilinganishwa na leseni 1,265 Mwaka 2023/24 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 9. Kati ya waliopewa leseni, 1,334 ni wanaume na 44 ni wanawake. Leseni hizo zinatolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 5 (a) na 8 (1) cha Sheria ya Umeme, Sura ya 131. Utoaji wa leseni hizo umesaidia kuwapata mafundi wenye ujuzi wa uwekaji wa mifumo bora ya umeme na salama kwa wananchi, hususan maeneo ya vijijini. Mchanganuo wa leseni hizo ni kama ifuatavyo:

(i) Leseni 69 za daraja “A” zimetolewa kwa wataalam wenye ujuzi wa kufunga mifumo ya umeme hadi kiwango cha msongo wa kilovoti 400;

(ii) Leseni 97 za daraja “B” zimetolewa kwa wataalam wenye ujuzi wa kufunga mifumo ya umeme hadi kiwango cha msongo wa kilovoti 33;

(iii) Leseni 778 za daraja “C” zimetolewa kwa wataalam wenye ujuzi wa kufunga mifumo ya umeme hadi kiwango cha msongo wa kilovoti moja (1);

(iv) Leseni 428 za daraja “D” zimetolewa kwa wataalam wenye ujuzi wa kufunga mifumo ya umeme hadi kiwango cha msongo wa kilovoti 0.23;

(v) Leseni moja (1) ya daraja “S1” imetolewa kwa mtaalam mwenye ujuzi wa kufunga mifumo maalum ya kitaalamu *(special work)* hadi kiwango cha msongo wa kilovoti 400; na

(vi) Leseni tano (5) za daraja "S3" zimetolewa kwa wataalam wenye ujuzi wa kufunga mifumo ya kitaalamu ya umeme *(special work)* hadi kiwango cha msongo wa kilovoti 1.


### B.2.9: HALI YA UAGIZAJI NA UPATIKANAJI WA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI NCHINI

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kusimamia Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (*Bulk Procurement System - BPS*) katika uagizaji wa bidhaa za mafuta ya petroli nchini tangu ulipoanza kutumika rasmi mwezi Januari, 2012. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 jumla ya lita bilioni 6.74 za bidhaa za mafuta ya petroli ziliagizwa ikilinganishwa na lita bilioni 6.28 zilizoagizwa katika kipindi kama hicho Mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 7.3 ambapo petroli ilikuwa lita bilioni 2.23, dizeli lita bilioni 4.24 na mafuta ya taa/ndege lita milioni 270. Aidha, bidhaa hizo ziliagizwa na kupokelewa kupitia Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya mafuta hayo yaliyoagizwa katika kipindi husika, lita bilioni 3.26 sawa na asilimia 48 yalikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani ikilinganishwa na lita bilioni 3.37 kwa Mwaka 2023/24. Vilevile, lita bilioni 3.48 sawa na asilimia 52 yalikuwa kwa ajili ya nchi jirani ikilinganishwa na lita bilioni 2.9 kwa Mwaka 2023/24. Mafuta kwa ajili ya nchi jirani yameongezeka kwa asilimia 16 kutokana na kuimarika kwa ufanisi wa mfumo wa BPS na hivyo kuendelea kuvutia nchi hizo kutumia mfumo huo.


***Kielelezo Na. 14*** kinaonesha jumla ya kiasi cha bidhaa za mafuta kilichoagizwa kwa mgawanyo wa kila aina ya mafuta kwa kipindi cha mwezi Julai 2024 hadi Machi 2025 na ***Kielelezo Na. 15*** kinaonesha jumla ya kiasi cha mafuta kilichoagizwa kwa ajili ya matumizi ya ndani na nchi jirani katika kipindi hicho.

***Kielelezo Na. 14:*** **Jumla ya Kiasi cha Bidhaa za Mafuta Kilichoagizwa kwa Kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025**




*Chanzo:* ***PBPA***

***Kielelezo Na. 15*****: Jumla ya Kiasi cha Mafuta Kilichoagizwa kwa Ajili ya Matumizi ya Ndani na Nchi Jirani Julai 2024 hadi Machi 2025**




*Chanzo****: PBPA***

**166. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya zabuni 100 zilitangazwa kwa njia ya ushindani wa kimataifa kwa kuzingatia kigezo cha gharama ndogo za uletaji wa mafuta nchini (*Premium*). Aidha, kati ya zabuni 10 hadi 13 zilishindanishwa kila mwezi ambapo wazabuni 9 hadi 10 ikiwemo TPDC walishiriki katika zabuni hizo. Ushiriki wa TPDC katika zabuni ulichochea ushindani na kuongeza uwazi katika zabuni za uagizaji wa mafuta na kuwezesha gharama za uletaji wa mafuta nchini kuanza kupungua.

**167.** ***Mheshimiwa Spika****,* Serikali imeendelea kutumia miundombinu ya Kampuni ya TIPER kama kituo cha kupokea mafuta kwa pamoja *(Single Receiving Terminal - SRT)*. Kituo hicho kina uwezo wa kupokea meli mbili (2) hadi tatu (3) za mafuta ya dizeli kwa mwezi ambapo kila meli ina ujazo wa hadi lita milioni 120. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) inaendelea na ujenzi wa kituo kipya cha kupokelea mafuta kwa pamoja (SRT) katika eneo la Kigamboni na ujenzi huo unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2026. Kukamilika kwa ujenzi wa kituo hicho kutasaidia kuondoa gharama za ucheleweshaji wa meli *(demurrage)* kwa kuongeza ufanisi wa upakuaji mafuta na kuendana na muda unaotakiwa kimataifa (chini ya saa 72 kwa meli kubwa na saa 36 kwa meli za kati).

**168.** ***Mheshimiwa Spika****,* Serikali kupitia PBPA imeendelea kuongeza ufanisi wa usimamizi wa upakuaji mafuta kutoka kwenye meli kwenda kwenye hifadhi za kampuni za mafuta kwa kutumia mfumo wa kielektroniki (SCADA). Hatua hii imeimarisha udhibiti wa upotevu wa mafuta wakati wa upakuaji wa mafuta hayo kutoka kwenye meli. Mfumo huu unasoma kiasi cha mafuta yanayopita katika mita (*flowmeter*) za Serikali zilizopo Kurasini (KOJ), Kigamboni (SBM), Tanga na Mtwara na kulinganisha kiasi hicho na mafuta yanayopita mita za kampuni za mafuta na kupokelewa kwenye maghala ya kuhifadhi mafuta. Uwepo wa mfumo huu umepunguza upotevu wa mafuta kutoka asilimia 0.5 kabla ya mfumo hadi asilimia 0.1 baada ya mfumo huo.

### B.2.10: USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI NA USHIRIKISHWAJI WA WATANZANIA KATIKA SEKTA YA MAFUTA NA GESI ASILIA

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa kampuni za uzalishaji wa gesi asilia nchini zinalipa fedha stahiki za tozo ya huduma kwa Halmashauri husika. Aidha, PURA imeendelea kusimamia mipango ya ushiriki wa wazawa kwenye miradi ya mkondo wa juu wa mafuta na gesi asilia ambapo kwa sasa ushiriki wa Watanzania ni zaidi ya asilimia 90 katika miradi ya utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesia asilia nchini. Vilevile, Watanzania wamenufaika kwa kutoa huduma za

afya, fedha, chakula, ulinzi, mafuta ya kuendesha mitambo na ukarabati wa miundombinu ya gesi asilia.

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka imeendelea kufuatilia suala la ushiriki wa watanzania katika shughuli zinazofanywa kwenye mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya gesi asilia. Kwa ujumla, kampuni zinazojishughulisha na shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya gesi asilia zilizingatia masharti na viwango vilivyowekwa kwenye Kanuni zinazosimamia masuala ya ushiriki wa wazawa (*the Petroleum (Local Content) Regulations, 2017*).

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha ushiriki wa Watanzania katika sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia ambapo kupitia EWURA na PURA imeendelea kuhuisha kanzidata za watoa huduma na wataalamu wa ndani katika mfumo wa "*Common Qualification System - CQS*". Kufikia Aprili 2025, jumla ya kampuni za wazawa 2,476 na wataalam wazawa 431 wamejisajili katika mfumo huo ambapo Kampuni 300 zimepata fursa za kuuza bidhaa na kutoa huduma mbalimbali kwenye miradi ya mafuta na gesi asilia. Aidha, Watanzania 6,763 wameajiriwa katika mradi wa EACOP ambapo kati ya hao kampuni ya EACOP imeajiri Watanzania 254, Wakandarasi wa mradi wameajiri Watanzania 6,050 na watoa huduma katika Mradi wameajiri Watanzania 459. Vilevile, Watanzania 225 wameajiriwa katika vitalu vya uzalishaji wa gesi asilia vya Mnazi Bay na Songo Songo.

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa EACOP umefadhili mafunzo kwa Watanzania kupitia programu yake ya *Industry Enhancement Centre* ambapo vijana wa Kitanzania 50 walipata fursa ya mafunzo kwa vitendo (*interships*) hapa nchini na katika nchi za Canada, Umoja wa Falme za Kiarabu, Uholanzi, Italia, na Uingereza. Pia wataalam 100 kutoka kampuni mbalimbali za Kitanzania walipata mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uwezo katika maeneo yao ya taaluma na ujuzi. Vilevile, wakufunzi (*Trainers of Trainees*) 250 walipata mafunzo mbalimbali kulingana na taaluma zao kwa ajili ya kukuza ujuzi. Aidha, mradi wa EACOP ulinunua bidhaa na huduma zenye thamani ya Dola za Marekani 271,113,488 sawa na takriban Shilingi bilioni 759 kutoka katika soko

la ndani. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 198 ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo manunuzi katika soko la ndani yalikuwa na thamani ya Dola za Marekani 90,999,585 sawa na takriban Shilingi bilioni 254.8.

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC imeendelea kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika shughuli za mafuta na gesi asilia ambapo kufikia mwezi Aprili, 2025 kampuni 61 zimeruhusiwa kufanya biashara ya CNG nchini. Katika hatua nyingine, TPDC inaendelea na majadiliano na Kampuni binafsi tatu (3) za Rosetta Energies Limited, KS Energies Limited na Taifa Group kwa ajili ya uendelezaji wa miradi midogo ya kubadili gesi asilia kuwa katika hali ya kimiminika (Mini – LNG) na kusafirishwa kwa magari maalum kwenda mikoa mbalimbali nchini ambayo haijafikiwa na miundombinu ya mabomba ya gesi asilia. Ushiriki wa kampuni hizo katika biashara ya gesi asilia utaongeza matumizi ya gesi asilia pamoja na kuongeza fursa za ajira kwa Watanzania hapa nchini.

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa miradi ya mafuta na gesi umewezesha kupatikana kwa ajira 8,453 kupitia miradi ya utafutaji, uendelezaji, uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa mafuta na gesi nchini. Ajira hizo zilihusisha makundi mbalimbali katika jamii yakiwemo wanawake (1,845), wanaume (6,557) na walemavu (51). Aidha, miradi ya nishati safi ya kupikia imezalisha jumla ya ajira 1,048 ambapo kati ya ajira hizo, wanawake (102) wanaume (422) na walemavu (524). Vilevile, kati ya ajira zilizopatikana katika miradi ya mafuta na gesi, ajira 2,491 ni za kudumu na 5,962 za muda mfupi.

### B.2.11: MASHIRIKIANO NA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KATIKA UENDELEZAJI WA SEKTA YA NISHATI

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Sekta ya Nishati inashamiri katika pande mbili za Muungano, Wizara zenye dhamana ya Nishati za pande mbili za Muungano pamoja na Taasisi zake zimeendelea kutekeleza masuala mbalimbali ya mashirikiano.

**176. *Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/25, Wizara zenye dhamana ya nishati za pande mbili za Muungano zilifanya kikao kilichojadili masuala mbalimbali yanayohusu uendelezaji wa Sekta ya nishati. Kupitia kikao hicho Wizara hizo zilijadili hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa maeneo ya mashirikiano yaliyobainishwa katika Hati ya Makubaliano (MoU) iliyosainiwa na Mawaziri wenye dhamana ya nishati wa pande mbili za Muungano tarehe 12 Novemba, 2023. Aidha, kikao hicho kilikubaliana kuundwa kwa Sekretarieti ya kuratibu utekelezaji wa MoU hiyo pamoja na kuandaa Mpango Kazi wa utekelezaji wa MoU husika. Vilevile, ilikubalika kuwa Taarifa za utekelezaji wa MoU hiyo zikihusisha pia masuala yanayohusu Taasisi zilizo chini ya Wizara ziwe zinawasilishwa kwenye vikao vya Ushirikiano ili kuweza kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa MoU kwa ujumla wake.

**177. *Mheshimiwa Spika,*** taasisi za PURA na ZPRA zimeendelea kushirikiana kwa kubadilishana ujuzi katika maeneo ya kaguzi za mikataba ya PSA; udhibiti wa shughuli za uzalishaji wa gesi asilia; uandaaji wa mikataba ya Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (PSA); na usimamizi wa taarifa za petroli. Aidha, TPDC na ZPDC zimeshirikiana katika mafunzo kuhusu uandaaji na utumiaji wa moduli za fedha na uchumi katika kufanya maamuzi ya uwekezaji katika tasnia ya mafuta na gesi asilia. Vilevile, EWURA na ZURA zimeendelea kushirikiana katika kubadilishana ujuzi katika udhibiti wa kiufundi na kiuchumi wa shughuli za umeme na bidhaa za petroli. Halikadhalika, TANESCO na ZECO zimeshirikiana katika usafirishaji wa umeme unaotumika Zanzibar, kubadilishana utaalam na uzoefu katika masuala ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ikiwa ni pamoja na uandaaji wa Mpango Kabambe wa Uendelezaji Sekta Ndogo ya Umeme *(Power System Master Plan - PSMP)*.

### B.2.12: UIMARISHAJI WA UTENDAJI KAZI NA UTOAJI HUDUMA

**178. *Mheshimiwa Spika***, Wizara ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha ujenzi wa jengo la ofisi za Wizara katika Mji wa Serikali Mtumba. Mradi huo unatekelezwa na Mkandarasi-Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na Mshauri Elekezi - ARU Built Environment Consulting Company Limited (ABECC) ambayo ni Kampuni Tanzu

ya Chuo Kikuu cha Ardhi. Hadi kufikia Machi, 2025 ujenzi ulikuwa umekamilika kwa asilimia 94 na Wizara inatarajia kuhamia katika jengo hilo Mei, 2025. Kukamilika kwa jengo hilo ni hatua muhimu ya kuhakikisha Watumishi wa Wizara wanatekeleza majukumu yao katika mazingira bora yatakayoleta tija na ufanisi zaidi.

**179.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha Wizara na Taasisi zilizo chini yake zinaimarisha utendaji kazi na utoaji wa huduma, Wizara iliendelea kusimamia matumizi ya Mfumo wa Usimamizi na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma (PEPMIS). Aidha, Wizara ilisimamia utumiaji wa Mfumo wa Taasisi ya Umma (PIPMIS) unaosimamia uandaaji wa Mkataba wa Utendaji Kazi wa Taasisi za Umma, utekelezaji na ufuatiliaji, mapitio ya utendaji kazi wa Taasisi na tathmini ya utendaji kazi wa Taasisi. Vilevile, Wizara na Taasisi ziliendelea kuwajengea uwezo watumishi ambapo jumla ya watumishi 2,643 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi kulingana na mahitaji. Kati ya hao, watumishi wa Wizara ni 98, TANESCO 2,051, TPDC 58, REA 58, PURA 90, PBPA 69 na EWURA 219. Pia, katika kuimarisha utendaji kazi, jumla ya watumishi 840 waliajiriwa, ambapo watumishi 18 waliajiriwa Wizarani na watumishi 822 kwa ajili ya Taasisi za Wizara.

### B.2.13: MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI

**180.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2024/25 Wizara imepata mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, Sekta ya Nishati imepiga hatua kubwa ambapo kumekuwepo na mafanikio mbalimbali ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

(i) Kuongezeka kwa uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika Gridi ya Taifa kutoka MW 1,601.84 Mwaka 2020/21 hadi MW 4,031.71 Aprili 2025 sawa na ongezeko la asilimia 151.7;

(ii) Kukamilika kwa mradi wa kielelezo wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) – MW 2,115 ambao umeiwezesha nchi kuondokana na tatizo la upungufu wa umeme na kuchochea

ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii, kukuwa kwa Pato la Taifa na kuimarisha mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara nchini. Aidha, kukamilika kwa mradi huu kumewezesha kufanyika kwa matengenezo kinga makubwa katika mitambo ya uzalishaji umeme ya Mtera, Kidatu na Kihansi bila kuathiri hali ya upatikanaji wa umeme;

(iii) Kukamilika kwa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Singida hadi Arusha ambayo imewezesha kuunganisha Gridi ya Taifa ya Tanzania na Kenya ili kuwezesha kuanza biashara ya kuuziana umeme baina ya Tanzania na nchi jirani kupitia *Eastern African Power Pool (EAPP)*;

(iv) Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 160 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Julius Nyerere hadi Chalinze mkoani Pwani umekamilika kwa asilimia 99.8. Aidha, ujenzi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Chalinze umekamilika kwa asilimia 97.6 na kwa sasa njia hii pamoja na kituo vinatumika kuingiza umeme unaozalishwa JNHPP kwenye Gridi ya Taifa;

(v) Kukamilika kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma ambao umefanikisha kuunganisha Mkoa wa Kigoma katika Gridi ya Taifa na kuwezesha kuzimwa kwa mitambo ya umeme wa mafuta. Aidha, TANESCO itaokoa kiasi cha Shilingi bilioni 58.4 zilizokuwa zinatumika kwa mwaka kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya dizeli;

(vi) Kukamilika kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 115 kutoka Tabora hadi Urambo na kuwezesha kuimarika kwa upatikanaji wa umeme katika Wilaya ya Urambo;

(vii) Kuimarika kwa upatikanaji wa umeme katika mikoa ya Lindi na Mtwara kutokana na kufungwa kwa mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wa **MW 20** katika eneo la Hiyari - Mtwara pamoja na kukarabatiwa kwa mitambo Namba 13 (**MW 4.3**) na Namba 8 (**MW 2**) mkoani Mtwara pamoja na mtambo Namba 3 (**MW 2.5**) Somanga mkoani Lindi;

(viii) Kuongezeka kwa wateja waliounganishiwa umeme nchini kutoka 2,766,745 Mwaka 2020/21 hadi 5,449,278 mwezi Aprili, 2025 ikiwa ni ongezeko la asilimia 97;

(ix) Kufikisha miradi ya umeme katika vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara kutoka vijiji 506 vilivyokuwa vimeunganishiwa umeme mwaka 2007 wakati REA inaanzishwa. Aidha, jumla ya vitongoji 33,657 kati ya 64,359 sawa na asilimia 52 vimeunganishiwa umeme;

(x) Kuunganishwa umeme katika taasisi na maeneo ya huduma 63,140 kutoka 15,200 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 315. Maeneo hayo ni vituo vya afya, taasisi za elimu, taasisi za biashara, nyumba za ibada na pampu za maji kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Na. 9****;*

(xi) Kuongezeka kwa matumizi ya nishati safi ya kupikia kupitia jitihada mbalimbali ikiwemo ugawaji wa mitungi ya gesi ya kupikia 266,000; majiko banifu 5,000; na kuwezesha ufungaji wa mifumo ya nishati safi ya kupikia kwa Taasisi za Umma zinazohudumia watu zaidi ya 100;

(xii) Kuongezeka kwa mafundi umeme waliosajiliwa na kupatiwa leseni na EWURA kufikia 6,614 mwaka 2025 kutoka mafundi 2,751 mwaka 2020/21 sawa na ongezeko la asilimia 240;

(xiii) Kuimarika kwa utendaji wa TPDC kibiashara na kupata faida kutokana na shughuli zake ambapo faida ya Mwaka 2021/22 ilikuwa Shilingi bilioni 97.78 na kuongezeka kufikia Shilingi bilioni 248.75 Mwaka 2023/24. Aidha, kuanzia Julai 2024, TPDC inalipa mishahara ya watumishi wake kutokana na mapato yake ya ndani, hivyo kuipunguzia mzigo Serikali wa kulipa mishahara hiyo;

(xiv) Kuongezeka kwa ushiriki wa TPDC katika Kitalu cha uzalishaji wa gesi asilia cha Mnazi Bay kutoka asilimia 20 hadi asilimia 40 baada ya kununua asilimia 20 ya hisa za Kampuni ya Wentworth na hivyo kuongeza mapato na ushiriki katika maamuzi ya uendeshaji wa kitalu husika;

(xv) Kutolewa Leseni ya Uendelezaji wa Kitalu cha kuzalisha gesi asilia cha Ntorya kwa TPDC ambayo itashirikiana na Kampuni ya ARA Petroleum katika uendelezaji wa kitalu hicho. Kitalu hicho kina Futi za Ujazo Trilioni 1.64, hivyo uzalishaji wake utaimarisha upatikanaji wa gesi asilia nchini kwa matumizi ya ndani na ziada kuuzwa nje ya nchi;

(xvi) Kuongezeka kwa vituo vya kujaza gesi asilia (*CNG filling stations*) kwenye vyombo vya moto kutoka vituo viwili (2) Mwaka 2020/21 hadi vituo tisa (9) mwezi Aprili 2025;

(xvii) TPDC imefanikiwa kuanza kushiriki katika biashara ya uagizaji wa mafuta kupitia mfumo wa BPS na kushinda jumla ya zabuni 10 zilizowezesha kuingiza nchini tani 900,000 za mafuta ya dizeli;

(xviii) Kuongezeka kwa mtandao wa usambazaji wa gesi asilia nchini kutoka kilomita 102.54 Mwaka 2020/21 hadi kilomita 241.58 mwezi Aprili 2025 ambao umewezesha kuunganishwa kwa jumla ya nyumba 1,514, taasisi 13 na viwanda 57. Aidha, zaidi ya

vyombo vya moto 15,000 vinatumia gesi asilia (CNG), hivyo kupunguza mahitaji ya petroli na dizeli katika uendeshaji wa vyombo vya moto nchini;

(xix) Kuongezeka kwa matumizi ya gesi asilia nchini kutoka futi za ujazo bilioni 59.83 Mwaka 2020/21 hadi futi za ujazo bilioni 82.91 mwezi Aprili 2025;

(xx) Kuimarika kwa kaguzi za mapato na gharama katika Mikataba ya Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (*PSA Audit*) na kupunguza gharama za uendeshaji kwa Shilingi bilioni 361.78 na hivyo kuongeza gawio la Serikali;

(xxi) Kuongezeka kwa ushiriki wa Watanzania katika shughuli za utafutaji na uzalishaji wa gesi asilia hadi asilimia 90 ikilinganishwa na mwaka 2021 ambapo ushiriki ulikuwa chini ya asilimia 5;

(xxii) Kuajiriwa jumla ya Watanzania 6,763 katika mradi wa EACOP, ambapo kampuni ya EACOP imeajiri Watanzania 254, Wakandarasi wa mradi wameajiri Watanzania 6,050 na watoa huduma katika Mradi wameajiri Watanzania 459. Vilevile, Watanzania 225 wameajiriwa katika vitalu vya uzalishaji wa gesi asilia vya Mnazi Bay na Songo Songo;

(xxiii) Kuendelea kuimarika kwa Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (*Bulk Procurement System – BPS*) ambao umeongeza uhakika wa upatikanaji wa mafuta nchini; na

(xxiv) Kuanza kutumika kwa mfumo wa kielekroniki wa “SCADA” katika usimamizi wa ushushaji wa mafuta nchini ambao umewezesha kupunguza upotevu wa mafuta kutoka asilimia 0.5 Mwaka 2020/21 hadi asilimia 0.1 mwezi Aprili 2025.

## B.2.14: CHANGAMOTO ZILIZOPO NA UTATUZI WAKE

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Nishati, ni vyema kutambua kuwa miradi ya utafutaji, uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme na gesi asilia inahitaji uwekezaji mkubwa katika utekelezaji wake. Hivyo, pamoja na juhudi kubwa za kutenga rasilimali fedha zitakazoendelea kutekelezwa na Serikali katika uendelezaji wa Sekta ya Nishati, Serikali pia itaendelea kuhamasisha, kuvutia na kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo ikiweno sekta binafsi ili kufanikisha upatikanaji wa rasilimali fedha zitakazochangia katika uendelezaji wa Sekta hii kwa kuzingatia mchango wake katika ukuaji wa uchumi, utoaji wa huduma na ajira.

## C. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa Mwaka 2024/25, sasa napenda kuwasilisha Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26.

**183.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka 2025/26 Wizara itaendelea kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme, ikiwa ni pamoja na kufikisha Gridi ya Taifa katika mikoa iliyosalia ya Rukwa, Kagera, Lindi na Mtwara. Aidha, Wizara itaanza utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Nishati wa Mwaka 2025 - 2030 (*National Energy Compact* 2025 - 2030) kuhusu upatikanaji na uunganishaji wa umeme kwa wananchi, kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika uzalishaji wa umeme na ushiriki wa Sekta Binafsi katika maendeleo ya Sekta ya Nishati. Vilevile, Wizara itaendelea kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kutekeleza Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa *(National Grid Stabilization Project)* pamoja na kufanya matengenezo na ukarabati wa mitambo ya kuzalisha umeme.

**184.** ***Mheshimiwa Spika*,** maeneo mengine ya kipaumbele katika Mwaka 2025/26 ni kuendelea na usambazaji wa nishati katika vitongoji, maeneo ya migodi, kilimo, viwanda na pampu za maji

pamoja na vituo vya afya ili kuwezesha shughuli za uzalishaji na utoaji wa huduma bora kwa wananchi; pamoja na kuhamasisha na kuwezesha watanzania kutumia nishati safi ya kupikia ikiwa ni utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024-2034) na Mpango wa Taifa wa Nishati wa Mwaka 2025 - 2030 (*National Energy Compact* 2025 - 2030). Wizara pia itaendelea kuwezesha upatikanaji wa bidhaa za mafuta vijijini kupitia ujenzi wa vituo vya mafuta katika maeneo hayo; pamoja na kutekeleza shughuli za utafutaji, uendelezaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia na kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati ya mafuta na gesi asilia ikiwemo Mnazi Bay Kaskazini, Eyasi – Wembere, mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (*Liquefied Natural Gas – LNG Project*) na ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania (*East African Crude Oil Pipeline - EACOP*).

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada zitaelekezwa pia katika kusimamia na kuhakikisha nchi yetu inakuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli pamoja kuimarisha matumizi ya gesi asilia (CNG) katika vyombo vya moto. Vilevile, Wizara itaendelea kutekeleza shughuli za kiudhibiti; kuimarisha ushiriki wa wazawa katika Sekta ya Nishati pamoja na kuimarisha nguvu kazi na kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi ili kuimarisha tija na ufanisi katika utendaji kazi. Pia, Wizara itaendelea kuimarisha utendaji wa Taasisi/ Mashirika yaliyo chini yake ya TANESCO, REA, TPDC, PBPA, EWURA na PURA pamoja na Kampuni Tanzu ili yaweze kuimarika zaidi katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi pamoja na tija na ufanisi katika utendaji.

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2025/26 pamoja na mambo mengine, umezingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III) 2021/22 – 2025/26, maagizo na maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa yaliyohusu Sekta ya Nishati, Maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Kamati nyingine za Bunge yaliyotolewa kwa nyakati tofauti, Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji, Mkakati wa Taifa wa Matumizi

ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 - 2034), Mpango Mkakati wa Wizara ya Nishati wa Mwaka 2021/22-2025/26 na Mpango Mahususi wa Taifa wa Nishati wa Mwaka 2025 - 2030 (*National Energy Compact* 2025 - 2030). Miongozo mingine iliyozingatiwa ni Sera, Mikakati na Programu mbalimbali za Kisekta na Kitaifa pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs) ya mwaka 2030 kuhusu masuala ya nishati.

## C.1 SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU

### C.1.1 MIRADI YA KUZALISHA UMEME

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuelekeza nguvu katika uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali ili kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na umeme wa kutosha; na ziada kutumika kuuzwa nje ya nchi na kulipatia Taifa fedha za kigeni na hivyo kunufaika ipasavyo na rasilimali za asili ambazo nchi imebarikiwa. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imepanga kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji wa umeme kama ifuatavyo:

**a) Miradi ya Kuzalisha Umeme Iliyopo katika Hatua za Utekelezaji**

**(i) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) – MW 2,115**

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukamilisha utekelezaji wa mradi huu, kazi zilizopangwa ni kufanya marekebisho yote ya kazi za mradi *(snags rectification)* pamoja na usimamizi wa mradi katika kipindi cha uangalizi; kuratibu shughuli za kuimarisha utunzaji wa vyanzo vya maji katika Bonde la Rufiji ili kuwezesha upatikanaji endelevu wa maji ya kuzalisha umeme katika Bwawa la JNHPP; uendeshaji na ufanisi wa mitambo; kukamilisha ujenzi wa ghala la kuhifadhia vifaa katika kituo cha kupoza umeme cha Chalinze; na kulipa malipo ya "*retention*" kwa Wakandarasi na Washauri Elekezi wa mradi wa kituo cha kuzalisha umeme cha JNHPP pamoja na njia ya kusafirisha umeme kutoka JNHPP hadi Chalinze na kituo cha

kupoza umeme cha Chalinze. Jumla ya **Shilingi bilioni 313** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**(ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi 1 Extension- MW 185**

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha kazi za uboreshaji wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Kinyerezi – Gongolamboto - Mbagala na upanuzi wa vituo vyake vya kupoza umeme ambao umefikia asilimia 62.18 pamoja na kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 3.5 kutoka Kinyerezi hadi Gongolamboto. Jumla ya **Shilingi bilioni 5.04** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**(iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa MW 49.5 kwa Kutumia Maji ya Mto Malagarasi**

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa kwa upande wa ujenzi wa Bwawa ni pamoja na kuchepusha mto ili kuruhusu kazi ya ujenzi wa tuta *(dam)* na njia za maji *(water ways)*; kuanza ujenzi wa nyumba ya mitambo *(power house);* kituo cha kupokelea umeme *(switch yard);* ujenzi wa barabara kwa kiwango cha changarawe; kusimika mtambo wa kuchanganyia zege *(concrete batching plant*); na kukamilisha ujenzi wa kambi za muda za mkandarasi na kuanza ujenzi wa kambi za kudumu ikiwemo nyumba za wafanyakazi, ofisi, zahanati na sehemu za burudani. Aidha, Serikali itakamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 54 kutoka kwenye kituo cha kuzalisha umeme hadi Kidahwe na kuendelea na usambazaji wa umeme katika vijiji saba (7) vya Igamba, Mazungwe, Mwamila, Kazuramimba, Kalenge, Mlela na Kidahwe vinavyopitiwa na mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 27.94** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

**(iv) Mradi wa Kuzalisha Umeme Jua Shinyanga – MW 150**

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itakamilisha utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi huu inayohusisha uzalishaji wa **MW**

**50**. Aidha, TANESCO itakamilisha taratibu za kumpata Mkandarasi na Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuanza awamu ya pili itakayozalisha **MW 100**. Jumla ya **Shilingi bilioni 122.21** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(v) Ukarabati wa Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Hale MW 21**

**192. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali itakamilisha ukarabati na uboreshaji wa mitambo ya kufua umeme katika kituo cha Hale chenye uwezo wa kuzalisha **MW 21** ambapo kufikia mwezi Aprili utekelezaji umefikia asilimia 74. Jumla ya **Shilingi bilioni 2.5** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

**(vi) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kakono – MW 87.8**

**193. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali imepanga kulipa fidia wananchi wanaopisha eneo la mradi pamoja na kuanza hatua za awali za utekelezaji wa mradi huu utakaokuwa na uwezo wa kuzalisha **MW 87.8** pamoja na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 38.7 kutoka Kakono hadi Kyaka. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.54** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 30** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**b) Miradi ya Kuzalisha Umeme Iliyopo katika Hatua za Maandalizi**

**(i) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Ruhudji – MW 358**

**194. *Mheshimiwa Spika,*** kufuatia kukamilika kwa mradi wa JNHPP, Serikali imepanga kuanza utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji ya Mto Ruhudji mkoani Njombe utakaokuwa na uwezo wa kuzalisha **MW 358**. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kulipa fidia wananchi wanaopisha eneo la mradi; kuwapata Mshauri Mwelekezi na Mkandarasi wa ujenzi; na kuanza kazi za awali za ujenzi wa mradi.

Kiasi cha **Shilingi bilioni 100.16** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

**(ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rumakali – MW 222**

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi wa Rumakali **(MW 222)** mkoani Njombe unakwenda sambamba na utekelezaji wa mradi wa Ruhudji **(MW 358)** ambapo kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kulipa fidia wananchi wanaopisha eneo la mradi pamoja na kuwapata Mshauri Mwelekezi na Mkandarasi wa ujenzi. Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

**(iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Mtwara (MW 300)**

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea na maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa **MW 300** kwa kutumia gesi asilia mkoani Mtwara. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha mradi pamoja na kutafuta fedha za ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 200** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(iv) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Upepo MW 100 Kititimo Mkoa wa Singida**

**197.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahusu ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme wa **MW 100** kwa kutumia upepo pamoja na njia ya kusafirisha umeme ya kilomita 8 ya msongo wa kilovoti 220 na kituo cha kupoza umeme katika eneo la Kititimo katika Mkoa wa Singida. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha Upembuzi Yakinifu na kuanza utekelezaji wa mradi kupitia Sekta Binafsi. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.2** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo. **(v) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Jua MW 100 Wilaya ya Manyoni**

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itatekeleza mradi wa ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme wa **MW 100** kwa kutumia jua pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme wilayani Manyoni katika Mkoa wa Singida. Mazungumzo kati ya Serikali na Wawekezaji walioonesha nia yanaendea. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na majadiliano na wawekezaji binafsi ili kuwezesha utekelezaji wa mradi kupitia sekta binafsi. Jumla ya **Shilingi milioni 100** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(vi) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Jua MW 130 Zuzu Dodoma**

**199.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme wa **MW 130** kwa kutumia jua mkoani Dodoma utatekelezwa na Serikali kwa ushirikiano na sekta binafsi. Aidha, Serikali itaendelea kukamilisha majadiliano na mwekezaji binafsi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Jumla ya **Shilingi milioni 100** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili mradi huu.

**(vii) Mradi wa Kuzalisha Umeme Jua - MW 100 Same**

**200.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umepangwa kutekelezwa wilayani Same mkoani Kilimanjaro ambapo kazi zitakazotekelezwa ni kufanya Upembuzi Yakinifu na Tathmini ya Athari kwa Mazingira. Jumla ya **Shilingi bilioni 2.45** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

### C.1.2 MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUSAMBAZA UMEME

**201.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha umeme wa uhakika unapatikana katika maeneo yote nchini, Serikali itaendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme kwa kutekeleza miradi mbalimbali kama ifuatavyo:

**a) Miradi ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme iliyopo Katika Hatua za Utekelezaji**

**(i) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Dodoma**

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANESCO itaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 345 kutoka Chalinze hadi Dodoma na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Chalinze na Dodoma. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa mradi ikiwemo usanifu, uchunguzi wa udongo na usafishaji wa maeneo ya mradi; ununuzi wa vifaa vya mradi; ujenzi *(civil works);* na usimamishaji minara *(tower erections)*, ufungaji wa mitambo kwenye vituo vya kupoza umeme; na ufungaji nyaya za umeme *(stringing works)*. Jumla ya **Shilingi bilioni 200** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

**(ii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze - Kinyerezi - Mkuranga**

**203.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Chalinze, Kinyerezi hadi Mkuranga na vituo vya kupoza umeme vya Chalinze, Kinyerezi, Mkuranga na Morogoro. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kufanya usanifu, uchunguzi wa udongo na usafishaji wa maeneo ya mradi; ununuzi wa vifaa vya mradi; ujenzi *(civil works)* na usimamishaji minara *(tower erections);* ufungaji wa mitambo ya umeme kwenye vituo vya kupoza umeme; na ufungaji nyaya za umeme *(stringing works)*. Jumla ya **Shilingi bilioni 4** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 9.96** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

**(iii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Rufiji – Mkuranga**

**204.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu utahusisha ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 400 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha JNHPP hadi Mkuranga. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kufanya Upembuzi Yakinifu wa mradi pamoja na Tathmini ya Athari kwa Mazingira *(Environmental Impact Assesment)*. Jumla ya **Shilingi bilioni 4.62** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

**(iv) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Dar es Salaam – Tanga – Arusha**

**205.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Chalinze kwenda Segera (km 181), kilovoti 220 (km 90) kutoka Segera kwenda Tanga na kilovoti 220 (km 130) kutoka Chalinze kwenda Ununio kupitia Bagamoyo pamoja na vituo vya kupoza umeme katika maeneo hayo. Aidha, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kulipa fidia wananchi watakaopisha mradi na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 15** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 1.22** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

**(v) Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Ibadakuli Shinyanga Kilovoti 400/220/33**

**206.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha msongo wa Kilovoti 400/220/33 Ibadakuli - Shinyanga. Kazi zitakazofanyika ni uagizaji wa vifaa pamoja na usimikaji wa mitambo ya kupoza umeme. Jumla ya **Shilingi milioni 236** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 5** fedha za nje zimetengwa kupitia mradi wa Gridi Imara.

**(vi) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma (TAZA)**

**207.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa TAZA ambapo kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha ulipaji wa fidia (*supplementary compensations*) kwa maeneo yaliyosalia; kuendelea na ujenzi wa misingi ya nguzo na kuanza maandalizi ya kusimika nguzo za umeme kwa ajili ya kuvuta nyaya za umeme; kukamilisha ununuzi na usafirishaji wa vifaa hadi katika eneo la mradi; kukamilisha usanifu na kuendelea na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Iringa, Kisada, Mbeya, Tunduma na Sumbawanga; na kuendelea na ujenzi wa majengo kwa ajili ya uendeshaji wa kituo, nyumba za wafanyakazi, ghala la kutunza vifaa na nyumba za walinzi. Jumla ya **Shilingi bilioni 4.34**

fedha za ndani na **Shilingi bilioni 279.30** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

### (vii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma

**208.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na kazi za ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe mkoani Kigoma, upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi mkoani Kagera na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme pamoja na kukamilisha maboresho ya vituo vya kupoza umeme wa msongo kilovoti 33/11 vya Kasulu na Kigoma Mjini. Jumla ya **Shilingi bilioni 16.67** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji.

### (viii) Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (*National Grid Stabilization Project*) – Gridi Imara

**209.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi huu utahusisha kuendelea na ujenzi wa njia za kusafirisha na kusambaza umeme za msongo wa kilovoti 220, 132 na 33 na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme *(switching stations)* katika maeneo ya usambazaji umeme kwa miradi 21 iliyobaki kati ya miradi 27 ya Gridi Imara awamu ya kwanza. Jumla ya **Shilingi bilioni 250** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

### (ix) Mradi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Gridi ya Taifa *(Grid Modernisation, Rehabilitation and Upgrading)*-TTGRUP

**210.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kuboresha miundombinu ya umeme kwa kukarabati na kuboresha vituo vya kupoza umeme katika maeneo mbalimbali nchini ili kuongeza ufanisi katika Gridi ya Taifa. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuwapata Mtaalamu Msimamizi *(Supervision Consultant)* na Mkandarasi kwa ajili ya kufanya *grid modernization* pamoja na kuendelea na ukarabati na maboresho ya vituo vya kupoza umeme nchini. Jumla ya **Shilingi bilioni 24.42** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji mradi huu.

### (x) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Benaco hadi Kyaka

**211.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 166.17 kutoka Benaco hadi Kyaka mkoani Kagera. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kulipa fidia wananchi wanaopisha mradi; kumpata Mkandarasi; na kuanza utekelezaji wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 5.82** fedha za ndani na **Shilingi bilion 3** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo**.**

### (xi) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Makutopora hadi Tabora (SGR Lot 3) na kutoka Tabora hadi Isaka (SGR Lot 4) kwa ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme

**212.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme za msongo wa kilovoti 220 kutoka Makutopora hadi Tabora (SGR Lot 3) na kutoka Tabora hadi Isaka (SGR Lot 4) kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kufanya uthamini wa mali za wananchi wanaopisha mradi; kulipa fidia; na kuanza taratibu za kupata Wakandarasi. Jumla ya **Shilingi bilioni 25** fedha za ndani zimetengwa kupitia Fungu la SGR.

### (xii) Mradi wa Njia ya Kusafirishi Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Mwanza hadi Isaka kwa ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR Lot 5)

**213.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 230 kutoka Mwanza hadi Isaka kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme. Aidha, Serikali itakamilisha malipo ya fidia kwa Wananchi wanaopisha eneo la mradi na kuendelea na shughuli za ujenzi. Jumla ya **Shilingi bilioni 13.8** fedha za ndani zimetengwa kupitia Fungu la SGR.

**(b) Miradi ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme Iliyopo Katika Hatua za Maandalizi**

**(i) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 Kutoka Sumbawanga hadi Kigoma Kupitia Mpanda (Km 480) na Kituo cha Kupoza Umeme cha Mpanda**

**214.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Sumbawanga hadi Kigoma kupitia Mpanda yenye urefu wa kilomita 480 na kituo cha kupoza umeme Mpanda. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kufanya tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi; kuweka mipaka ya mkuza wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Sumbawanga kupitia Mpanda hadi Kigoma; na kutafuta fedha za kutekeleza mradi.

**(ii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 Kutoka Segera – Same – Lemugur (Kisongo) Arusha**

**215.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Segera hadi Lemugur (Kisongo) Arusha kupitia Same. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kukamilisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA); usanifu wa mradi; kufanya tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi; kuanza kulipa fidia; na kuendelea kutafuta fedha za utekelezaji wa mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 150** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(iii) Ujenzi wa Njia za Kusafirisha Umeme *(Submarine Cables)* Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar na Mafia**

**216.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANESCO itaendelea na utekelezaji wa miradi ya njia za kusafirisha umeme za msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 49.95 kutoka Ununio – Dar es Salaam kwenda Unguja na msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 87 kutoka Tanga kwenda Pemba kupitia chini ya Bahari *(submarine cables)*. Aidha, mradi huu unahusisha pia ujenzi

wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 109.2 kutoka Mkuranga hadi Mafia.

Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kuwapata Mshauri Mwelekezi wa usimamizi wa mradi pamoja na Mkandarasi wa ujenzi; kulipa fidia wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa mradi. Aidha, kukamilika kwa miradi hii kutaimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika Zanzibar na kuchochea ukuaji wa sekta za viwanda, biashara na kuimarisha upatikanaji wa huduma za kijamii ikiwemo afya, elimu na huduma nyingine. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.32** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 2.33** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

**(iv) Mradi wa Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Tanzania hadi Uganda (Ibadakuli - Masaka)**

**217.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 na urefu wa kilomita 566 kutoka Ibadakuli – Nyakanazi - Kyaka hadi Mutukula pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kyaka kwa ajili ya kuunganisha nchi ya Tanzania na Uganda kupitia Mkoa wa Kagera. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na taratibu za utwaaji wa ardhi na kumpata Mshauri Mwelekezi. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.82** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 3.66** fedha za nje zimetengwa.

**(v) Miradi ya Ujenzi wa Njia za Kusafirisha Umeme kwa Ajili ya Kuunga Gridi ya Taifa na Nchi za Jirani kwa Msongo wa Kilovoti 400 Kutoka Tanzania Hadi Malawi (TAMA); Kilovoti 400 Kutoka Tanzania Hadi Msumbiji (MOTA) na Kilovoti 400 Kutoka Tanzania hadi DRC**

**218.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kushirikiana na nchi jirani za Malawi, Msumbiji na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kupitia biashara ya kuuziana umeme ili pamoja na mambo mengine kuimarisha upatikanaji wa nishati hiyo, kukuza diplomasia ya uchumi na kuongeza mapato ya Serikali. Katika kufikia malengo hayo, Serikali itatekeleza miradi ya njia za umeme kwa ajili ya kuunganisha Gridi ya Taifa na nchi hizo. Kazi

zitakazofanyika ni kuanza taratibu za utwaaji wa ardhi ya mradi na kufanya Upembuzi Yakinifu wa ujenzi wa njia za kusafirisha umeme za msongo wa kilovoti 400 kutoka: Tanzania – Malawi; Tanzania – Msumbiji; na Tanzania – DRC ambapo majadiliano yanaendelea. Aidha, Serikali itaendelea kutafuta fedha za kutekeleza kazi hizo pamoja na uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 500** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

**(vi) Mpango Kabambe wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme Msongo wa Kilovoti 220 katika Majiji ya Mbeya, Arusha na Mwanza**

**219.** ***Mheshimiwa Spik***a, Serikali kupitia TANESCO itaanza kufanya Upembuzi Yakinifu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya usambazaji umeme ili kukidhi ongezeko la mahitaji na kupunguza upotevu wa umeme katika njia za usambazaji kwa Majiji ya Arusha, Mwanza na Mbeya. Mpango huu pia unahusisha ujenzi wa njia za mzunguko za kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220. Vilevile, utahusisha ujenzi wa vituo vipya vya kupoza umeme pamoja na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vilivyopo. Aidha, mpango huu unalenga kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika katika Majiji hayo. Jumla ya **Shilingi bilioni 1** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(vii) Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme katika Jiji la Dodoma**

**220.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekusudia kuendelea kuboresha muonekano wa Jiji la Dodoma kwa kuboresha na kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme katikati ya Jiji hilo na viunga vyake. Kazi zitakazofanyika ni kuendelea kubadilisha miundombinu ya usambazaji umeme inayotumia nguzo na kuweka miundombinu inayopita chini ya ardhi kwa kuanzia kituo cha kupoza umeme cha Mjini-Kati kwenda Ofisi za Bunge. Hatua hii itawezesha kuendelea kusambaza umeme wa uhakika na wenye kukidhi mahitaji kwa wateja wapya wanaoendelea kuongezeka Jijini Dodoma. Jumla ya **Shilingi milioni 200** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huo.

### (viii)Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Kupoza Umeme katika Kila Wilaya Nchini

**221.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Gridi ya Taifa katika Wilaya zote nchini hususan Wilaya ambazo hazina vituo hivyo. Mradi huu ni sehemu ya mradi wa Gridi Imara na unatekelezwa kwa awamu tano (5) ambapo kwa kila awamu vitajengwa vituo 15 vya kupoza umeme na tayari Upembuzi Yakinifu umeanza kufanyika katika awamu ya kwanza ya mradi huu. Mpango wa utekelezaji wa mradi kwa awamu nne (4) zilizobaki ni kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Na. 10A, 10B, 10C na 10D***. Utekelezaji wa mradi unalenga kuboresha miundombinu ya usambazaji na kupunguza upotevu wa umeme unaotokana na umbali mrefu wa njia za usambazaji umeme katika maeneo mbalimbali nchini. Jumla ya **Shilingi bilioni 5** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

### (ix) Miradi Mingine ya Matengenezo ya Mitambo Itakayotekelezwa

**222.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANESCO itaendelea kufanya matengenezo kinga katika vituo vya kuzalisha umeme, miundombinu ya usafirishaji, usambazaji pamoja na vituo vya kupoza umeme. Vilevile, TANESCO itaendelea kutekeleza miradi ya kuongeza uwezo wa miundombinu ya kusafirisha umeme, kuweka mifumo ya kisasa ya mawasiliano na kuboresha mfumo wa uendeshaji wa Gridi ya Taifa pamoja na kujenga vituo vidogo vya kuendesha Gridi *(unmanned substations)*. Miradi hii kwa kiasi kikubwa inatekelezwa na fedha za ndani za TANESCO. Aidha, Serikali imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 1.41** fedha za nje kwa ajili ya kazi hizo.

## C.1.3 UTENDAJI WA KAMPUNI TANZU ZA TANESCO (ETDCO, TCPM NA TGDC)

### a) Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji Umeme (ETDCO)

**223.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Kampuni Tanzu ya TANESCO ya ETDCO, itaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 132 kutoka Urambo hadi Kidahwe kupitia kituo cha kupoza umeme cha Nguruka ambacho kimekamilika kwa asilimia 99. Aidha, ETDCO itakamilisha utekelezaji wa miradi ya umeme katika vitongoji mkoani Mbeya inayosimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA); kuendelea na usambazaji wa umeme katika maeneo ya Kilindi na Simanjiro; na kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilometa 128 kutoka Masasi hadi Mahumbika.

### b) Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania (TCPM)

**224.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya TCPM itaendelea na uzalishaji na usambambazaji wa nguzo za zege kupitia kiwanda chake cha Tabora na viwanda vya ubia vitakavyokuwa vimekamilika. Aidha, TCPM itaanza taratibu za ujenzi wa kiwanda chake cha pili mkoani Mbeya na kuendelea kuingia ushirikiano *(joint venture)* na wawekezaji wazawa wa kujenga viwanda vya kuzalisha nguzo za zege katika mikoa ambayo haina viwanda hivyo.

### c) Kampuni ya Uendelezaji wa Rasilimali ya Jotoardhi (TGDC)

**225.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TGDC itaendelea na utekelezaji wa miradi ya jotoardhi kama ifuatavyo:

**(i)** ***Mradi wa Jotoardhi Ngozi (Mbeya) – MW 70:*** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na ukodishaji wa ardhi; ulipiaji wa leseni ya eneo la mradi; uchorongaji wa visima vitatu (3) vya uhakiki; ukusanyaji

na uchakataji wa taarifa za visima; na kuanza taratibu za ununuzi wa mtambo mdogo wenye uwezo wa kufua **MW 5** za umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 10.00** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**(ii)** ***Mradi wa Jotoardhi Kiejo-Mbaka (Mbeya) – MW 60:*** kazi zitakazotekelezwa ni uchorongaji wa visima vitatu (3) vya uhakiki; kuendelea na ulipiaji wa leseni ya eneo la mradi; kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya usanifu wa uchorongaji wa visima; kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya barabara na maji; na ununuzi wa vifaa vya uchorongaji *(drilling consumables)*. Jumla ya **Shilingi bilioni 11.00** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 10.37** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(iii)** ***Mradi wa Jotoardhi Natron (Arusha) – MW 60:*** kazi itakayotekelezwa ni kukamilisha utafiti wa kina wa kijiosayansi wa juu ya ardhi *(detailed surface exploration)* katika eneo la mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 350** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 1.23** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

### C.1.4 MIRADI YA NISHATI VIJIJINI

**226.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA itaendelea kutekeleza programu na miradi mbalimbali ya nishati vijijini ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kijamii katika maeneo hayo. Programu na miradi itakayotekelezwa ni kama ifuatavyo:

#### a) Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji Awamu ya Pili B (*Hamlet* Eletrification Project – HEP IIB)

**227.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaanza utekelezaji wa mradi wa uunganishaji wa umeme katika vitongoji 9,009 kwa kujenga miundombinu ya kilomita 13,180.56 za njia za msongo wa kati, kilomita 14,016.50 za msongo mdogo, ufungaji wa transfoma 8,003

za kVA 100 na 1,006 za kVA 200, na uunganishaji wa wateja wa awali 290,300. Gharama ya mradi huu ni takriban **Shilingi trilioni 1.39** ambapo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3). Kwa Mwaka 2025/26, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 350.00** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 2.26** fedha za nje kutoka Serikali ya Norway kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

**b) Mradi wa Kuunganisha Wateja – *Last Mile Customer Connection***

***228. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mpango Mahsusi wa Taifa wa Nishati (National Energy Compact 2025 - 2030) inakusudia kuunganisha watumiaji wa umeme kufikia asilimia 75 ifikapo mwaka 2030. Katika kufikia azma hiyo, Serikali kupitia REA inakusudia kutekeleza mradi wa kuunganisha wateja 40,000 katika maeneo ya vijijini na vijiji - miji. Utekelezaji wa awali (pilot project) utaanza katika mikoa mitatu (3) ambayo ni Morogoro, Dodoma na Pwani. Jumla ya Shilingi bilioni 2 fedha za nje kutoka Benki ya Dunia zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

**c)Mradi wa Ujazili Awamu ya Pili B *(Rural* Electrification Densification II B Project)**

**229.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itakamilisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji umeme kwenye vitongoji 1,686 katika mikoa tisa (9) ya Arusha, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Morogoro, Njombe na Songwe ambapo kazi za mradi zinahusisha ujenzi wa njia za msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 3,860, ufungaji wa transfoma 1,272 na uunganishaji wateja wa awali 95,334. Jumla ya **Shilingi bilioni 28.89** fedha za nje kutoka Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

**d) Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji Mkoa wa Lindi (*Hamlet Electrifcation* Project - Lindi)**

**230.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kushirikiana na Serikali ya Norway katika utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa umeme katika Mkoa wa Lindi. Mradi huu unahusisha ujenzi wa

miundombinu ya usambazaji umeme kwenye vitongoji 293 katika mkoa huo kwa kujenga kilomita 254.5 za msongo wa kati, kilomita 644.6 za msongo mdogo, ufungaji wa transfoma 293 na uunganishaji wa wateja wa awali 9,669. Jumla ya **Shilingi bilioni 2** fedha za nje kutoka Serikali ya Norway zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**e) Mradi wa Ufungaji wa Mifumo ya Umeme Jua Katika Maeneo ya Visiwani na Yaliyo Mbali na Gridi ya Taifa**

**231.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA itaendelea na utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme unaozalishwa kutokana na jua katika maeneo ya visiwani na yaliyo mbali na Gridi ya Taifa. Mradi huu unahusisha ufungaji wa mifumo ya umeme jua 6,000 kwenye kaya na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza na kuunganisha wateja 3,200. Mradi huu utanufaisha jumla ya visiwa 120. Jumla ya **Shilingi bilioni 15** fedha za nje kutoka Benki ya Dunia zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

**f) Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia**

**232.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 – 2034) kwa lengo la kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034. Katika kufikia lengo hilo, Serikali katika Mwaka 2025/26 itatekeleza shughuli mbalimbali zikiwemo kuendelea kusambaza mitungi ya LPG kwa bei ya ruzuku, kusambaza majiko banifu 370,000 katika maeneo ya vijiji na vijiji-miji *(Peri Urban)*; kuwapata wasambazaji na kusambaza majiko 40,000 yanayotumia umeme katika maeneo ya pembezoni mwa vijiji-miji *(peri-urban)* ambayo yatauzwa kwa bei ya ruzuku na wasambazaji na kuanza kutekeleza mradi; kuendelea kutoa ruzuku kwa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ili liweze kununua na kufunga mashine moja (1) ya kuzalisha mkaa wa mawe wa kupikia kutokana na makaa ya mawe *(Rafiki Briquette)*; na kusambaza mitambo 50 ya kutengeneza mkaa mbadala na kutoa mafunzo ya utengenezaji wa mkaa kwa makundi maalum

ya wanawake na vijana. Serikali imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 4.70** fedha za nje kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

**233.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwezesha ufungaji wa mifumo ya nishati safi ya kupikia katika Taasisi za umma zinazolisha zaidi ya watu 100 kwa siku, Serikali itafunga mifumo ya nishati safi ya kupikia kwa Taasisi za Umma 400 zikijumuisha shule kongwe, vyuo vya ufundi na magereza. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kufanya tathmini ya mahitaji ya nishati ya kupikia katika taasisi hizo ili kubaini kiasi na aina ya nishati ya kupikia inayofaa kutumika kwa kila taasisi nufaika; kuwapata wasambazaji wa mifumo hiyo; na kuanza utekelezaji wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zitatumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

### g) Kuwezesha Ufungaji wa Mitambo ya Kukausha Dagaa

**234.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Nishati Vijijini kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) inakusudia kuanzisha vituo vya kukausha dagaa vinavyotumia nishati safi na endelevu ya kukuza matumizi ya mwanga wa jua na nishati ya gesi (LPG) katika shughuli za kuchemsha, kukaanga na kukausha dagaa. Mpango huu utawezesha kuongeza thamani ya zao la dagaa, kupunguza hasara baada ya mavuno na kuboresha ubora na hivyo kuboresha maisha ya wavuvi, wasindikaji na wafanyabiashara wa zao hilo. Mradi huu pia utatoa mafunzo kwa wanufaika ili kujifunza mbinu bora na endelevu kwa ajili ya kukuza biashara ya dagaa na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Serikali imetenga **Shilingi bilioni 10** fedha za nje kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kufanya tathmini ya maeneo yanayohitaji vituo hivyo na kuanza utekelezaji wa mradi.

### h) Kufanya Tathmini ya Matokeo ya Miradi *(Impact Evaluation)* Iliyotekelezwa na Wakala na Nishati Vijijini

**235.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itafanya tathmini ya miradi iliyotekelezwa na REA katika kipindi cha miaka minne (4) kuanzia mwaka 2021/22 hadi 2024/25 ikiwa ni takwa la kisheria la kufanya

tathmini ya miradi hiyo kila baada ya miaka minne. Tathmini hiyo itatoa mrejesho wa utekelezaji wa miradi ya nishati vijijini kwa Serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo wanaoshirikiana na Serikali katika miradi ya nishati vijijini. Aidha, matokeo ya tathmini hiyo yatatumika kuboresha mipango mbalimbali ya ufikishaji na utumiaji wa nishati katika maeneo ya vijijini na vijiji – miji. Jumla ya **Shilingi bilioni 1** fedha za nje kutoka Benki ya Dunia zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya tathmini hiyo.

### C.1.5 USHIRIKISHWAJI WA SEKTA BINAFSI KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UMEME

**236.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuvutia Sekta Binafsi katika miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini. Miradi hiyo inajumuisha uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo jadidifu na mbadala ikiwemo upepo, jua, maji, jotoardhi, tungamotaka, makaa ya mawe na gesi asilia. Aidha, Serikali itafanya tathmini na kutangaza miradi yote yenye utayari *(readiness projects)* kwa njia ya zabuni ili iweze kutekelezwa kupitia mfumo wa EPC na kutoa fursa kwa kampuni binafsi zenye nia ya kuwekeza katika miradi ya umeme kuweza kushiriki kikamilifu. Vilevile, Serikali itaendelea kuwashirikisha wawekezaji binafsi katika utekelezaji wa miradi ya usafirishaji na usambazaji wa umeme hususan katika maeneo ya uzalishaji ya viwanda na migodi ambapo uchambuzi wa maeneo ya miradi utafanyika kabla ya kuingia makubaliano na wawekezaji.

**237.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea pia kushirikiana na sekta binafsi katika miradi ya nishati vijijini. Ili kuimarisha zaidi ushiriki wa kampuni za ndani, REA imeweka utaratibu wa kutangaza zabuni za miradi katika mafungu madogo madogo *(lots)* ili sekta binafsi za wazawa waweze kukidhi vigezo vya kushiriki katika zabuni hizo. Aidha, Serikali kupitia REA itaendelea kutoa fursa ya mikopo yenye riba nafuu kwa waendelezaji binafsi wa miradi ya umeme katika maeneo yaliyopo mbali na Gridi ya Taifa. Mikopo hiyo inatolewa kupitia dirisha maalum linalosimamiwa na Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) ambayo imeingia mkataba na REA kusimamia mikopo hiyo. Kupitia dirisha hilo Serikali imepunguza

gharama za uwekezaji kwa sekta binafsi katika miradi ya umeme vijijini. Vilevile, Serikali kupitia REA itaendelea kutoa fursa za mikopo nafuu kwa waendelezaji wa vituo vya mafuta vijijini kupitia utaratibu ulioainishwa kwenye Mwongozo wa Kutekeleza Mradi wa Kuwezesha Ujenzi wa Vituo Vidogo vya Kuuza Mafuta Vijijini.

### C.1.6 UTEKELEZAJI WA MIPANGO NA MIKAKATI MBALIMBALI YA UENDELEZAJI WA SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU

**238.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Nishati itaendelea kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Mipango na Mikakati mbalimbali iliyojiwekea kwa ajili ya kuimarisha na kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme na Nishati Jadidifu nchini. Mipango na Mikakati hiyo ni Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme *(Power System Master Plan 2020 Update)*; Mpango Kabambe wa Kupeleka Nishati Vijijini *(Rural Energy Master Plan - REMP)* wa Mwaka 2022; Mkakati wa Nishati Jadidifu *(Renewable Energy Strategy and its Implementation Roadmap)* wa mwaka 2024 -2034*;* Mkakati wa Matumizi Bora ya Nishati (*Energy Efficiency Strategy*) wa Mwaka 2024 - 2034; Mpango Mahsusi wa Taifa wa Nishati *(National Energy Compact 2025 - 2030);* na Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya kupikia *(National Clean cooking Strategy 2024-2034)*. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu pamoja na kusimamia uandaaji wa Mkakati *wa* Maboresho ya Sekta Ndogo ya Umeme (*Electricity Supply Industry Reform Strategy and Roadmap – ESI-RSR)*.

### C.2: SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI

**239.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26, Serikali itaendelea kuchukua hatua za kuendeleza na kusimamia Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi kwa kuchukua hatua mbalimbali, kwa lengo la kuhakikisha mchango wa Sekta hiyo katika Pato la Taifa unaendelea kuimarika.

## C.2.1: MIRADI YA UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI

**240.** ***Mheshimiwa Spika***, Mwelekeo wa Serikali na Wizara ninayoiongoza ni kuona siku moja, Shirika letu la Maendeleo ya Petroli (TPDC) linakuwa Kampuni Kubwa ya Mafuta na Gesi Asilia yenye ushiriki mkubwa katika shughuli za mnyororo wote wa thamani wa mafuta na gesi asilia kwa Tanzania na Kikanda. Katika kuliendea na kufanikisha azma hiyo, ushiriki wa TPDC katika shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji katika Vitalu vyake yenyewe ni wa muhimu sana ili siku moja TPDC imiliki na kuendesha Kitalu kinachozalisha mafuta na gesi asilia. Katika mwaka 2025/26, kwa upande wa utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika Vitalu vya Kimkakati, Serikali kupitia TPDC imepanga kufanya yafuatayo:

### (i) Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini

**241.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TPDC itaendelea kufanya stadi za kijiolojia na kijiofizikia na kuandaa mpango wa uchorongaji kisima katika mashapo yaliyogundulika; pamoja na kutafuta mbia *(strategic partner)* mwenye uzoefu, utaalamu na fedha atakayeshirikiana na TPDC katika uchorongaji wa kisima cha utafutaji. Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

### (ii) Kitalu cha Eyasi – Wembere

**242.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha uchukuaji wa taarifa za mtetemo za mfumo wa 2D za urefu wa kilometa 484.7; na kuchakata na kutafsiri taarifa za mtetemo za mfumo wa 2D za urefu wa kilomita 1,174.7. Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

### (iii) Kitalu cha Songo Songo Magharibi

**243.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC itaendelea na shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika kitalu hiki

ambapo kazi zitakazo tekelezwa ni pamoja na: ukusanyaji na uchakataji wa taarifa za mitetemo za mfumo wa 3D katika eneo la kilomita za mraba 240; na kumtafuta mbia *(strategic partner)* mwenye uzoefu na utaalamu wa kiteknolojia na fedha wa kushirikiana na TPDC katika hatua ya kuchoronga kisima cha utafutaji. Jumla ya **Shilingi bilioni 54.7** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

### (iv) Kitalu cha Lindi-Mtwara

**244.** ***Mheshimiwa Spika,*** TPDC itaendelea na uchukuaji wa taarifa za mitetemo za mfumo wa 3D katika eneo la kilomita za mraba 780 na kuchakata na kutafsiri taarifa hizo. Jumla ya **Shilingi bilioni 47.19** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya shughuli hizo.

## C.2.2: MIRADI YA UENDELEZAJI NA UZALISHAJI WA GESI ASILIA

### (i) Kitalu cha Ruvuma (Eneo la Ntorya)

**245.** ***Mheshimiwa Spika,*** TPDC itaendelea kushirikiana na Kampuni ya ARA Petroleum katika shughuli za uendelezaji wa gesi asilia katika eneo la Ntorya. Shughuli hizo zitahusisha ujenzi wa miundombinu itakayowezesha kuanza uzalishaji katika visima vya ugunduzi vya Ntorya1 & 2 na kuchoronga kisima cha utafutaji cha Chikumbi -1. Aidha, kama sehemu ya CSR ya mradi, ujenzi wa Kituo cha Afya cha Dihimba utaanza pamoja na uchimbaji wa kisima cha maji katika eneo la kata ya Namayakata shuleni. Jumla ya **Shilingi bilioni 11.82** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

### (ii) Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(Liquefied Natural Gas – LNG)*

**246.** ***Mheshimiwa Spika***, katika maandalizi ya utekelezaji wa mradi huu kwa mwaka 2025/26 Serikali itatekeleza kazi mbalimbali ikiwemo: kuendelea kuwajengea uelewa wananchi kuhusu umuhimu na manufaa ya mradi; kushiriki katika utayarishaji wa mpango wa uendelezaji *(Development Plan)*; kuendelea na majadiliano na wawekezaji; kumpata Mshauri Mwelekezi

atakayeishauri Serikali kuhusu mikataba itakayoingiwa baada ya kusainiwa kwa mkataba wa nchi hodhi (HGA) na Mkataba wa Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (PSA) kati ya Serikali na wawekezaji; na kuendelea na utekelezaji wa miradi ya uwajibikaji kwa jamii kwa kushirikiana na kampuni za Shell na Equinor. Miradi hiyo ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa shule ya msingi ya Likong'o katika Manispaa ya Lindi; na uboreshaji wa hali ya maisha kwa wanachi waliopisha eneo la mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

### C.2.3: MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI WA GESI ASILIA

**247. *Mheshimiwa Spika*,** matumizi ya gesi asilia yana faida mbalimbali ikiwemo kupunguza matumizi ya hewa ukaa majumbani na uchafuzi wa mazingira kutokana na matumizi ya mkaa, kupunguza gharama ya nishati kwa watumiaji, kuokoa fedha za kigeni kwa matumizi ya gesi kama nishati mbadala, kuchochea uwekezaji katika viwanda na manufaa mengineyo. Kutokana manufaa hayo, azma ya Serikali ni kuona siku moja nchi yetu inakuwa na mtandao wa mabomba ya usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia ulioenea maeneo mbalimbali nchini ili kuweza kuwafikishia Watanzania nishati ya gesi asilia kama nishati mbadala kwa shughuli mbalimbali ikiwemo uzalishaji viwandani, kuzalisha umeme, matumizi katika taasisi na majumbani pamoja na kwenye vyombo vya moto kama mbadala wa mafuta. Katika kuiendea azma hiyo, shughuli na miradi ya kuongeza mtandao wa usambazaji wa gesi asilia nchini ni endelevu ambapo katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali kupitia TPDC imejipanga kutekeleza yafuatayo:

#### (i) Ujenzi wa vituo vya kujazia gesi asilia vinavyohamishika (*Mobile Compressed Natural Gas Stations*)

**248. *Mheshimiwa Spika*,** kazi zitakazotekelezwa katika mradi huu zitahusisha kuendelea na ujenzi wa vituo vidogo vitatu (3) vinavyohamishika vilivyo na miundombinu ya kujazia gesi asilia

katika magari. Aidha, vituo vitatu (3) vya kujazia gesi vinavyohamishika vitajengwa katika mikoa ya Morogoro na Dodoma, ambapo kila kituo kitakua na uwezo wa kuhudumia angalau magari mia tatu (300) kwa siku. Vituo hivi vitapokea gesi kwa njia ya magari kutoka katika kituo mama kilichopo katika eneo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kiasi cha **shilingi bilioni 8.26** zitatumika kutekeleza kazi za mradi.

### (ii) Mradi wa Usambazaji wa Gesi Asilia Mkoa wa Dar es Salaam

**249.** ***Mheshimiwa Spika***, kufikiwa kwa malengo ya Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 - 2034), hususan kuwezesha angalau asilimia 80 ya Watanzania kuwa wanatumia nishati hiyo ifikapo mwaka 2034 kunahusisha pia kuwawezesha wananchi kutumia gesi asilia katika kupikia. TPDC imejipanga kuunganisha nyumba na Taasisi 1,000 zilizopitiwa na miundombinu ya mabomba ya gesi asilia katika mikoa ya Dar es Salaam. Kazi zitakazotekelezwa katika mradi huu ni pamoja na kuongeza mtandao wa usambazaji wa gesi asilia kwa njia za mabomba kutoka katika miundombinu ya usambazaji wa gesi iliyopo Mbezi beach, Temeke na Mikocheni pamoja na miundombinu wezeshi. Aidha, TPDC itakamilisha kazi ambazo utekelezaji wake umeanza katika mwaka 2024/25 zinazohusisha ujenzi wa bomba la kusambaza gesi asilia katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam (DUCE), uunganishwaji wa mfumo wa kutumia gesi asilia katika maabara na migahawa mitatu (3) iliyopo chuoni hapo na migahawa 12 iliyopo katika eneo la kibiashara la Mlimani City. Jumla ya **Shilingi bilioni 8.11** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

### (iii) Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mkoa wa Pwani

**250.** ***Mheshimiwa Spika***, Uwepo wa gesi asilia nchini unaendelea kuvutia wawekezaji wengi nchini kujenga viwanda na kuzalisha bidhaa mbalimbali ambapo kwa upande wa mkoa wa Pwani, Kongani ya viwanda ya SINOTAN iliyopo Kwala Kibaha Mkoani Pwani, ni mojawapo ya eneo la kimkakati ambalo linatarajiwa kuvutia wawekezaji wengi kujenga viwanda mbalimbali zaidi ya

2,000. TPDC imejipanga kujenga bomba la kusafirisha gesi asilia lenye urefu wa kilomita 102 kutoka Dar es Salaam kuelekea Chalinze mkoani Pwani na kuweka matoleo eneo la Kwala ambapo kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kutafuta mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu hiyo ili kuanza kazi za ujenzi. Jumla ya **Shilingi bilioni 69.6** fedha za ndani zimetengwa kutekeleza kazi za mradi.

### (iv) Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Gesi kutoka Ntorya (Kitalu cha Ruvuma) hadi Madimba

**251.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya gesi asilia nchini, Kitalu cha Ruvuma ni cha kimkakati ambapo kitakapoanza uzalishaji wa gesi asilia kitasaidia kuongeza upatikanaji wa gesi asilia kwa matumizi mbalimbali nchini. Serikali kupitia TPDC itaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia lenye urefu wa kilomita 34.2 kutoka eneo la Ntorya (Kitalu cha Ruvuma) hadi Madimba kwa ajili ya kuchakatwa. Bomba hili litakuwa na kipenyo cha inchi 14 na uwezo wa kubeba futi za ujazo milioni 140 kwa siku. Jumla ya **Shilingi bilioni 23.2** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi za mradi.

### (v) Mradi wa Usambazaji wa Gesi Asilia kwa Ufadhili wa Mfuko wa Nishati Vijijini Unaosimamiwa na REA

**252.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC na REA inatekeleza mradi wa usambazaji wa nishati ya gesi asilia katika vijiji vya mikoa ya Pwani na Lindi ambapo jumla ya nyumba za awali 980 (Lindi – 451 na Pwani - 529) zitaunganishwa na miundombinu ya gesi hiyo. Kwa sasa Mkandarasi anaendelea na ujenzi wa miundombinu na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Septemba 2025. Mradi huu unagharimu **Shilingi bilioni 6.23.** Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza matumizi ya gesi asilia majumbani na hivyo kuchangia matumizi ya nishati hiyo katika maeneo ya vijijini.

**(vi) Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mkoa wa Dodoma**

**253.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika Mji wa Serikali Mtumba mkoani Dodoma. Mradi pia unahusisha ununuzi wa vifaa kwa ajili ya usafirishaji wa gesi asilia kutoka kituo mama cha kujazia gesi cha Dar es Salaam (*UDSM CNG Mother Station*), ujenzi wa kituo cha kupokelea gesi hiyo katika Mji wa Serikali Mtumba, ujenzi wa mtandao wa usambazaji wa gesi katika majengo ya Mji wa Serikali Mtumba na ujenzi wa kituo cha kujaza gesi cha CNG (CNGV) kitakachojengwa Mtumba. Kazi zitakazotekelezwa ni ujenzi wa miundombinu ya kupokelea gesi asilia pamoja na ujenzi wa kituo cha kujaza gesi cha CNG eneo la Mtumba. Jumla **Shilingi bilioni 9.65** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

**C.2.4: MIRADI YA KUSAFIRISHA GESI ASILIA KWENDA NCHI JIRANI**

**254.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwelekeo wa Serikali ni kuona siku moja Tanzania inakuwa kitovu cha upatikanaji wa nishati ya gesi asilia katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini. Azma hii itahusisha uunganishwaji wa mabomba ya kusafirisha gesi asilia kutoka Msumbiji katika miundombinu ya Taifa ya Gesi Asilia na kujenga bomba la kusafirisha gesi kwenda nchi za Kenya, Uganda, Zambia na nyingine zitakazoinyesha nia ya kupatiwa nishati hiyo. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali kupitia TPDC katika mwaka 2025/26 imejipanga kutekeleza yafuatayo:

**(i) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia Kutoka Tanzania hadi Uganda**

**255.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Dar es Salaam hadi Uganda. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuanza hatua za awali za Upembuzi Yakinifu ambao utasaidia kubainisha gharama, masuala ya kiufundi na mahitaji ya gesi asilia katika maeneo

yatakayopitiwa na bomba hilo. Jumla ya **Shilingi milioni 483.84** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(ii) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia Kutoka Tanzania hadi Kenya**

**256.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kujenga bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Dar es Salaam hadi Mombasa (Kenya). Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kukamilisha uidhinishwaji wa nyaraka muhimu za mradi (*Bilateral Agreements & Joint Procurement Rules*), na nyaraka za zabuni ya kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya Upembuzi Yakinifu. Jumla ya **Shilingi milioni 502.24** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**C.2.5: MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUHIFADHI MAFUTA**

**257.** ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imekuwa ikihudumia nchi jirani katika kupitisha mafuta yao kwa matumizi mbalimbali ambapo Tanzania imekua ikinufaika kwa kampuni zetu kupata biashara za usafirishaji, kodi na ajira kwa wananchi wetu. Vilevile, ni azma ya Serikali kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa kitovu cha uagizaji na usafirishaji wa mafuta kwa matumizi ya ndani na majirani zetu ikiwa ni pamoja na nchi yetu kutumika kama kitovu cha kupokea na kusafirisha mafuta ghafi kutoka nchi jirani ambapo kwa mwaka 2025/26, Serikali kupitia TPDC imejipanga kutekeleza yafuatayo:

**a) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania *(East African Crude Oil Pipeline -* EACOP)**

**258.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa katika mradi huu ni pamoja na kushiriki kwenye uwekezaji wa mtaji katika kampuni; kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha mradi; kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu utekelezaji wa mradi na fursa zilizopo hususan katika maeneo yanayopitiwa na mradi; na kuendelea na kazi za ujenzi hususan katika maeneo ya kambi, matenki ya kupokelea mafuta, gati na vituo vya kupunguza

msukumo wa mafuta. Jumla ya **Shilingi bilioni 100** fedha za ndani zimetengwa kutekeleza kazi za mradi huu.

**b) Ujenzi wa Miundombinu ya Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta Pamoja na Miundombinu ya Kuwezesha Biashara ya Mafuta**

**(i) Uanzishaji wa Hifadhi za Mafuta katika maeneo ya Kimkakati na Ukarabati wa Tenki Namba 8**

**259.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC imedhamiria kuanzisha hifadhi ya kimkakati ya mafuta nchini ambapo katika mwaka 2025/26 Andiko la mradi ambalo limezingatia maoni ya wadau mbalimbali wa sekta ya mafuta litakamilishwa na kuwasilishwa Serikalini kwa ajili ya hatua za maamuzi. Aidha, TPDC itaanza ukarabati wa Tenki Na. 8 ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 3.89** fedha za ndani zimetengwa kutekeleza kazi hizo.

**(ii) Ukarabati wa Vituo Vitatu (3) vya Mafuta Vilivyopo Segera (Tanga), Musoma na Tarime (Mara) Pamoja na Kujenga Kituo kipya Kimoja (1) Makuyuni (Arusha)**

**260.** ***Mheshimiwa Spika***, TPDC inatarajia kuanza ukarabati wa vituo vya mafuta vya Segera, Musoma na Tarime kuanzia mwezi Agosti 2025 baada ya kupata vibali kutoka NEMC pamoja na kuwapata Wakandarasi watakaotekeleza kazi hizo. Ukarabati huo unakadiriwa kufanyika kwa muda wa miezi sita. Aidha, ujenzi wa kituo kipya cha Makuyuni unatarajia kuanza mwezi Agosti 2025 kwa muda wa miezi minane.

**(iii) Mradi wa Usimamizi wa Rasilimali za Ndani na Utawala wa Rasilimali za Asili Tanzania**

**261.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha kazi ya uandaaji wa Mpango Mkakati wa Kuendeleza na Kuhamasisha Matumizi ya Gesi ya Mitungi (LPG) na gesi ya CNG kwa ajili ya vyombo vya moto; kukamilisha ununuzi wa kituo cha CNG kinachohamishika (Mobile CNG); na kuendelea kuwajengea uwezo wataalam wa Serikali kupitia mafunzo ya

muda mfupi kuhusu masuala ya mafuta na gesi. Jumla ya **Shilingi bilioni 4.3** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi za mradi huu.

### C.2.6: UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMPUNI TANZU

#### a) TANOIL

**262.** ***Mheshimiwa Spika,*** TANOIL itaendelea kushiriki katika biashara ya kununua na kuuza mafuta kwa jumla na rejareja; na kukamilisha kazi ya kufanya utafiti wa awali ili kuweza kuingia katika biashara ya LPG na vilainishi vya vyombo vya moto na mitambo. TPDC kupitia TANOIL inatarajia kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 345.37** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza shughuli hizo.

#### b) GASCO

**263.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya GASCO itaendelea kutekeleza majukumu yake ya uendeshaji na matengenezo ya miundombinu ya gesi asilia nchini pamoja na vituo vya CNG vinavyomilikiwa na TPDC. Vilevile, GASCO itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia majumbani, viwandani, taasisi na katika vituo vya CNG. TPDC kupitia GASCO imetenga **Shilingi bilioni 101.38** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza shughuli hizo.

### C.2.7 UDHIBITI WA MASUALA YA MKONDO WA JUU WA PETROLI KUPITIA PURA

**264.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia PURA itafanya tathmini ya zabuni zitakazowasilishwa pamoja na kuandaa mikataba ya Uzalishaji na Ugawanaji Mapato *(Production Sharing Agreement - PSA)* kwa wawekezaji watakaoshinda zabuni hizo. Aidha, PURA itafanya maboresho ya usimamizi wa taarifa za mkondo wa juu wa petroli kwa kusimika programu maalum za kisasa za kuchakata na kutafsiri taarifa hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi na upatikanaji wa taarifa za petroli kwa ajili ya uwekezaji kwenye shughuli za mkondo wa juu wa petroli. PURA itasimamia na kuhakikisha Watanzania wanashiriki katika miradi ya

utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia hususan katika shughuli za uchorongaji wa visima ili kuongeza ujuzi kwa wataalamu wa ndani. Vilevile, PURA itaendelea na kaguzi na usimamizi wa shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa gesi asilia nchini katika vitalu vya utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini. Jumla ya **Shilingi bilioni 6.77** fedha za ndani zimetengwa ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za udhibiti za mkondo wa juu wa petroli nchini.

### C.2.8 UDHIBITI WA MASUALA YA NISHATI KUPITIA EWURA

**265.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/26 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) itaendelea kusimamia Sekta ya Nishati nchini kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma iliyo bora na uhakika na kuimarisha ustawi wa jamii ya Watanzania. Mamlaka pia imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 2.98** kwa ajili ya kukamilisha usanifu na kuanza ujenzi wa Ofisi za Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kaskazini ambapo kukamilika kwa ofisi hizi kutaongeza tija zaidi katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

### C.2.9 KUIMARISHA UTENDAJI KAZI NA UTOAJI HUDUMA

**266.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya kuimarisha utendaji, Wizara na Taasisi zake zinatarajia kuajiri watumishi 1,071 na kupandisha vyeo watumishi 1,901. Aidha, jumla ya watumishi 606 wanatarajiwa kuhamia Wizarani na katika Taasisi za Wizara kwa lengo la kukabiliana na upungufu wa watumishi. Vilevile, jumla ya watumishi 6,204 watajengewa uwezo kupitia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili kuongeza tija katika utendaji. Pia, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi ikiwa ni pamoja na kuwapatia vitendea kazi ili kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao.

## C. USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA KATIKA SEKTA YA NISHATI

**267.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara inaendelea kushirikiana na washirika mbalimbali wa maendeleo, Jumuiya za

Kikanda, nchi wahisani na wadau wengine katika utekelezaji wa miradi ya nishati. Kwa niaba ya Serikali, napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo, Jumuiya na nchi wahisani ambao wameendelea kushiriki katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara na maendeleo ya Sekta ya Nishati kwa ujumla. Napenda kutambua mchango wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB); Benki ya Dunia (WB); Arab Bank for Economic Development in Afrika (BADEA); Economic Development Cooperation Fund (EDCF - Korea); Geothermal Risk Mitigation Facility (GRMF) pamoja na Taasisi na Mashirika ya JICA (Japan), KfW (Germany), AFD (Ufaransa); Shirika la Fedha Duniani (IMF); Sida (Sweden), NORAD (Norway); Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Mitaji ya Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNCDF), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO), Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA); Saudi Fund for Development (SFD); OPEC Fund for International Development; na Abu - Dhabi Fund for Development (ADFD).

**268.** ***Mheshimiwa Spika***, nitumie nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa Serikali za Afrika Kusini, Algeria, Angola, Burundi, Canada, China, Ethiopia, Falme za Kiarabu, Japan, India, Indonesia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Korea Kusini, Malawi, Misri, Morocco, Msumbiji, Namibia, Norway, Oman, Rwanda, Saudi Arabia, Sweden, Ufaransa, Uganda, Ujerumani, Urusi, Zambia na nchi nyingine kwa kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kuendeleza Sekta ya Nishati. Aidha, nazishukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Afrika (AU) kwa ushirikiano katika masuala ya kikanda yanayohusu Sekta ya Nishati.

## E. HITIMISHO

**269.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia umuhimu wa Sekta ya Nishati kiuchumi na kijamii na mchango wake mkubwa katika maendeleo ya Sekta nyingine mijini na vijijini, katika mwaka 2025/26 Wizara itaendelea kutekeleza mikakati, programu na miradi mbalimbali inayolenga kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na nishati ya uhakika, nafuu na endelevu. Aidha, mwelekeo

wa Serikali ni kuhakikisha shughuli za mafuta na gesi asilia zinakuwa na kushamiri zaidi na mchango wake katika Pato la Taifa unaendelea kuimarika. Katika kufikia azma hiyo, Wizara itaendelea kushirikiana na Wadau mbalimbali katika uendelezaji wa Sekta hii muhimu na pia kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa programu na miradi ya nishati inayotekelezwa ili malengo na manufaa yaliyokusudiwa yaweze kupatikana kwa wakati na viwango stahiki.

**270.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe Bajeti ya jumla ya **Shilingi Trilioni Mbili, Bilioni Mia Mbili Arobaini na Sita, Milioni Mia Saba Arobaini na Tano, Mia Nne Arobaini na Tano Elfu** (**Shilingi 2,246,745,445,000)** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

**(i)** **Shilingi Trilioni Mbili, Bilioni Mia Moja Sitini na Saba, Milioni Mia Tano Kumi na Tatu, Mia Mbili Kumi na Tisa Elfu (Shilingi 2,167,513,219,000)** sawa na asilimia **96.5** ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Nne Sitini na Sita na Milioni Ishirini, Mia Mbili Sabini na Nne Elfu (Shilingi 1,466,020,274,000)** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Mia Saba na Moja, Milioni Mia Nne Tisini na Mbili, Mia Tisa Arobaini na Tano Elfu (Shilingi 701,492,945,000)** ni fedha za nje; na

**(ii)** **Shilingi Bilioni Sabini na Tisa, Milioni Mia Mbili Thelathini na Mbili, Mia Mbili Ishirini na Sita Elfu (Shilingi 79,232,226,000)** sawa na **asilimia 3.5** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni Sitini na Tisa, Milioni Mia Tisa Thelathini na Mbili, Mia Tatu na Sita Elfu (Shilingi 69,932,306,000)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Mbili Tisini na Tisa, Mia Tisa Ishirini Elfu (Shilingi 9,299,920,000)** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) ya Watumishi wa Wizara na Taasisi ya PURA.

**271.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa unyenyekevu mkubwa sana naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.nishati.go.tz. Vilevile, Hotuba hii ina vielelezo mbalimbali ambavyo vimeambatishwa kwa ajili ya ufafanuzi wa masuala muhimu yanayohusu Sekta ya Nishati.

**272.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, hoja imeshawasilishwa. Sasa nimwite Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, aje awasilishe maoni ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kuhusu utekelezaji wa majukumu na Bajeti ya Wizara ya Nishati (Fungu 58) kwa mwaka wa fedha 2024/2025, pamoja na maoni, ushauri, na mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, ninaomba taarifa yote ya Kamati iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Wizara ya Nishati (Fungu 58) kwa

mwaka wa fedha 2025/2026 ulijikita katika maeneo makuu matano kama ifuatavyo:-

(a) Ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025;

(b) Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(c) Uchambuzi kuhusu ukusanyaji wa maduhuli katika mwaka wa fedha 2024/2025;

(d) Uchambuzi kuhusu upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari, 2025; na

(e) Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri, na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025; ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, Kamati ilifanya ziara tarehe 16 – 20 Machi 2025 katika mikoa mitatu ambayo ni Njombe, Iringa, na Dodoma na kukagua jumla ya miradi saba inayotekelezwa na Serikali chini ya Wizara ya Nishati, ambayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Rumakali na Njia ya Kusafirisha Umeme, Mradi Na. 3167 – Njombe;

(ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji ya Ruhudji na njia ya kusafirisha umeme, Mradi Na. 3165 – Njombe;

(iii) Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Kisada, Mradi Na. 3166 – Mufindi – Iringa.

(iv) Utekelezaji wa Mradi wa *REA*, Mradi Na. 3113 katika Wilaya ya Njombe na Makete, Mkoa wa Njombe; na

(v) Mradi wa Jengo la Wizara, Mradi Na. 6389 Mtumba – Dodoma.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi wa miradi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Rumakali na Njia ya Kusafirisha umeme, Mradi Na. 3167 – Njombe; mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rumakali katika Mkoa wa Njombe na njia ya kusafirisha umeme msongo wa *kilovolt* 220, yenye urefu wa kilometa 65 kutoka mitambo ya kuzalisha umeme hadi kituo cha kupoza umeme cha Iganjo katika Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu wa mradi huu uliofanyika mwaka 1998 na kuhuishwa katika mwaka 2020 – 2024. Ilionekana kuwa, mradi huu una uwezo wa kuzalisha umeme megawati 222 na una manufaa makubwa kiuchumi na kijamii. Gharama za utekelezaji wa mradi huu zinakadiriwa kuwa Dola za Kimarekani milioni 634.5, takribani shilingi trilioni 1.586.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, mradi huu ulitengewa shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuanza zoezi la ulipaji wa fidia kwa wananchi 5,508 wanaopaswa kuachia maeneo yao ili kupisha utekelezaji wa mradi. Kamati ilipohoji kuhusu hatua iliyofikiwa katika ulipaji wa fidia na iwapo fedha hizo zilitosheleza, ilifahamishwa kwamba, hadi wakati huo hapakuwa na mwananchi yeyote aliyelipwa fidia licha ya zoezi la uthamini kukamilika. Aidha, ufafanuzi zaidi ulitolewa kwamba, kiasi cha fedha kinachohitajika ili kulipa fidia kwa wananchi wote 5,508 ni shilingi bilioni 26.42, kiasi ambacho kinakusudiwa kutengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Ruhudji na Njia ya Kusafirisha umeme, Mradi Na. 3165 – Njombe. Mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhudji katika Mkoa wa Njombe na njia ya kusafirisha Umeme wa Msongo wa *kilovolt* 400,

yenye urefu wa kilometa 170 kutoka kwenye mitambo ya kuzalisha umeme hadi kituo cha kupoza umeme kinachojengwa eneo la Kisada – Mufindi, Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Spika, Upembuzi Yakinifu wa mradi huu uliofanyika mwaka 1998 na kuhuishwa kati ya mwaka 2020 – 2024, na ulionesha kwamba mradi una uwezo wa kuzalisha kiasi cha umeme wa Megawati 358 na una manufaa makubwa kiuchumi na kijamii. Gharama za utekelezaji wa mradi huu zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 976.61, takribani shilingi trilioni 2.44.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, mradi huu ulitengewa shilingi bilioni 37 kwa ajili ya kulipa fidia wananchi 2,601 walioachia maeneo yao ili kupisha utekelezaji wa mradi huu. Hata hivyo Kamati ilielezwa kwamba, zoezi la kulipa fidia halijaanza kutokana na fedha kusubiriwa kutoka Hazina.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mradi wa *REA*, Mradi Na. 3113 katika Wilaya ya Njombe na Makete, Mkoa wa Njombe; Jumla ya miradi mitano inatekelezwa na *REA* katika Mkoa wa Njombe kwa gharama ya shilingi bilioni 81.613. Baadhi ya miradi hiyo ni Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya III Mzunguko wa II, wenye gharama ya shilingi bilioni 41.53, mradi wa kupeleka umeme kwenye kituo cha afya na pampu za maji kwa gharama ya shilingi bilioni moja na Mradi wa Kupeleka Umeme Vitongojini, Awamu ya II A *(HEP IIA)*, kwa gharama ya shilingi bilioni 10.07.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea baadhi ya miradi katika Wilaya ya Njombe na Wilaya ya Makete ili kuona hatua za utekelezaji. Katika Wilaya ya Njombe ilibainika kuwa, hadi Februari 2025 vijiji vyote 103 vilikuwa vimefikishiwa huduma ya umeme wa *REA*. Aidha, vitongoji 314 kati ya 518 vilikuwa vimefikishiwa huduma ya umeme wa *REA* ambapo ni sawa na asilimia 60.61 kwa vitongoji vyote.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Wizara, Mradi NA. 6389 Mtumba – Dodoma. Mradi huu unahusu ujenzi wa jengo la ghorofa sita kwa ajili ya Ofisi za Wizara ya Nishati na

unatekelezwa katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma. Gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 25.22 ambapo kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 1.55 ni kwa ajili ya Mkandarasi Mshauri *(TBA)* na shilingi bilioni 23.68 ni kwa ajili ya mkandarasi wa ujenzi *(National Housing Cooperation)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea mradi huu tarehe 20 Machi, 2025. Utekelezaji wake ulikuwa umefikia 94%, na kiasi cha shilingi bilioni 22.21 sawa na 80.06% kilikuwa kimeshalipwa na Serikali kwa wakandarasi wanaotekeleza mradi huu. Maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa miradi ni kama ilivyoonekana katika ukurasa wa 3 – 14 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ilipanga kutekeleza vipaumbele tisa. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Wizara imetekeleza vipaumbele hivyo kwa kiasi cha kuridhisha, isipokuwa kwa vipaumbele vichache ambavyo Kamati imeshauri utekelezaji wake ufanyike kwa kadri ulivyopangwa. Baadhi ya vipaumbele hivyo ni pamoja na hivi vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupeleka umeme katika vitongoji vya Tanzania Bara. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, kati ya mwezi Februari, 2024 na Februari, 2025, vitongoji vilivyofikishiwa umeme katika kipindi hicho ni 927 tu, ambapo ni sawa na asilimia 2.89 ya vitongoji 32,030 vilivyokuwa vimesalia. Kamati ilifahamishwa kuwa, upelekaji wa huduma ya umeme kwenye vitongoji umepangwa kutekelezwa kikamilifu katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2025 – 2030), baada ya kukamilika kwa mpango wa kufikisha umeme takribani katika vijiji vyote vya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, ufikisha umeme wa Gridi ya Taifa katika Mikoa iliyosalia ya Kigoma, Katavi, Rukwa, Kagera, Lindi na Mtwara; uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, hadi Februari 2025 ni Mkoa wa Kigoma pekee ndio uliokuwa umeunganishwa na Gridi ya Taifa. Aidha, Mkoa wa Katavi uko katika hatua ya

mwisho na unatarajiwa kuunganishiwa umeme kabla ya kumalizika kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi kuhusu upatikanaji wa fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2025. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Nishati (Fungu 58) iliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi trilioni 1.88. Fedha hizi zinajumuisha fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi bilioni 88.89, sawa na asilimia 4.7 ya bajeti yote ya Wizara, ambapo shilingi bilioni 19.34 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 69.52 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)*. Aidha, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya maendeleo kilikuwa ni shilingi trilioni 1.79, sawa na 95.3% ya bajeti yote, ambapo shilingi 1.54 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 258.85 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa upatikanaji wa fedha umeonesha kuwa, hadi kufikia Februari, 2025 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi trilioni 1.076, sawa na 57.08% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa shilingi trilioni 1.06 sawa na 59% ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, shilingi bilioni 16.22 sawa na 27% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 10.99 sawa na 16% ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* na shilingi bilioni 5.23 sawa na 27% ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na taasisi ya *PURA*. Ufafanuzi zaidi kuhusu mapokezi ya fedha hizo ni kama ilivyoonyeshwa katika kielelezo Na.2 cha taarifa hii. Maelezo zaidi kuhusu upatikanaji wa fedha ni kama ilivyoonyeshwa katika ukurasa wa 17 – 19 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 iliyowasilishwa Bungeni tarehe 24 Aprili, 2024 pamoja na mambo mengine ilijumuisha maoni, ushauri na mapendekezo 30 ili yafanyiwe kazi na Wizara. Katika kikao chake cha tarehe 21 Machi, 2025, Kamati ilichambua taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati na kubaini kuwa utekelezaji wa Wizara ni wa kuridhisha. Hata hivyo,

Kamati ilishauri Wizara iongeze msisitizo kwenye utekelezaji wa maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Wizara ifuatilie na kuhakikisha shilingi bilioni 53.2 za Matumizi Mengineyo *(OC)* kutoka *IMF* zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 zinatolewa kabla mwaka huu haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, Wizara iongeze kasi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji 32,030 vilivyobakia. Utekelezaji umeonesha kuwa, vitongoji vilivyofikishiwa na umeme viliongezeka kutoka 32,730 mwezi Februari, 2024, hadi 33,657 mwezi Februari, 2025. Ongezeko hili ni sawa na ongezeko la vitongoji 927 sawa na asilimia 2.89 ya utekelezaji. Maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa maoni ni kama ilivyoandikwa katika ukurasa wa 20 – 22 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa ili kufikia malengo yake, Wizara inakusudia kutekeleza jumla ya vipaumbele 11, ambavyo takribani vyote isipokuwa kimoja, ni mwendelezo wa vipaumbele vya Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, kipaumbele kipya kinahusu Mpango wa Taifa wa Nishati wa Mwaka 2025 – 2030 *(National Energy Compact)*, ambacho ni sehemu ya utekelezaji wa mpango ulioidhinishwa na Wakuu wa Nchi za Afrika katika Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika uliofanyika tarehe 27 na 28 Januari, 2025, Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kushawishi na kuwezesha Mkutano ule mkubwa kufanyika hapa nchini. Maelezo zaidi kuhusu vipaumbele vya Wizara ni kama ilivyoonyeshwa katika ukurasa wa 23 – 26 wa taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi kuhusu makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026; katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya

maduhuli ya shilingi milioni nne kutoka kwenye vyanzo vyake viwili. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio hayo ni pungufu kwa kiasi cha shilingi milioni nne, sawa na 50%, ikilinganishwa na makadirio ya shilingi milioni nane katika Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kielelezo Na.3 kinafafanua kuhusu ulinganisho wa maduhuli. Maelezo zaidi ya makadirio ya maduhuli yanapatikana katika ukurasa wa 26 – 27 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026; katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Nishati (Fungu 58) inaomba kuidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi trilioni 2.25, ambazo zinajumuisha matumizi ya kawaida shilingi bilioni 79.23 na matumizi ya maendeleo shilingi trilioni 2.17. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida ambazo ni sawa na asilimia 3.5 ya bajeti yote ya Wizara shilingi 9.23 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi ya *PURA* na shilingi 69.93 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa kati ya hizo fedha za matumizi ya *OC*, shilingi 53.2 ni fedha za nje *(IMF)* kwa ajili ya matumizi mengineyo na miradi ya kuimarisha Gridi ya Taifa na umeme vijijini *(REA)*. Aidha, kati ya fedha za maendeleo ambazo ni sawa na 96.5% ya bajeti yote ya Wizara shilingi 1.47 ni fedha za ndani na shilingi 701.49 ni fedha za nje. Maelezo zaidi kuhusu makadirio na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 yanapatikana ukurasa wa 28 – 30 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi kuhusu masuala mahsusi. Katika eneo hili uchambuzi ulihusu mwenendo wa uzalishaji, usafirishaji, usambazaji wa umeme nchini na hali ya upatikanaji wa mafuta nchini. Maelezo kuhusu uchambuzi wa masuala mahsusi yanapatikana katika ukurasa wa 32 – 36 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati. Baada ya uchambuzi huu Kamati inatoa ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati kutokupokelewa kwa fedha za nje shilingi bilioni 53.2 kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* na utekelezaji juu ya miradi ya gridi imara na kufikisha umeme vitongojini, kumeathiri utekelezaji uliokuwa umepangwa, wizara ifuatilie kuhakikisha fedha hizi zinapatikana kabla ya kukamilika kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ili kutekeleza malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, mbili, kwa kuwa nchi inazalisha umeme toshelevu kiasi cha kuwa na ziada na kwa kuwa kuna faida nyingi zinazotokana na matumizi ya umeme huo ikiwemo kuchochea ukuaji wa uchumi ili kuchochea faida hizo, wizara ibadili sera za malipo yanayotozwa kwa wananchi kutokana na huduma ya kuunganishiwa umeme kutoka mfumo wa kulipa gharama zote kwa mkupuo mmoja kabla ya huduma hiyo na kuwa na mfumo wa kulipia gharama hizo kwa awamu baada ya huduma ya kukatwa deni hilo kupitia ankara za manunuzi ya umeme yanayofanywa na wateja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika la Umeme - *TANESCO*. Kazi ya utathimini kuhusu wananchi waliyopisha maeneo yao, kuwezesha utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa vituo vya kuzalisha umeme katika Mto Ruhudji na Rumakali Mkoani Njombe imekamilika, Serikali ifuatilie kwa karibu upatikanaji wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kulipa fidia, wananchi waliyopisha maeneo yao na maeneo mengine ya aina hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Mwaka wa Fedha 2025/2026 na kuhakikisha wananchi wote wanaostahili fidia wanalipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mbili, *TANESCO* iongeze kasi ya kutekeleza mradi wa kujenga miundombinu ya kusafirisha umeme na kuimarisha gridi ya Taifa ili kuondoa changamoto ya mgao wa umeme katika baadhi ya maeneo na umeme kukosa nguvu kutokana na uwezo mdogo wa miundombinu ya usafirishaji na ukosefu wa miundombinu na uchakavu wa miundombinu ya kusafirisha umeme.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi katika Wilaya ya Njombe na Makete, Kamati ilibaini uwepo wa

matukio ya mara kwa mara ya kuharibiwa kwa mashine umba kutokana na radi na mvua kali. Serikali ifunge vifaa vya mfumo wa kuzuia radi *(lightning protection system)* katika maeneo yote ambayo yana mvua nyingi na radi ili kuzuia radi kuleta madhara katika mashine umba na kusitisha au kuathiri ukosefu wa umeme kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Umeme wa Vijijini *(REA);* kasi ya kufikisha umeme vitongojini kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilikuwa ni ndogo kwani ni vitongoji 927 tu ndiyo vilivyofikishiwa umeme sawa na asilimia 2.89 katika kipindi cha mwezi wa Februari, 2024 hadi Februari, 2025. Katika kipindi hicho mradi huu ulipangiwa shilingi bilioni 350, kama ilivyo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo fedha hazikutolewa kwa kiwango cha kutosha na hivyo kuathiri ufikishaji wa umeme vitongojini, Serikali ihakikishe kikamilifu fedha hizo zinatengwa kwa ajili ya Miradi ya *REA*. Aidha kwa upande wa Taasisi ya *REA*, ihakikishe inaongeza bidii katika kufikisha umeme vitongojini.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ya pembezoni mwa miji yaani *peri urban*, hususani miji midogo yanakumbwa na changamoto ya kukosa huduma ya umeme na hivyo kuzuia malalamiko miongoni mwa wananchi wa maeneo hayo. Ili kuondoa malalamiko hayo Serikali iongeze wigo wa miradi ya kufikisha umeme kwenye maeneo ya vijiji, miji ili sehemu kubwa ya maeneo hayo ifikiwe na huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo ya *Petrol (TPDC);* katika mwaka wa fedha 2024/2025 *(TPDC)* ilikuwa na kazi ya kusambaza gesi asilia majumbani na kwenye taasisi kwa ajili ya kupikia. Hata hivyo, idadi ya kaya zilizofikishiwa gesi hiyo bado ipo chini na hivyo kuathiri mpango wa kaya kutumia nishati safi ya kupikia yenye gharama nafuu. Hivyo basi *TPDC* iongeze kasi ya ujenzi wa bomba la gesi pamoja na kuongeza idadi ya nyumba za taasisi zinazotumia gesi asilia ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhibiti ya Huduma za Nishati na Maji *(EWURA);* kumekuwa na utofauti wa gharama za kuunganishiwa umeme kwa wananchi waishio vijijini, ambapo wateja wa njia moja waliyo ndani ya mita 30 kutoka kwenye miundombinu ya umeme ni shilingi 27,000 wateja waliyo umbali wa mita 70 kutoka kwenye miundombinu ni shilingi 515,617 na wateja walio umbali wa mita 120 kutoka kwenye miundombinu ni shilingi 696,669.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa hali hiyo inatokana na mwongozo kuhusu gharama za kuunganishiwa umeme unaotolewa na *EWURA*. Baadhi ya wananchi wamekuwa wakilalamika gharama hizo kuwa ni kubwa na pia zinaleta utofauti miongoni mwa wananchi waishio vijijini. Ili kuondokana na malalamiko hayo na kukuza ustawi wa wananchi *EWURA* ipitie upya mwongozo huo kwa kuusianisha gharama hizo ili kuweka unafuu kwa wananchi wote waishio vijijini.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa vituo vya mafuta katika baadhi ya maeneo nchini unaonesha kufanyika kwa namna inayohusu kituo kimoja kuwa jirani ikilinganishwa na kingine na wakati mwingine vituo kujengwa karibu na makazi ya watu. Hali hiyo inahatarisha usalama wa wananchi waishio maeneo ya jirani na vituo hivyo sambamaba na kuchochea vituo hivyo kutumika kama maegesho ya magari ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, *EWURA* ipitie upya mwongozo unaohusu utekelezaji wa ujenzi wa vituo vya mafuta na kuwezesha vituo vya mafuta kujengwa kwa umbali stahiki.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa maghala ya kuhifadhia mafuta nchini, unaifanya nchi kukosa uhakika wa usalama wa uhifadhi wa mafuta kwa muda mrefu, jambo linaloweza kuwa na athari mbalimbali ikiwemo kupanda kwa bei ya mafuta. Ili kuondokana na changamoto hiyo Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa mradi wa hifadhi ya kimkakati ya mafuta *(Strategic Petroleum Reserve)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mazingira yanayozunguka *flow meter* na mabomba ya mafuta Kigamboni Dar es Salaam si salama kutokana na ufinyu wa eneo na kuzungukwa kwa karibu na makazi binafsi. Kwa kuwa kuna ongezeko la kiwango cha kushusha na kupakia mafuta katika eneo hilo, shughuli zinazohitaji usalama wa eneo kubwa zaidi ya hili lililopo, Serikali iongeze ukubwa wa eneo hilo kwa kutoa maeneo yaliyolizunguka eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; naomba kuhitimisha hoja ya Kamati kama ifuatavyo: Kwa namna ya pekee nakushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu Tukufu katika utekelezaji wa majukumu yake. Namshukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika, Mussa Azzan Zungu, Mbunge pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa namna wanavyokusaidia katika uendeshaji wa vikao vya Bunge.

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kutoa shukrani za dhati kwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa ushirikiano mkubwa wanaoonipatia ambao umewezesha kutekeleza kikamilifu na kwa ufanisi majukumu ya Kamati. Kwa namna ya pekee naomba majina yao yatambuliwe na kuingizwa kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa ushirikiano wake kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake. Vilevile natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Naibu Waziri wa Nishati kwa namna alivyoshirikiana na Kamati katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha ninawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Nishati, taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu Mhandisi Felchesmi Mramba, akisaidiwa na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Khatibu Kazungu na Dkt. James Mataragio kwa namna

walivyoshirikiana na kamati na kuiwezesha utekelezaji wa majukumu yake kuwa ya ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard pamoja na watendaji wake wote Ofisi ya Bunge, kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza kikamilifu majukumu yake ya kikatiba.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati, Fungu Na. 58 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NISHATI (FUNGU 58) KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023[1], natumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara ya Nishati **(Fungu 58)** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

[1] 118 (9) Baada ya Waziri kuwasilisha Hotuba ya Bajeti kwa mujibu wa fasili (1), Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia makadirio husika na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni watatoa maoni yao kwa muda usiozidi dakika thelathini kila mmoja.

Msingi wa uchambuzi na maoni hayo ni kutokana na majukumu ya Kamati kadiri yalivyoainishwa katika kanuni ya 117(2) ikisomwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023[2].

### 1.1 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, muundo wa taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na imegawanyika katika sehemu zifuatazo:

(a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, msingi na muundo wa taarifa hii;

(b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na namna Wizara ilivyotekeleza ushauri na mapendekezo ya Kamati;

(c) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(d) Sehemu ya Nne inahusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa Wizara na Serikali kwa ujumla; na (e) Sehemu ya Tano ni hitimisho ikijumuisha shukrani.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA UZINGATIAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, inaweka masharti kwa Kamati za kisekta kuchambua taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara

[2] 7.-(1) Majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge za kisekta yatakuwa yafuatayo:- (a) kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia;

zinazozisimamia na kufanya ulinganisho wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata[3]. Kwa kuzingatia masharti hayo, kuanzia tarehe 12 hadi 29 Machi, 2025 Kamati ilitekeleza wajibu huo kwa kufanya uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na kufanya ulinganisho dhidi ya mapendekezo ya bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati ilijielekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

(a) Ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025;

(b) Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(c) Uchambuzi kuhusu ukusanyaji wa maduhuli katika mwaka wa fedha 2024/2025;

(d) Uchambuzi kuhusu upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari, 2025; na

(e) Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati.

**2.1 Ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge[4] inaweka masharti kwa Kamati za kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha (2024/2025). Katika kuzingatia masharti hayo,

[3] Baada ya kutembelea miradi, Kamati za Bunge za Kisekta, kwa kipindi kisichozidi siku tisa, zitafanya vikao vya kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata

[4] Toleo la Februari 2023

katika sekta ya nishati, Kamati ilifanya ziara katika mikoa mitatu ambayo ni Njombe, Iringa na Dodoma na kukagua jumla ya miradi saba (7) inayotekelezwa na Serikali chini ya Wizara ya Nishati.

Lengo la ukaguzi huo ni kutathmini utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na kubainisha mafanikio na changamoto ili kuweza kulishauri Bunge kuhusu hatua za kuchukua katika kuisimamia Serikali. Uchambuzi wa baadhi ya miradi iliyokaguliwa na matokeo ya ukaguzi wake ni kama ifuatavyo: -

**2.1.1 Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Rumakali na Njia ya Kusafirisha umeme (Na. 3167), Njombe.**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Rumakali katika mkoa wa Njombe na njia ya kusafirisha umeme msongo wa **Kv 220** yenye urefu wa **kilomita 65** kutoka kwenye mitambo ya uzalishaji hadi kituo cha kupoza umeme cha Iganjo katika mkoa wa Mbeya.

Upembuzi yakinifu wa mradi huu uliofanyika mwaka 1998 ulionesha kuwa mradi una uwezo wa kuzalisha umeme **MW 222**. Aidha, kutokana na upembuzi huo kuwa wa muda mrefu, mwaka 2020 hadi 2024 Serikali ilihuisha upembuzi wa mradi huo na kujiridhisha kuwa mradi huo unatekelezeka na una manufaa makubwa kiuchumi na kijamii.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa mradi huu, Serikali kupitia Wizara ya Nishati iliuainisha kuwa miongoni mwa miradi ya kielelezo katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, awamuya Tatu (FYDP III) wa mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026. Gharama za utekelezaji wa mradi huu zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani Milioni 634.5 (takribani shilingi Trilioni 1.586)**.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, mradi huu ulitengewa **shilingi bilioni mbili (Tzs 2,000,000,000/=)** kwa ajili ya kuanza zoezi la ulipaji wa fidia kwa wananchi **5,508**

wanaopaswa kuachia maeneo yao ili kupisha utekelezaji wa mradi.

Kamati ilipohoji kuhusu hatua iliyofikiwa katika ulipaji wa fidia na iwapo fedha hizo zinatosheleza, ilifahamishwa kwamba hadi wakati huo hakukuwa na mwananchi aliyelipwa fidia licha ya zoezi la uthamini kukamilika. Aidha, ufafanuzi zaidi ulitolewa kwamba, kiasi cha fedha kinachohitajika ili kulipa fidia kwa wananchi wote 5,508 ni **shilingi Bilioni 26.42**, ambacho kinakusudiwa kutengwa katika bajeti ya mwaka 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu kuchelewa kuanza kwa utekelezaji wa mradi huu Kamati ilifahamishwa kwamba, changamoto kubwa ni ukosefu wa fedha. Aidha, Serikali ilieleza kwamba, ilijaribu kutekeleza mradi huu kwa ubia na sekta binafsi (PPP), hata hivyo mbinu hiyo ilishindikana kutokana na wabia wengi katika sekta binafsi kutokuwa tayari. Ili kuhakikisha mradi huu unatekelezwa, Serikali iliieleza Kamati kwamba, inaendelea na jitihada za kutafuta fedha kutoka vyanzo vingine. **Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali iongeze jitihada katika kutafuta fedha, ili mradi huu uweze kutekelezwa katika muda mfupi ujao.**

### 2.1.2 Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Ruhudji na Njia ya Kusafirisha umeme (Na. 3165), Njombe

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Ruhudji katika mkoa wa Njombe na njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **Kv400** yenye urefu wa **kilomita 170** kutoka kwenye mitambo ya uzalishaji hadi kituo cha kupoza umeme kinachojengwa eneo la Kisada – Mufindi, mkoa wa Iringa.

Upembuzi yakinifu wa mradi huu uliofanyika mwaka 1998 ulionesha kwamba, mradi una uwezo wa kuzalisha kiasi cha umeme **MW 358**. Aidha, kutokana na upembuzi huo kuwa wa muda mrefu, kati ya mwaka 2020 hadi 2024 Serikali ilihuisha upembuzi huo na kujiridhisha kuwa utekelezaji wa mradi huo una manufaa makubwa kiuchumi na kijamii.

Kutokana na umuhimu wake, Serikali kupitia Wizara ya Nishati iliubaini mradi huo kuwa miongoni mwa miradi ya kielelezo katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, awamu ya Tatu (FYDP III) wa mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026. Gharama za utekelezaji wa mradi huo zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani Milioni 976.61 (takribani shilingi Trilioni 2.44)**.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, mradi huu ulitengewa **shilingi Bilioni thelathini na saba (Tzs 37,000,000,000)** kwa ajili ya kulipa fidia wananchi 2,601 walioachia maeneo yao ili kupisha utekelezaji wa mradi huu.

Kamati ilipohoji kuhusu hatua iliyofikiwa katika zoezi la ulipaji fidia ilielezwa kwamba, zoezi la uthamini lilikuwa limekamilika lakini hakuna mwananchi aliyelipwa fidia. Aidha, ilielezwa kwamba, Wizara imewasilisha hazina maombi ya fedha ili kufanikisha ulipaji wa fidia. Vilevile, Kamati ilielezwa kwamba, ili kuhakikisha zoezi la fidia kwa wananchi wote linakamilika Wizara imetenga fedha katika mwaka ujao wa fedha (2025/2026).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba, changamoto kubwa inayokwamisha utekelezaji wa mradi huu ni ukosefu wa fedha, na ili kuikabili Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha kutoka vyanzo vingine.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Serikali imedhamiria kutekeleza mradi huu kwa kuhuisha upembuzi yakinifu na kutenga fedha za fidia kwa wananchi watakaoathirika, **ni mtazamo wa Kamati kuwa Serikali itafute fedha haraka ili utekelezaji wa mradi huu uanze mapema. Aidha, iwapo utekelezaji wa mradi utaendelea kuchelewa, kunaweza kusababisha wananchi kuvamia maeneo yaliyotwaliwa na hivyo kusababisha migogoro ya ardhi.**

**2.1.3 Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Kisada (Na. 3166), Mufindi, Iringa.**

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Kisada ni miongoni mwa vituo vitano (5) vya kupoza umeme,

ambavyo ni sehemu ya mradi mkubwa wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **Kv 400** yenye urefu wa kilomita 616 kutoka Tagamenda - Iringa hadi Sumbawanga - Rukwa. Aidha, njia hiyo inahusisha ujenzi wa kipande cha njia ya kusafirisha umeme msongo wa **Kv 400** yenye urefu wa kilomita 4 kutoka Tunduma hadi Nakonde nchini Zambia.

Gharama za ujenzi wa njia za kusafirisha na vituo vya kupoza umeme ni **Dola za Marekani milioni 827.3**. Hadi wakati wa ukaguzi wa mradi huu mwezi Machi, 2025 utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 51**. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuleta faida za kiuchumi na kijamii kama ifuatavyo:-

(a) Kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme katika mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe na Rukwa;

(b) Kuunganisha mkoa wa Rukwa katika gridi ya Taifa; na

(c) Kuunganisha Gridi za Taifa za Tanzania na Zambia na hivyo kuwezesha Tanzania kufanya biashara ya umeme na nchi za Kusini mwa Afrika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kituo cha kupoza umeme cha Kisada kilichopo umbali wa kilomita 15 kutoka mji mdogo wa Nyololo, ujenzi wake unatekelezwa na Kampuni ya ujenzi ya ***TBEA*** na mshauri elekezi Kampuni ya ***PowerGrid Ltd*** zote za nchini India. Ujenzi ulianza mwezi Mei, 2024 na umepangwa kukamilika mwezi Mei, 2026.

Kamati ilipotembelea na kukagua ujenzi wa kituo hiki ambao utagharimu dola za Marekani **milioni 61.5**, ujenzi wake ulikuwa umefikia asilimia **17.8**. Gharama hizo zinahusisha fidia ya shilingi **milioni 78.52** kwa wananchi tisa (9) walioachia maeneo yao, ambapo tayari kiasi cha **shilingi milioni 70** kimelipwa kwa wananchi saba (7) na wamebaki wawili kutokana na changamoto binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa kituo hiki unatarajiwa kuwa na faida za muda mrefu na muda mfupi. Miongoni mwa faida za

muda mfupi ni pamoja na ajira kwa watu sabini (70), kuchochea biashara ya bidhaa na huduma katika mji wa Nyololo na ujenzi wa barabara ya **kilomita 15** kutoka Nyololo hadi Kisada. Aidha, ujenzi wa kituo hiki utawezesha kusimikwa kwa mashine umba mbili zenye uwezo wa **Kv 32** na hivyo kuongeza umeme kiasi cha **MW 200** kwa ajili ya matumizi ya mkoa wa Iringa. Vilevile, Kamati ilifahamishwa kwamba ujenzi wa kituo hicho utarahisisha upozaji wa umeme unaotarajiwa kuzalishwa katika mradi wa Ruhudji katika mkoa wa Njombe na kuingizwa katika gridi ya taifa.

### 2.1.4 Utekelezaji wa Miradi ya REA (Mradi Na. 3113) katika Wilaya ya Njombe na Makete, mkoa wa Njombe

**Mheshimiwa Spika,** Njombe ni miongoni mwa mikoa inayonufaika na miradi ya umeme inayotekelezwa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA). Jumla ya miradi mitano (5) inatekelezwa Njombe kwa gharama ya **shilingi bilioni 81.613.** Baadhi ya miradi hiyo ni mradi kabambe wa kusambaza umeme vijijini, awamu ya III, mzunguko wa II wenye gharama **shilingi bilioni 41.53**; mradi wa kupeleka umeme kwenye vituo vya afya na pampu za maji kwa gharama ya **shilingi bilioni moja** (**1,000,000,000**) na mradi wa kupeleka umeme vitongojini, awamu ya II A (HEP IIA) kwa gharama ya **shilingi bilioni 10.07**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea baadhi ya miradi katika wilaya ya Njombe na wilaya ya Makete ili kuona hatua za utekelezaji. Katika wilaya ya Njombe ilibainika kuwa hadi Februari, 2025 vijiji vyote 103 vilikuwa vimefikishiwa huduma ya umeme wa REA. Aidha, vitongoji 314 kati 518 vilikuwa vimefikishiwa huduma ya umeme wa REA ambayo ni sawa na **asilimia 60.61** ya vitongoji vyote.

Kwa upande wa wilaya ya Makete, **vijiji 92** kati **93** vilikuwa vimefikishiwa huduma ya umeme wa REA, na **vitongoji 323** sawa na asilimia **73.07** ya vitongoji vyote **442** pia vilikuwa vimefikishiwa huduma hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifahamishwa kuwa, kijiji kimoja cha wilaya ya Makete hakijafikiwa na huduma ya umeme wa

REA kutokana na kutofikika kwa njia ya barabara. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa tayari REA imetoa zabuni kwa SUMA JKT ili kufikisha umeme katika kijiji hicho kwa kutumia mbinu za kijeshi katika kusafirisha vifaa vya mradi, kazi ambayo itatekelezwa kuanzia Aprili hadi Juni, 2025.

**Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hii ya kutumia vyombo vya ndani kufikisha huduma ya umeme kwenye maeneo yanayohitaji mbinu za kipekee, jambo linalookoa fedha ikilinganishwa na matumizi ya wakandarasi wa kawaida. Ni rai ya Kamati kwamba, mbinu za aina hii zitumike pia katika maeneo mengine yasiyofikika kwa urahisi.**

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme vijijini na vitongojini, Kamati ilifanya ziara katika kijiji cha Mang`oto, wilaya ya Makete na vijiji vya Lwangu na Welela vilivyopo wilaya ya Njombe.

Katika vijiji hivyo, Kamati ilishuhudia huduma ya umeme katika zahanati za vijiji, na hivyo kuwezesha utunzaji wa chanjo katika majokofu yanayotumia umeme. Hatua hiyo imechangia kuboresha utolewaji wa huduma ya chanjo muhimu, sambamba na huduma za kimatibabu. Aidha, Kamati ilishuhudia mashine za kusaga nafaka zinazotumia umeme, na hivyo kupunguza gharama za kusaga kwa wananchi wa maeneo hayo. Baadhi ya wananchi walieleza kwamba, huduma ya umeme imesaidia kupunguza gharama ya kusaga kutoka **shilingi 3,000** kwa debe kabla ya umeme hadi **shilingi 1,000.**

**Mheshimiwa Spika,** licha ya mafanikio hayo, baadhi ya wananchi katika vijiji hivyo walilalamikia hali ya kukosa huduma ya umeme kutokana na mashine umba kupigwa na radi, na waliojenga nyumba mbali na vyanzo vya umeme kulipa gharama kubwa zaidi ya **shilingi 27,000**.

Katika ufafanuzi wa changamoto hizo, Wizara ilieleza kwamba maeneo ya Makete na Njombe yamekuwa yakikumbwa na changamoto ya mashine umba kupigwa na radi kutokana na uwepo wa mvua kubwa inayoambatana na radi.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu gharama za kuunganishiwa umeme ilielezwa kwamba, gharama za kuunganisha umeme wa njia moja kwa wateja walio ndani ya umbali wa mita thelathini (30) kutoka kwenye miundombinu maeneo yote ya vijijini ni **shilingi 27,000.**

Aidha, kwa wateja walio nje ya umbali huo gharama za kuunganishwa ni tofauti, ambapo katika umbali wa mita sabini (70) gharama ni **shilingi 515,617.52** na umbali wa mita mia moja ishirini (120) ni **shilingi 696,669.64**. Vilevile, kwa wateja wa maeneo ya mijini gharama ya kuunganishiwa umeme ni **shilingi 320,960.**

**2.1.5 Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Wizara (Na. 6389) Mtumba, Dodoma**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ujenzi wa jengo la ghorofa sita (6) kwa ajili ya ofisi za Wizara ya Nishati na unatekelezwa katika mji wa Serikali Mtumba, Dodoma. Gharama za mradi ni **shilingi bilioni 25.22** ambapo kati ya kiasi hicho, **shilingi bilioni 1.55** ni kwa ajili ya mkandarasi mshauri (TBA) na **shilingi bilioni 23.68** ni kwa ajili ya mkandarasi wa ujenzi (NHC).

Kamati ilipotembelea mradi huu tarehe 20 Machi, 2025, utekelezaji wake ulikuwa umefikia asilimia 94. Kiwango cha utekelezaji kimeongezeka kwa asilimia 19 ikilinganishwa na asilimia 75 ya mwezi Machi, 2024 wakati Kamati ilipokagua mradi huu. Aidha, hadi tarehe 20 Machi, 2025, kiasi cha **shilingi bilioni 22.21** sawa na **asilimia 80.06** kilikuwa kimeshalipwa na Serikali kwa wakandarasi wanaotekeleza mradi huu. Kiasi hicho ni ongezeko la **shilingi bilioni 5.73** ikilinganishwa na **shilingi bilioni 16.48** (asilimia 65.33) kilichokuwa kimelipwa hadi mwezi Machi, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu ulianza Novemba, 2021 na ulitakiwa kukamilika Novemba, 2023. Hata hivyo, mradi umechelewa kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo uhaba wa fedha za kigeni (dola za marekani) uliochelewesha malighafi za ujenzi kutoka nje ya nchi, na mabadiliko (variations) katika mfumo wa pampu ya maji ya zimamoto. Kamati ilihakikishiwa na Wizara kuwa jengo hilo

litakamilika na kuanza kutumika kabla ya mwezi Juni, 2025 kwa kuwa malighafi zote zimefikishwa eneo la ujenzi na kazi zilizobaki ni za umaliziaji.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na jengo kutokamilika, Kamati ilishuhudia hatua kubwa ya utekelezaji wake ikilinganishwa na hali ilivyokuwa wakati wa ukaguzi wa mwaka 2024. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kiasi cha **shilingi bilioni 5.7** na kuwezesha ujenzi wa mradi huu kupiga hatua kubwa. **Ni rai ya Kamati kuwa Serikali itoe kwa ukamilifu fedha zilizobaki ili kukamilisha mradi huo mapema na kuwezesha jengo hilo kuanza kutumika kabla ya mwezi Juni, 2025 na hivyo kukidhi matarajio ya Wizara.**

**2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ilipanga kutekeleza vipaumbele tisa (9). Asilimia kubwa ya vipaumbele hivyo ilikuwa ni kuendeleza miradi ambayo imekuwa ikitekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa sehemu kubwa Wizara imetekeleza vipaumbele hivyo kwa kiasi cha kuridhisha isipokuwa kwa vipaumbele vichache ambavyo utekelezaji haukuwa wa kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa vipaumbele ambavyo utekelezaji wake unahitaji juhudi kuongezwa, Kamati imetoa ushauri kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wake kufanyika kadri ulivyopangwa. Baadhi ya vipaumbele hivyo ni pamoja na:-

(a) Kupeleka umeme katika vitongoji vya Tanzania Bara. Utekelezaji wake umeonesha, kati ya mwezi Februari, 2024 na Februari, 2025, vitongoji vilivyofikishiwa umeme katika kipindi hicho ni **927** tu sawa na **asilimia 2.89** ya **vitongoji 32,030** vilivyokuwa vimesalia.

Kamati ilifahamishwa kuwa upelekaji wa huduma ya umeme vitongojini umepangwa kutekelezwa kikamilifu katika kipindi cha

miaka mitano ijayo (2025 - 2030) baada ya kukamilika kwa mpango wa kufikisha umeme takribani katika vijiji vyote vya Tanzania Bara. **Licha ya mpango huo, Kamati inaendelea kushauri kuwa kasi ya utekelezaji wa kipaumbele hicho iongezeke ili kufikisha umeme kwenye vitongoji vingi mapema na kuondoa malalamiko ya wananchi waishio vitongojini kutokana na kukosa huduma ya umeme**.

(b) Kufikisha umeme wa gridi ya Taifa katika mikoa iliyosalia ya Kigoma, Katavi, Rukwa, Kagera, Lindi na Mtwara.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba hadi Februari, 2025 ni mkoa wa Kigoma pekee ndiyo ulikuwa umeunganishwa na gridi ya Taifa. Aidha, mkoa wa Katavi upo katika hatua za mwisho na unatarajiwa kuunganishwa kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2024/2025. **Ni ushauri wa Kamati kuwa, jitihada zaidi zifanyike ili kuunganisha mikoa iliyosalia katika gridi ya taifa**.

### 2.3 Uchambuzi kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli hadi kufikia mwezi Februari, 2025

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Nishati (Fungu 58) ilipangiwa kukusanya **Shilingi 8,000,000.00** kutoka katika vyanzo mbalimbali zikiwemo shughuli za utawala. Hadi kufikia mwezi Februari, 2025 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha **Shilingi 4,891,537** sawa na **asilimia 61.14** ya lengo kama inavyofafanuliwa katika Kielelezo Na. 01 cha taarifa hii.

Kielelezo NA. 1: Makusanyo ya Maduhuli hadi kufikia Februari, 2025

| Chanzo cha Mapato | Kiasi kilichopangwa | Kiasi kilichokusanywa | Asilimia ya lengo |
|---|---|---|---|
| Stakabadhi nyinginezo | 1,000 | 0 | 0 |
| Marejesho ya fedha za Umma | 7,999,000 | 4,891,537 | 61.15 |
| **JUMLA** | **8,000,000** | 4,891,537 | **61.14** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa ukusanyaji wa maduhuli kwa Wizara hii ulikuwa chini ya lengo la kufikia **asilima 66** katika kipindi rejewa. Hata hivyo, ilielezwa kuwa hali hiyo imesababishwa na Wizara kutegemea kwa asilimia kubwa (**99.9%**) makusanyo kutoka chanzo kimoja ambacho ni urejeshaji wa masurufu (*imprest*). **Ni mtazamo wa Kamati kwamba Wizara ibuni vyanzo vipya vya mapato badala ya kuendelea kutegemea chanzo kimoja tu**.

### 2.4 Uchambuzi kuhusu Upatikanaji wa Fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2025

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Nishati (**Fungu 58**) iliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 1,883,759,455,000.00**. Fedha hizi zinajumuisha fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 88, 892, 623, 000/=** sawa na **asilimia 4.7** ya bajeti yote ya Wizara. Katika fedha hizo, **shilingi 19, 368, 422, 000.00** ni kwa ajili ya mishara (PE) na **shilingi 69, 524, 201, 000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

Aidha, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya maendeleo kilikuwa ni **shilingi 1,794,866,832,000.00** sawa na **asilimia 95.3** ya bajeti yote, ambapo **shilingi 1,536,020,274,000.00** ni fedha za ndani na **shilingi 258,846,558,000.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa upatikanaji wa fedha unaonesha kuwa, hadi kufikia Februari, 2025 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 1,075,388,821,935.69** sawa na **asilimia 57.08** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, **Shilingi 1,059,172,224,067.48** sawa na **asilimia 59** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, **shilingi 16,216,597,868.21** sawa na **asilimia 27** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo **Shilingi 10,982,800,665.3** sawa na **asilimia 16** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC), na **Shilingi 5,233,797,202.88** sawa na **asilimia 27** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na taasisi ya PURA. Ufafanuzi zaidi kuhusu mapokezi ya fedha hizo ni kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 02 cha taarifa hii.

**Kielelezo NA. 2: Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Februari, 2025**

| Na. | Matumizi | Bajeti ya Mwaka 2024/25 | Fedha zilizopokelewa hadi Februari, 2025 | Asilimia ya Fedha Zilipokelewa |
|---|---|---|---|---|
| A | **Matumizi ya Kawaida** | | | |
| 1. | Matumizi Mengineyo (OC) | 69,524,201,000 | 10,982,800,665.30 | 16 |
| 2. | Mishahara (PE) | 19,368,422,000 | 5,233,797,202.88 | 27 |
| | **Jumla Ndogo** | **88,892,623,000** | **16,216,597,868.21** | 18 |
| **B** | **Matumizi ya Maendeleo** | | | |
| 3. | Fedha za Ndani | 1,536,020,274,000 | 894,168,139,088.25 | 58 |
| 4. | Fedha za Nje | 258,846,558,000 | 165,004,084,979.23 | 64 |
| | **Jumla Ndogo** | **1,794,866,832,000** | **1,059,172,224,067.48** | 59 |
| | **JUMLA KUU** | **1,883,759,455,000** | **1,075,388,821,935.69** | 57 |

***Chanzo**: Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo (OC) siyo wa kuridhisha kwani kiasi kilichopokelewa ni **Shilingi 10,982,800,665.30** kati ya **shilingi 69,524,201,000.00** zilizoidhinishwa. Aidha, kiasi hicho kilichopokelewa ni sehemu tu ya fedha za ndani za matumizi mengineyo (OC) zilizoidhinishwa **shilingi 16,324,201,000.** Hivyo kiasi

cha **Shilingi 10,982,800,665.30** ni utekelezaji wa **asilimia 67.27** ya fedha za ndani za matumizi mengineyo (OC).

Uchambuzi zaidi wa Kamati umeonesha kuwa, asilimia ya kupokelewa kwa fedha za OC inaonekana kuwa ndogo (16%) kunatokana na Wizara kujumuisha fedha za nje ambazo hazikupokelewa kutoka *IMF* **shilingi 53,200,000,000**. Fedha hizo zilipangwa kutumika kwa ajili ya kutekeleza miradi ya TANESCO (Gridi imara), umeme vitongojini na OC ya Wizara na taasisi zake za PURA na TPDC.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile uchambuzi zaidi umebaini kuwa, fedha hizo zimekuwa zikitengwa katika bajeti ya Wizara kwa miaka miwili mfululizo (2023/2024 na 2024/2025) lakini Wizara haijawahi kupokea kiasi chochote. Aidha, Kamati ilibaini kuwa, matarajio ya kupatikana kwa fedha hizo kwa robo ya mwisho ya mwaka wa fedha 2024/2025 ni madogo.

**Ni mtazamo wa Kamati kwamba, upatikanaji wa fedha hizi hauna uhakika. Hivyo, ni vyema Wizara ikahakikisha inapata uhakika kutoka kwa wahusika wa kutolewa kwa fedha hizo kabla ya kuzitenga kwenye bajeti yake.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fedha za mishahara, hadi mwezi Februari, 2025 kiasi kilichopokelewa kilikuwa **shilingi 5,233,797,202.88** kati ya kiasi cha **shilingi 19,368,422,000.00** kilichoidhinishwa**.** Kamati ilifahamishwa kuwa, kupokelewa kwa kiasi kidogo cha fedha za mishahara kunatokana na kutopokelewa kwa mishahara ya TPDC kiasi cha **shilingi 11,658,374,000** kilichoidhinishwa kwenye bajeti kutokana na taasisi hiyo kuanza kulipa mishahara ya watumishi wake kutoka kwenye fedha za mapato ya ndani. Kuondolewa kwa fedha za mishahara ya TPDC kunafanya bajeti halisi ya mishahara kuwa **shilingi 7,710,048,000.00** na hivyo kiasi cha **shilingi 5,233,797,202.88** kilichopokelewa ni sawa na **asilimia 67.88** ya bajeti ya mishahara kwa ajili ya Wizara na PURA, kiwango ambacho ni cha kuridhisha.

**2.5 Uchambuzi kuhusu Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2024/2025 iliyowasilishwa Bungeni tarehe 24 Aprili, 2024, pamoja na mambo mengine, ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo thelathini (30) ili yafanyiwe kazi na Wizara. Katika kikao chake cha tarehe 21 Machi, 2025, Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Tathmini inaonesha kuwa, Wizara imetekeleza maoni, ushauri na mapendekezo kwa kiwango kinachoridhisha. Aidha, baadhi ya maoni, ushauri na mapendekezo utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya utekelezaji mzuri na wenye muendelezo wa maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa, ni rai ya Kamati kwamba, Wizara iongeze bidii kwenye utekelezaji wa maoni yafuatayo:-

(a) Kufuatilia kwa ukaribu na kuhakikisha **shilingi bilioni 53.2** za matumizi mengineyo (OC) kutoka *IMF* zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2024/2025, zinatolewa kabla mwaka wa fedha 2024/2025 haujakamilika. Taarifa ya utekelezaji ilionesha kuwa, hadi tarehe 21 Machi, 2025, hakukuwa na kiasi chochote cha fedha kilichopokelewa.

(b) Kuongeza kasi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji **32,030** vilivyobakia. Utekelezaji umeonesha kuwa, vitongoji vilivyofikishiwa umeme viliongezeka kutoka **32,730** mwezi Februari, 2024 hadi **33,657** mwezi Februari, 2025. Ongezeko hilo ni sawa na **vitongoji 927** ambalo ni ongezeko sawa na asilimia **2.89** ya utekelezaji. Kiasi hicho ni kidogo ikilinganishwa na idadi ya vitongoji vilivyosalia. Wizara iongeze kasi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji ili kuondoa malalamiko ya kukosa huduma ya umeme kutoka miongoni mwa wananchi waishio katika vitongoji visivyo na huduma hiyo.

(c) Serikali ihakikishe Kampuni ya TANOIL inaongeza kasi ya ukusanyaji wa madeni chechefu yaliyobakia kiasi cha **shilingi bilioni 21** kutoka kwa wadaiwa sugu ili kuepusha upotevu wa fedha hizo. Taarifa ya utekelezaji ilionesha kwamba, TANOIL ilikusanya **shilingi bilioni 1.43** tu ambazo ni sawa na **asilimia 6.8** kwa mwaka. Kiwango hicho ni kidogo na kinaashiria kasi ndogo ya ukusanyaji wa madeni hayo.

(d) Serikali iondoe tofauti ya gharama za kuunganishiwa umeme na kuziwianisha kuwa **shilingi 27,000** kwa wananchi wote wa vijijini ili kuondoa matabaka ambayo yanasababisha malalamiko kutoka kwa wananchi.

Utekelezaji umeonesha bado Serikali inatumia mwongozo wenye gharama tofauti kwa njia moja ya umeme kulingana na umbali kutoka miundombinu ya umeme. Gharama hizo ni **shilingi 27,000** kwa wateja walio ndani ya mita 30 kutoka kwenye miundombinu ya umeme, **shilingi 515,617** kwa wateja walio umbali wa mita 70, na **shilingi 696,669** kwa wateja walio umbali wa mita 120. Aidha, kwa wateja wote wa njia moja waishio mijini gharama ya kuunganishiwa umeme ni **shilingi 320,960**.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati (Fungu 58) kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

(a) Uchambuzi wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(b) Uchambuzi wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(c) Uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(d) Ulinganisho kati ya Bajeti ya Wizara na Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na 2025/2026; na

(e) Uchambuzi wa masuala mahsusi ya kisekta.

### 3.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati kuhusu makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2025/2026 umebaini kuwa, malengo na vipaumbele vya Wizara vimezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo:-

(a) Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26);

(b) Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020;

(c) Mpango Mkakati wa Wizara ya Nishati wa mwaka 2021/2022 - 2025/2026;

(d) Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa mwaka 2024-2034; na

(e) Mpango wa Taifa wa Nishati wa mwaka 2025-2030 ulioidhinishwa katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati uliofanyika jijini Dar es Salaam mwezi Januari, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ambayo yamefafanuliwa kwa kina kupitia mpango mkakati wa Wizara wa mwaka 2021/2022 – 2025/2026 Wizara inakusudia kutekeleza jumla

ya vipaumbele kumi na moja (11). Baadhi ya vipaumbele hivyo ni:-

(a) Kuendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ikiwa ni pamoja na kufikisha gridi ya Taifa katika mikoa iliyosalia ya Rukwa, Kagera, Lindi na Mtwara;

(b) Kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa kuimarisha Gridi ya Taifa (National Grid Stabilization Project);

(c) Kutekeleza Mpango wa Taifa wa Nishati wa Mwaka 2025-2030 (National Energy Compact) kuhusu upatinakaji na uunganishaji wa umeme kwa wananchi, kuongeza mchango wa nishati jadidifu na ushiriki wa sekta binafsi katika maendeleo ya sekta ya nishati;

(d) Kuendelea kufikisha umeme vitongojini, maeneo ya migodi, kilimo, viwanda, pampu za maji na katika vituo vya huduma za afya;

(e) Kuendelea kuwawezesha watanzania kutumia nishati safi ya kupikia;

(f) Kuwezesha upatikanaji wa bidhaa za mafuta vijijini; na

(g) Kuendelea na kazi ya utafutaji, uendelezaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia nchini pamoja na ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania (*East African Crude Oil Pipeline -EACOP*).

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba asilimia kubwa ya vipaumbele vya mwaka wa fedha 2025/2026, ni mwendelezo wa vipaumbele vya mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, katika mwaka wa fedha 2025/2026, kimeongezwa kipaumbele kipya kinachohusu Mpango wa Taifa wa Nishati wa mwaka 2025-2030 (*National Energy Compact*)

kuhusu upatinakaji na uunganishaji wa umeme kwa wananchi, kuongeza mchango wa nishati jadidifu na ushiriki wa sekta binafsi katika maendeleo ya sekta ya nishati. Kipaumbele hiki ni sehemu ya utekelezaji wa mpango ulioidhinishwa na Wakuu wa Nchi za Afrika katika Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika uliofanyika tarehe 27 na 28 Januari, 2025 jijini Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, Kamati inatoa pongezi nyingi kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kushawishi na kuwezesha Mkutano ule mkubwa kufanyika hapa nchini. Ni wazi kuwa kufanyika kwa mkutano huo kumeleta manufaa makubwa kwa nchi yetu yakiwemo ya kidiplomasia, kiuchumi na kijamii. Aidha, Kamati inatoa pongezi kwa Wizara ya Nishati chini ya Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa kufanya maandalizi mazuri yaliyowezesha mkutano huo kufanyika kwa ufanisi mkubwa**.

**3.2 Uchambuzi kuhusu Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara inaomba kuidhinishiwa kukusanya maduhuli ya **shilingi 4,000,000.00** kutoka kwenye vyanzo vyake viwili. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio haya ni pungufu kwa kiasi cha **shilingi 4,000,000.00** sawa na **asilimia 50** ikilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha 2024/2025 ambayo yalikuwa **shilingi 8,000,000.00**. Kielelezo Na. 03 kinafafanua kuhusu ulinganisho wa maduhuli.

Kielelezo NA. 3: Ulinganisho wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026

| CHANZO | 2024/2025 | 2025/2026 | ONGEZEKO/ UPUNGUFU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| Marejesho ya Fedha za Umma (Recovery of Public Money) | **7,999,000** | **3,999,000** | **4,000,000** | **50** |
| Stakabadhi nyinginezo | **1,000** | **1,000** | **0** | **0** |
| **JUMLA** | **8,000,000** | **4,000,000** | **4,000,000** | **50** |

***Chanzo**: Randama ya Wizara ya Nishati Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa vyanzo vya maduhuli kwa mwaka 2025/2026 vinafanana na vyanzo katika mwaka 2024/2025. Aidha, katika vyanzo hivyo, hadi kufikia mwezi Februari, 2025, Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha **shilingi 4,891,537** sawa na **asilimia 61** ya kiasi kilichoidhinishwa. Mwenendo huo unaonesha kuwa, hadi kumalizika kwa robo ya nne ya mwaka wa fedha 2024/2025 kuna uwezekano kiwango cha makusanyo kikaongezeka. Kutokana na mantiki hiyo, Kamati inaishauri Wizara kuongeza kiwango cha makadirio ya maduhuli kutoka **shilingi 4,000,000.00** na kuwa **shilingi 8,000,000.00** kama ilivyo katika mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, ili kuongeza kiwango cha maduhuli, **Kamati inashauri Wizara ifanye jitihada zitakazoibua vyanzo zaidi vya mapato na hivyo kuongeza wigo wa mapato yatokanayo na maduhuli.**

### 3.3 Uchambuzi kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Nishati (Fungu 58) inaomba kuidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 2,246,745,445,000.00** ambazo zinajumuisha fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 79, 232, 226, 000.00** na fedha za maendeleo **shilingi 2,167,513,219,000.00** Katika fedha za matumizi ya kawaida ambazo ni sawa na **asilimia 3.5** ya bajeti yote ya Wizara, **shilingi 9, 299, 920, 000.00** ni kwa ajili ya mishara (PE) ya

watumishi wa Wizara na taasisi ya PURA, na **shilingi 69, 932, 306, 000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Kamati ilielezwa kuwa, katika fedha za matumizi mengineyo (OC), **shilingi 53, 200, 000, 000.00** ni fedha za nje (IMF) kwa ajili ya matumizi mengineyo na miradi ya kuimarisha gridi ya Taifa na umeme vijijini (REA-HEP). Kwa msingi huo, fedha za ndani kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) ni **shilingi 16, 732, 306, 000.00** Hata hivyo, Kamati ina wasiwasi kuhusu upatikanaji wa fedha za nje za OC **shilingi bilioni 53.2.** Uzoefu unaonesha kwamba, fedha hizi zimekuwa zikitengwa katika miaka ya fedha miwili mfululizo (2023/2024 na 2024/2025), lakini zimekuwa hazitolewi.

**Kutokana na mwenendo huo, ni rai ya Kamati kuwa, iwapo Wizara inaona kuna umuhimu wa kuendelea kuweka chanzo hiki katika bajeti yake, ni vyema ikabuni njia sahihi na itakayohakikisha kupatikana kwa fedha hizo ili kutoendelea kuathiri utekelezaji wa bajeti.**

**Mheshimiwa Spika**, katika fedha za maendeleo ambazo ni sawa na **asilimia 96.5** ya bajeti yote ya Wizara, **shilingi 1, 466, 020, 274, 000.00** ni fedha za ndani na **shilingi 701, 492, 945, 000.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imeongezeka kwa kiasi cha **shilingi 362, 985, 990, 000.00** sawa na **asilimia 19.27** ikilinganishwa na **shilingi 1, 883, 759, 455, 000.00** zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2024/2025. Kielelezo Na.4 kinafafanua ulinganisho huo.

**Kielelezo NA. 4: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026**

| WIZARA YA NISHATI - FUNGU 58 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **FEDHA** | **CHANZO** | **2024/2025** | **2025/2026** | **ONGEZEKO/ UPUNGUFU** | **ASILIMIA** |
| **Maendeleo** | Fedha za Ndani | 1,536,020,274,000 | 1,466,020,274,000 | 70,000,000,000 | -(4.56) |
| | Fedha za Nje | 258,846,558,000 | 701,492,945,000 | 442,646,387,000 | 171 |
| | **Jumla ndogo** | **1,794,866,832,000** | **2,167,513,219,000** | **372,646,387,000** | **20.76** |
| **Matumizi ya Kawaida** | Mengineyo (OC) | 69,524,201,000 | 69,932,306,000 | 408,105,000 | 0.58 |
| | Mishahara (PE) | 19,368,422,000 | 9,299,920,000 | 10,068,502,000 | -(51.98) |
| | **Jumla ndogo** | **88,892,623,000** | **79,232,226,000** | **9,660,397,000** | **-(10.87)** |
| **JUMLA KUU** | | **1,883,759,455,000** | **2,246,745,445,000** | **362,985,990,000** | **19.269** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Wizara kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na 2025/2026 na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa ongezeko la bajeti ya mwaka 2025/2026 kwa kiasi cha **shilingi 362, 985, 990, 000.00** limechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa fedha za maendeleo katika sekta ya nishati. Aidha, uchambuzi zaidi umebaini kuwa ongezeko la fedha hizo liko katika fedha za nje ambazo zimeongezeka kwa **shilingi bilioni 442.65** sawa na **asilimia 171** ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaoisha.

**Ni matumaini ya Kamati kwamba, ingawa fedha hizo ni za nje, Wizara itaweka mazingira yatakayowezesha wakandarasi wazawa na wa ndani kupata zabuni zinazokusudiwa kutekelezwa kwa fedha hizo ili ziweze kuchangia kukuza uchumi wa taifa.**

### 3.4 Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara na Bajeti ya Taifa

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulienda mbali zaidi kwa kulinganisha Bajeti ya Wizara hii na Bajeti ya Taifa.

Ulinganisho huo uliangalia bajeti ya Wizara kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 ambayo ni **shilingi 1,883,759,455,000.00** na bajeti pendekezwa ya mwaka wa fedha 2025/2026 ambayo ni **shilingi 2,246,745,445,000.00** kwa kuwianisha na bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ambayo ni **shilingi 50,291,408,000,000.00** na bajeti pendekezwa ya mwaka wa fedha 2025/2026 ya **shilingi 57,040,252,000,000.00**. Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini masuala mbalimbali yafuatayo:-

(a) Bajeti ya Wizara imeongezeka kutoka **asilimia 3.8** mwaka wa fedha 2024/2025 hadi kufikia **asilimia 3.9** katika mwaka wa fedha 2025/2026 ikilinganishwa na Bajeti ya Taifa.

(b) Fedha za Matumizi mengineyo (OC) kwa Wizara zimeongezeka kutoka **asilimia 0.26** mwaka 2024/2025 hadi kufikia **asilimia 1.09** mwaka 2025/2026 ikilinganishwa na bajeti ya Taifa.

(c) Fedha za ndani kwa ajili ya maendeleo katika Wizara zimepungua kutoka **asilimia 12.64** mwaka 2024/2025 hadi kufikia **asilimia 11** mwaka 2025/2026 ikilinganishwa na fedha za ndani za maendeleo za bajeti ya Taifa.

(d) Fedha za maendeleo za nje katika Wizara zimeongezeka kutoka **asilimia 7.11** mwaka 2024/2025 hadi kufikia **asilimia 11.4** mwaka 2025/2026 ikilinganishwa na fedha za nje za bajeti ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kumekuwa na uwiano mzuri kati ya ongezeko la bajeti ya Taifa na ongezeko la bajeti ya Wizara. Uchambuzi zaidi kuhusu ulinganisho wa bajeti ya Wizara na bajeti ya Taifa ni kama inavyoonekana katika kielezeo Na. 05 cha Taarifa hii.

**Kielelezo NA. 5: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| ULINGANISHO WA BAJETI YA TAIFA DHIDI YA BAJETI YA WIZARA MWAKA 2025/2026 | | | |
|---|---|---|---|
| **AINA** | **BAJETI YA TAIFA** | **BAJETI YA NISHATI** | **ASILIMIA** |
| **OC** | 6,444,293,900,000 | 69,932,306,000 | 1.085 |
| **Mishahara** | 13,174,240,500,000 | 9,299,920,000 | 0.07 |
| **Maendeleo ndani** | 13,320,501,900,000 | 1,466,020,274,000 | 11 |
| **Maendeleo nje** | 6,150,902,600,000 | 701,492,945,000 | 11.4 |
| **Deni la Serikali** | 17,950,311,400,000 | - | - |
| **JUMLA KUU** | **57,040,250,300,000** | **2,246,745,445,000** | **3.938** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Mapendekezo ya Mpango na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/2026; Randama ya Wizara ya Nishati 2025/2026 na Usanifu wa Kamati*

### 3.5 Uchambuzi kuhusu Masuala Mahsusi

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uchambuzi wa bajeti, Kamati imejiwekea utaratibu wa kufuatilia masuala mahsusi ya kisekta kwa kuwa masuala hayo yana maslahi mapana kwa wananchi na nchi kwa ujumla. Masuala hayo ni mwenendo wa uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini na hali ya upatikanaji wa mafuta nchini. Uchambuzi kuhusu masuala hayo ni kama ifuatavyo: -

#### 3.5.1 Mwenendo wa Uzalishaji wa Umeme nchini

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa kipengele hiki Kamati ilijikita katika masuala yafuatayo: -

#### (a) Uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, hali ya uzalishaji wa umeme nchini imekuwa ya kuridhisha ikilinganishwa na mwaka 2023/2024. Uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa

umeongezeka kwa kiasi cha **MW 1,666.86** kutoka mwezi Februari, 2024 ambapo uwezo ulikuwa ni **MW 2,129.85**, ikilinganishwa na **MW 3,796.71** zilizofikiwa mwezi Februari, 2025 ikiwa ni ongezeko la **asilimia 78.26**.

Ongezeko hili kwa sehemu kubwa limetokana na kukamilika kwa mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Julius Nyerere (JNHPP) ambapo mitambo yote tisa (9) imekamilika na ina uwezo wa kuzalisha umeme jumla ya **MW 2115**.

Uchambuzi zaidi wa Kamati kuhusu uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika gridi ya Taifa ni kama unavyoonekana kwenye kielelezo Na. 06 cha taarifa hii.

**Kielelezo NA. 6: Ulinganisho wa uwezo wa vyanzo vya kuzalisha Umeme katika Gridi ya Taifa dhidi ya uzalishaji unaopatikana hadi kufikia mwezi Februari, 2025**

| Chanzo | Uwezo wa Mitambo (MW) | | Hali ya Uzalishaji kwa sasa (MW) | |
|---|---|---|---|---|
| | MW | Asilimia (%) | MW | Asilimia (%) |
| Maji | 2481.270 | 65.35 | 1288 | 60.3 |
| Gesi Asilia | 1198.82 | 31.58 | 796 | 37.3 |
| Mafuta | 101.12 | 2.66 | 41 | 1.9 |
| Solar | 5.00 | 0.13 | 0 | 0 |
| Tungamotaka | 10.50 | 0.28 | 10.50 | 0.5 |
| **Jumla** | **3796.708** | **100** | **2135.5** | **100** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Wizara kwenye Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2024/2025 na Usanifu wa Kamati*

**(b) Ulinganisho wa uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme na uzalishaji halisi**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, mitambo iliyopo ina uwezo mkubwa wa kuzalisha umeme, hata

hivyo, mitambo hiyo inatumika chini ya uwezo wake. Uwezo wa mitambo uliopo ni kuzalisha **MW 3,796.708**, lakini inaruhusiwa kuzalishaji **MW 2,135.5**. Mfano; uwezo wa mitambo yote ya kuzalisha umeme kwa njia ya maji hadi mwezi Februari, 2025 ilikuwa ni kuzalisha **MW 2481.27**. Hata hivyo, taarifa imeonesha kuwa uzalishaji halisi wa mitambo hiyo ulikuwa ni **MW 1,288** tu sawa na **asilimia 51.9** ya mitambo yote ya maji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa, Shirika la Umeme – TANESCO limekuwa likilazimika kuruhusu mitambo kuzalisha umeme wa kiasi cha chini ikilinganishwa na uwezo wake ili kuendana na uwezo wa miundombinu ya usafirishaji wa umeme iliyopo na wakati mwingine kulingana na mahitaji. Ilielezwa zaidi kuwa, miundombinu ya usafirishaji iliyopo ina uwezo mdogo ikilinganishwa na uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuondokana na changamoto hizo, Kamati ilielezwa kuwa Serikali imejikita katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati ambayo itakapokamilika itachangia katika utatuzi wa changamoto hiyo kwa kiasi kikubwa. Miongoni mwa kazi zinazofanyika kutekeleza mkakati huo ni ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **Kv 400** kutoka kituo cha kupoza umeme cha Chalinze hadi Dodoma na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **Kv 400** kutoka kituo cha kupoza umeme cha Tagamenda - Iringa hadi Sumbawanga kupitia Tunduma.

Aidha, Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi ya kuimarisha gridi ya Taifa, ambapo hadi mwezi Februari, 2025 kiasi cha **shilingi bilioni 150,** sawa na **asilimia 75** ya fedha za kuimarisha miradi ya gridi imara **shilingi bilioni 200** zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 kilikuwa kimetolewa. Vilevile, Serikali imeongeza kiasi cha fedha za mradi huo kutoka **shilingi bilioni 200** mwaka 2024/2025 hadi kufikia **shilingi bilioni 250** mwaka 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika, licha ya jitihada zinazotekelezwa na Serikali, ni matumaini ya Kamati kwamba, Serikali itatekeleza miradi hiyo kwa kasi ili kuondoa changamoto zinazokwamisha**

**upatikanaji wa umeme wa uhakika katika baadhi ya maeneo nchini.**

### 3.5.2 Hali ya upatikanaji wa mafuta nchini

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu uagizaji wa mafuta nchini kupitia Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kwa kutumia mfumo wa manunuzi ya pamoja (*Bulk Procurement System* – BPS). Uchambuzi wa Kamati kuhusu hali ya upatikanaji wa mafuta unaonesha kuwa, kumekuwa na ongezeko la mafuta yaliyoingizwa nchini kutoka **tani 2,083,795** kwa mwaka wa kalenda 2023 hadi **tani 2,512,895** kwa mwaka wa kalenda 2024. Ongezeko hili ni wastani wa **tani 429,100** za mafuta sawa na **asilimia 20.59**. Ongezeko hilo limeiwezesha nchi iendelee kuwa na akiba ya mafuta inayotosheleza mahitaji.

Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025, tathmini imeonesha kuwa kumekuwa na ongezeko la matumizi ya mafuta nchini kwa siku kwa wastani wa **asilimia 9.1** kwa mafuta ya dizeli na **asilimia 12.9** kwa mafuta ya petroli ikilinganishwa na mwaka 2023/2024. Uchambuzi umeonesha kuwa, ongezeko hilo la matumizi limechangiwa na ukuaji wa shughuli za kiuchumi nchini. Aidha, uchambuzi zaidi umebaini kuwa ongezeko la matumizi ya mafuta nchini ni kubwa ikilinganishwa na ongezeko la uwezo wa maghala ya kuhifadhi mafuta.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2024, bei ya mafuta iliendelea kupungua duniani. Matokeo ya kupungua huko yameendelea kuonekana nchini, ambapo bei ya mafuta imeendelea kushuka katika mkoa wa Dar es Salaam ikilinganishwa na mwaka 2023. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa, kuimarika kwa shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani kulichangia bei ya mafuta kuendelea kuwa himilivu.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi huu, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kama ifutavyo:-

### 4.1 Wizara ya Nishati

(a) Kutokupokelewa kwa fedha za nje **shilingi 53,200,000,000.00** kwa ajili matumizi mengineyo (OC) na utekelezaji wa miradi ya gridi imara na kufikisha umeme vitongojini, kumeathiri utekelezaji uliokuwa umepangwa. Wizara ifuatilie na kuhakikisha fedha hizo zinapatikana kabla ya kukamilika kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ili kutekeleza malengo yaliyokusudiwa.

(b) Kwa kuwa nchi inazalisha umeme toshelevu kiasi cha kuwa na ziada, na kwa kuwa kuna faida nyingi zinazotokana na matumizi ya umeme huo ikiwemo kuchochea ukuaji wa uchumi. Ili kuchochea faida hizo, Wizara ibadili sera ya malipo yanayotozwa kwa wananchi kutokana na huduma ya kuunganishiwa umeme kutoka mfumo wa kulipia gharama zote kwa mkupuo mmoja kabla ya huduma na kuwa mfumo wa kulipia gharama hizo kwa awamu baada ya huduma kwa kukatwa deni hilo kupitia ankara za manunuzi ya umeme yanayofanywa na wateja.

### 4.2 Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

(a) Kazi ya uthamini kuhusu wananchi waliopisha maeneo yao ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa vituo vya kuzalisha umeme katika mto Ruhudji na Rumakali mkoani Njombe imekamilika. Serikali ifuatilie kwa karibu upatikanaji wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi waliopisha maeneo hayo na maeneo mengine ya aina hiyo kwa mwaka 2024/2025 na mwaka 2025/2026, na kuhakikisha

wananchi wote wanaostahili fidia wanalipwa kwa wakati.

(b) TANESCO iongeze kasi ya kutekeleza miradi ya kujenga miundombinu ya kusafirisha umeme na kuimarisha gridi ya Taifa ili kuondoa changamoto ya mgawo wa umeme katika baadhi ya maeneo na umeme kukosa nguvu kutokana na uwezo mdogo wa miundombinu ya usafirishaji, ukosefu wa miundombinu na uchakavu wa miundombinu.

(c) Mpango wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji ya mto Ruhudji na mto Rumakali ni wa muda mrefu tangu mwaka 1998. Aidha, upembuzi yakinifu uliorudiwa mwaka 2020 hadi 2024 umeendelea kuonesha kuwa miradi hiyo inatekelezeka na ina manufaa kwa nchi kiuchumi na kijamii. Serikali iendelee na jitihada za kuhakikisha miradi hii inatekelezwa sambamba ili kuongeza manufaa ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **Kv 400** kutokea Iringa hadi Sumbawanga kupitia Tunduma inayotekelezwa.

(d) Wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi katika wilaya za Njombe na Makete, Kamati ilibaini uwepo wa matukio ya mara kwa mara ya mashine umba kuungua kutokana na kupigwa na radi. Hali hiyo inachangiwa na mvua nyingi zinazoambata na radi katika maeneo hayo, na hivyo kusababisha wananchi wa maeneo hayo kukosa huduma ya umeme. Ili kuondokana na changamoto hiyo, ni rai ya Kamati kwamba, Serikali ifunge vifaa vya mifumo ya kuzuia radi (*Lightning Protection Systems – LPS*) katika maeneo hayo ili kuzuia radi kuleta madhara katika mashine umba.

### 4.3 Wakala wa Umeme Vijijini –REA

(a) Katika kipindi cha mwaka mmoja kati ya februari, 2024 na Februari, 2025 idadi ya vitongoji vilivyofikishiwa umeme katika kipindi hicho ni **927** tu sawa na **asilimia**

**2.89** ya vitongoji vyote vilivyokuwa vimesalia, idadi ambayo si kubwa. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, mradi huu ulipangiwa bajeti ya **shilingi bilioni 350**, kama ilivyo katika mwaka wa fedha 2025/2026. Hata hivyo, imeonekana kuwa utolewaji wa fedha zilizotengwa ulikuwa kwa kiwango cha chini, na hivyo kuathiri ufikishaji wa umeme vitongojini. Ili kufikisha umeme kwenye vitongoji vingi zaidi, Serikali ihakikishe inatoa kikamilifu fedha zilizopangwa kwa ajili ya miradi ya umeme vitongojini.

(b) Maeneo mengi ya pembezoni mwa miji (peri-urban) hususani miji midogo yanakumbwa na changamoto ya kukosa huduma ya umeme, na hivyo kuzua malalamiko miongoni mwa wananchi wa maeneo hayo. Ili kuondoa malalamiko hayo, Serikali iongeze wigo wa miradi ya kufikisha umeme kwenye maeneo ya vijiji miji ili sehemu kubwa ya maeneo hayo ifikiwe na huduma ya umeme.

### 4.4 Shirika la Maendeleo la Petroli (TPDC)

Katika mwaka wa fedha 2024/2025 TPDC ilikuwa na kazi ya kusambaza gesi asilia majumbani na kwenye taasisi kwa ajili ya kupikia. Hata hivyo, idadi ya kaya zilizofikishiwa gesi hiyo bado iko chini, na hivyo kuathiri mpango wa kaya kutumia nishati safi ya kupikia yenye gharama nafuu. Hivyo basi, TPDC iongeze kasi ya ujenzi wa bomba la gesi pamoja na kuongeza idadi ya nyumba na taasisi zinazotumia gesi asilia katika kupikia.

### 4.5 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)

(a) Kumekuwa na utofauti wa gharama za kuunganishiwa umeme kwa wananchi waishio vijijini, ambapo wateja wa njia moja walio **ndani ya mita 30** kutoka kwenye miundombinu ya umeme ni **shilingi 27,000**, wateja walio **umbali wa mita 70** kutoka kwenye miundombinu ni

**shilingi 515,617.52**, na wateja walio **umbali wa mita 120** kutoka kwenye miundombinu ni **shilingi 696,669.64**.

Kamati ilielezwa kuwa hali hiyo inatokana na muongozo kuhusu gharama za kuunganishiwa umeme uliotolewa na EWURA. Baadhi ya wananchi wamekuwa wakilalamikia gharama hizo kuwa ni kubwa, na pia zinaleta utofauti miongoni mwa wananchi waishio vijijini. Ili kuondokana na malalamiko hayo na kukuza ustawi kwa wananchi, EWURA ipitie upya muongozo huo kwa kuwianisha gharama hizo ili kuweka unafuu kwa wananchi wote waishio vijijini.

(b) Ujenzi wa vituo vya mafuta katika baadhi ya maeneo nchini umeonekana kufanyika kwa namna inayoruhusu kituo kimoja kuwa jirani ikilinganishwa na kingine, na wakati mwingine vituo kujengwa karibu na makazi ya watu. Hali hiyo inahatarisha usalama wa wananchi waishio maeneo ya jirani na vituo hivyo sambamba na kuchochea vituo hivyo kutumika kama maegesho ya magari. Ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza, EWURA ipitie upya muongozo unaohusu ujenzi wa vituo vya mafuta na kuwezesha vituo vya mafuta kujengwa kwa umbali stahiki.

**4.6 Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA)**

(a) Uhaba wa maghala ya kuhifadhia mafuta nchini unaifanya nchi kukosa uhakika na usalama wa hifadhi ya mafuta kwa muda mrefu, jambo linaloweza kuwa na athari mbalimbali ikiwemo kupanda kwa bei ya mafuta. Ili kuondokana na changamoto hiyo, Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa Mradi wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta (*Strategic Petroleum Reserve - SPR*).

(b) Mazingira yanayozunguka *flow metres* na bomba la mafuta, Kigamboni Dar es Salaam si salama kutokana na ufinyu wa eneo na kuzungukwa kwa karibu na makazi binafsi. Kwa kuwa, kuna ongezeko la kiwango

cha kushusha na kupakia mafuta katika eneo hilo, shughuli zinazohitaji usalama na eneo kubwa zaidi ya lililopo, Serikali iongeze ukubwa wa eneo hilo kwa kutwaa maeneo yanayolizunguka.

## SEHEMU YA TANO

### 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuhitimisha hoja ya Kamati kama ifuatavyo:-

### 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee nakushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu tukufu katika utekelezaji wa majukumu yake. Namshukuru Naibu Spika Mhe. Mussa Azzan Zungu, (Mb) pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa namna wanavyokusaidia katika uendeshaji wa vikao vya Bunge.

Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa ushirikiano mkubwa walionipatia ambao umewezesha kutekeleza kikamilifu na kwa ufanisi majukumu ya majukumu ya Kamati. Kwa namna ya pekee naomba majina yao yatambuliwe na kuingizwa kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*hansard*) kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. David Mathayo David, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Aleksia Asia Kamguna, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Tabasamu Hamisi Mwagao, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Sophia Hezron Mwakagenda, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb - Mjumbe

10. Mhe. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mb- Mjumbe
11. Mhe. Iddi Kassim Iddi, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb - Mjumbe
13. Mhe. John Marko Sallu, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Juliana Didas Masaburi, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Maimuna Ahmad Pathan, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Masache Njelu Kasaka, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Ndaisaba George Ruhoro, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Nicodemas Henry Maganga, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Joseph Kasheku Musukuma, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Saada Mansour Hussein, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Eng. Samwel Hhayuma Xaday, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Martha Festo Mariki, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Janeth Elias Mahawanga, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kumshukuru Mhe. Dotto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa ushirikiano wake kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake. Vilevile, natoa shukrani zangu kwa Mhe. Judith Salvio Kapinga (Mb), Naibu Waziri wa Nishati, kwa namna alivyoshirikiana na Kamati katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Aidha, ninawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Nishati na taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu Mhandisi Felschesmi Mramba, akisaidiwa na Naibu Makatibu Wakuu Ndg. Dkt. Khatibu Kazungu na Dkt. James Mataragio, kwa namna walivyoshirikiana na Kamati na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa fanisi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Ildephonce Leonard pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza kikamilifu majukumu yake ya Kikatiba.

### 5.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati (**Fungu 58)** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Dkt. David Mathayo David, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**
28 Aprili, 2025

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa wasilisho hilo la maoni ya Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati yetu ya Nishati na Madini.

Waheshimiwa kama ilivyoada sasa tutaanza na uchangiaji, ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameonesha nia ya kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar na Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya, ajiandae.

Kabla hujasimama Mheshimiwa nimeletewa hapa tangazo la wageni ambao wamepata nafasi ya kuingia hapa Bungeni baada ya tangazo la awali la wageni.

Wapo wageni wengine 120 wa Mheshimiwa Dkt. Biteko, ambaye ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, hawa ni wadau wa maendeleo *(development partners)* wa wizara hii wameingia baadaye.

Haya, washirika wa maendeleo, wakurugenzi na maafisa kutoka wizarani na taasisi zake, sijajua wapo upande gani maana wote hawasimami, kwa hivyo sijui kama wote wapo humu ndani au hawapo. Haya karibuni sana. *(Makofi)*

Watumishi wa Ofisi ya Mbunge, bila shaka hawa wanatoka Bukombe hawa, haya karibuni sana wageni kutoka Bukombe. Makatibu Wenezi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Bukombe, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni kutoka Chama cha Wasambazaji Mitungi ya Gesi Tanzania, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, ambaye ni mpigakura wake, anatokea Dar es salaam, haya. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ambaye ni mjomba wake kutoka Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni ndugu Novia Mazima kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika wizara hii muhimu ya Nishati na kwanza naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kutupa afya na uzima ili tuendelee kuwatumikia Watanzania wenzetu waliyotuamini na kutuleta katika jumba hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote niruhusu nitoe pongezi nyingi sana sana kwa kiongozi wetu, Rais wetu, kipenzi chetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya katika Sekta ya Nishati na kutambulika kama *champion* katika masuala ya nishati siyo tu Tanzania bali Afrika na duniani.

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia nimshukuru Waziri mwenye dhamana ambaye pia ni Naibu Waziri Mkuu na Naibu wake Waziri, Katibu Mkuu na Manaibu Makatibu Wakuu kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakiutoa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambayo nami pia naihudumu kama Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia nitoe pongezi nyingi kwa kazi kubwa inayofanywa na mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Nishati, yaani *TANESCO*, *REA*, *TPDC*, *EWURA*, *PDPA* na *PURA* hapa wapo wananchi wazalendo na wasomi wa nchi yetu wanafanya kazi kubwa sana ya kutafsiri miongozo inayotolewa na nchi yetu kwa vitendo na kuleta tija katika Sekta ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ninataka Watanzania wajue kupitia nafasi hii yangu ya mchango, kwamba tunapoona umeme unawaka kama sisi tulivyo humu Bungeni tunapata mwangaza, tujue wapo Watanzania wenzetu saa hizi wataalam wengine wapo chini ya ardhi umbali wa mita 150, au 200 wakiangalia hayo matabani na hizo dira zinazoendesha shughuli za umeme kila siku wanapokezana usiku na mchana. Kwa hiyo, wapo watu wanaofanya kazi kubwa sana ya kizalendo ya mafanikio haya tunayoyaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza na kutoa shukrani kwa Serikali kwa mkoa ambao nami pia ni Mbunge wa Kigoma kuunganishwa katika gridi ya Taifa na niseme jambo hili sio tu limeipunguzia gharama *TANESCO* kwa kutumia umeme wa mafuta ambao ni gharama kubwa na ambao Serikali imekuwa ikiweka ruzuku, lakini pia unachochea uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi leo ninavyoeleza hapa Bungeni, tangu umeme wa gridi ya Taifa umekuja kipo kiwanda cha *WHI (Tanzania Cement Limited)* kimejengwa katika Mkoa wa Kigoma na tarehe 15 ya mwezi Mei kitafunguliwa kuanza kuzalisha *cement*.

Mheshimiwa Spika, jambo hili litaongeza wigo wa kodi kwa Serikali yetu, litaongeza wigo wa ajira kwa wananchi wetu, lakini pia litaongeza mzunguko wa fedha kwa wafanyabiashara katika mkoa wetu na maeneo mengine. Haya ndiyo mambo tuliyokuwa tunayaomba, tuwe na umeme wa kutosha ili usaidie katika mchakato wa kukuza uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, nawapongeza sana Wizara ya Nishati na *TANESCO* kwa kazi kubwa hii ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo limeelezwa hapa katika maoni ya Kamati nami ningependa kuliwekea mkazo, nalo ni uunganishaji wa umeme kwa wananchi wa mijini. Sasa hivi tumeanzisha Mradi wa *REA* ambao Mradi wa *REA* wa Nishati Vijijini umesaidia na umefanya kazi kubwa sana ya kuleta maendeleo ya nishati vijijini kwa kuwapelekea wananchi umeme kwa gharama ya shilingi 27,000 kuunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, sasa hii imegeuka kama tatizo tulilonalo sasa hivi ambapo tulifika mahali tukawa tunahangaika sana sana kuwalinda na kuwasaidia kuwainua watoto wa kike, tumefanya hivyo kwa muda mrefu sasa inaonekana sasa inabidi turudi kuwasaidia watoto wa kiume maana sasa na wao wanataka kuharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tumesaidia wananchi wa vijijini kuhusu umeme na nishati, lakini sasa turudi mijini maana tunatengeneza tabaka sasa katika nchi yetu. Wapo wananchi mijini ambao wanaishi mijini, lakini hawana uwezo wa kulipia shilingi 321,000 kuunganishiwa umeme. Sasa wanashuhudia mafanikio makubwa ya matumizi ya nishati vijijini lakini wao wakiwa mjini hawana nishati ya umeme. *(Makofi)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**TAARIFA**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mchangiaji anayechangia kwa makini na vizuri sana. Pia ugawaji wa mipaka ya nchi yetu kiutawala huwa hatuzingatii hali za kiuchumi za wananchi, hivyo kuanza kuzingatia hali za mipaka kwa kuwahukumu wananchi kwamba wote wachangie kiasi kadhaa kwa sababu wapo kwenye mipaka ya mjini wakati tunapogawa mipaka huwa hatuangalii hali zao za kiuchumi ni kuwaonea wananchi wa mijini waliokaa kwenye

kipato kidogo cha uchumi, hivyo kuwanyima fursa za kupata huduma kama hizi za umeme. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nimeipokea taarifa na hii inaboresha mchango wangu kwamba sasa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, imeishauri Serikali kupitia bajeti hii kwamba tuone uwezekano wa kuwapa hawa wananchi wa mijini umeme na kulipa kwa awamu awamu kile kiwango cha shilingi 21,000 badala ya kuwanyima na kuwataka walipe kwanza ndipo waunganishiwe umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inataka hawa watu wapewe umeme halafu katika ankara zao za malipo ya kila mwezi tuweke kiwango cha pesa kama ni shilingi elfu kumi kumi kama ni shilingi elfu tano tano mpaka pale watakapomaliza, kwa sababu tunajua, kuunganisha umeme ni gharama kama hakukuwekewa ruzuku na Serikali *TANESCO* hawawezi kutekeleza. Kwa hiyo, tunachotaka ni kwamba uwepo utaratibu wa kuchangia wao kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limeelezwa kwa msisitizo katika Kamati ni suala zima la mchango wa pesa za nje katika bajeti ya Wizara ya Nishati. Hili limeonekana katika mwaka wa fedha uliopita ambapo karibu shilingi bilioni 53.2 hazikupatikana kutoka nje, na hivyo kuathiri mradi wa gridi imara, kuathiri upelekaji wa umeme vitongojini na kuathiri ruzuku iliyotakiwa itolewe kwa *PURA* na *TPDC* katika uendeshaji wa shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme kwamba imeonekana fedha zetu za ndani zimekuwa ni za uhakika zaidi katika utekelezaji wa bajeti kuliko hata tunazoziomba kutoka nje. Kwa hiyo, tunataka Serikali sasa iwe makini kwa kile inachoomba kutoka nje, inapokiingiza kwenye bajeti iwe na uhakika na *commitment* ya hao wanaokileta kwamba kitaingizwa kwa wakati ili bajeti yetu isiweze kuyumba.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumze na niipongeze sana Serikali kupitia Wizara ya Nishati ni suala zima la kupungua kwa malalamiko ya ubora wa mafuta au kutokuwepo kwa ubora wa mafuta katika vituo vya mafuta.

Mheshimiwa Spika, hatua iliyochukuliwa na Serikali kupitia *bulk procurement*. Hawa *PBPA* na *EWURA*, kwa kweli taasisi hizi mbili zimefanya kazi nzuri sana katika kipindi hiki. Ni vizuri ziendelee kupewa nguvu ili ziendelee kufanya kazi kwa sababu huko nyuma kulikuwa na malalamiko makubwa ya magari ya watu kuharibika kutokana na kutokuwepo kwa ubora wa mafuta katika vituo vya mafuta.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi utaratibu wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja umesaidia uwepo wa uhakika wa mafuta, umesaidia ubora wa mafuta, na pia ukusanyaji mzuri wa kodi kupitia mafuta, na hivyo kuwezesha watu kupata mafuta bora katika vituo vya mafuta.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme napongeza hatua hii na ninaomba Wizara iendelee kuzipa nguvu taasisi hizi *(PBPA na EWURA)* ili mafuta ya nishati yanayokuja katika vituo vyetu yaendelee kuwa bora na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumze ni ulipaji wa fidia kwa wananchi. Sisi ambao tunahudumu katika Kamati hii kwa niaba ya Wabunge wenzetu, maeneo tuliyotembelea ambayo yanatakiwa kuwekwa miradi ya umeme kumekuwa na malalamiko makubwa ya wananchi kuchukuliwa maeneo yao kwa miaka miwili, mitatu, minne, au mitano wakiwa hawajalipwa fidia na hawaruhusiwi kuyaendeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kumekuwa na malalamiko makubwa kweli na hili suala la fidia linakwenda mpaka kwenye miradi mingine ya Serikali. Ukienda kule Jimboni kwangu, kuna watu wametoa maeneo yao kwa ajili ya kutaka eneo la uwanja wa ndege liongezwe, lakini ulipaji wa fidia umesuasua kiasi ambacho unazusha malalamiko makubwa sana kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuitaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na kiongozi mahiri, makini na mwenye huruma kwa wananchi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, iangalie kwanza kabisa kama tunachelewa kutekeleza mradi, lakini tulipe kwanza wananchi fidia.

Mheshimiwa Spika, nimeona umewasha kisemeo, kwa maana hiyo unaniashiria nishukuru.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe na ninawashukuru pia Wabunge wenzangu. Ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Nassor Amar atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Shukrani Elisha Manya, Mheshimiwa Rose Vicent Busiga, ajiandae.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nami pia nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kunipa uhai na afya njema na kuweza kusimama kwenye Bunge lako hili Tukufu kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza sana wewe mwenyewe kwa namna unavyoliendesha ama kutuongoza katika hili Bunge. Nasema kwamba hatukukosea kukupa nafasi hiyo, lakini pia nawaomba Wanambeya 2025 wasikuache nyuma wakurudishe tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, anafanya kazi kubwa sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati pamoja na msaidizi wake Naibu

Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya kwenye hii Wizara ya Nishati. Kwa kweli hongereni sana Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati pamoja na Mheshimiwa Judith. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nampongeza Katibu Mkuu na Watendaji wote, wakiwemo Mameneja wetu wa Mkoa wa Geita pamoja na Wilaya ya Nyang'hwale kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya. Nawaomba Wanabukombe, wapo hapa, 2025 turejesheeni Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, kwani anafanya kazi kubwa sana na hajawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha nyingi sana kwenye miradi ya maendeleo kwenye nchi yetu na hususan Wilaya yetu ya Nyang'hwale. Mimi kama mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale tunasema kwamba Mama anatudai, na hususan kwenye upande wa nishati.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyozungumza, Jimbo la Nyang'hwale lina vijiji 62 na vitongoji 273. Vijiji vyote 62 vina umeme na vitongoji 88 pia vina umeme. Hongera sana Mama kwa kazi kubwa unayotufanyia sisi Wananyang'hwale. Tunasema 2025 tupo na wewe, hatutakuangusha na kura zote tutakupa Mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kwa kuunga mkono hoja hii iliyopo mbele yetu. Ni hoja ambayo imesheheni na imeeleza vizuri mipangilio na mipango mizuri kuhusu masuala ya nishati namna gani tunakwenda huko mbele.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Nyang'hwale sisi tunasema hivi, Mama tunamuunga mkono kwenye lile suala la kusema tunataka tuondoke kwenye kutumia kuni tutumie nishati safi. Sisi Wananyang'hwale tumemuunga mkono na tunafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe ushauri kidogo kwenye hili suala. Wapo hapa wasambazaji wa mitungi na gesi, tunaiomba Serikali na ninaishauri ipunguze gharama ya mitungi ya gesi, lakini

pia na gesi yenyewe kwa sababu wananchi wetu kule vijijini vipato vyao ni vidogo. Wamemuunga mkono na tunakubali kutumia kabisa nishati iliyo salama na nishati nzuri ambayo ni ya gesi, punguzeni gharama za mitungi pamoja na gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wananyang'hwale tunasema kwamba usambazaji wa umeme umefanyika, lakini kuna baadhi ya maeneo kwenye Jimbo la Nyang'hwale nadhani pia na kwa nchi nzima, wananchi wamehamasika kuutumia umeme kwa kufunga viwanda vidogo vidogo. Umeme huu umeenea maeneo mengi kwenye Jimbo langu, lakini kuna baadhi ya viwanda vimefungwa zile *transformer* zimezidiwa.

Mheshimiwa Spika, nawaomba sana Wizara, fanyeni tathmini ya kwenda kuzunguka na kubaini zile *transformer* ambazo zimezidiwa, mtuwekee *transformer* kubwa ili wananchi waendelee kufunga mitambo kwa ajili ya uzalishaji wa miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna *transformer* ambazo zilianza kufungwa za *KVA 50,* kwa kweli zimezidiwa. Pia, naomba nishauri kwamba kwenye migodi yetu midogo midogo pia na penyewe nendeni mkafanye tathmini, *transformer* zinahitajika ziende kule ili wananchi wetu na wachimbaji wetu waendelee kutumia umeme huu ambao sasa hivi tunao mwingi. Mtuwekee *transformer* maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Nyang'hwale wananchi wangu wanaulalamikia Mgodi wa Nyanzaga. Nyanzaga wanaenda kuchukua umeme mkubwa kutoka kwenye Mgodi wa Barrick, Bulyanhulu kuupeleka Nyanzaga, lakini kuna wananchi ambao wamepitiwa na mradi huu, wameshafanyiwa tathmini leo takribani zaidi ya miaka mitatu hawajalipwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri Mkuu alichukue hilo, awasiliane na hawa; kwa nini hawataki kulipa kwa wakati na sasa hivi ni zaidi ya miaka mitatu tathmini imeshafanywa?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba walichukue hilo ili wananchi wangu waweze kupata hiyo fedha ili iweze kuwasaidia kwa mambo mengine. Kwa leo hii mimi napenda sana kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri mliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, naungana na ushauri wa Kamati. Leo hii Serikali imeamua kumfungia umeme mwananchi wa kijijini kwa gharama ya shilingi 27,000 lakini kuna wananchi ambao wapo mjini na maisha yao na nyumba zao ni kama zile za watu wa vijijini. Kwa nini, na hawa wananchi waliopo mjini na hasa ambao wapo kwenye ile miji inayonyanyukia mfano Mji wa Kharumwa, nao wasifungiwe kwa shilingi 27,000 tuondokane na ile shilingi 500,000 ama zaidi ya shilingi 500,000? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ukiangalia tunawapelekea umeme vijijini kwa gharama ya shilingi 27,000 na yawezekana yule unayempelekea umeme huo, mteja yupo mbali anataka apelekewe kwa nguzo tatu au nne. Huyo huyo aliyepo mjini hahitaji hata nguzo moja, ni kuvuta tu waya, kwa nini naye asilipe gharama ya shilingi 27,000?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali na kuishauri ijaribu kuangalia hizo sheria kwamba na sasa tuwafungie hawa kwa shilingi 27,000 ili tuweze kuwaongezea na wao kuweza kutumia umeme wanufaike kama wale watu wa kijijini. Leo hii unakuta mtu ana nyumba ya kawaida kabisa mjini lakini kijijini ana nyumba nzuri kabisa anaenda kufungiwa kwa shilingi 27,000. Huyu mwenye kipato cha chini na nyumba yake ni ya kawaida ananyimwa umeme kutokana na kwamba hana uwezo, lakini uwezo wa shilingi 27,000 anao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba sana chukueni ushauri wa Kamati kaliangalieni upya. Wapo wananchi mjini, lakini uwezo wao ni mdogo, nao wafungiwe kwa shilingi 27,000.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Prof. Shukrani Elisha Manya, atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Vicent Busiga, Mheshimiwa Festo Richard Sanga, ajiandae.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu, ambaye anaomba bajeti ya shilingi trilioni 2.2 ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitangulie kuunga mkono hoja, lakini pia nikiungana na maoni ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, moja ya eneo ambalo Serikali yetu imefanya vizuri sana katika hatua ya maendeleo ni katika kutoa huduma ya nishati. Hii imetokana na ukamilishwaji wa Mradi mkubwa wa Bwawa la Nyerere na ule Mradi wa Rusumo ambayo ni miradi ya hivi karibuni iliyokamilishwa katika awamu hii.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, ni kweli kwamba tumekuwa na nishati ambayo ni imara na ni furaha kwa Watanzania kwamba tumeweza kufikia hatua hii ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, nawapongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Naibu wake na Watendaji Wakuu wote wa Taasisi za Wizara hii ambao kwa utaalamu wao na ushirikiano wao wameweza kutufikisha hapa ambapo Watanzania tuna furaha kwa sababu ya hatua hii kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yote haya yameweza kutufikisha kuwa na uwezo wa *Gigawatt* nne za nishati katika nchi yetu. Nikisema *Gigawatt* nne nina maana ya zile zile Megawati 4,000 ambazo ndiyo *capacity* yetu kama Taifa. Ni kweli kwamba pia Serikali imeendelea na ukarabati na uboreshaji wa gridi ya Taifa kwa ujenzi wa njia za kusafirisha umeme katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili tunaomba Wizara yetu na Serikali yetu iendelee na jitihada hizi na kwa kutumia *REA*, basi nishati ya umeme iweze kuwafikia hata wale wa vitongoji ambavyo bado havijafikiwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, utakuta maswali ya Wabunge wengi wakati wa maswali na majibu ni kuhusu vitongoji ambavyo havijafikiwa na umeme. Kwa hiyo, tunaomba hatua inayofuata sasa iweze kuhakikisha kwamba vitongoji vyote nchini vinafikiwa na huduma ya nishati ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha njia za usafirishaji umeme, naomba niwakumbuke Watanzania waliopo visiwani, maana mimi natoka Ukerewe na Ukerewe ina visiwa vingi sana, 38 kwa ujumla wake. Kwa sababu ya njia za usafirishaji umeme kuwa chakavu, mara nyingi sana umeme unaofika visiwani hata mahali pale kwenye gridi ni umeme ule ambao umepungua nguvu, na kwa jinsi hiyo unakuwa hauwezi kutosheleza mahitaji ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiacha kwamba umeme huu unafika ukiwa na uwezo mdogo sana, wale ambao hawapo kwenye gridi na badala yake wanatumia zile gridi za *solar,* mahitaji yao ni makubwa kuliko uwezo wa zile gridi za *solar.* Mara nyingi umeme huu unapatikana kwa saa chache katika siku nzima. Kwa hiyo, inakuwa kama kuwepo kwa zile *mini grid* za *solar* katika visiwa hivi haziwasaidii sana wananchi kwa sababu nyakati nyingine umeme unapatikana mchana pekee yake, halafu usiku inabaki ni giza na hivyo inaonekana kwamba suluhisho yawezekana siyo tu hizi *mini grid.* Wizara ione jinsi ya kuwafikishia gridi ya Taifa hata wale walio katika visiwa pale itakapokuwa inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, utagundua bado eneo la uchimbaji mdogo linahitaji kufikishiwa umeme ili waweze kufanya shughuli zao kwa gharama ambayo ni nafuu. Hili ni eneo ambalo pia Serikali inaweza ikaliangalia ili uchumi wetu uweze kuwa jumuishi na watu wote waweze kufurahia maendeleo ambayo yamepatikana kutokana na kuongezeka kwa nishati nchini.

Mheshimiwa Spika, nirejee katika vyanzo vyetu vya nishati ya umeme. Katika taarifa na hotuba ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ameitoa, vyanzo vyetu vinaendelea kuwa maji yanatoa asilimia karibu 70 halafu na gesi asilia kama 25% hivi lakini umeme wa jua ni 0.1% pekee.

Mheshimiwa Spika, sasa tutakapokuwa na viwanda vingi na shughuli nyingi za uchumi zimechachamaa hapa nchini, *Gigawatt* nne haiwezi kuwa ni umeme tutakaojivunia sana. Hii inatupelekea kwamba lazima tuone sekta hii ni sekta ambayo ni *dynamic,* itahitaji kuongeza vyanzo vingi sana vya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umeme wetu mwingi 70% unatokana na maji, lazima kama Serikali tuweze kuona kwamba kuna kihatarishi cha mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo katika mipango yetu kila wakati kama Wizara ya Nishati lazima tuliangalie kwamba umeme wetu mwingi unatokana na maji na maji ni jambo ambalo linaweza likaathirika haraka sana na mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi hiyo, mradi wetu wa *LNG* ni mradi mkubwa. Tungeomba sana yale majadiliano baina ya Serikali na kampuni za nje yaweze kukamilika kwa wakati na kwa sababu ni mradi mkubwa wa kimkakati na kwa sababu pia utahusisha kusainiana mikataba, tujifunze kutoka uzoefu wa nyuma, maslahi ya Taifa yazingatiwe sana katika mradi huu mkubwa wa *LNG*. Ikiwezekana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu atuambie hata angalau kwa kionjo, lini tutarajie kukamilika kwa mradi huu mkubwa wa *LNG? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, Mradi wa *CNG* ni mradi mzuri. Wale ambao tunatumia *Uber* kule Mjini Dar es Salaam, mtu wa *Uber* anakwambia akiweka gesi yake pale ya shilingi 15,000 anasafiri mwendo mrefu kweli miezi inakatika. Sasa tungeomba Mradi huu wa *CNG* uongeze vituo katika hii njia kuu ya Dar es Salaam hadi Dodoma na Mwanza kuwe na vituo vya kutosha ili watu wengi waweze kuwa na hakika ya kwamba nikifunga gesi kwenye gari yangu, basi nikifika kule Dodoma au Mwanza nina sababu ya kutoathirika nikarudi tena kwa chanzo kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa *way forward;* wapi tuelekee? Wenzetu wa Kenya ambao tupo nao katika bonde la ufa, uwezo wao wa kuzalisha jotoardhi ni Megawati 890. Sisi *potential* yetu kama Taifa ni Megawati 650, ningetamani kwamba tuendelee kuweka fedha nyingi huko ili tafiti zinazoendelea zikamilike ili hiki nacho kiweze kuwa chanzo ambacho kitakuwa kina-*boost* pale mabadiliko ya tabianchi yanapokuja, tunajua tunaweza tukaenda upande wa pili wa jotoardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dunia imeanza kupinga matumizi ya makaa ya mawe kama chanzo cha nishati. Naomba tusiache wakati bado nafasi hii ipo na yenyewe kiwe ni chanzo ambacho mnaweza mkakitumia.

Mheshimiwa Spika, pia katika *literature*, Singida na Makambako ni mahali ambapo upepo wake unaweza kuzalisha umeme, ningetamani katika hotuba zijazo za Wizara ya Nishati, tuwe tunakumbuka chanzo hiki hata kama kwa sasa hatukitengei fedha, lisiwe ni jambo ambalo litaondoka katika mipango yetu kwa sababu *speed* ya upepo tayari ipo, inajulikana, ni suala la kuweka *turbans* na kupata namna nyingine ya kupata njia ya nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa sababu naona umewasha kisemeo, niseme kwamba wananchi wanachotamani ni kupata umeme wa kutosha, na umeme unaopatikana kwa bei nafuu. Nadhani malengo ya mwisho kabisa ya Serikali yawe ni kuona kwamba umeme wetu unapatikana kwa bei ambayo kila Mtanzania ataweza kumudu, na kwa jinsi hiyo uchumi wetu utakuwa unawagusa watu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Rose Vicent Busiga, atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mheshimiwa Michael Joseph Mkundi, ajiandae.

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia. Nianze kwa kumshukuru

Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na siku ya leo tupo humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, nampongeza kwa namna kubwa ameendelea kutuwakilisha vizuri Watanzania. Mheshimiwa Rais ameendelea kufanya kazi katika mikoa yote. Ni sawa sawa nikisema sisi wamama nyumbani unaweza ukawa na watoto 20, lakini wote unawahudumia. Ndivyo Mheshimiwa Rais ameendelea kuhudumia watoto wake wote bila ubaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupongeza pia kwa kuendelea kusimamia hili Bunge. Nisiposema nitakuwa nimejidhulumu. Nakupongeza sana, umeendelea kutuongoza vizuri kwa upendo, na kwa kutumia nafasi hii nawaomba wananchi wa Mbeya, nami nimewahi kuwa mkazi wa Mbeya; wananchi wa Mbeya wananisikia, na watendaji wenzangu wananisikia, Mungu akitujalia 2025 ukapate kura nyingi za kishindo. Nawaomba wananchi wa Mbeya wasipoteze tunu hii ambayo Mwenyezi Mungu amewajalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Bukombe. Pongezi nyingi sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, ameendelea kumsaidia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika majukumu aliyompatia. Nasi Wanabukombe tunajivunia yeye, wananchi wa Geita kwa ujumla tunajivunia yeye kwa sababu ni mtoto wetu. Ameendelea kuwa kinara akituwakilisha vizuri na Watanzania wote wanaijua Geita na Watanzania wote wanaijua Bukombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini wanawake wa Bukombe na wananchi wote tumejipanga, hakuna kura itakayopotea juu yake. Nampongeza mdogo wangu Mheshimiwa Judith Kapinga. Nimeendelea kumfuatilia, ameendelea kufanya kazi vizuri, kujituma, Mungu ambariki sana Mheshimiwa Judith Kapinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba nijielekeze kwenye mchango wangu. Nina mambo mawili tu machache. Mwaka 2024 nilisimama nikachangia hapa, nikazungumzia Bwawa la Mwalimu Nyerere, wakati huo nilitamani kuingia na kile kipimo ambacho kilikuwa kinaonesha, maana niliangalia kilikuwa kinaonesha mafundi wapo kazini, wanachapa kazi; leo nimesimama kuishukuru Serikali yangu ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ninavyoongea hivi Bwawa la Mwalimu Nyerere limeshakamilika, na hivi lina uwezo wa kuzalisha megawati 2,115. Nani kama Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ifike mahali Watanzania tuambiane ukweli, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Mheshimiwa Dkt. Samia ameendelea kufanya kazi kubwa katika nchi hii. Nawaomba Watanzania, ifikapo mwaka 2025 na ndiyo tuko sasa hivi Oktoba, twendeni tukamuunge mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, niwaulize ndugu zangu, ni nani aliyewahi kumchukia mzazi wake? Mtu mmoja asimame aniambie ni nani ambaye amewahi kumchukia mzazi wake? Kila mtu anampenda mzazi wake, ndivyo ambavyo Mheshimiwa Rais amesimama kwa watoto wake wote kuendelea kutulea na kututunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema katika vilindi vya moyo wangu, na wewe unanifahamu vizuri mdogo wako, huwa sifichi, ndivyo ninavyosema, ifike mahali, watu wanaotaka kutugawa tuwakemee kabisa washindwe, sisi tusonge mbele, Taifa letu liwe la mfano na tumtangulize Mungu.

Mheshimiwa Spika, ninavyoongea hivi, katika Mkoa wangu wa Geita ufikishaji wa umeme kwenye Wilaya zangu zote tano ni 99.9%, sawa sawa na 100%. Nisiposema hapa, nitasemea wapi? Nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, amefanya kazi kubwa sana ya kumsaidia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mungu akubariki sana na sisi tunaendelea kukuombea baba, uendelee kupiga kazi, uendelee kumheshimisha Daktari wetu Samia nasi tunamwombea Mheshimiwa Rais wetu,

tunamwahidi Mkoa wetu wa Geita anatudai, tunasubiri muda ufike tukaweke tiki tu, tulipe deni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kudaiwa ni kubaya, tunadaiwa, tuna deni na dawa ya deni ni kulipa. Nasi tumekubaliana wananchi wa Geita tutalipa deni Oktoba.

Mheshimiwa Spika, Geita shughuli kubwa ni uchimbaji wa migodi. Ninavyoongea hivi, kipindi cha nyuma migodini walikuwa wanatumia mafuta kusaga yale mawe, majenereta, lakini Serikali yangu ya Awamu ya Sita imeendelea kuwasaidia wachimbaji wadogo, wachimbaji wakubwa, na kwa wachimbaji wadogo wadogo ufikishaji wa umeme katika migodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninajua mwanzo ni mgumu, lakini najua tutafikia pazuri. Serikali imeshaanza kuwafikishia umeme migodini, nawaomba Watanzania, hata leo mama ukishajifungua hospitali unapewa katoto kadogo, unaanza kukalealea kidogo mara kanatembea. Ninaamini ufikishaji wa umeme katika migodi ya Mkoa wa Geita tunaenda kufanikiwa kwa kiwango kikubwa sana. Naiomba Serikali yangu, Mheshimiwa Waziri unanisikia hapo baba yangu, ninaamini wataongeza kasi na wakandarasi wapo kazini.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa wangu wa Geita Ndugu Joakim. Meneja yule hata upige simu una shida yoyote, anatekeleza vizuri pamoja na Mameneja wa Wilaya akiwemo Meneja wa Wilaya yangu ya Mbogwe, nimemsahau jina. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Meneja wa Wilaya Ndugu Lugiko, kukiwa na changamoto yoyote ukimpigia simu anafanya kazi. Hivyo ninamshukuru sana Naibu Waziri Mkuu pamoja na Naibu Waziri wa Nishati kwa kuendelea kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, na ninawaomba Watanzania wote kwa sauti hii twendeni tukampe Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan maua yake, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Festo Richard Sanga atafutaiwa na Mheshimiwa Michael Joseph Mkundi, na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyopo Mezani ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. Jambo la kwanza naunga mkono bajeti hii na ninaunga mkono maoni yote ya Kamati yale ambayo wameyapendekeza, nami nitakuwa na mambo machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Hii ni kwa sababu, hii ni Wizara ambayo ina mambo mengi kidogo ambayo yanahusu nishati kwenye Taifa letu, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, kazi yao ni njema na kuna wakati wanapitia misukosuko fulani, lakini wamekuwa pamoja nasi kutokana na ukatikaji wa umeme, unakuwa unajumuisha Taifa zima na muda mwingine Watanzania wanakuwa hawajui changamoto ni nini? Hata hivyo wamekuwa wakisimama pamoja na kuisimamia Wizara vizuri na kufanya vizuri hadi sasa hivi hali ya umeme imetulia nchini na nampongeza sana kwa hatua ambayo Mheshimiwa Waziri amekuwa akiifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa ni kuwa mkweli kwamba, kunapokuwa na changamoto Watanzania unawaambia kuna changamoto; kunapokuwa kumetatuliwa Watanzania tunaona kumetatuliwa, hii imekuwa ni sifa ya Mheshimiwa Waziri kwamba ni Kiongozi ambaye pia amekuwa ni muwazi na mkweli kwa Watanzania na ndiyo maana mambo yamekuwa yakienda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, hususan ya kampeni yake ya nishati safi ambayo inamfanya abaki kuwa *champion* kwenye ulimwengu huu na kwa Afrika kwa kuhamasisha matumizi ya nishati safi, vilevile kwa kazi kubwa

ambayo anaifanya. Niseme wazi, tunapomzungumzia Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana na Watanzania lazima wafahamu, mambo mengi ambayo yanaendelea kwenye nchi yetu Mheshimiwa Rais amejitahidi kwa *level* kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ninazungumza tu kwa mfano mambo machache ambayo Mheshimiwa Rais ameyafanya. Ukiangalia tu kwenye suala la usambazaji wa umeme vijijini, Mheshimiwa Rais alikuta ipo zaidi ya 52% lakini sasa hivi amepeleka zaidi ya 100% kwenye usambazaji wa umeme vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapomzungumzia Mheshimiwa Samia, tunamzungumzia Mheshimiwa Samia ambaye alikuta Bwawa la Mwalimu Nyerere lipo kwa 20% na sasa hivi limekamilika. Hizi ni jitihada za Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapomzungumzia Mheshimiwa Rais, tunazungumzia *SGR* ambayo ilikuwa na 49%, yaani unazungumzia ni 100% imekamilika. Unapomzungumzia Mheshimiwa Samia unamzungumzia Samia ambaye Makao Makuu ya Mahakama ambayo juzi ameizindua ilikuwa 30% na sasa hivi ni 100%.

Mheshimiwa Spika, unapomzungumzia Samia, unazungumzia Mji wa Serikali alioukuta una 20%, leo una 89% katika ujenzi. Kwa hiyo, tunapomzungumzia Mheshimiwa Rais, tunajua tunamzungumzia kwa takwimu na tunamzungumzia Rais ambaye amefanya kazi katika upana na ukubwa ambao kila mmoja anatakiwa ajivunie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumhakikishie Mheshimiwa Rais, sisi kama Wabunge na wawakilishi wa wananchi, tunamuunga mkono katika uchaguzi wa mwaka huu, atembee kifua mbele kwa sababu sisi tupo pamoja naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utakuwa na mambo machache sana ambayo yamejikita kwenye Jimbo la Makete na wananchi wa Makete. Jambo la kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Kamati ya Bunge, nawapongeza kwa kufika

Makete na kwenda kujua changamoto za umeme kwenye Jimbo la Makete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Makete wakati tunaingia mwaka 2020 kwenye nafasi ya Ubunge, katika vijiji 93 ni vijiji 32 tu vilikuwa na umeme. Leo ninavyozungumza vijiji 93 vyote vimepata umeme na kijiji ambacho kilikuwa kinasumbua kijiji cha Kiguru, Mkandarasi amepatikana na anaendelea na kazi. Namshukuru sana Mkurugenzi wa *REA* kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa sababu kile kijiji kilikuwa kinasumbua, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni rahisi mtu aliyeko Mjini kuizungumzia Makete kama unazungumzia kamji kadogo hivi, kutoka Kata moja kwenda Kata nyingine unazungumzia zaidi ya kilomita 150. Unazungumzia mazingira ambako kuna mabonde, kuna milima, kuna miinuko, wananchi wanapoona umeme umefika huko, kwa kweli wanaipongeza sana Serikali. Hata Mbunge mwenyewe, kuna eneo ukifika huamini kama umeme umefika kwenye lile eneo, ni kwamba Serikali imefanya kazi kubwa kwenye usambazaji wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa tu ambalo tunaliomba ni kwamba, kuna vijiji ambavyo kumekuwa na changamoto ambayo Mheshimiwa Kirumbe Ng’enda, Makamu Mwenyekiti wa Kamati amezungumza, kwamba Makete mvua inanyesha sana. Kwa hiyo, radi zimekuwa zikipiga sana, kwa hiyo, kumekuwa na changamoto kubwa ya kuungua kwa *transformer* kutokana na radi nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali, maeneo haya ambayo yana mvua, tuweke sana mitego ambayo inaweza kuwa inanasua hiyo changamoto ambayo tumekuwa tukiipata. Unakuta muda mrefu wananchi wanakosa umeme kwa sababu ya kubadilisha transfoma zinazoungua kutokana na radi nyingi. Kumekuwa kukitusumbua kwa muda mrefu, mathalan Kata ya Lupila, Kata ya Ukwama, Kata ya Ipepo, Kata ya Mbalache, haya ni maeneo ambayo yamekuwa na changamoto kubwa sana. Wananchi wanaomba sana muwasogezee huduma ya

kupambana na radi ili kusiwe na kuungua mara kwa mara kwa transfoma hizi ambazo zimekuwa zikisambazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, sisi tuna Bwawa la Rumakali, ambalo ni la pili baada ya Mwalimu Nyerere endapo litejengwa. Kwa kuwa hili ni bwawa ambalo wewe Mheshimiwa Waziri wa Nishati ulifika Makete na kwenye eneo ambalo maji yanapatikana, tunawaomba, wananchi wa Makete kwa muda mrefu wamekuwa wakisubiria ndoto hii iweze kutimia ya kuhakikisha kwamba mradi unaanza kujengwa, na tayari mlishaweka alama kwenye eneo hilo ambalo mradi utakuwa unapita lile bwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili eneo wananchi wamesimamisha shughuli za kiuchumi kwa takribani inaenda miaka miwili sasa wakisubiria mradi utekelezwe. Tunatamani sana muweze kutuambia na kutupa majibu, ni lini fidia italipwa ili watu walipwe, wapishe lile eneo na mradi uanze kutekelezwa?

Mheshimiwa Spika, Prof. Manya amezungumza hapa, moja kati ya marejeo ambayo aliyazungumza Mheshimiwa Waziri alisema, "kwa nini tumefika leo hapa, umeme unakatika mara kwa mara au tuna *shortage* ya umeme nchini?" Alisema kuna wakati tulijisahau hatukuongeza vyanzo, kwa hiyo, matumizi ya umeme yameongezeka. Usambazaji wa leo umesambaa na matumizi ya umeme yamekuwa ni makubwa, kwa hiyo, vyanzo vingi vimezidiwa nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilikuwa ni hoja yake ya msingi sana, ninaamini anaendelea kusimamia hoja hiyo, kwa sababu kama tutajenga Bwawa la Rumakali pale Makete, tukaenda kuzalisha umeme wa upepo kule Makambako, tukaenda kuzalisha umeme wa upepo kule Same, tukiongeza vyanzo hivi, tunaamini kabisa kwamba, tukiwa na umeme toshelevu unaweza kutusaidia kwa sababu nchi yetu ni nchi ambayo inaelekea kuwa na viwanda na migodi mingi, kwa hiyo, tunahitaji matumizi makubwa ya umeme.

Mheshimiwa Spika, mathalan, *Geita Gold Mining* ni mgodi ambao umeme wake unaotumika pale unazidi matumizi yote ya

Mkoa wa Iringa. Mkoa wa Iringa umeme wanaotumia hauwezi kufikia matumizi ambayo yanatumika kwa mwezi ndani ya *Geita Gold Mining. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama migodi hiyo ikiwepo 10 au 20 na kwa sababu madini yamekuwa yakiibuliwa mara kwa mara tunatamani kuwa na umeme mwingi, nasi Makete tuingie kwenye rekodi ya kuzalisha na kulifaidisha Taifa kwenye uzalishaji wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Makete wamenituma nimwombe sana Mheshimiwa Waziri na Wizara ya Nishati na wataalam wake hapa, watusaidie upatikanaji wa umeme kwenye Bwawa la Rumakali.

Mheshimiwa Spika, hii imekuwa ni *story* ya muda mrefu sana, mimi tokea nazaliwa nasikia kwamba kuna mradi huo na wameonesha kwamba kuna *green light* inakuja ya kuanza kutekeleza mradi huo, lakini sasa ni lini wanaanza kulipwa? Tunatamani waanze kulipwa mapema ili wapishe na mradi uanze. Nasi tumeupokea mradi ule kwa mikono miwili na tupo tayari kutoa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tunaipongeza Serikali, Makete toka mwaka 1997 tulikuwa tunatumia *lane* ya umeme ya kutokea Mbeya, lakini mwaka huu wa 2024 mwezi Novemba, mmetubadilishia line sasa tunachukulia Njombe kuelekea Makete.

Mheshimiwa Spika, *lane* hii imetufanya tuwe na umeme wa uhakika kwenye Jimbo letu, kwa sababu tulipokuwa tunatumia umeme wa Makete tulikuwa hatuna *substation*, kwa hiyo, *substation* ilikuwepo kule Mbeya na ikawa inazidiwa nguvu, lakini sasa hivi *substation* tuliyonayo imejengwa Wanging'ombe inayotusaidia watu wa Makete, kidogo kumekuwa na uimarishaji wa upatikanaji wa umeme Jimbo la Makete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana sana, changamoto ambazo zimejitokeza za kukatikakatika umeme muweze kuzitatua kwa sababu *substation* bado haijatengamaa, lakini tunaamini

kwa jitihada ambazo Wizara hii imekuwa ikifanya mnaweza mkatusaidia utulivu wa umeme kwenye ile *lane* ya kuelekea Makete ukapatikana na wananchi wa Makete wakapata umeme wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa sababu umeme wa Makete ulileta na Mzee wangu Tuntemeke Mesaka Nnun'gwa Sanga, nami sasa nimekuja kubadilisha *lane,* nimeitoa kutokea Njombe kuelekea Makete, hii inatufanya tubaki kuwa na rekodi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni la *energy saving campaign*. Kama nchi ni lazima tukaanza kuwa na *energy saving campaign* ili kuelimisha Watanzania. Matumizi ya umeme ni sahihi lakini ni lazima tuwe na matumizi sahihi ya umeme.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi tumekuwa na *behavior*, unaweza ukawasha umeme ukaacha taa zinawaka siku nzima na maeneo mengine tumekuwa tukifanya hivyo. Ni muhimu kama nchi tukaiga utamaduni wa Mataifa mengine ambavyo wanafanya kama Wizara, kuwa na kampeni ya *energy saving.* Hiki ni kitu muhimu sana kwenye nchi, siyo tu kuzalisha umeme. Tunazalisha umeme ndiyo, lakini je, tuna-*save* ule umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana teknolojia zimekuwa zikija, kwamba, kwa sababu ya *behaviours* za binadamu anatoka chumbani bila kuzima taa, kwenye hoteli watu wameanza kufunga *appliances* ambazo mtu ukitoka umeme unajizima kwa sababu, watu wamekuwa hawana utamaduni wa kutunza *energy*.

Mheshimiwa Spika, kama Taifa ni lazima tuwe na utaratibu wa ku-*save energy* ambayo tuko nayo, ili tuweze kuendana na mifumo ya kiuchumi na kusaidia watu wetu wa *TANESCO* na *line* nyingine kuendelea kupata umeme kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natamani sana *energy saving campaign* iwe ni moja kati ya kampeni yao, kutoa vipindi kwenye *TV,* shuleni na kuielimisha jamii, kwamba, unapotoka ndani ya nyumba yako uwe na tabia hii ya kuzima taa, kuzima *switch,* ili kuhakikisha kwamba, tuna-*save* umeme kwenye nchi yetu kwa sababu, matumizi ya umeme yamekuwa ya kiholela sana, kitu ambacho siyo sahihi kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nami nakutakia kila la heri kwa sababu, tunaamini kwa jitihada kubwa ambazo unazifanya na uwakilishi wako kwenye Bunge la Umoja wa Mabunge Duniani, umekuwa ukitupa heshima, kama nchi. Sisi kama Waheshimiwa Wabunge, tunajivunia na tunawaomba Wanambeya kwamba, wakupe haki yako, wakurejeshee haki yako na kwamba, mwezi wa Kumi na Moja mwaka huu uwepo hapa kwenye kuapa pamoja na sisi. Ninaamini kabisa kwamba, utaendelea kuipeperusha bendera ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunakutakia kila la heri na tupo tayari, kwa sababu, sasa hivi tunajiandaa kwenda kwenye *Tulia Marathon* kule Mbeya, tutaenda kuwatangazia pia kwamba, tunamhitaji Mheshimiwa Dkt. Tulia tena ndani ya Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Michael Joseph Mkundi, atafuatiwa na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga. Kama muda utasalia, Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka atachangia pia.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naanza kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, ambaye kwa mara nyingine katupa fursa ya kusimama kutoa mchango wetu, hususan kwenye bajeti ya Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa uwasilishaji mzuri pamoja na Kamati, zaidi kwa utendaji wake katika Wizara hii. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati hongera sana na Mwenyezi Mungu akubariki wewe pamoja na Naibu wako na timu nzima mnayoshirikiana nayo kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais. Kihistoria huko nyuma tulikuwa na changamoto nyingi sana kwenye sekta hii ya nishati, lakini leo tunapojadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii kuna mabadiliko makubwa, mojawapo ikiwa ni kuongezeka kwa kiwango cha umeme tulichonacho.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2024 wakati tunajadili tulikuwa na megawati 2,000, lakini leo tuna megawati 4,000 baada ya kukamilika kwa ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Nina kila sababu ya kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa sana anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama wengine walivyotangulia, ninakupongeza wewe vilevile kwa namna unavyoendesha Bunge letu hili. Kwa kweli, wewe ni bingwa sana na Wanambeya wanastahili kukupa unachostahili, kura nyingi na kurudi Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina hoja chache kwenye sekta hii. Kwanza, kuna kazi kubwa imefanyika kwenye Wizara ya Nishati, hususan kwenye kuboresha miundombinu na kusambaza umeme. Kazi kubwa sana imefanyika na tukiangalia kwenye *energy mix, proportionality* iliyopo katika uzalishaji kwenye njia ya maji, mafuta gesi na kadhalika, imeegemea sana kwenye eneo la maji.

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema wachangiaji kadhaa, natamani pia tuwekeze kwenye eneo la upepo pamoja na nishati ya jua. Hii inaweza kutusaidia sana kujenga uwiano mzuri na kuwa na tahadhari iwapo linaweza likatokea lolote kwenye eneo moja ambalo tumewekeza sana, ambalo ni eneo la maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwenye *energy mix* ninashauri vilevile tuwekeze sana kwenye eneo la umeme jua pamoja na upepo. Kwa sababu, ninaamini, kama Taifa, tuna maeneo mazuri tu ambayo tunaweza kuwa na vyanzo vizuri vinavyoweza kutusaidia kupata umeme wa uhakika kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye Jimbo la Ukerewe. Ukerewe, kama yalivyo maeneo mengine nimekuwa nalisema mara kwa mara hapa, tuna changamoto moja kubwa ya kukatikakatika sana kwa umeme.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu, pamoja na kwamba, tunapata umeme kutoka kwenye chanzo cha umeme kutoka Kibara, lakini *voltage drop* ni kubwa sana mpaka kufika Ukerewe. Kwa maana hiyo, umeme unapofika Ukerewe; moja, unakuwa na nguvu kidogo, lakini inapotokea hitilafu yoyote katikati ya safari hapa, Kisiwa cha Ukerewe chote kinaathirika kwa kukosa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa natambua, tuna Mradi wa kuongeza nguvu ya umeme na kuvuta kutoka Bunda kwenda Ukerewe na kujenga *substation* kwenye eneo la Magea pale Ukerewe. Mradi huu unasuasua sana na ni kwa sababu, baada ya kufuatilia, wananchi wanaopaswa kulipwa fidia kwenye eneo ambako mradi huu unapita, hawajalipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, Mheshimiwa Waziri tafadhali, wananchi wa Ukerewe wanapata shida sana kutokana na kukatikakatika kwa umeme. Hali yao ya kiuchumi inaathirika, hali ya kipato kwa ujumla wake inaathirika na hali ya kimaisha inaathirika kwa sababu ya tatizo hili la kukatikakatika kwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba hawa wananchi, basi walipwe fidia, ili huu mradi uendelee kuwa na kasi yake na uweze kukamilika. Ile *substation* ijengwe, wananchi wa Ukerewe wapate umeme wa uhakika. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ilipe kipaumbele jambo hili, ili wananchi wa Ukerewe waondokane na adha ya kukatikakatika kwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ni kuhusu umeme wa visiwani. Nimeona kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Ukurasa wa 53, inaongelea juu ya usambazaji wa umeme kwenye visiwa 120 kwenye mradi wa kupeleka umeme kwenye maeneo ambayo yako nje ya gridi ya Taifa, Mheshimiwa Manya amegusia katika mchango wake.

Mheshimiwa Spika, Ukerewe tuna visiwa zaidi ya 30. Katika visiwa hivyo, natambua kazi kubwa iliyofanywa na Wizara kwa sababu, ukiondoa visiwa katika vijiji 76 tulivyonavyo, vijiji 14 viko kwenye visiwa vidogo. Vijiji vingine 62 mpaka mwaka 2020 tulikuwa na vijiji 18 ambavyo havikuwa na umeme, lakini leo vyote vina umeme.

Mheshimiwa Spika, pia, vile vijiji 14 vilivyoko katika visiwa vidogo bado vijiji vitatu pekee, ni vijiji 11 ambavyo vimepata umeme kupitia umeme jua, lakini vijiji hivi na vitongoji vyake kupitia kampuni zilizowasambazia umeme, wanapata umeme saa tano asubuhi, saa nne usiku umeme unakatika. Achilia mbali umeme ule wananunua shilingi 2,000 kwa *unit*. Kwa hiyo, wananchi wanateseka sana, wanaishi maisha magumu na maisha yao ya kiuchumi yanaathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mradi huu mnaotarajia kuuleta ninawaomba sana, wananchi wa visiwa hivi wameteseka sana kwa muda mrefu kupitia umeme jua kwa kampuni ambazo zimewapelekea umeme, basi mradi huu uanze haraka na ukamilike haraka. Natamani Ukerewe ndiyo wawe wanufaika wakubwa kwenye mradi huu ili wananchi hawa kutokana na mateso waliyoyapata huko nyuma waweze kusahau uchungu ambao wamekuwanao kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Wizara iliangalie sana hili, lakini mbali na hivi vijiji, kuna visiwa vingine zaidi ya 30 ambavyo bado havina umeme. Kwa hiyo, kuja kwa mradi huu itakuwa ni mkombozi mkubwa kwa wananchi wale. Mheshimiwa Waziri, nakuomba sana muutumie mradi huu kama mkombozi kwa wananchi wa Ukerewe, hasa wa visiwa vidogo, kwani wanapata wakati mgumu sana na hasa hawa ambao wanapata

umeme kupitia umeme jua. Wanalipa *unit* moja kwa shilingi 2,000 na bado wanapata umeme kwa saa chache sana.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara iliangalie kwa uzito mkubwa. Natamani hata wakati wa kuhitimisha hoja, Mheshimiwa Waziri akasema lolote kuhusu maeneo haya ya visiwa vidogo, hasa Visiwa vya Ukerewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naunga mkono Taarifa ya Kamati. Taarifa ya Kamati katika Ukurasa wake wa 12, wanaongelea juu ya gharama ya kuunga umeme kwenye maeneo ya mjini na vijijini. Ni kweli kwa mwongozo uliopo, kupitia Mradi wa *REA* ambao umefanya kazi kubwa sana, na ninampongeza Mkurugenzi wa *REA,* wamefanya kazi kubwa sana. Kwenye Jimbo langu tuna vitongoji vingi sana ambavyo vimepata umeme, na juzi nimepata taarifa, vitongoji vingine 96 vitapata umeme hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, ili kuweka uwiano sawa kwenye gharama ya kuvuta umeme kwenye maeneo haya, tukitoa umeme kwa wananchi wa vijijini kwa shilingi 27,000/= na wananchi wa mjini wakapata umeme kwa shilingi 300,000/= tutakuwa hatutendi haki kwenye maeneo haya. Kuna wananchi wanaishi mjini, sawa, lakini kiwango chao cha aina ya maisha wanayoishi inawezekana wako chini zaidi ukilinganisha na baadhi ya wananchi walioko vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba liangaliwe hili kupitia taasisi zinazohusika, fanyeni tathmini, mtoe mwongozo mpya ili tujenge uwiano kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, natoa pongezi kwa Meneja wangu wa *TANESCO,* Wilaya ya Ukerewe. Pamoja na changamoto zote hizi amekuwa anafanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba, wanazitatua kwa haraka na wananchi wanaendelea kupata nishati ya umeme. Kwa hiyo, nina kila sababu ya kumpongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, atuangalie sana watu wa visiwa hasa vya Ukerewe ambao tuko *off grid*. Mazingira yetu ni magumu sana kwenye nishati ya umeme, hasa vile visiwa vidogo ambavyo wananunua umeme kwa bei kubwa, lakini wanaupata umeme kwa saa chache, wanahangaika sana. Naomba sana msaada ili kuwasaidia wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia katika Wizara hii. Kwanza nami naungana na wenzangu kuunga mkono hoja hii kwa asilimia zote. Pili, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Pia, nampongeza Naibu wake Mheshimiwa Judith pamoja na wataalam wote katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayasema haya kwa moyo wa dhati kabisa, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa namna anavyoitendea haki Wizara hii. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kabla ya kuwa hapa, alikuwa Waziri wa Madini. Tunaona jinsi alivyoyafanya vizuri mazingira katika Wizara ya Madini. Namshukuru na kumpongeza sana. Akiwa Waziri wa Madini, aliwahi kufanya Mkutano Mkubwa wa Wadau wa Madini, Songea na ilikuwa ni historia kwetu Songea mkutano ule kufanyika. Alitupa matumaini mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Songea, pamoja na madini mengine, kwetu sisi Mbinga ni wachimbaji wa makaa ya mawe. Kwa hiyo, kulikuwa na mambo mengi yanazungumzwa pale, lakini kupitia yeye na kupitia uratibu wake, alifanya mkutano ule. Kwa kweli, mambo yalikuwa mazuri na sasa kero nyingi zimepungua. Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa yuko hapa kwenye nishati akishirikiana na mdogo wangu, Mheshimiwa Judith, wanafanya

kazi nzuri sana. Mheshimiwa Judith ni lazima nikupongeze kwa sababu, umekuwa msaada mkubwa kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu Naibu Waziri Mkuu ana majukumu mengi na mazito. Kwa hiyo, Mheshimiwa Judith amechukua nafasi hii na anafanya vizuri sana. Hongera sana mdogo wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, nije kwenye mchango. Mchango wangu mimi leo, namkushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. Nashukuru nini? Wakati tunaingia madarakani, mimi Benaya, hali ya usambazaji wa umeme ilikuwa ni ndogo sana. Nina vijiji 117 na kati ya vijiji hivyo, vijiji 24 tu ndiyo vilifikishiwa umeme. Siyo vyote, vijiji tisa kati ya hivyo 24 kulikuwa na harakati ya kufikisha umeme, Kwa hiyo, tulikuwa na vijiji vingi zaidi ya 96 ambavyo havikuwa na umeme. Leo hii nashukuru na ninafurahi kwamba, vijiji vyote 117 vimefikishiwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haikuwa rahisi kufikisha umeme kwenye vijiji hivi, ilikuwa ni kazi kubwa sana, kubwa mno, kwa sababu, unaweza kuona upelekaji wa umeme umeanza awamu nyingi tu, lakini ni awamu hii ndiyo umeme umefika katika vijiji vyote 117. Kwa hiyo, ilikuwa ni awamu iliyopita, iliyofuata, lakini awamu hii ndiyo umeme umefika katika vijiji vyote 117. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naweza kuiona kazi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na mdogo wangu Mheshimiwa Judith ya kusukuma umeme kufika kwenye vijiji vyote. Hii ilikuwa ni kazi ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ninampongeza sana Mkurugenzi wa *REA,* aliwahi kufika mpaka kijijini kwangu ninakotoka. Baada ya kuona kijiji kile kiko pembezoni zaidi na inawezekana pengine umeme usingefika, basi alifika mpaka kijijini. Alipofika pale akanipigia simu, "nipo nyumbani kwako."

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana na ninampongeza sana *Eng.* Hassan, ile nayo ilitoa msukumo wa kupeleka umeme

kwenye vijiji vile. Sasa tunashukuru umeme huu umefika katika vijiji vyote, lakini kwa sababu, tumechelewa sana sana kupeleka umeme kwenye vijiji hivyo kwa hiyo, tuko nyuma kwa upande wa vitongoji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi juzi hapa tumefanya Kikao cha *RCC,* tulikuwa na halmashauri mbili au majimbo mawili; la mwenzangu pamoja na la kwangu, ndiyo tuko chini sana katika upelekaji umeme kwenye vitongoji. Hatujafika hata 50%; sisi tuko chini ya 40%. Mimi katika vitongoji 782 ni vitongoji 293 tu ndivyo tulivyofikisha umeme kwa hiyo, bado tuna mzigo mkubwa wa kupeleka umeme.

Mheshimiwa Spika, ilivyo vizuri, Wanambinga sisi tuna vita ya maendeleo. Sisi huwa hatupendi kukubali mmoja hapa ameweka kitu, mimi nikakosa. Kwa hiyo, sasa hivi Mbinga kuna vita kubwa sana ya kutaka kupata umeme. Nakuomba sana, tulikuwa tuna vitongoji vile 15, najua mchakato unaendelea, lakini sasa awamu hii kwa vile sisi tulikuwa nyuma sana, basi mtupe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tuko chini ya 50%, maana yake wenzetu angalau wamevuka 50%. Najua kuna kazi kubwa ya namna ya kupeleka umeme katika hivi vitongoji, ni vizuri tukatembea wote kwa pamoja. Siyo wengi wako mbele sana na wengine wanawabeba wenzao kwa nyuma zaidi ikiwemo Mbinga vijijini.

Mheshimiwa Spika, nakuomba sana, na hapa leo utakapokuja kuhitimisha hoja hii, utupe matumaini. Katika awamu hii unatupa kipaumbele kiasi gani nasi ili tulingane na wenzetu hata tukawazidi zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, Mbinga pana changamoto kubwa, nimeisema hapa na niliuliza hapa mara kadhaa. Umeme unakatika sana. Yaani kule umeme kukatika mara 20, ni jambo la kawaida. Kwa hiyo, hali hiyo inasababisha shida sana kwa wafanyabiashara wetu na wajasiriamali. Wengine wamefunga

mpaka biashara kwa kuhofia, leo nitaweka kitu, umeme utakatika.

Mheshimiwa Spika, najua iko mikakati ya kupeleka hizi *substation* na ndiyo ilikuwa ahadi ya Serikali kutuletea *substations,* sasa nimeangalia hapa sijaona kwa sababu, andiko lenyewe ni refu. Najua unaweza ukatamka kitu, tutaipata lini hiyo *substation* ili isaidie kwa sababu, watumiaji kule ni wengi mno?

Mheshimiwa Spika, umeme ukifika, wanaotaka kutumia ni wengi mno kwa sababu ya ile niliyosema, vita ya maendeleo. Kila mtu anataka apate umeme. Sisi Wamatengo hatuwezi kukubali wewe una umeme, mimi nikose umeme. Aahaa, lazima na mimi niwe na umeme, ndivyo ilivyo. Hayo ni maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tupate fursa, sisi Wamatengo tupate fursa umeme ufike, wote tuweke umeme. Ukiona huko kwenye maeneo mengine watu wanasuasua kufungiwa umeme, wewe lete Mbinga, wananchi wote watafunga umeme na tutachangia vizuri, *TANESCO* watapata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, nawapongeza sana kwa hamasa hii ya nishati mbadala na hapa kipekee nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kafanya kazi kubwa sana katika nchi hii kiasi kwamba, sasa kila mtu ndani ya nchi hii anajua kumbe kuliko kutumia kuni kuna nishati mbadala, kuna gesi. Kwa kweli, hapa inabidi tumpongeze sana mama yetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale Mbinga pamoja na ugawaji mzuri na usambazaji huu wa gesi, sisi pale tuna makaa ya mawe na makaa ya mawe yanaweza kutumika kwa kuwa, nishati mbadala. Hapa nawapongeza sana akina mama wa Mbalawala, wao muda mrefu wamekuwa wanatoa hamasa ya namna ya kutumia haya makaa ya mawe kwa kupikia na yanapika vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, hamasa hii tuliyoweka ya kusambaza gesi, tufanye hivi hivi kwenye makaa ya mawe kwa sababu, ni ya kwetu, hatuendi kuyachota kwa watu huko, ni ya kwetu wenyewe hapa hapa. Tunayachimba hapa, tunayachakata, yanakuwa rahisi *then* tunatumia kwa kupikia. Yanaweza kuwa suluhisho zaidi kuliko hii gesi ambayo sasa hivi, pengine zile tulizogawa wengine sasa wamegeuza viti, japo siyo vizuri sana kwa sababu, wanashidwa ku-*refill*.

Mheshimiwa Spika, ku-*refill* huko nako ni gharama kidogo. Kwa hiyo, tunaomba tuone ni namna gani tunaweza kuwafanya hawa Watanzania wa kawaida nao waweze ku-*refill* hiyo mitungi ambayo wanayo. Nina uhakika kwenye maeneo mengi ile mitungi ilivyoisha, pengine watu wengi hawaja-*refill*. Makaa ya mawe hayana ku-*refill,* yenyewe ukushayatengeneza ni kuweka tu mkaa mmoja au miwili unapikia vizuri chakula kinaiva. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. Ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa kipindi cha kwanza cha kukutana leo umekwisha. Kwa hiyo, nitatangaza majina tutakayoanzanayo alasiri.

Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao na wengine wataendelea kutajwa kwa kadri muda utakavyokwenda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni, leo.

*(Saa 7.03 Mchana, Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11:00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo niwe mchangiaji wenu wa kwanza. Vilevile namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha jioni hii kupata uhai wa kuweza kusimama kwenye Bunge hili Tukufu na kusema machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru sana au kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maono ya kufanya mageuzi makubwa kwenye Sekta hii ya Nishati. Tukiangalia namna tulivyoweza kumaliza mradi ule mkubwa wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, kwa kweli juhudi hiyo ni kubwa sana. Siyo hivyo peke yake, hata kwenye hii ya kuwa *champion* wa nishati safi ya kupikia nayo ni juhudi kubwa ameifanya kwenye hii sekta ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya yasingeweza kufikiwa, ndoto za Mheshimiwa Rais zisingeweza kufikiwa bila kupokewa vizuri na wasaidizi wake wakiongozwa na Naibu Waziri

Mkuu, Mheshimiwa Doto Biteko na dada yangu Mheshimiwa Kapinga, Watendaji Wakuu na Watendaji wote walioko kwenye Wizara Nishati wakiongozwa na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Wizara hii nitakuwa nina mambo makubwa mawili. Jambo la kwanza litakuwa ni maombi, na la pili litakuwa ni ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyopongeza, baada ya Bwawa la Mwalimu Nyerere kukamilika kwenye makaratasi, tayari tuna ongezeko kubwa la umeme. Naomba tu niseme ukweli hapa, kwamba sisi watu wa Mikoa ya Lindi na Mtwara bado *physically* hatujapata hili ongezeko kwa sababu bado tuna shida ya kukatikakatika kwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa napo napongeza sana juhudi za Serikali. Nimeangalia hata kwenye bajeti imo, kwamba Mkoa wa Lindi na Mtwara tunakwenda kuingizwa kwenye Gridi ya Taifa, ni jambo jema. Ushauri wangu kwenye hili, naomba jambo hili liharakishwe na ikiwezekana Naibu Waziri Mkuu atakapokuja kuhitimisha atuambie sisi watu wa Lindi na Mtwara, hii kazi inakwenda kukamilika lini ili nasi tufaidi hili ongezeko la kuwepo kwa umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwenye hili, Wilaya ya Liwale tunapokea umeme kutoka Maumbika, na kutoka Maumbika mpaka Liwale ni zaidi ya kilomita 300; na ndiyo maana umeme wa kule unakatikakatika sana. Kwa hiyo ombi langu kwenye hili ninaomba tujengewe kituo cha kupoozea umeme Liwale ili huu umeme unapotoka Mahumbika mpaka Liwale, na sisi tuweze kuupata kwa kiwango kinachohitajika na uweze kustahimili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nilipigiwa simu na mwananchi kutoka Liwale, ananiambia, “Mheshimiwa, hebu waambie hao watu wa Wizara, umeme unavyokatika Liwale ni nafuu wakati ule wa mgao, kwa sababu wakati ule wa mgao tulikuwa tunajua leo hatuna umeme kama siku nzima, lakini sasa kama umeme unakatika kwa siku zaidi ya mara sita, tayari

unaunguza vyombo vyetu. Unaunguza majiko, unaozesha vyakula kwenye friji na mambo mengine kama hayo. Wakati ule wa mgao ananiambia kwamba wakati ule tulikuwa na uwezo wa kujua kwamba leo kutwa nzima hatuna umeme, au kesho usiku kucha hatuna umeme. Kwa hiyo, tulikuwa tuna uwezo wa kujipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana sikubaliani naye sana, lakini jambo aliloniambia, naona kama lina mantiki. Kwa hiyo, naomba sana, sana, sana, hili jambo tuone kwamba na sisi tunahitajika kufanyiwa huo utaratibu wa kuingia kwenye gridi ya Taifa na hatimaye tujengewe *substation* pale Liwale ili umeme uweze kupatikana kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais kwenye Nishati Safi ya Kupikia. Hapa napo naomba nitoe ushauri mmoja. Tumejenga shule nyingi sana za sekondari, vituo vya afya na hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ndugu zangu wa Serikalini, watusukilize. Pengine waanze kufikiria, tunapopeleka miradi hii ya ujenzi wa shule na zahanati, hebu waweke na *package* ya majiko ya gesi. Kwa sababu ukienda kumwulizia Mwalimu Mkuu wa shule fulani, anakwambia ni mpaka apate ile *capitation* ndipo aweze kukusanya apate fedha za kujenga mtambo wa kutengeneza gesi pale kwenye shule yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili kuungana na Mheshimiwa Rais katika kuondokana na utumiaji wa majiko ya mkaa na kuni shuleni, basi waone namna ya kuwezesha hizi shule zetu mpya tunazozijenga, hata zile za zamani tulizojenga, basi wapeleke *package* ambayo itaweza kujenga haya majiko ya umeme na kupunguza matumizi ya majiko ya mkaa na kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, naomba nisisitize kuhusu hili jambo la gharama za kuingiza umeme nyumbani kati ya vijijini na mijini. Kule kwetu Liwale hatuna miji, sisi kule ni vijiji. Sasa unapomwambia mwanakijiji wa pale Liwale Mjini eti kwa sababu tu yuko mjini, wanaita vijiji miji kwamba alipe shilingi

350,000 wakati wenzake wa kule vijijini wanalipa shilingi 27,000, kidogo kunakuwa na kigugumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hapa naomba niungane na wenzangu wote waliosema hapa kwamba, wapo wakulima vijijini wamepata fedha za korosho, wamejenga majumba makubwa mpaka ma-*pub* yapo kule, lakini kuingiza umeme anaingiza kwa shilingi 27,000. Mwenzangu na mimi pale mjini amegalagala amepata shilingi zake mia mbili amejenga vyumba vyake viwili na ukumbi, kuingiza umeme shilingi 350,000. Kwa hiyo, unakuta uwiano hauko sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu watafute *model* nzuri ya kwanza kuwatambua hao watu wa vijijini ni nani wana kipato kikubwa, na nani wana kipato kidogo? Waje na *model* nzuri. Hata kama wakisema kwamba watusogeze kutoka shilingi 27,000 iende kwenye shilingi 50,000, halafu huyu wamshushe ifike kwenye shilingi 100,000, angalau kidogo unaona kwamba kuna kitu kinatembea hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema tu kwamba watu wanaokaa mijini ambavyo wao wanaviita vijiji miji, kwanza namna ya kuvipata vile vijiji miji, lile jambo halijawa shirikishi. Hii elimu haijawafikia, kwamba wengi ni wapi wapo kwenye vijiji miji na wapi vijiji kabisa. Kwa hiyo, ombi langu kwenye hili, waone na watafute *model* nzuri ya kutuletea umeme huu kwenye hivi vijiji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati naendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na ninaendelea kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, lakini vilevile nisiache kumshukuru Meneja wangu wa Wilayani pale, anaitwa Hamisi Kaduma. Kwa kweli yule kijana anafanya lazi ya ziada. Kwa mazingira ya Liwale na namna umeme unavyokatikakatika na mvua hizi zinavyonyesha, saa saba ya usiku mtoto wa watu yuko porini na timu yake wanahangaika kutupatia umeme. Jambo hili ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linakwenda sambamba na uhitaji wa nguzo za zege, kwa sababu kule kwetu sisi eneo kubwa

ni misitu. Sasa zile nguzo za umeme sana sana ni za miti. Kuna mambo mawili; aidha ziungue moto au zikipitiwa na maji zianguke. Sasa tukiletewa hizi nguzo za zege zitasadia zaidi. Najua kwamba wameanza kubadilisha nguzo, lakini naomba ziongezwe, kwani zile nguzo hazitoshi, na ule mji ni mkubwa, na mtawanyiko ni mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo niongeze na la watumishi. Unajua Wilaya yetu ya Liwale imewatanyika sana na kama nilivyosema, Mheshimiwa Rais ameweza kufikisha umeme karibu vijiji vyote 72. Mimi nina kijiji kinafika kilomita 114 kutoka Liwale Mjini. Sasa unamwambia Meneja kuwa nguzo imekatika huko kilomita 120 au 114, yuko huko na huku kwingine kilomita 80 nguzo nako imeanguka. Kwa hiyo utakuta tatizo linalokuja pale ni vifaa vya kufanyia kazi, kwamba magari ni machache. Unaweza ukakuta gari analo moja tu, na gari hilo ndilo analolitumia Meneja, na gari hilo hilo ndilo la *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana watuongezee vifaa ili tuweze kukabiliana na hizi changamoto za umeme kukatika mara kwa mara. Pamoja na vifaa, tuongezewe na watumishi. Nilijaribu kukutana naye akaniambia kuwa ikama yao pale ni 15, lakini wako nane tu. Sasa utaona; ina maana kwamba kazi ya watu 15 inafanywa na watu nane. Hapo napo waone mzigo mkubwa walionao hawa watumishi wetu pale Wilayani Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nina hayo tu ya kuyasema kwa kipindi hiki; na baada ya kuyasema hayo, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, ajiandae.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Nami ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye anatupatia uhai, afya njema kuyafanya haya

tunayoweza kuyafanya katika Bunge hili. Pili, namshukuru Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuliongoza Taifa, lakini hususan kwenye hii sekta ya nishati. Nampongeza Waziri na Naibu Waziri Mkuu, Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara. Kusema kweli Kaulimbiu ya *TANESCO* kwamba Tunaiwasha Nchi, wanaitekeleza kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza wafanyakazi wa Shirika la Umeme Mkoa wa Kagera. Wanafanya kazi nzuri na kubwa ya kujituma na iliyotukuka. Nawapongeza wafanyakazi wa *TANESCO* Wilaya ya Muleba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwapongeza huku, namwomba Mheshimiwa Waziri asije akawahamisha. Wawahamishe kama wanapanda cheo. Ni wachapa kazi, wanajituma na wanastahili hizi pongezi, isipokuwa kuwahamisha labda kama anawahamisha kwa kuwapandisha vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia machache. Naipongeza Serikali kwa uwekezaji mkubwa ambao umefanyika. Napongeza kwa kukamilisha Bwawa la Mwalimu Nyerere, ni hatua kubwa sana, na miradi mingine ambayo imesemwa kwenye hotuba ya Waziri wakati anawasilisha hapa mbele yetu, yote ikikamilika, na nina uhakika itakamilika, nadhani suala la umeme kukatikakatika litakuwa limekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kidogo kuhusu Mkoa wangu wa Kagera. Kwa kipindi kirefu Mkoa wa Kagera, ukiondoa Wilaya mbili za Biharamulo na Ngara, Wilaya zote zilizobaki ziko nje ya gridi ya Taifa. Tunapata umeme kutoka Uganda, na tumekuwa na tatizo kubwa sana la umeme huo kukatikakatika, hasa katika Wilaya yangu ya Muleba. Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake, tunamwomba atupatie mwarobaini au suluhu ya umeme kukatikakatika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wilaya yangu, tatizo kubwa tulilonalo pamoja na kwamba tuko nje ya gridi ya Taifa, tunahitaji kituo cha kupoozea umeme katika Wilaya ya Muleba.

Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu anajua kwamba Wilaya ya Muleba ni kati ya wilaya kubwa. Tunazo kata 43, hatuwezi kuichukulia kama wilaya nyingine ndogo, ni wilaya kubwa. Nimewapongeza watumishi wake. Pamoja na matatizo haya ya umeme kukatikakatika, lakini bado tuna changamoto ya vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema ni wilaya kubwa, tuna ofisi moja ya *TANESCO* watumishi ni walewale wachache, hawajitoshelezi. Namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu mwenye hii sekta atuangalie kwa jicho la huruma, watupatie vitendea kazi, wawaongezee vijana magari ili wakakimbizane na hizo kata 43 katikati ya kukatikatika kwa umeme wakatuhudumie kwa ufasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera Wilaya ya Muleba tunavyo visiwa 39. Ndugu yangu Mheshimiwa kutoka Ukerewe amechangia asubuhi hapa, anaongelea tunawafikia vipi wananchi ambao wanaishi kwenye visiwa? Kwa Wilaya ya Muleba kwa vile visiwa 39 tuna kata tano ziko katikati ya Ziwa Victoria, watu hawa wamekuwa kwenye giza kwa kipindi kirefu, Serikali ilitupatia huduma ya Juameme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulitaarifu Bunge lako kuwa Juameme wamezidiwa na kazi, hawawezi kutosheleza mahitaji ya hizi kata tano. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu atuisaidie kwenye hizi kata tano ili nao wapate umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusikia kwamba Serikali ilikuja na pendekezo la kuhakikisha kwamba na hawa ambao wako *off grid* tunawapatia mwarobaini katika kuhakikisha kwamba nao wanapata umeme wa uhakika. Kwetu Muleba biashara yetu, siasa zetu ni uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wanahitaji zaidi umeme hata kuliko walioko nchi kavu, kwa sababu kazi yao kubwa ni uvuvi. Kwa hiyo, wangependa kupata umeme, wakawa

na mafriji, wakahifadhi mazao ya uvuvi wao, hasa dagaa na samaki, wangeweza kutengeneza uchumi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema kata tano ninaziongelea Kata za Ikuza, Mazinga, Bumbire, Kerebe na Kata ya Goziba ambazo ziko Wilaya ya kule Jimbo la Muleba Kusini na Jimbo la Muleba Kaskazini. Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hotuba yake atupe matumaini. Wamefanya kazi nzuri, wanatuhudumia vizuri, lakini na kwenye hili, tutafute njia mbadala wa kuwasaidia hawa wananchi na wapiga kura wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa kazi kubwa ambayo imefanyika nchi nzima. Muleba tuna vijiji 166, vijiji 162 vimepata umeme ambayo ni 97.6%. Kwetu walimu unapoongelea 97.6% ni *grade A,* tena ya nguvu. Kwa hiyo, tunawapongeza sana kwa kazi kubwa ambayo wameifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, bado tuna vijiji vinne ambavyo havijafikiwa na huduma ya umeme. Najua kuwa juhudi kubwa inaendelea, lakini namwomba, kabla hatujamaliza hili Bunge, atupe neno ili na vile vijiji vya Bulungura na Bihanga ambavyo kila nikienda kilio chao ni kwamba watapata lini nishati ya umeme? Nimeongea na Mkurugenzi Mkuu wa *REA*, amenipatia matumaini, lakini naomba nipate matumaini makubwa zaidi kupitia hitimisho la hoja yake Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vitongoji; nashukuru, tuna vitongoji 752; vitongoji 387 sawa na 54.5% vinapata umeme. Bado tuna kazi kwenye vitongoji. Sasa hivi tunavyoongea, zamani umeme ulikuwa ni kama anasa. Sasa hivi umeme ni hitaji la lazima kwa kila mmoja. Kila mmoja anataka umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua, kulingana na uwezo wa Serikali yetu, hatuwezi kuwafikia watu wote kwa wakati mmoja. Tungeomba, na hiyo ndiyo ingekuwa sala yetu kwa kila mmoja, kwamba iwezekane tupate umeme wa kutosha angalau miaka 10 ijayo kila mmoja apate umeme kulingana na mahitaji yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Kamati, imeongelea ujenzi wa vituo vya mafuta hasa barabara kuu na kwenye miji. Kuna kipindi nilisoma mahali fulani sikumbuki ni wapi, wanasema kitaalamu kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine cha mafuta inapaswa iwe kilomita saba kwa sababu za kiusalama. Sasa sijui sisi tunatumia *standard* ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili naomba tuliangalie kwa macho mapana, ikitokea ajali ya moto tunaweza kuwa katika matatizo makubwa sana kutokana na ukaribu wa vituo vya mafuta hasa barabarani na mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo lingine, vituo hivi sasa vinajengwa hata kwenye makazi ya watu, kwenye misongamano ya watu, makazi vijijini watu wanawekeza kwenye vituo vya mafuta. Najua *EWURA* wapo wanafanya kazi nzuri, lakini na hili naomba walitupie macho waweze kulisaidia Taifa letu kwa sababu za kiusalama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wachangiaji wengi wameongelea suala la matumizi ya gesi kwa vyombo vyetu vya moto. Nadhani hii ndiyo suluhu ya kupunguza matumizi ya pesa yetu kwenda nje. Kama Mungu ametujalia gesi yetu, tusichelewe na wala tusisite, na kama ningeshauri tungewaongezea hawa Wizara pesa kuhakikisha kwamba tunajenga vituo vingi vya gesi kuhudumia magari yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na hapa niendelee kushauri, na miaka yote tumeshauri na tutaendelea kushauri na Serikali ianze kutumia gesi kwenye magari yake tupunguze matumizi ya dola yetu kuagiza petroli kutoka nje, tuoneshe kwa mfano na wengine wote watafuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho tunaagiza mitungi ya gesi kutoka nje, sijaona mtungi ambao unazalishwa hapa nchini. Tunayo gesi yetu, lakini bado tunatumia dola kuagiza mitungi ya gesi. Nilikuwa naangalia kwenye soko tumewajengea *appetite* wananchi wetu hata ukienda vijijini sasa hivi sisi tunaotoka majimbo ya vijijini; uende Muleba, Nsambo, Chuchoro,

Byengeregere kule ndani kabisa akina mama wanatumia gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kutengeneza hii *appetite* ya wananchi wetu, naishauri Serikali tuwatafute wawekezaji wa kuwekeza hapa nchini, tutengeneze mitungi yetu ya gesi tuweze kuwauzia hawa wananchi ambao tumewatengenezea *appetite* ya kutumia gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga hoja mkono kwa 100% nakwenda mpaka 250% ila naomba vijiji vyangu viwili Bihanga na Burungura tukaviwashe, wananchi wakashangilie, wakapige vigelegele kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tumeshamaliza kazi huko, tunahitaji mwanga wa kuja kuhesabu na kulinda kura zetu na kulinda kura za Mama. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma ajiandae.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami kuwa mchangiaji wa siku ya leo katika Wizara hii muhimu. Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kuniwezesha nami leo kwenda kusimama katika Bunge hili ambalo linakwenda ukingoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, napenda nikishukuru na kukipongeza Chama changu cha Mapinduzi kwa kunilea vyema na kuniongoza vyema kwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum toka Mkoa wa Dar es Salaam kwa vipindi vitatu mfululizo. Siyo suala dogo, ni suala kubwa; UWT niwapongeze sana, wamenibeba, wamenilea vizuri Mwenyezi Mungu awabariki wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa niende kwenye Wizara. Wizara yetu ya Nishati kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi

kubwa aliyoifanya ya kuhakikisha anakuwa kinara wa nishati safi ya kupikia kwa akina mama wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu ametuamsha akina mama. Ajenda ya Mama Mkoa wa Dar es Salaam tumeipokea. Leo hii ukienda katika Mkoa wa Dar es Salaam matumizi ya nishati ya gesi ya kupikia ni makubwa sana kuliko matumizi ya mkaa. Ni jambo kubwa ambalo Dar es Salaam ilikuwa ni kinara wa matumizi wa mkaa, sasa hivi ukienda kila kona Dar es Salaam utakuta wanauza mitugi ya gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, tuna matumizi pia ya umeme, tumepata elimu na tumetoa elimu ya kutosha kwa akina mama waone umuhimu sasa wa kutumia nishati ya umeme katika kupikia, ni nishati ambayo ina gharama nafuu kuliko hata ya gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na ninamwombea Dua Mwenyezi Mungu amwezeshe, ampe afya njema aweze kwenda kupambana 2025 na ninahakikisha katika Mkoa wa Dar es Salaam Mheshimiwa Rais ana kura zote za kishindo zitajaa mpaka nyingine zitamwagika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, pia napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Waziri wa Nishati pamoja na Mheshimiwa Naibu wake Waziri na Makatibu Wakuu wote wa Wizara hiyo pamoja na watendaji wote wa taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo. Hongereni sana kwa kufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiyopingika, miaka ya nyuma tunapoizungumzia Wizara ya Nishati kulikuwa na hekaheka ambayo haieleweki. Tulikuwa na michango mikubwa mikubwa, tunaitamani lini itakuja Wizara ya Nishati tuje kuongea. Leo hii maongezi hayapo, wala kelele hazipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini kelele hazipo? Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kujenga au

kukamilisha ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. *Project* ile ilikuwa ni kubwa mno haijawahi kutokea, lakini leo hii bwawa lile limekamilika kwa karibu 100%, siyo jambo dogo kwa nchi yetu, ni jambo kubwa sana, tunapaswa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kishindo kwa kazi kubwa aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usioaminika na hakuna aliyeamini kwamba ipo siku lile bwawa litakuja kukamilika, lakini pia hakuna aliyeamini kwamba Tanzania hii ipo siku tutapata treni inayoendeshwa na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu tuna-*enjoy* sasa na *SGR* inayoendeshwa na umeme, watu walikuwa hawadhani kwa sababu walikuwa wanaona umeme wenyewe wa majumbani na viwandani haututoshi, je, hiyo treni itaendaje? Leo hii kuchwa, kutwa watu wanarukia treni saa saba, saa sita kila mmoja anapanga muda wa kuondoka na treni. Ni usafiri rahisi, usafiri salama ni usafiri mzuri mno.

Mheshimiwa Mwenyeiti, hongera sana kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pia na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu pamoja na watendaji wake wote, wamefanya kazi nzuri katika sekta ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nimeona kuna miradi kadha wa kadha ambayo ilikuwa inaendelea pamoja na Bwawa la Mwalimu Nyerere. Pia amefanya maboresho ya miundombinu ya gesi za kwenye magari, ongezeko la vituo vya uuzaji gesi kwenye magari, maendeleo ya usambazaji wa gesi za majumbani, utulivu wa biashara ya mafuta nchini, kuimarika kwa hali ya umeme nchini, na kuimarika kwa umeme vijijini. Hayo yote amefanya na Serikali yetu hii, na yamefanyika vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua panapo mazuri hapakosi changamoto. Changamoto ni kitu cha kawaida, hata mwanadamu unapoishi wewe mwenyewe ndani kwako kuna changamoto. Katika changamoto hizo, sasa nitajikita katika mchango wangu kwa Mkoa wangu wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maboresho ya umeme, kweli kabisa katika Mkoa wa Dar es Salaam bado kuna maeneo yana changamoto ya umeme ikiwepo maeneo ya Kigamboni, Temeke, Mbagala, Buza, Kilakala, Vituka, na maeneo mengine mengi tu katika Wilaya ya Temeke na wilaya nyingine huko mara nyingi bado kunakuwa na changamoto za umeme kukatikakatika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa, tunaona jinsi Serikali inavyoendelea kubadilisha nguzo za umeme kutoka kwenye miti inayooza kwenda kwenye zege, hilo lilikuwa ni changamoto kubwa, zile nguzo kuoza ovyo ovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya Dar es Salaam kutokana na mabadiliko ya tabianchi kumekuwa na mvua nyingi zikinyesha, lakini maji kujaa, hivyo nguzo zile zilikuwa zinakatika na zinasababisha tusipate umeme kwa masaa kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali na ninaona haja kabisa ya kuiambia Serikali sasa tutoke kabisa katika Mkoa wa Dar es Salaam kutengeneza nguzo za miti, tuelekee kwenye nguzo za zege ili kuondoa changamoto ya umeme kukatika katika kutokana na miundombinu iliyochakaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuchangia, lakini pia nataka ni-*declare interest* kwamba mimi ni mdau katika sekta ya biashara ya mafuta. Biashara ya mafuta imeimarika katika nchi yetu, niwapongeze sana *EWURA* wanafanya kazi nzuri, wameweka vigezo mbalimbali wafanyabiashara wanavipitia hivyo vigezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo changamoto tunaomba *EWURA* wakakae pamoja na wadau wengine wote wa mafuta wafanye tafiti, hali ya vituo vya mafuta vinaongezeka kwa kasi hali ambayo inasababisha vijana wa Kitanzania waliojikita katika sekta hiyo kuondoka na madeni makubwa, kushindwa kufanya biashara kudaiwa madeni makubwa benki na hatimaye na wengine kufilisiwa. Sasa naiomba Serikali waiangalie tena upya biashara hii, kwani ina changamoto zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa EWURA wanaweka vigezo, watu wanavifikia. Ndugu zangu nami nitakuwa kidogo tofauti kwa sababu yawezekana natambua hilo jinsi vigezo vinavyowekwa kwa *EWURA* na tunamwomba Mwenyezi Mungu atujalie hivyo, hatujawahi kupata *shortage* yoyote katika mlipuko au nini kwenye hivyo kulingana na vigezo wanavyoviweka *EWURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto inakuja, huwezi ukajenga vituo vyote porini, magari yapo *Oyster Bay,* yapo Masaki, Mwenge, Temeke, Mbagala na kadhalika. Sasa utachukua vituo vyote utaenda kuviweka porini, hawa huku mjini watapata huduma wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha msingi, vigezo na masharti lazima vizingatiwe ili kuwe na usalama, lakini pia kama na wao wanaliona pia hili la kujaza wafanyabiashara, wanadhani kwamba wanakwenda kuzungusha pesa na kupata pesa, lakini kuna vijana ambao waliingia kwenye hiyo sekta sasa hivi taabani hawajiwezi tena, alikuwa anauza kwa siku lita 5,000, lakini leo hii anauza kwa siku lita 500, anashindwa kurudisha mikopo ya benki, anashindwa kulipa mapato ya *TRA*, anashindwa kufanya kitu chochote, matokeo yake wanaishia vijana kuuza makampuni na kutokomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunawawezesha vijana waliopo katika sekta mbalimbali, lakini tunavyokuta kijana amejipambanua, amehangaika, amepata mtaji, lakini anakuja kupotea hivi hivi, hilo litatusikitisha. Naiomba Serikali waangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia ujenzi wa miundombinu ya gesi za majumbani, naipongeza Serikali, wamefanya jitihada kubwa ya kujenga miundombinu ya gesi, naona Mikocheni wamejenga, inaelekea sasa Mbezi, Mbezi *Beach* na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba tufanye *win win* tuhakikishe tunafanya kidogo kwenye eneo la Mikocheni,

tunahama tunaenda kwenye Wilaya ya Ilala, tunawafanyia nao kidogo, tunahama, tunaenda Wilaya ya Temeke, nao waonje ile keki kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema tung'ang'anie eneo la Mikocheni, watu wa Dar es Salaam, akina mama wa Dar es Salaam wanasubiri gesi hiyo yenye gharama nafuu, wanaita gesi ya kupimiwa, nami wananiambia kila siku Mheshimiwa Mbunge wetu hakikisha tunaletewa gesi ya gharama nafuu, gesi ya kupimia ili tuweze kuitumia. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umeisha?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo malizia.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nakishukuru sana Chama cha Mapinduzi kwa kuisimamia Ilani yake katika kipindi hiki cha mwaka 2025. Hakika Ilani ya Chama cha Mapinduzi imefikiwa kwa zaidi ya 95%. Hilo ni jambo la kupongeza chama chetu, na Serikali yetu imefanya vizuri hata sisi wengine tutakwenda kifua mbele na tunahakikisha tutarudi kifua mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi. Nilimtaja Mheshimiwa Eng. Samweli Xaday Hhayuma, Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai ajiandae.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia jioni ya leo na mchango wangu nianze kwa kuleta shukrani za Wanahanang kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo imefanyika kwenye sekta ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani hizi zikimfikia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, moja kwa moja ziende kwa Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Judith Kapinga na wataalamu wote wa Wizara ya Nishati, kwani kwa kipindi kifupi Wilaya ya Hanang imepata umeme kwenye vijiji 46, tumepata umeme kwenye vitongoji 49 na pia tunaendelea na mchakato wa vitongoji 15 na Mheshimiwa Waziri nimemwona, amenieleza kwamba tutapata pia kwenye vitongoji 81. Kwa jumla, tutapata vitongoji 305 kuunganishiwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *TANESCO* wameendelea kupeleka umeme kwa wananchi, kwenye maeneo ambayo yalikuwa yamepata umeme kabla na hii niliiomba kwenye bajeti ya mwaka 2023/2024 mahususi eneo la Kateshi ambalo lilipata umeme muda mrefu, eneo la Giting, Nangwa, Miaskoni, Jorodom, Ganana, Gendabi maeneo haya umeme umeongezwa kwa maana ya kujazilisha yale maeneo ambayo yalipata umeme siku nyingi. Nashukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Hanang. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine napongeza kazi kubwa inayofanywa na Wizara, pia kwa uwekezaji ambao Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameruhusu fedha nyingi ziende kwenye sekta ya nishati hasa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizi ukiangalia taarifa tuliyonayo au taarifa tuliyopewa hapa Bungeni Machi, 2024 uwezo wetu wa kuzalisha mitambo yote ilikuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 2,138 lakini taarifa ya Februari mwaka huu tulikuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 3,796.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Waziri ametoa Taarifa hapa Bungeni kwamba uwezo wetu wa uzalishaji umepanda mpaka kufikia megawati 4,031.71. Hii ni hatua kubwa sana kwenye uzalishaji wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana kazi kubwa inayofanyika. Pamoja na pongezi hizi, nafahamu tunao umeme mwingi na chenji sasa hivi tunayo kwenye uzalishaji. Umeme huu unatakiwa uwafikie wananchi, na ili uwafikie wananchi, lazima tuendelee kuwekeza kwenye usafirishaji wa umeme, kwenye usambazaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu umeme huu tukipeleka kwenye vitongoji, pamoja na kwamba tumesogea sana, tukipeleka kwenye viwanda, migodi, huduma nyingine za jamii ndani ya muda mfupi utakuwa mdogo. Kwa hiyo, tuendelee kuwekeza kwenye uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yangu ya Hanang pamoja na kwamba tumeshafika vitongoji 305, bado vitongoji 101. Pia kwa sasa Wilaya ya Hanang nafikiri kama siyo namba moja kwa kukatika kwa umeme Tanzania labda itakuwa namba mbili. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati nimeomba mara nyingi kujengewa kituo cha kupooza umeme, pale Wilaya ya Hanang ili kuondoa adha ya umeme kukatika mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliahidiwa kujengewa kwenye mwaka wa fedha 2022/2023 mpaka sasa Wanahanang wanasubiri adha ya umeme ni kubwa. Jumamosi hii nilikuwa wilayani kwenye Kata za Magharibi, siku tatu hawakuwa na umeme kwa sababu kulikuwa na hitilafu. Changamoto kubwa tuliyonayo, *line* ndefu sana, ukiwa na kituo cha kupooza umeme, pakiwa na hitilafu sehemu moja, sehemu nyingine zinaendelea kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni hitaji la wananchi wa Hanang. Tunaomba mtusaidie, tukipata umeme wa uhakika ambao haukatikikatiki Hanang tutawekeza kwenye ujenzi wa kiwanda cha simenti, tutawekeza kwenye kiwanda cha kuchakata chumvi kwa sababu tuna akiba ya chumvi pale Ziwa Gendabi, tutawekeza kwenye viwanda vya kuchakata mazao, na baada ya hapo tutatengeza ajira kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama na Watanzania wa Hanang watapata ajira ya uhakika, na hili ni hitaji namba moja, hitaji kubwa la wananchi wa Hanang. Ninachoomba, kwenye bajeti hii ya mwaka 2025/2026 shilingi bilioni 250, sehemu yake iende Hangang ikajenge kituo cha kupooza umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Meneja wangu wa Wilaya anafanya kazi nzuri sana na timu yake, lakini wanayo changamoto ya usafiri. Nimeshaongea na Katibu Mkuu, aliniahidi, naomba gari iende angalau tuwasaidie wale vijana wafanye kazi yao vizuri kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kuchangia ni eneo la nishati safi ya kupikia ambapo Mheshimiwa Dkt. Kikoyo pia amechangia. Kwa sasa hamasa kubwa tunayoifanya ni kuhakikisha ile mitungi ya gesi tunawafikishia wanachi wengi. Gesi tunayopeleka ni *LPG* ambayo haipatikani hapa nchini, bali tunaiagiza kutoka nje ya nchi. Hamasa inayofanyika ni nzuri sana ya kuhakikisha tunatumia nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba kwenye eneo hili, tutafute namna ya kutumia teknolojia zinazopatikana nchini. Kwa mfano, hayo majiko banifu tunayoyasema au tutafute majiko ambayo yanatumia umeme kidogo, umeme ambao tunazalisha kwa rasilimali ambayo iko hapa nchini kama vile maji, gesi, upepo, na jua, itasaidia nchi yetu kujitegemea na kuepuka kupeleka fedha nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuangalie teknolojia kama *biogas* ili angalau sasa nishati safi tutakayoipata iwe inapatikana hapa nchini badala ya kuwa wategemezi kuagiza sehemu kubwa ya nishati kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitamani niliongelee ni eneo la makaa ya mawe. Imekuwa ni wimbo wa muda mrefu, yale makaa ya mawe hatujayatumia kuzalisha umeme. Ombi langu kwenye eneo hili, kwa kuwa ule mgodi wa makaa ya mawe uko chini ya *STAMICO* ambayo ipo Wizara ya

Madini, lakini anayehitaji umeme ili tuzalishe kwa kutumia makaa ya mawe ni *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni Wizara mbili tofauti. Yawezekana kuna ukinzani kwa sababu ya utendaji kazi ndani ya Serikali. Kwa makusudi kabisa Serikali iamue namna ambavyo tunaweza kutumia yale makaa ili hatimaye tuweze kupata manufaa kwayo kwa sababu baada ya muda, dunia inakoenda ni nishati safi, yale makaa ya mawe yanaweza yasitumike na tutakuwa tumepoteza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni mradi wa muda mrefu ambao tumeuongelea wa gesi asilia kwa maana ya kuisindika ili iwe *LNG*. Mradi huu tumeusema miaka mingi na ninaamini kwamba tungeanza kutekeleza, ungetusaidia kwa kiasi kikubwa kwenye eneo la nishati kwa sababu sehemu kubwa ya magari yetu yote yanatumia mafuta ambayo tunaagiza nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tumeanza kidogo kwenye *CNG*. Tukianza kuwekeza kwenye *LNG* tunaweza kusafirisha gesi ambayo tunayo kwa urahisi ikawafikia wananchi wakapikia, tukayatumia kwenye magari na hatimaye tukapunguza utegemezi wa nishati nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka niseme, ukienda kwenye suala la kuwapelekea wananchi wetu umeme, Kamati ambayo na mimi ni mjumbe, tumelisema kwa sauti kubwa. Chini ya mita 30 wananchi wanaunganishiwa kwa shilingi 27,000, ambapo bei hii imepangwa na *EWURA*. Ikifika mita 70 wananchi wanaungiwa kwa shilingi 515,617 na chenji, lakini ikifika mita 120 inakaribia shilingi 700,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hao wanaopelekewa ni hao hao maskini wa Tanzania. Hizi gharama ni kubwa, *TANESCO* na Wizara waangalie namna bora ya kupunguza gharama kwa sababu ni kweli miundombinu ile ikiwekwa ni mali ya *TANESCO,* siyo mali ya mwananchi anayepelekewa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uwekezaji ule ni mali yao, waone namna ambavyo wanaweza waka-*recover* taratibu kutoka kwa wananchi wanaounga umeme ili hatimaye wananchi wapate umeme wa uhakika kwa gharama nafuu baada ya kuwaunganishia. Inawezekana tuka-*recover* zile fedha kwa kupitia *bills* za umeme ambazo wananchi wanalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Eng.* Samweli Xaday Hhayuma. Nilimtaja Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam ajiandae.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Nishati. Nitangulize kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunilinda niweze kuwa hai na kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiwafanyia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nampongeza kwa kupitishwa na Mkutano Mkuu wa CCM Taifa kuwa mgombea wa Urais kupitia Chama chetu cha Mapinduzi. Pia, nampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi kwa kupitishwa kuwa mgombea mwenza wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati pamoja na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi pamoja na watendaji wote wa taasisi zilizopo chini ya Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba naunga mkono hoja kabla ya kuchangia ili baadaye kule mbele nisije nikasahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu pamoja na Naibu Waziri wake, mmekuwa mkifikika. Kiuhalisia mmekuwa ni watu ambao mnatupokea kama Wabunge na kutusikiliza na kutatua changamoto zilizopo ndani ya wilaya zetu na majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, amepokea Wizara hii ikiwa na changamoto. Nakumbuka wakati anateuliwa na Mheshimiwa Rais, tulikuwa na tatizo la mgao wa umeme, na kwa wakati huo alikuwa kwenye *cross road* kwamba nichague njia ipi? Hata hivyo, kwa kuwa yeye ni kiongozi mtulivu, ameweza kutuvusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angepokea kiongozi mwingine ambaye hafikirii vizuri, angetupeleka kwenye kununua ma-*generator* au kukodisha, lakini kwa kuwa yeye ni kiongozi aliyetulia, ametusaidia, tumeenda kama nchi na sasa tumetoka kwenye mgao wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu anapokea Wizara, tulikuwa na tatizo hilo la mgao wa umeme, lakini kwa sasa hivi tunapozungumza kutokana na mikakati iliyowekwa na Wizara, kwa sasa tuna utoshelevu mzuri wa umeme ambao umefika 100%. Hiyo, ni hatua kubwa sana na kwa kukamilika kwa Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ni mapinduzi makubwa sana kwenye sekta hii ya nishati. Kwa hiyo, nawapongeza sana kama Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwa Wilaya yangu ya Ngorongoro na Jimbo la Ngorongoro kwa ujumla, wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani mwaka 2021, Wilaya ya Ngorongoro kulikuwa na umeme kwenye kata tatu tu na vijiji vitatu, lakini leo tunapozungumza, umeme kwenye Wilaya ya Ngorongoro kwenye Tarafa ya Sale na

Loliondo, umeme umefika kwenye kata zote 17 pamoja na vijiji 40. Kwa hiyo, ni hatua kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Wizara hii, wamefanya kazi kubwa, nami kama Mbunge, nimekuwa nikiwafikia, na kweli wamekuwa wakinisikiliza na kufanyia kazi yale ambayo wananchi wetu wanahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, tuna umeme kwenye vitongoji nane. *Densification;* vile vitongoji kwa ajili ya *densification* au ujazilizi, kwenye maeneo hayo yote ambayo umeme ulifika kipindi cha nyuma, vile vitongoji ambavyo vimeachwa, vitongoji 12 navyo vimepata umeme. Pia, tuna vitongoji vingine 12 ambavyo umeme umefika katika yale maeneo ya migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ngorongoro pia ina migodi mbalimbali. Kwa kipindi cha nyuma hatukuwa na umeme, lakini kwa sasa hivi umeme umefika na wananchi wale ambao wanajishughulisha na shughuli za uchimbaji wananufaika na umeme na uzashaji wao umeongezeka mara dufu. Kwa hiyo, nawapongeza pia kwa hilo kwa sababu ni kazi kubwa iliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, pia tuna umeme kwenye vile vitongoji 15. Kwa Wilaya yangu, vile vitongoji 15 vya jimbo tayari vitongoji 13 vimewekwa nguzo, vimebaki vitongoji viwili tu. Kwa hiyo, tuna uhakika mpaka mwisho wa bajeti hii ya mwaka 2024/2025, nafikiri vitongoji vile umeme utakuwa umewashwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika vijiji vyote 40 ambavyo kuna umeme bado kuna vijiji vitatu ambavyo umeme haujawashwa; Kijiji cha Naan, Kijiji cha Piyaya na Olalaa. Hata hivyo, nina uhakika baada ya muda mfupi umeme pia utawashwa katika yale maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo nataka kusema, kwa Wilaya yangu ya Ngorongoro, kuna maeneo kwa mfano,

tuna vijiji 65, lakini vijiji ambavyo vina umeme ni 40. Kwa hiyo, vijiji 25 havina umeme. Ninaamini kwamba Wizara itaangalia namna na wao wapate umeme hata kama ni umeme wa jua waweze kupata kwenye hivyo vijiji 25 ambavyo bado havina umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nilihitaji kuliongelea ni kwamba kwenye Wilaya ya Ngorongoro, umeme umekuwa ukikatika sana. Hili ni tatizo ambalo wananchi wanaona kama vile umeme kwao siyo manufaa, kwa sababu umeme unatoka Longido, tunachukulia *line* ya Longido unasafiri kilometa nyingi mpaka ufike kwenye Wilaya ya Ngorongoro. Kwa hiyo, kwa siku moja umeme unaweza ukakatika zaidi ya mara 10 na wakati mwingine unaweza ukakatika saa nne usiku na kurudi labda kesho saa nne. Kwa hiyo, wananchi wamekuwa wakipoteza mali zao, umeme unaporudi na kukata ghafla tunajua madhara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Wizara itusaidie jambo moja la kuhakikisha kwamba, kwenye hii bajeti tunaenda kujenga *substation* Wilaya ya Ngorongoro ambayo itatusaidia kuondoa tatizo la umeme. Najua sasa hivi Serikali ina mpango wa kujenga *substation* hapo Makuyuni na kuendelea mpaka kule Engaruka, lakini huo ni mkakati wa muda mfupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa muda mrefu kwa ajili ya Wilaya ya Ngorongoro na wananchi waweze kunufaika na umeme, ni lazima tuwe na *substation* ya kule kwetu ya *KV 132* kama walivyofanya wataalamu wetu. Wataalamu wetu wanafanya kazi kubwa sana. Ngazi ya mkoa na ngazi ya wilaya wanafanya kazi kubwa kila wakati, pamoja na mazingira magumu yaliyopo ndani ya Wilaya ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ukikatika leo uko katikati Mundarara, wataalamu wale wanatoka Ngorongoro zaidi ya saa nne kwenda kuangalia tatizo na wale wa Longido waliopo kule. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara tuangaalie namna kama tunaweza kujenga hiyo *substation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, tumepata mitungi ya gesi. Mheshimiwa Naibu Waziri, nafikiri kuna siku nilikwambia hili,

kwamba kwa Wilaya ya Ngorongoro unapeleka gesi kule Loliondo ambapo kutoka Tarafa ya Ngorongoro ni kilometa 400 na kule ndiyo makao makuu; naomba, kwa kuwa kazi hii inafanyika kwa Watanzania wote, basi wataalamu pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, kwa sisi ambao tuna mazingira magumu na jiografia yetu kwa ajili ya upatikanaji wa hizo gesi, tungegawa kwa zile tarafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarafa ya Ngorongoro, Sale na Loliondo kuwepo na wale wasambazaji, kwa sababu haiwezekani unapitisha mitungi kwenda mpaka Waso, mwananchi aliyepo Engaresero atoke aende Waso akafuate mitungi na kurudi tena zaidi ya kilometa 70. Kwa hiyo, tuweke mikakati ambayo itawasaidia wananchi kupata hiyo mitungi kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na niwapongeze sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai. Nilimtaja Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie katika Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini na Kamati hii inasimamia Wizara mbili; Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini. Kule Wizara hii inafanya kazi kubwa sana katika maeneo mengi ya huduma za kijamii. Hata hivyo, pamoja na kazi hii, kazi hizi zinafanywa na binadamu na hawa binadamu wanaofanya hii kazi ni watu ambao miongoni mwao ni sisi tukiwemo Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa sana aliyoifanya katika Sekta hii. Kwanza kufanya maboresho ya watendaji katika Sekta hii, lakini pia na kubadilisha mawaziri, hili ni jambo kubwa sana. Mheshimiwa Rais,

anaona ni wapi pamepungua, anafanya mabadiliko na hayo mabadiliko yanafanyika kwa ajili ya kupata tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba binadamu katika hulka yake huwa anapenda akifanya jambo zuri asifiwe, siyo anafanya jambo zuri anapingwa. Hili jambo linakuwa siyo sawa. Sisi kama Tanzania ni kwamba tutapita katika hatua ngumu sana ili kwenda kujiondoa katika haya matatizo mnayoyaona ya umeme, matatizo ya matumizi ya gesi na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Rais katika uteuzi wake katika hizi nafasi. Amemteua Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko na akampa nafasi nyingine ya kuwa Naibu Waziri Mkuu. Siyo kwamba kampa nafasi hiyo kwa bahati mbaya, ni kwamba ameangalia yeye mwenyewe akaona kabisa kwamba ana uwezo wa kufanya kazi hii kwa ufasaha na Wizara hii inafanya kazi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naongea na kiti, lakini pia naongea na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. Sasa yupo pale Mheshimiwa Mbunge anamnyima nafasi ya kunisikiliza, sasa linakuwa siyo jambo jema sana, naomba unilinde. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Wizara watendaji wake wanafanya kazi usiku na mchana. Watanzania wanatakiwa wajue umeme ukiwa unakatika, kuna tatizo la kiufundi au kuna tatizo gani? Kwa hiyo, hivi ni vitu ambavyo Watanzania wanatakiwa waelezwe na baadaye wataelewa, lakini hitaji la umeme pia kwa Tanzania ni kubwa mno kwa sababu imeingia kuwa sehemu ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watendaji wanafanya kazi. Sisi tunafanya kazi kama Kamati, tunapita maeneo mengi sana kuona tatizo ni nini, na tunakwenda tunaoneshwa hatua kwa hatua. Miongoni mwa watu ambao walikuwa wabishi katika jambo hili ni pamoja na mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwenda mpaka *underground* palipo mitambo ya kuzalisha umeme, nimetembea maeneo yote yanayofua umeme katika nchi hii, na tumekwenda kule kuona kama kuna hujuma ya aina yoyote. Hakuna hujuma hata moja isipokuwa kama nchi tumelemewa na tunahitaji kazi ya nguvu kubwa sana kuwekeza katika miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya umeme katika nchi hii, kwa siku, watu wanaoomba umeme tu ni karibu *Megawatts* moja kwa siku nchi nzima. Maombi peke yake ya mahitaji ya umeme, ni zaidi ya *Megawatts 30*. Sasa kama mahitaji ya umeme ni *Megawatts 30,* mahitaji mapya ya wananchi ambao wametengeneza viwanda huko migodini na sehemu zote, tunahitaji kuwekeza sana katika suala la umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wabunge, tunatakiwa tuishauri sana Serikali kwenye eneo hili, hatuna jinsi. Leo hata hili Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo tulikuwa tunasifia kwamba tumepata bwawa tutapunguza mahitaji ya umeme ndivyo yanavyoongezeka. Ni sawasawa na walivyokuwa wanapata hofu wawekezaji wa mabasi waliyokuwa Dodoma kwamba baada ya Treni ya Mwendokasi kuanza kazi, mabasi yao yatakosa abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, treni mpaka sasa hivi inajaa halafu na mabasi yanajaa na ma-*traffic* wako barabarani wanakamata mabasi ya akina Shabiby yamejaza watu na yanakwenda kasi. Siyo suala la kuchezea, yaani kila mnavyoongeza na mahitaji ya watu na yenyewe kuhitaji umeme ndiyo yanaongezeka kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika jambo hili la miundombinu ya umeme, mimi leo hapa nataka kushauri tu. Ni kwamba, kwa sababu tunayo makaa ya mawe na uzalishaji wa makaa ya mawe ni mkubwa, hatuna jinsi, ni lazima tuhakikishe tunatafuta wadau wa kuja kuongeza nguvu katika Sekta hii ya Umeme. Tusipozalisha kwa mahitaji ya umeme ambayo sisi tumeyapitia kama Kamati, tumegundua mahitaji ya umeme ni makubwa sana katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko Lijualikali kuna maeneo mengi, Mto Malagarasi na kwingineko na haya maeneo yote kama vile umeme wa joto ardhi, wote unahitajika umeme wa gharama. Lazima tuwekeze kwa gharama kubwa sana katika umeme, kwani baada ya miaka 10 ijayo, hali ya mahitaji ya umeme na huu uwekezaji unaowekwa wa viwanda, hali itakuwa ngumu kuliko sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imepata matatizo juzi kwa kufiwa na Mtendaji wa TANESCO. Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema Peponi. Eng. Nyamhanga ni miongoni mwa wazalendo, miongoni mwa watu walioumia japo familia yake itakuwa imepoteza zaidi, Wizara itakuwa imepoteza zaidi, na mimi nimeumia kwa sababu tumefiwa na mzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule bwana alikuwa, ukikatika umeme, kama mko naye, yaani anashika kifua, anaona tayari balaa kubwa limeingia. Sasa mtu wa namna hiyo na alivyokuwa anafanya kazi, amekufa. Alikuwa anatoka kufanya kazi; alikuwa Dodoma ametokea Sengerema; tulikuwa naye kule Sengerema, amekwenda kuangalia maeneo ya kwenda kuweka *substation* kule Sengerema, namna ya kuhakikisha umeme mwingine unaotokea Ibadakuli, umeme mwingine unaotokea Mpomvu Geita unakuja kupozwa Sengerema wasaidie tena kuingiza umeme mwingine Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile kuhakikisha tu kwamba Jiji la Mwanza na wananchi wa Mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa wanapata nafuu ya kukatikiwa umeme, yule bwana anakwenda kupata ajali anakufa, na bado alikuwa anasafiri tena kutoka kwenda nje ya nchi. Ndiyo ujue watu walikuwa wanafanya kazi; usiku kucha anatembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanatakiwa kujua, Mheshimiwa Rais suala la ukatikaji wa umeme linampa maumivu makubwa. Wabunge, Wajumbe tulioko katika Kamati hii tunapata maumivu makubwa, tunafanya kazi. Kwa hiyo, Eatanzania wanatakiwa waunge mkono juhudi inayofanyika katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la gesi, hili suala la gesi nilikuwa namwomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, hebu waitishe semina ya Wabunge wote hata siku mbili waweze kujua aina za gesi tunazozalisha, na aina ya gesi inayoagizwa kutoka nje. Hizi gesi ziko za aina ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naogopa kuchukua nafasi hii mimi tena kuanza kusema hili jambo ni la kwako Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, lakini ninachotaka kukuomba suala la kutoa semina Mbunge mmoja kama Tabasam mimi nina watu zaidi ya 450,000 - 500,000 nikijua hii mifumo ya gesi yote naweza kwenda kuwaambia Watanzania walioko Sengerema bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hali hii, naomba tu unipe dakika moja niweze kusema ni kwamba gesi imesambazwa, Serikali iliagiza gesi na ikatoa ruzuku. Hii gesi imeleta chachu kubwa sana ya watumiaji wa gesi. Naomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu hii mitungi ya gesi iliyoagizwa, basi aje awaambie Watanzania, lini mitungi hii itaingia ili kusudi sasa wananchi ambao wanatusumbua kule katika Majimbo yetu wapate kauli ya Serikali, mitungi hii inaingia lini? Maana mitungi hii ina ruzuku ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani mitungi ni ya ghali na haipatikani hapa. Sisi tumetembea nchi nyingi zinazozalisha mitungi. Serikali ya Tanzania bado na yenyewe ina mipango mikubwa ya kuleta wawekezaji waje wafanye kazi hii ya kuzalisha mitungi na uagizaji wa gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kushauri na wenyewe uagizwe kwa *bulk* ili kupunguza gharama, kwa sababu watu wanavyoleta gesi labda tani 5,000, labda meli dogo tani 5000. Kwa hiyo, bei za gesi zinakuja kuwa kubwa kiasi ambacho watumiaji wa nchi hii wanakuja kuwa na mzigo mkubwa wakati gesi haitakiwi kuzidi shilingi 1,500 hadi 2,000 kwa ajili ya matumizi. Kwa hiyo, mtu akinunua kilo sita anajua atanunua kwa shilingi 12,000 au kwa shilingi 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingine kama India huko gesi inauzwa gharama ndogo sana na gesi hii inatoka Brazil inapita hapa, inatoka Angola inakwenda mpaka Brazil inakwenda mpaka India. Sasa kwa hatua hiyo, tunaiomba Serikali itengeneze miundombinu ya gesi kama hivi wanavyojenga miundombinu ya kuhifadhi mafuta walete na miundombinu ya kuhifadhi gesi ili Watanzania sasa ambao lengo la Mheshimiwa Rais ifikapo mwaka 2034 Watanzania zaidi ya milioni 48 wawe wanatumia gesi kwa 80% ya wananchi, kwa mfumo huu bila kuanza kuandaa miundombinu ya gesi, hatuwezi kufika kwenye takwa la Mheshimiwa Rais na Wabunge ambao ni watetezi wa wanyonge huko kwenye Majimbo yetu tutashindwa kutimiza wajibu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam. Nilimtaja Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, ajiandae.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo kuweza kulihutubia Bunge katika kuchangia Wizara yetu ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natangulia kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwezesha miradi mingi tangu alipoingia madarakani tarehe 19 Machi, 2021. Kwa hakika miradi mingi imetekelezwa katika kila kona ya nchi, mikubwa na midogo kwenye sekta nzima ya nishati ukianzia kwenye umeme wenyewe kwa maana ya bwawa la Mwalimu Nyerere, lakini hata kule kwenye umeme wa *REA*, miradi ya gesi siku hadi siku uwekezaji umekuwa ukiongezeka na tumeanza kupata tija kubwa kwa kupata umeme mwingi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri na uwekezaji mkubwa ambao ameufanya katika sekta hii ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda pia kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, dada yangu, mtani wangu Judith Kapinga kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya tangu alipoingia madarakani katika nafasi hii, kwa kweli ametuonesha utofauti na kule tulikotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi umeimarika, umekuwa na usimamizi makini katika Wizara yake, pia miradi kwa kweli imekuwa ikitoa matunda kwa haraka sana. Hata ile ambayo ilikwama kwa miaka mingi sasa imeanza kutoa matunda na tija kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Mwalimu Nyerere ni kielelezo tosha, lakini kule Kusini tulipata mradi wa kuhamishwa kwa ule mtambo wa umeme wa gesi, *megawatt* 20, Mtwara; pia pale Somanga ukarabati unaendelea wa kituo kile cha kuzalisha umeme *megawatt* 7.5. Kwa kweli mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu mwaka 2024 tulimlalamikia baada ya kuwa tumekumbwa na kadhia ya mafuriko yaliyotokana na mvua za El-Nino na Kimbunga Hidaya ambapo nguzo nyingi ziliondolewa ambazo zilikuwa za miti. Tunashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Waziri Mkuu alilifanyia kazi, tumeona sasa hivi nguzo za zege zimekuwa zikisambazwa na hivyo kuimarisha huduma ya upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maombi au ushauri ufuatao, kwamba, kwenye njia ya umeme wa gridi ya Taifa, kwa sababu tayari Serikali imeanza kushughulikia jambo hili kutokea gridi ya Taifa ambayo inatokea Songea, itapita Tunduru - Masasi kwenda mpaka Mnazi Mmoja na baadaye Lindi na Mtwara, tunaomba ule mradi uboreshwe au utekelezwe kwa kasi zaidi kusiwe na *delay* ili sasa kwa kuwa *transmission line* zinaenda kuboreshwa, tuna uhakika gridi ya Taifa ikifika Lindi na Mtwara, basi huduma ya umeme itapatikana zaidi.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa inatokea wapi? Mheshimiwa Yahya.

**TAARIFA**

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana mchangiaji, anachangia vizuri sana. Kwa suala la gridi ya Taifa naomba niipongeze sana Wizara kwamba ile changamoto ya wananchi wa Jimbo langu kutolipwa fedha za fidia, wameanza kulipa kuanzia jana. Jambo hili nalipongeza sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unaipokea hiyo Taarifa?

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea kwa mikono miwili, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukiwezeshwa zaidi kuboresha ile miundombinu ya zile nguzo za zege kwa sababu hazijafika maeneo yote, zimepita kwenye barabara kuu tu, nina hakika na hii gridi ya Taifa itasaidia sana kupunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya umeme ambayo bado kwa kiasi fulani inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napongeza juhudi ambazo zimefanyika kwenye mradi wa *REA* na tuliongozana wakati fulani na Mkurugenzi Mkuu wa *REA* mwezi Agosti mwaka 2024, tukaweza kwenda kutembelea baadhi ya miradi kule Zinga na maeneo mengine na tukagawa na mitungi ya gesi. Tunaishukuru Wizara kwa kweli kwa kuweza kuwaona wananchi wa Jimbo la Kilwa Kaskazini na Kilwa kwa ujumla, lakini sasa kuna changamoto kwenye vile vinavyoitwa vijiji miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo mimi nimepitapita huko kwenye *Local Government,* sielewi hivi vijiji miji vinapatikana katika sheria na taratibu zipi? Kwa sababu ninavyojua kuna Majiji, Manispaa, Miji na kuna Mamlaka za Miji Midogo. Sasa unakuta kwa mfano, pale Somanga Kaskazini na Somanga Kusini ambako wenzetu wa *TANESCO* wamekuja na *definition* yao, wanasema eti ni vijiji miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiri turudi kwenye *standards* zetu za nchi ambazo zinapatikana kupitia Wizara yetu ya TAMISEMI katika kutambua haya maeneo. Kama bado ni Kijiji kama ilivyo Somanga Kusini na Kaskazini wanapaswa kulipa shilingi 27,000, na hili jambo tumelizungumza tangu mwaka 2023, mwaka 2024, mwaka 2025, Wabunge wengi wamechangia kuhusu jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara iharakishe hili jambo ili kuwapa fursa hii miradi ya *REA* ilete tija zaidi kwa wananchi wetu wa vijijini. Kwa hiyo, nilikuwa naomba pale Somanga Kaskazini, Somanga Kusini na vijiji vingine vya Wilaya ya Kilwa, basi viweze kulipa shilingi 27,000 ili waweze kunufaika na hii miradi ya *REA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la vitongoji 15 katika Jimbo langu vinakwenda kusaidiwa katika ule mradi wa vitongoji 15 kila Jimbo, lakini kuna mradi wa ujazilizo. Kwa jimbo langu kuna vitongoji 14. Kwa hiyo, jumla vitongoji 29 vimelengwa kuboreshewa huduma ya umeme. Sasa ile miradi inakwenda taratibu sana, kuna *delay* kubwa sana katika ile miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Wizara iweze kutekeleza hii miradi kwa *speed* inayotakiwa ili wananchi wetu waweze kupata tija kwa haraka na hatimaye waweze kutumia huu umeme kama fursa kwa ajili kuendeleza uchumi na maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mradi wa *REA* katika jimbo la Kilwa Kaskazini tuliwahi kukaa tukakubaliana na wenzetu wa *REA* na *TANESCO* kwamba, kuutoa umeme kutoka Kandawale kuupeleka katika Kijiji cha Ngarambilihenga ni kilomita 27, wakati kuna Kijiji cha jirani kule Rufiji kinaitwa Ngarambe Matingi ni kilomita saba tu ambako tayari umeme wa *REA* ulishafika.

Mheshimwia Mwenyekiti, kwa hiyo, tulikubaliana na wakatekeleza, kukawa na *balance* ya kilomita 20. Hii kilomita 20 tukakubaliana kwamba basi iende itoe umeme kutoka Kijiji cha

Zinga kwenda katika Kitongoji kinachoitwa Nambunju. Ule umeme umetengenezwa tu kama nguzo 40 halafu hatuoni kinachoendelea, na kwa taarifa tulizonazo, mradi umekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba kwa kuwa mradi sasa umekabidhiwa *TANESCO,* waharakishe hoja hii ili watu wa Zinga, Nambunju waweze kupata umeme haraka na kuweza kuutumia kwa ajili shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa gesi na petroli mara nyingi wenzetu wa *TPDC* wamekuwa wakiongelea zaidi masuala ya gesi, lakini bado wana jukumu la kufanya *exploration* ya petroli vilevile kuendeleza upatikanaji wa hii nishati ya petroli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo letu na Jimbo jirani la Kilwa Kusini kumekuwa na miradi ambayo ilitelekezwa kama miaka 19 hadi 20 iliyopita. Ukienda Kinjumbi pale, ukienda Pande, ukienda Likawage kuna alama pale zimeachwa na watafiti walikuwa wametoka Ujerumani na Canada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali ikumbuke ile miradi, Mungu akijalia pale tunaweza tukapata nishati ya petroli ikasaidia vilevile katika uendelezaji wa Taifa letu kiuchumi, na pia ikazalisha ajira pia kwa wananchi wetu wa maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala la *CSR,* Serikali yetu na hasa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ulipotembelea kwa mara ya kwanza Mikoa ya kusini ulishuhudia namna ambavyo wananchi ambao wanaishi katika maeneo ambayo aidha, kuna uzalishaji wa gesi au kuna mikuzo ya gesi imepita, namna ambavyo bado hawajanufaika sawasawa na fursa hiyo kuwepo katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijaribu kuomba katika Bunge lililopita la Bajeti kwamba pale Somanga ambako kuna uzalishaji wa nishati ya umeme, *megawatt* 7.5 bomba linalotoka Songosongo linapita pale na kuna *plant* pale ya ku-*control valve* zile za gesi, pia lile linalotoka Mtwara na kuna kituo kikubwa pale

cha ku-*control* ile gesi, basi angalau mngetusaidia kuweka umeme angalau mitaani, lakini hilo zoezi bado halijafanyika, ningeomba lifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Kata zangu tatu ambazo bomba la gesi kutoka Mtwara linapita, Kata ya Miteja yenyewe ndiyo bado ina huduma duni sana katika Kituo cha Afya. Akina mama wanahangaika kwenda maeneo ya mbali kufuata huduma ya afya. Kwa kweli watu wanaseka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa kweli atuangalie katika eneo hilo ikiwezekana hata kama ikibidi kwa awamu, anaweza akatuletea shilingi milioni 250 au shilingi milioni 300 tukaanza kujenga kituo cha afya pale Miteja, baadaye kadri siku zinavyosonga mbele fursa ikipatikana zaidi, basi tutaendelea kujenga na hatimaye kuweza kukamilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru; na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na labda nikumbushie tu jambo moja. Mmetuzoesha Wabunge utaratibu wa kutuwekea mabanda pale, tunapata elimu motomoto ya mambo ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunashuhudia kwa vitendo kwenye Majimbo yetu na maeneo tunayotoka, namna ambavyo Wizara yako inatekeleza majukumu yake, lakini mwaka huu naona kimya, sasa sijui kuna tatizo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Francis Kumba Ndulane. Nilimtaja Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki ajiandae.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kwa kupata nafasi jioni hii kuchangia hoja iliyoko Mezani kuhusu Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa watu wa Tunduru. Tunamshukuru sana kwa kutuletea mradi mkubwa wa gridi ya Taifa wenye thamani ya shilingi bilioni 150, tunashukuru sana, sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu una changamoto, uliokuja kwa kasi kubwa sana; wananchi walipisha maeneo yao tunashukuru, lakini ule mradi umesimama kwa muda mrefu, zaidi ya miezi minne na changamoto ya umeme wa Tunduru inatokana na *low voltage* kutokana na umeme wa gridi ya Taifa kuwa na *low voltage*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifika Tunduru sasa, kwa kasi ya usambazaji wa umeme vijijini na umeme unaoletwa Tunduru na kugawana na wenzetu wa Nayumbu mpaka Masasi, unasababisha kukatika katika kwa umeme mara kwa mara. Kwa hiyo. Ombi langu kwa Serikali na kwa Wizara, ni kuweka kipaumbele kabisa cha kuhakikisha kwamba mradi ule unaisha kama ulivyokusudiwa ili adha ya kukatika umeme Tunduru na vijijini hasa vijiji vya Jimbo vya Tunduru Kusini iwe imeisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, adha hii kwa upande wa Jimbo la Tunduru Kusini kuna vijiji vipo mpakani na Mto Ruvuma ambapo upande wa pili ni Msumbiji wanapata umeme kwa masaa nane tu. Inawezekana ukawaka kuanzia saa nane mchana, ikifika saa nne usiku, ukizima ni mpaka asubuhi, umeme haupatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, adha hii shida kubwa ni *low voltage* ambayo inasababishwa na hii gridi ya Taifa ya KV 32 kutokutosheleza kwa niaba ya Jimbo zima la Tunduru Kusini. Katika hili lazima niwashukuru sana wafanyakazi wa *TANESCO* hasa Meneja wa Mkoa wa Ruvuma, Meneja wa Namtumbo, Meneja wa Tunduru Ndugu Mollel, kwa kazi kubwa sana wanayoifanya

kila siku, kuhangaika kila unapokatika umeme kujua tatizo liko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa upande wa Tunduru, wafanyakazi hawa wanastahili tuzo na wanastahili pongezi za hali ya juu kwa sababu wamefanya ile kazi kwa moyo. Mara nyingi umeme wa Tunduru unakatika kuanzia usiku hata mchana zaidi ya mara nne mpaka mara 20 kwa kutwa. Hili jambo kwa kweli wenzetu wa *TANESCO* wanajitahidi kuhangaika kuhakikisha kwamba umeme unapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye umeme wa *REA,* tunashukuru sana tumepata miradi ya umeme jazilizi, tumepata vitongoji 15, lakini ninawashauri watu wa *REA,* wanapoongeza umeme jazilizi waangalie maeneo yale ambayo *line* za *high tension* zimepatikana ambazo ni *meter* 30 kutoka kwenye *line*. Tunaposema vitongoji havina umeme, maana yake ni hakuna kabisa *line* iliyokwenda katika maeneo yale. Sasa tunajikuta umeme jazilizi tunaenda kwenye maeneo yale yale ambayo *line* ya umeme imepita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, malalamiko ya wananchi wa vile vitongoji ambavyo umeme haujafika kabisa yamekuwa ni makubwa, waangalie namna ya ujazilizi huu kwenda sambamba na kuongeza *line* za *high tension,* ili yale maeneo ambayo umeme haujafika kabisa waweze kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili hili suala la *REA,* naomba ndugu zangu wa *REA,* hasa Mollel na mwenzake Mrope Hamisi, wajitahidi watusaidie. Kuna maeneo ya huduma za jamii, kama Sekondari ya Tuwe Macho, haina umeme. Niliongea na Naibu Waziri na niliandika barua, lakini naona bado mpaka leo ile sekondari haijapatiwa umeme, na pale tumeongeza Kidato cha Tano na Sita, ikiwezekana Mwezi Julai watoto wataanza kwenda pale na shule ile haina umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba ipelekewe umeme, pamoja na Zahanati ya Tuwe Macho, ambapo zote hizi zipo katika Kitongoji cha Zimamoto. Tunaomba kitongoji kile

kipelekewe *line* ya umeme, ili Sekondari ya Tuwe Macho na Zahanati ya Tuwe Macho zipate umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tuna sekondari mbili mpya zinajengwa katika Kata ya Mbati iliyopo katika Kijiji cha Mdabwa, Kitongoji cha Chapakazi, *line* ya umeme kule hakuna. Tunaomba tusaidiwe *line* iende kule, ili shule ile itakapoanza kazi watoto wawe wanaendana na hali ya kisasa ya shule kuwa na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, katika Shule ya Sekondari mpya pale Mtina, tunajenga katika Kitongoji cha Sauti Moja, Kijiji cha Muungano, napo pale shule kubwa ya amali inategemewa kuanza hivi karibuni, lakini bado kitongoji kile hakina *line* ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Wizara, watu wa *REA* watusaidie katika maeneo hayo matatu ya huduma za jamii tuweze kupata umeme, ili huduma zile ziende vizuri. Tunaomba sana, ili mambo haya yafanikiwe, gridi ya Taifa, kasi ya ujenzi kutoka Namtumbo kuja Tunduru pamoja na ujenzi wa *extension* pale Tunduru uende kwa kasi mliyokubaliana, ili na wenzetu wa Nanyumbu na Masasi wapumzike kukatikakatika kwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda sana nichangie ni suala la matumizi ya gesi. Tunaishukuru Wizara, mwaka 2024 tulipata mitungi ya gesi, tumegawa kwa viongozi wetu wa vyama vijijini, lakini ile mitungi haitoshi. Ili kuhamasisha zaidi, tunaomba tena tupewe angalau mitungi mia mbili mbili kila Mbunge aende kugawa kwenye vitongoji na vijiji ili tuhamasishe matumizi ya gesi. Hili jambo liwasaidia sana wenzetu wale walioko kijijini kuacha kutumia kuni na kukata miti ovyo, ili kuhakikisha kwamba, wanakwenda kisasa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia punguzeni na bei ya gesi, imekuwa changamoto kwa watu wa vijijini kwa sababu, bei ya shilingi 25,000/= kwa kilo 14 au 13 ambayo inaweza ikatumiwa kwa muda wa mwezi mmoja, watu wa vijijini wameshindwa

kununua gesi hiyo. Kwa hiyo, tunaomba angalau ruzuku ile iongezwe ili wananchi wa vijijini waweze kupata mitungi ya gesi na gesi yenyewe kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili nitakwenda moja kwa moja kwenye ujenzi wa *NLG* pale Lindi, hili litakuwa ni suluhisho maalumu kwa matumizi bora ya gesi. Kama walivyozungumza Wabunge wenzangu waliotangulia, gesi nyingi tunayotumia kwenye nyumba zetu inatokana na *NLG,* ambayo inatoka nje ya Tanzania. Ni kitu cha ajabu wakati sisi wenyewe tuna gesi ambayo tunaweza kuweka katika *form* hiyo ya *NLG* ikasambazwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana jambo la *discussion* ya *NLG* lifikie mwisho. Huu wimbo wa kila siku kuhusu *NLG* na matokeo yake hatuyaoni kwa kweli, tunajirudisha nyuma kiuchumi. Naomba sana Serikali kwenye jambo hili iliangalie kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye *NLG,* naomba *TPDC* waongezewe pesa za kujenga vituo vya kujaza gesi kwenye magari. Nimefurahi kuona kwenye hotuba ya bajeti ya Waziri, amesema kuna vituo vya *mobile* vitakuwepo viwili Dodoma, kimoja Morogoro na vitatu pale Dar es Salaam. Ninadhani bado havitoshi kwa jinsi uchumi wetu unavyokua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza gharama ya kutumia mafuta, tunatakiwa tuweke msisitizo mkubwa kwenye suala la vituo vya kujaza gesi kwenye magari, ili matumizi ya gesi yaongezeke na matumizi ya mafuta yapungue, ili kuchechemua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuunga mkono Mheshimiwa Mbunge mmoja, alisema kwanza tuweke lengo. Serikali ndiyo watumiaji wakubwa wa mafuta ya *petrol* na *diesel.* Tukiweka malengo ya kuhakikisha kwamba, ndani ya miaka mitatu au mitano magari yote ya Serikali yatumie gesi, inawezekana na itatusaidia kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni muhimu sana kwa sababu, bei ya mafuta kila siku inapanda, gesi nchini tunayo. *NLG* ikijengwa, gesi itatumika sana kujaza kwenye magari na *speed* ya matumizi ya gesi nyumbani nayo imekuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mkoa wa Ruvuma, Lindi na Mtwara matumizi ya gesi nyumbani yatiliwe mkazo ili wananchi wafaidike na gesi yao inayochimbwa katika ardhi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, ahsante sana. Kabla sijamtaja mchangiaji anayefuata, naomba niwatangaze wageni ambao wapo Bungeni jioni hii.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 36 wa Mheshimiwa *Eng*. Samwel Xaday Hhayuma, Mbunge. Hawa ni Wanakwaya wa CCM kutoka Hanang, Mkoani Manyara. Karibuni sana wanakwaya kutoka Hanang.

Pia tuna wageni 67 wa Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge, ambao ni Taasisi ya Mtetezi wa Mama kutoka Mkoani Mwanza. Karibuni sana wageni wetu wa Taasisi ya Mtetezi wa Mama kutoka Mkoani Mwanza.

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, ambao ni wapiga kura wake kutoka Mbulu Vijijini, Mkoani Manyara, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, pia, tuna wageni ambao wametembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo. Wapo wanafunzi 60 wa Chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo, kutoka Kampasi ya Dodoma Mjini. Karibuni sana wanafunzi wetu wa Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo.

Vilevile, tuna wanafunzi 32 kutoka Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini cha Jijini Dodoma. Karibuni sana wanafunzi kutoka Chuo cha Mipango.

Nilimtaja Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki na Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, ajiandae.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kwa kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake kwa nchi yetu. Kuiongoza nchi ni kazi ngumu, haiwezi kulingana na kuongoza kijiwe cha kahawa au shikome. Kule kwetu kuna vitu tunaviita hivyo, ni kazi ngumu, ni mfupa mgumu. Sasa tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu ameweza kuendeleza mshikamano, amani na utulivu wa nchi yetu ambayo pia ni mfupa mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunaelewa Mheshimiwa Rais aliichukua nchi kwenye mazingira gani? Ilikuwa ni mfupa mgumu kweli kweli, lakini tunampongeza pia kwa sababu ya miradi ya maendeleo, ambayo nayo ilikuwa ni mifupa migumu. Mradi wa maendeleo wa Mwalimu Nyerere ulikuwa ni mfupa mgumu, Mradi wa kuendeleza Makao Makuu ya Nchi, Dodoma ulikuwa ni mfupa mgumu, mradi wa kuendeleza madaraja na kuanzisha mengine ilikuwa ni mifupa migumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuendeleza Shirika letu la ndege kwa kununua na kuongeza ndege nyingine ni mfupa migumu, lakini yote hiyo Mheshimiwa Rais ameitafuna na kuisagasaga na baadhi ya miradi imekamilika. Sasa watu wengine tukimpongeza wanasema, Mbona ninyi CCM mnampongeza tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni lazima tumpongeze kwa sababu, anayoyafanya Mheshimiwa Rais. siyo ya kawaida na ndiyo maana kwenye Mkutano wetu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Januari, 2025, tulipotafakari sana tukasema tunamtuma nani kutoka CCM ili kugombea Kiti cha Urais? Sisi Wajumbe wa Mkutano Mkuu hatukusita kusema huyu huyu mtafuna mifupa migumu aende. Sasa kwa nini tusimpongeze? Kwa kweli, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, amefanya yaliyo ya kweli kwa wananchi wake na kwa Watanzania wenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, ndugu yangu Dkt. Dotto Biteko. Huyu naye ni simba mwendapole. Mambo yake yanaeleweka na yanajulikana pamoja na vitengo vyake. Alipokuwa Wizara ya Madini aliipandisha sana, mapato kutoka Wizara ya Madini yaliongezeka na kelele za wachimbaji wadogo wadogo zilizokuwepo zikanyamaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati anashika Wizara hii ya Nishati, kulikuwa na vikelelekelele hivi, tulikuwa tunavisikia na Wizara hii siyo rahisi sana. Wizara hii ya Nishati na Wizara ya Madini zilipokuwa pamoja na Wizara nyingine, kama Kilimo na Utalii, siyo Wizara rahisi sana, ni Wizara ngumu. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Dotto Biteko kwa kufanya kazi vizuri, kwa usikivu wake na kwa kutuliza dhoruba zilizokuwa zinataka kujitokeza kwenye Wizara hii. Kwa kweli, nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nampogeza Naibu Waziri wake, ni mama mtulivu sana, ametokea kwa vijana, lakini kwa namna alivyoshika na kusaidiana na Naibu Waziri Mkuu amekuwa mama mtulivu na ambaye anaweza kufanya mambo yakaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Watendaji wote wa Wizara ya Nishati kuanzia Katibu Mkuu, wao na watendaji wakubwa wote. Poleni kwa Kiongozi Mkuu wa *TANESCO,* ndugu yangu Nyamuhanga. Ndiyo hivyo, duniani tunapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mambo machache tu. La kwanza ni umeme kwenye vitongoji. Tumesikia namna Kamati yetu ya Nishati na Madini ilivyosema, na kwa kweli naungananayo kwamba, tunakwenda polepole. Hatujaenda kwa kasi ambayo inatakiwa, na kama lengo letu ni kupata umeme kwenye vitongoji vyote ifikapo 2030, kwa kasi hii, bado hatuwezi kufika. Waongeze kasi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji, kwa sababu hivi tunaviita tu vitongoji, lakini kusema ukweli ni vijiji kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitongoji vingine ni vikubwa sana, vinatosha kuwa vijiji. Sasa watu walioko kwenye vitongoji hivyo kutokuwa na umeme ni kama tunawabagua hivi. Kwa hiyo, kwenye eneo hili, Wizara waongeze kasi ili tupate umeme kwenye vitongoji vyote ifikapo 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wilaya yetu ya Maswa, tuna vitongoji 510. Vilivyopata umeme ni vitongoji kama 200, vitongoji kama 310 hivi havina umeme kabisa. Kwa hiyo, naomba sana Wizara iongeze kasi kwenye eneo hili kwa sababu, wananchi wetu wote sasa hivi wanataka umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha pili ninachotaka kuzungumzia ni *low voltage* kwenye Mkoa wetu wa Simiyu. Kwa kweli, tunapata umeme kidogo kwenye mkoa wetu. Tuna umeme unaotoka Mkoa wa Mara na Mkoa wa Shinyanga *kilovolt* 33, lakini kwa sababu, unasafiri kutoka mbali sana unafika mkoani kwetu ukiwa kidogo sana. Sasa unapokuwa kidogo hivi, tuna umeme unaokatikakatika na usiotosha kwa shughuli za maendeleo zinazofanywa na wananchi kwenye mkoa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tatizo kubwa linakuwepo, hasa wakati wa kuanzia mwezi wa Tano na kuendelea wakati viwanda vya pamba vinapoanza kufanya kazi yake, *low voltage* inaongezeka zaidi, kwa hiyo, wananchi wanapata shida sana kupata umeme kwenye maeneo yetu. Naomba sana kwamba, tatizo hili lishughulikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwamba, wameanza ujenzi wa kituo cha kupozea umeme pale Imalilo, lakini tunaomba, huyu mkandarasi anaenda taratibu sana. Sababu mojawapo ya yeye kwenda taratibu ni kwamba, halipwi pesa yake kwa muda akimaliza kazi anazozifanya. Kwa hiyo, tunaiomba sana Wizara ifanye juu chini kuweza kumlipa huyu mkandarasi ili aweze kuharakisha kutandaza umeme kutoka Shinyanga mpaka Simiyu ili na sisi tuweze kufaidika na kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yupo mkandarasi wa pili anayejenga mitambo baada ya huyu kufikisha umeme kwenye mkoa wetu, huyu sasa hajaripoti kabisa kazini. Naiomba Wizara, huyu aripoti kazini na alipwe pesa yake; anadai *advance payment,* alipwe ili naye aweze kuja *site* aanze kazi nasi tuweze kupata umeme wa uhakika wa *kilovolt* 220 kutoka Mkoa wa Shinyanga. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara watusaidie kwenye eneo hili ili sisi pia tuwe na umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ninalolizungumzia ni magari kwa ajili ya Watendaji wa *TANESCO* kwenye Mkoa wangu wa Simiyu, hasa kwenye Wilaya yetu ya Maswa. Maswa ina gari lililonunuliwa mwaka 2003, ndilo linalotumika huko *field*. Naiomba sana Wizara watusaidie kutupatia gari kwa muda unaotakiwa ili meneja wangu wa *TANESCO* wa Wilaya ya Maswa aweze kwenda *field,* aweze kutuhudumia na kutufikishia umeme kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umewasha *mic* yako, muda wangu umeisha. Nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki. Nilimtaja Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga ajiandae.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na kukushukuru wewe pia kwa kunipatia nafasi kuwa miongoni mwa watakaochangia hotuba yetu hii ya Wizara ya Nishati, ambayo imewasilishwa leo hii asubuhi na Mwenyekiti wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza na kumshukuru kwa njia zote Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo amekuwa anafanya kazi kubwa sana. Sote ni mashahidi, na kwa jinsi ambavyo ameisimamia sekta hii ya nishati, wapi ameikuta, wapi ilipo na wapi inaelekea? Anahitaji pongezi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, pia kiranja ambaye anaongoza ndani ya Wizara yetu hii ya Nishati; Waziri wetu Mheshimiwa Dkt. Dotto na Naibu wake wamekuwa ni msaada mkubwa sana kwa Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha yale malengo yake ambayo anayo katika sekta hii ya nishati yanaweza kukamilika kwa muda na wananchi wote wanaona nini kinafanyika ndani ya Wizara hii ya Nishati. Hongereni sana kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitumie nafasi hii kuwapongeza Katibu Mkuu, Mameneja wote pamoja na Wakuu wa Idara za *Distribution* ambao ndio msaada mkubwa katika kuhakikisha Wizara hii inafanya yale ambayo wananchi wanayategemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wakati anaingia madarakani, ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ulikuwa umefikia 37%. Kwa hali ambayo tuliokuwanayo, ni wachache ambao walikuwa wanaweza kuona au kuhisi kama tunaweza kulikamilisha na kwa muda ambao umepangwa na kuweza kuleta matumaini ambayo sasa hivi sote tunajivunia humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ningependa nitumie nafasi hii nami nitoe mchango wangu ambao siyo mkubwa, lakini una nafasi yake katika Kamati yangu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya Nishati na Madini, napenda nili-*clear* hili kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niishauri taasisi yetu ya *REA,* imekuwa humu ndani tangu tumeanza kuchangia asubuhi, na Wajumbe wengi wamekuwa wakilalamikia bei ya shilingi 27,000. Mimi ninachokiona, tatizo ambalo lipo, tafsiri ya shilingi 27,000 inakuwaje? *REA* wametoa mwongozo wao kuwa 27,000 ni mita 30 kutoka kwenye chanzo cha umeme, lakini wananchi wengi miongoni mwao wakiwemo na Wabunge wengine humu ndani, wanajua kila kijiji ndiyo shilingi 27,000. Sasa hapa kilichopo ni tafsiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nichukue nafasi hii niwashauri *REA;* na Kamati yetu imeshakushauri sana *REA* kupitia Waziri wetu wa Nishati, kwamba utolewe mwongozo. Wananchi vijijini wengine wako mita, 30 na ukisema mita 120 ndiko kijijini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ambaye anakaa nje kidogo ya mji maana yake akikaa mita 120 maana yake huyu ndio maskini zaidi, hana uwezo wa kujenga mjini. Sasa anapokaa mita 120 maana yake anatakiwa alipe zaidi ya shilingi 512,000 ambayo tafsiri sisi kama Kamati ya Nishati na Madini tulisema wenzetu wa *REA* wachukue juhudi, na juhudi ambayo wanatakiwa kuchukua ni kuweka bei moja, kwamba vitongoji na vijiji wote wapewe *definition* moja ya kulipa kiasi chochote, hata kama itakuwa zaidi ya shilingi 27,000, basi iwe ni bei ambayo ni elekezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, wananchi wamekuwa wakienda *REA* kulalamika, kwa nini mnatufanyia bei hii kubwa zaidi ya hivi? *REA* wanasema sisi tunafuata mwongozo wa *EWURA*. *EWURA* nao ukiwauliza ni kwa nini mnapanga bei hii? Wanasema, tumeshatoa *justification,* shilingi 27,000 ni kutoka wapi mpaka wapi? Kwa hiyo, hii imekuwa ikileta mchanganyiko mkubwa, ndiyo maana kila Mjumbe ambaye anasimama hapa jambo la mwanzo anaanza na bei ya umeme ya shilingi 27,000 na jinsi gani kitongoji na umbali wa mita 100 unakuwaje? Ningependa niwashauri wenzetu wa Nishati kwamba, hili walichukulie kwa uzito ambao uliokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu kukatika kwa umeme. Jambo hili ni kutokana na tatizo la miundombinu, hakuna ambaye hafahamu. Vilevile, asubuhi hapa tumepata taarifa, Mheshimiwa Waziri amesoma, tunao umeme, sasa hivi uzalishaji wetu tumefika megawati 4,000 *which is good* na jambo zuri. Tujipongeze kutokana na wapi tulikuwa na wapi tumefika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nataka niuweke hapa sasa katika Wizara hii ya Nishati, lakini katika kitengo cha *TANESCO.* Umeme tunaouzalisha nchini tunao mwingi, zaidi ya

4,000, lakini usambazaji sasa, *transmission line,* hazipo za kutosha. Umeme ambao tunapigia kelele humu ndani, tuna umeme Bwawa la Mwalimu Nyerere, 2,115, lakini ukitoka Bwawa la Mwalimu Nyerere umeme unakuja mpaka Chalinze, ukitoka Chalinze umetulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu ya Nishati sasa hivi ina mradi mkubwa, ambapo miezi miwili iliyopita tulishuhudia pale Zuzu Wakandarasi wamepatikana ili kutoa *transmission line* kutoka Chalinze mpaka hapa Zuzu ya *400 kilovolts*. Hii itasaidia sasa kuutoa ule umeme kule ukaja hapa, halafu hapa tukajenga *line* nyingine kutoka Zuzu kwenda Singida, na Singida tutapata *line* nyingine ambayo inaunganisha sasa ile ya Arusha kwenda mpaka Namanga ili kuweza kutimiza ile azma na nia ya Mheshimiwa Rais kuuza umeme nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa kuuza tunao, umeme tunao tunachokosa tu ni *transmission*. Wananchi wengi wana hamu na wana haraka ya kuupata umeme kama wanavyoona sehemu nyingine. Kweli nia ipo, Serikali mipango yote hii imeiweka sisi Wajumbe wa Kamati tuna-*declare* humo kuwa mipango yote iko wazi na Serikali imekuwa ikifanya kila aina ya juhudi. Kikubwa zaidi, tuhakikishe usambazaji wa umeme mkubwa wa kilovoti 400 tuhakikishe unaenda kwa haraka na Serikali iweke bei yake hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda niwapongeze Wajumbe wenzangu wa Kamati kwa kuweza kuisimamia Wizara hii ya Nishati kuweza kufanya haya yote ambayo mnawasifu Waziri na Naibu wake na Watendaji. Bila ya mwongozo wetu sisi kama Kamati yasingefikiwa. Kwa hiyo, nasi pia mtupigie makofi tuseme tumewasimamia, tunajipongeza sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *(Alizungumza bila kutumia kipasauti, hakusikika)*.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Wewe siyo Kamati yako, haikuhusu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza. Nilimtaja Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mheshimiwa Jonas William Bunda ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi niweze kuchangia Bajeti hii ya Wizara ya Nishati. Niungane na Wabunge wenzangu wote kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Daktari Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana anayoifanya kwenye sekta hii ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nampongeza pia Mheshimiwa Dotto Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Kwa kweli kazi anayoifanya ni nzuri sana. Alipokuwa Njombe niliweza kueleza changamoto za Kata ya Lumbila na Kata ya Kilondo kule Jimboni kwangu, Mheshimiwa Biteko aliunda timu ya wataalam mchanganyiko wa *TANESCO* na *REA,* waliweza kwenda Kijiji cha Nkanda, walienda Kijiji cha Lumbila, Kijiji cha Chanjale na sehemu ile ya Kata ya Kilondo. Nashukuru sana Kamati ile ambayo aliunda iliweza kuleta matokeo makubwa, kuna hatua mbili, tatu tulisogea kwenye changamoto za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kumtuma Naibu Wake Mheshimiwa Judith Kapinga Jimboni Ludewa ambako aliweza kutusaidia kutatua changamoto ya umeme katika Kata ya Milo, Kata ya Mawengi ambao ulikuwa una mzalishaji binafsi anaitwa Jumah. Wananchi wale walikaa miezi tisa gizani, lakini baada ya ujio wa Mheshimiwa Waziri hatua za haraka zilichukuliwa na wananchi wale wa Mawengi, Milo waliweza kuwashiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, Mheshimiwa Kapinga alitusaidia kutatua changamoto ya umeme wa Madope ambao unasambaza kwenye vijiji 20, na ulikuwa ni umeme ambao unazalishwa na mzalishaji binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya yalikuwa na changamoto za mgao wa umeme kwa zaidi ya masaa 12. Kwa hiyo, kwa kitendo cha Mheshimiwa Waziri kumtuma Naibu wake tuliweza kutatua changamoto hizi kwa kiasi kikubwa, kwani wazalishaji hawa binafsi waliweza kuingizwa kwenye gridi ya Taifa na mgao ulimalizika pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani zangu hizi naomba pia kuwakumbusha watu wa *REA*. Kulikuwa kumetengwa kiasi cha shilingi bilioni sita ambayo walikuwa wapewe watu wa Madobe kwa ajili ya kurekebisha changamoto ya miundombinu ya umeme wa Madope. Ninapozungumzia hili, nitoe pole nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri kwa kuondokewa na Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO.* Nina imani barua za mwisho mwisho alizozishughulikia ni pamoja na barua hii ya Ludewa ya shilingi bilioni sita ambazo zinapaswa kutoka *REA* kwenda *TANESCO* kwa ajili kwenda kurekebisha miundombinu ya umeme wa Madobe. Kwa hiyo, nitoe pole nyingi na tumwombee marehemu apumzike kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa *REA* walitenga hizi shilingi bilioni sita kwa sababu mzalishaji binafsi aliyejenga miundombinu ya umeme ule wa Madope, nyaya ambazo aliziweka zilikuwa ni milimita 20 wakati *standard* ya *TANESCO* kwa sasa ni milimita 100. Kwa hiyo, inatakiwa zile nyaya zibadilishwe, nguzo zile ambazo ziliwekwa nazo zilikuwa chini ya kiwango, nyingi zilikuwa zinadondoka na zilikuwa zinadondoka na kusababisha kukosekana kwa umeme muda mwingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa wameunganishwa kwenye gridi ya Taifa, maana yake umeme unavyokatika kutokana na miundombinu hii ambayo nimeisema, basi Wilaya nzima inaathirika na kuleta kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukipokea hizi shilingi bilioni sita, kwa sababu bajeti yote ilikuwa ni shilingi bilioni nane, lakini hizi zipo na barua zile za mwezi Septemba kulikuwa na *correspondence* kati ya *TANESCO* na *REA*. Wiki iliyopita nilimwona Mheshimiwa Naibu Waziri, namshukuru alinisikiliza. Kwa hiyo, fedha hii

tunaiomba iweze kuharakishwa ili Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa aweze kwenda kufanya *operation* kule au kwa kutumia wakandarasi ili wafanye kazi kubwa kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pia nimeona katika tangazo kwenye mfumo wa *NEST* vitongoji ambavyo havikuwa na umeme takribani 35 vimeweza kuingia kwenye orodha. Hii itaondoa kero kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa na Mheshimiwa Mkuu wangu wa Wilaya, tulifanya mkutano pale Ludewa Mjini, baada ya kutoka kwenye Baraza la Madiwani tukafanya mkutano na pale Makao Makuu ya Wilaya. Kuna wananchi wengi wanaotoka maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, waliomba sana niweze kufikisha hoja hii Bungeni kwamba tuweze kusaidiwa kutatua hii changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Ludewa sasa lina uwekezaji mkubwa. Kuna mwekezaji anakwenda kuchimba dhahabu Irininda, pia kuna wawekezaji pale Kata ya Lubonde Kijiji cha Mkiu wanakwenda kuchimba hizo zinaitwa *rare earth element/minerals.* Kwa hiyo, wataweka pale migodi yao wanahitaji umeme mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika kuna Liganga na Mchuchuma. Mheshimiwa Jafo alitembelea Jimboni kwangu, ilionekana kwamba, uwekezaji unakuja kuanza mapema sana. Sasa uwekezaji huu unakwenda sambamba na uwepo wa umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie fursa hii kuomba Bunge lako Tukufu kupitia Wizara hii tuweze kuletewa kituo cha kupoozea umeme pale Ludewa, kwa sababu kwa sasa tunategemea kituo cha kupoozea umeme ambacho kipo Madaba, ni kilometa nyingi sana, ni zaidi ya kilometa 200 kutoka Wilayani Ludewa. Kwa hiyo, kituo hiki kitakuja kusaidia wawekezaji hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hao wawili tu niliowasema, Kijiji cha Mdilidili pia kuna wawekezaji wameshaleta mitambo mikubwa kwa ajili ya uchimbaji wa madini mbalimbali pale. Kwa hiyo, nao watahitaji umeme mkubwa sana. Kwa hiyo, tukiletewa kituo cha kupoozea umeme, na huu uwekezaji wa Liganga na Mchuchuma unavyoanza, kwa kweli tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wilaya ya Ludewa tuna changamoto ya gari la kubebea nguzo. Ilitokea Kata ya Ibumi, kuna nguzo ziliungua au kata nyingine ambapo zinahitajika kubadilishwa nguzo. Kwa mfano, Kisaula, au Iwela, ilichukua muda mrefu kwa sababu ma-*engineer* wa *TANESCO* walikuwa hawana gari la kubebea nguzo, lakini namshukuru Meneja wa Mkoa amekuwa mwepesi kuwasaidia kuwaazima gari. Kwa hiyo, ili tuweze kutatua changamoto za wananchi kwa haraka, naomba Wizara hii iweze kutuletea gari lile lenye *winch* kwa ajili ya kubebea nguzo ili changamoto za wananchi ziweze kutatuliwa kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuomba hili gari la kubebea nguzo, napenda pia kuomba Wizara hii iweze kutuma wataalam wake pia Kata ya Kilondo ili wakaangalie ule mradi wa umeme wa Maji. Kwa sasa nimshukuru Mkurugenzi Mkuu wa *REA*, kwa maelekezo aliyopewa na Mheshimiwa Waziri, alituahidi anatafuta mkandarasi aende kuwafungia *solar* wananchi wale wakati wakisubiri mradi wa umeme wa maji kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wale wananchi wako tayari hata kukabidhi mradi huu Serikalini kwa sababu ule mradi ulikuwa ni mali ya Serikali ya kijiji. Kwa hiyo, wako tayari hata kukabidhi Serikalini na wale wakina Mwambeleko ambao walikuwa wanazalisha umeme wao, wanachohitaji ni wananchi wapate huduma. Kwa hiyo, wanaomba wataalam waende wakaangalie ili waweze kupata ruzuku kutoka *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme huu wa solar, kule Ziwa Nyasa kunakuwa na dhoruba, mawimbi makali. Kunapokuwa na mawimbi, kunakuwa na mawingu. Kwa hiyo, kukiwa na mawingu

umeme huu wa jua unaweza usipatikane wakati wote. Kwa hiyo, wanaomba sana mpango ule wa kuzalisha umeme wa kutumia maji uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijahitimisha, kuna ule mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Kikonge ambao kwenye jimbo langu, wananchi wa Liugai wameshakwenda kufanyiwa uthamini tangu mwaka 2024. Kwa hiyo, wananchi wale robo tatu ya kijiji wameshafanyiwa uthamini na wameambiwa wakati wowote wanaweza kulipwa fidia ili wahame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Serikali iweze kwenda kutoa kalenda ya utekelezaji wa mipango hii ili wananchi wale nao waweze kupanga ratiba zao za kilimo, kwa sababu maeneo hayo wanayategemea kwa kilimo. Wanaomba sana waweze kujua ni lini wananchi wale wa Liugai watalipwa fidia ili mradi huu uweze kutekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naomba tu, kuna shule tatu; Shule ya Sekondari Lubonde, nimetembelea juzi, haina umeme, na iko kwa hawa wazalishaji binafsi ambao tayari wameshaingia kwenye gridi ya Taifa. Kuna Shule ya Sekondari *Mount Masusa* ambayo iko Kata ya Lupanga na Shule ya Sekondari Madilu. Shule hizi zina watoto wengi na wanafanya vizuri. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iweze kuwapelekea umeme haraka ili watoto hawa waweze kutumia katika masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nashukuru sana kwa kupewa nafasi hii, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga. Nilimtaja Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo ajiandae.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Nishati. Kwanza kabisa naomba nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa

Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi alivyosimamia na kuhakikisha kwamba anatekeleza mambo mengi sana yanayohusiana na Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu pia Waziri wa Nishati kwa jinsi anavyofanya kazi vizuri ya kuhakikisha kwamba anatatua changamoto za wananchi kwenye masuala ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Dkt. Biteko kwa sababu anafanya kazi za kizalendo. Kama ukiangalia kipindi kile alikuwa kwenye Wizara ya Madini alifanya kazi vizuri na leo anafanya kazi kwenye nafasi ya Unaibu Waziri Mkuu, na pia nafasi ya Waziri wa Nishati. Wakati anateuliwa, mimi nilisema huyu mtani wangu ataweza kweli kumudu nafasi zote mbili? Lakini leo tunampongeza kwa sababu amefanya vizuri na anaendelea kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Judith Kapinga, Naibu Waziri wa Nishati, dada yangu, anafanya kazi nzuri. Anatoa ushirikiano mkubwa sana kwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Wakati anaingia pale Wilayani kwetu Mbinga tulikuwa na changamoto, baadhi ya vijiji vilikuwa bado havijafikiwa na umeme, na alipoingia alifanya kazi nzuri, alifanya kazi kwa bidii ya kusimamia kuhakikisha kwamba, vijiji vyote mpaka sasa hivi vimepata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie pia nafasi hii kumpongeza *Eng.* Mramba, Katibu Mkuu wa Wizara. Pia nawapongeza Dkt. Mataragio na Dkt. Kazungu Manaibu Katibu Wakuu. Pia, bila kuwasahau Wakurugenzi kutoka kwenye taasisi mbalimbali zinazosimamiwa na Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii nimpongeze sana Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa Ruvuma na Meneja wa *TANESCO* wa Wilaya Mbinga, kwa jinsi wanavyojitahidi kutatua

changamoto mbalimbali zinazotokana na hitilafu za umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majukumu mengine ya *TANESCO,* lakini bado *TANESCO* ina jukumu kubwa la kuhakikisha Wizara ya Nishati inasimamia uzalishaji wa umeme, inasimamia usafirishaji wa umeme na inasimamia usambazaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia taarifa ya Waziri wa Nishati ambaye ni Naibu Waziri Mkuu, ukiangalia takwimu za uzalishaji kufikia mwezi wa Nne tulikuwa tunazalisha megawati 4,031, lakini ukiangalia kwenye matumizi, tulikuwa tumefikia megawati 1,921.44. Kwa hiyo, unakuta kabisa kwamba kuna tofauti, yaani kuna ziada ya megawati 2,110. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo huu unaona kwamba ziada hiyo siyo kwamba imetokana na kwamba tumetosheka kwenye matumizi ya umeme, hapana. Bado tuna changamoto, inatakiwa tufanye kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba tunaweka miundombinu ya kutosha kusafirisha umeme, lakini pia tunaweka miundombinu ya kutosha kusambaza umeme kwa wananchi katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu lingine ambalo lilikuwa ni mpango mzuri sana wa Serikali ni kuhakikisha kwamba inapeleka umeme vijijini na inapeleka umeme kwenye maeneo ya mjini. Naomba nichukue nafasi hii niipongeze sana Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba umeme umepelekwa vijijini takribani vijiji vyote katika Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali inaendelea kusambaza umeme kwenye maeneo ya mjini kwa sababu miji yetu inazidi kukua. Kwa hiyo, kwa hilo naomba niwapongeze sana na ninaomba mwendelee kuhakikisha kwamba umeme huu unasambazwa katika hayo maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu lingine ni kuhakikisha kwamba tunasimamia kufanya utafiti na kuhakikisha kwamba

tunafanya *extractions* ya kwenye mafuta na gesi. Nalo naiomba Serikali iendelee kuweka msisitizo mkubwa sana kwenye maeneo hayo mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze pia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka kipaumbele kusimamia kwenye kuhakikisha kwamba kuna matumizi ya nishati safi. Hilo ni suala la msingi, kwanza linarahisisha upatikanaji wa nishati kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukiangalia taarifa ya Wizara ya Nishati kwenye masuala ya uzalishaji umeme, tunakuta kwamba 67.4% umeme huo unazalishwa kwenye vyanzo vya maji. Kwa hiyo, tusiposimamia utunzaji wa maliasili kwenye misitu na vyanzo vya maji, ni wazi kwamba hivi vyanzo ambavyo vinazalisha umeme kuna siku tutakuja kukwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba Wizara waendelee kusimamia kuhakikisha kwamba tunapata nishati safi ya gesi kama tulivyoanza kugawa, lakini na vitu vingine ambavyo ilitakiwa viendelee kuhakikisha kwamba tunalinda maliasili ya misitu ili kutunza uoto wa asili na kuhakikisha kwamba tunapata umeme wa maji kwa muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu lingine la Wizara ya Nishati ni kuhakikisha kwamba tunazalisha gesi kupitia *LNG*. Kwenye *LNG* tuna uhakika wa kupata umeme wa kutosha, na pia tunakuwa na uhakika wa kupata umeme kwa ajili ya kutumia majumbani. Vilevile tutaendelea kupata umeme gesi kwa ajili ya kutumia kwenye magari yetu, na hiyo itatusaidia sana kupunguza kutumia fedha nyingi za kigeni kuagiza mafuta kutoka nje. Kwa hiyo, naomba Serikali iendelee kuweka mkazo mkubwa kuhakikisha tunaimarisha umeme wetu kwa kupitia *LNG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna njia nyingine ya kupata umeme kupitia jotoardhi. Niliona wakati wa kongamano la umeme jotoardhi wakati inafanyika Dar es Salaam ilionekana Mbeya tayari wameanza kufanya utafiti na kuanza kuzalisha umeme huo. Kwa hiyo, naomba Serikali iendelee kuwekeza fedha

nyingi sana kuhakikisha kwamba tunazalisha umeme kupitia jotoardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata bahati katika nchi yetu tunazalisha na tuna maeneo mengi sana yenye makaa ya mawe. Kwa mfano, nikichukulia eneo la Liganga, sisi kule Mbinga tunazalisha makaa ya mawe, lakini Liganga tumepata bahati kuna makaa ya mawe, na madini ya chuma yako pale. Kwa hiyo, ni wazi kwamba kama Serikali itawekeza fedha nyingi sana kwenye kuzalisha umeme kupitia makaa ya mawe, wakati wa kuvuna chuma, hatutatumia gharama kubwa sana ya kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile njia nyingine mojawapo ya kuongeza umeme ni kuzalisha umeme kupitia makaa ya mawe. Katika *literature* mbalimbali ambazo nilizisoma nilikuta kwamba kuna wenzetu wa India, kuna kampuni moja inaitwa *Adam Power Generations Limited,* inazalisha umeme megawati 17,500 kwa kupitia makaa ya mawe. Wanasafirisha makaa ya mawe kutoka Tanzania na sehemu nyingine, lakini sisi makaa ya mawe tunayo Tanzania na tuna eneo moja ambalo tunaweza tukazalisha makaa ya mawe tukavuna chuma na tukayeyusha kupitia makaa ya mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi zote nilizotoa pamoja na mchango mwingine wa nyongeza ambazo nimechangia upande wa Serikali ili iweze kufanya, lakini bado kuna changamoto kwenye eneo langu la Jimbo la Mbinga Mjini. Kama nilivyosema awali kwamba Serikali imejitahitadi, imesambaza umeme katika vijiji vyote vya Jimbo la Mbinga Mjini na vijiji 78, na pale mjini umeme unaendelea kusambazwa, lakini kuna changamoto kubwa sana ya kukatika umeme mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba Serikali kwanza iendelee kuimarisha miundombinu ya kusambaza umeme, lakini pia tujengewe kituo kidogo cha kupooza umeme ili kuhakikisha kwamba umeme ule unaimarika katika maeneo yale. Pia kama tulivyosema, tumefanikisha kupeleka umeme kwenye vijiji vyote,

lakini bado tuna changamoto ya kupeleka umeme kwenye vitongoji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wale wanahitaji sana kupata umeme na wengi wapo kwenye vitongoji ambavyo vijiji vyao vimepata umeme. Kwa hiyo, naomba Serikali iendelee kupeleka umeme na kuusambaza kwenye vitongoji mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto zote ambazo nimezisema, lakini pale wilayani kwangu kuna changamoto ya gari kwa wale watumishi. Wilaya ya Mbinga ina majimbo mawili na maeneo ya Mbinga maeneo mengi ni miinuko, gari iliyopo pale ni *pickup* ambayo ni ya muda mrefu. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati katika bajeti yao waangalie ni namna gani tutakavyopata gari ili iweze kuwasaidia wale watumishi kwenda kufuatilia na kuhakikisha kwamba wanapeleka umeme kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jonas William Mbunda, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, na huyu ndiyo atakuwa mchangiaji wa mwisho kwa leo.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuwa mchangiaji wa mwisho jioni hii ya leo. Nami nianze kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake kubwa za kuhakikisha umeme unafika kwenye maeneo yote ya wananchi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuteua timu imara ya Wizara ya Nishati ikiongozwa na kaka yetu, kiongozi wetu Naibu Waziri Mkuu, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko. Kwa kazi kubwa kubwa wanayofanya akisaidiwa na mdogo wangu Mheshimiwa Judith Kapinga, kwa kweli wanafanya kazi njema. Nilikuwa najiuliza, timu

ya hii Wizara na Wasaidizi wao kule; Katibu Mkuu na Wakurugenzi, ni watu *humble* sana na wanafanyakazi vizuri sana, lakini nikajua ni jitihada za Naibu Waziri Mkuu na zile hotuba zake za kila wakati kutufundisha. Kwa hiyo zinachangia pia kila wakati kujielimisha na hivyo kutuboresha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, aendelee kutupatia zile hotuba za kufikirisha, za kimaisha ili tuendelee kutafakari na kujisahihisha na kujikosoa ili tuweze kuwa bora kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tushukuru sana wananchi wa Mbarali, tunashukuru sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo mmetufanyia ya kuhakikisha tunapata umeme. Sisi kwenye kazi ya vijiji, vijiji 102 vilivyopo Wilaya ya Mbarali tayari mmetupatia umeme, tunashukuru sana kwa jitihada hizo, lakini kwenye upande wa vitongoji, kati ya vitongoji 712 tayari tumepata umeme kwenye vitongoji 510 ni kazi kubwa, wanastahili pongezi na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna kazi ya vitongoji 202 na nimefarijika leo asubuhi nilimwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusiana na Mkandarasi kufika, amenihakikishia wiki hii mkandarasi atafika. Hivyo sasa, vitongoji vile 15 na nimeona vitongoji 53 tayari mmeshatangaza *tender,* kwa sasa tutabaki na vitongoji 134 kwa siku zijazo kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru sana, tunawasubiri kwa hamu sana, tunahitaji umeme uwake maeneo yote, kwa sababu sasa hivi umeme siyo jambo la *luxury* tena, ni hitaji la msingi, ni Uchumi, ni ajira. Kwa hiyo, tunawatakia kila la heri na tutafurahi zaidi mkitusaidia tupate hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wilaya ya Mbarali tumeshapokea shilingi bilioni 9.2 kwa ajili ya shughuli ya kupeleka umeme. Hizi ni fedha nyingi na Wilaya yetu tunashukuru sana kwa kazi kubwa hii ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu amefanya. Sasa naomba kwa unyenyekevu sana Jimbo la Mbarali lina changamoto kutokana na jiografia yake, lakini tuna

changamoto kubwa, na wale watu hawana usafiri. Jimbo hili lina changamoto ya usafiri, lazima upite mashambani ndiyo ukatafute kijiji kilipo. Kwa hiyo, hata nguzo ikianguka ni lazima mtu akae siku mbili au tatu, aazime gari kwenye Wilaya ya jirani ndiyo wakafanye shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imekuwa ni changamoto kubwa sana, na wananchi sasa imekuwa kilio wanapopata tatizo inachukua siku tatu, nne ili waweze kwenda kuhudumiwa. Naomba sana sana tusaidiwe tupate gari la nguzo ili Wilaya hii ambayo jiografia yake inasumbua sana waweze kupata usafiri huu na kuweza kuhudumiwa kwa wakati. Vilevile magari ya watumishi ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo ni changamoto, tunatambua Serikali wanayo jitihada kubwa ya kuhakikisha kumtua mama kuni kichwani, na hilo zoezi limefanyika kwa kweli wanajitahidi, lakini tunaomba, kuna mitungi ilikuja ya bei elekezi. Kwa mazingira haya, niishauri tu Serikali kwa siku zijazo, lazima tuangalie mazingira tuliyonayo. Sisi kule vijijini mtu yuko radhi kutoka tu hapo nje akikuta kuna kuni, anaichukua na kuiweka jikoni, maisha yakaendelea. Sasa mpaka umwelimishe kwamba zina athari na vitu kama hivyo, itachukua muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata kama ni ruzuku, hebu tuangalie kwa sababu mitungi mingi huko vijijini sasa hivi ikishaisha gesi, haiendi tena kwenye mzunguko kutokana na gharama kubwa. Kwa hiyo, hebu mfanye tathmini kubwa ya kuhakikisha kwamba tunawasaidia wale ambao wako karibu na wanaweza wakapata kuni hata kwa shilingi 2,000, kwa kuwandolea mzigo mkubwa, hebu tuangalie ili tuweze kuwasaidia ili azma ya Mheshimiwa Rais ya kwamba wanawake sasa watuliwe kuni kichwani iweze kutumia kulingana na nishati hii kupatikana kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, tunafahamu sasa hivi shida iliyopo ni kukatika umeme kwa ajili ya kurekebisha miundombinu, na changamoto hii pia imekuwa kero kwa wananchi. Basi angalau tuwe tunapata taarifa kuliko kutokee tu

hitilafu ghafla. Angalau watengeneze utaratibu kwamba leo tuna matengenezo ya umeme maeneo fulani na maeneo fulani umeme utazimika saa fulani na saa fulani ili kuondoa hasara ambazo zinaweza zikapatikana kwa kuzimika haraka bila taarifa yoyote. Hiyo itatusaidia ili tuweze kupata umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. Ahsante kwa kuchangia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, ahsante sana. Huyo ni mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana na kuwapongeza wote kwa michango yenu na hoja zetu ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati pamoja na Naibu Waziri wake wako makini toka asubuhi kwa kusikiliza hoja zenu. Basi nami niwatakie kila la heri na niwatakie jioni njema.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.13 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 29 Aprili, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*